

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

BUNGE LA TANZANIA

MAJADILIANO YA BUNGE

MKUTANO WA NNE

Kikao cha Ishirini na Tano – Tarehe 14 Julai, 2011

(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)

D U A

Spika (Mhe. Anne S. Makinda) Alisoma Dua

HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (ELIMU):

Taarifa ya Mwaka ya Hesabu zilizokaguliwa kwa Mwaka 2009/2010 za Shirika la Elimu Kibaha (*Kibaha Education Centre Annual Report and Audited Accounts 2009/2010*).

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:

Randama za Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Nishati na Madini kwa Mwaka wa Fedha 2011/2012.

NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:

Hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha ya Wizara ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia kwa Mwaka wa Fedha 2011/2012.

MWENYEKITI WA KAMATI YA MIUNDOMBINU:

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu Kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia kwa Mwaka 2010/2011 Pamoja na Maoni ya Kamati Kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2011/2012.

MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI KUHUSU WIZARA YA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:

Taarifa ya Msemaji Mkoo wa Kambi ya Upinzani juu ya Wizara ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia Kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2011/2012.

MASWALI KWA WAZIRI MKUU

SPIKA: Maswali kwa Waziri Mkoo. Bahati nzuri leo Kiongozi wa Kambi ya Upinzani yupo. Mheshimiwa Mbewe.

MHE. FREEMAN A. MBOWE: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa fursa ya kumwuliza Waziri Mkoo, swali. Mheshimiwa Waziri Mkoo, kwa sababu hali Taifa letu sasa katika masuala ya umeme inatishia uchumi, ajira na sasa inaelekeea kutishia usalama wa Taifa letu.

Serikali unayoiongoza hapa Bungeni, imetoa matamko kadha wa kadha kwa muda mrefu sasa, ikiwataka Watanzania wawe na subira na tatizo la umeme litatatuliwa. Na kwa sababu Tatizo la umeme halionekani kuwa na ufumbuzi wa muda mfupi ujao.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri Mkoo, wewe binafsi kama Waziri Mkoo na kama Kiongozi wa Serikali hapa Bungeni, unatumia fursa hii kulieleza nini Taifa? Kuhusiana na hili tatizo kubwa la umeme ambalo kumekuwa na vilio vya mara kwa mara kwamba Wahusika wajiu zulu ili kuwajibishana katika utendaji kazi, lakini Serikali imekuwa kimya kuhusu suala hili? Mheshimiwa Waziri Mkoo, tunaomba kauli yako binafsi na kauli rasmi ya Serikali yako. (*Makofî*)

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Spika, naomba kwa heshima nimjibu Mheshimiwa Mbewe, au nitoe maelezo labda kwa Mheshimiwa Mbewe, kuhusiana na jambo hili.

Mheshimiwa Spika, kwanza nataka nikubaliane na yeye kwamba suala la umeme ni tatizo kubwa hapa nchini. Na hilo, sisi Serikalini tunalijua na kwa sababu Watanzania wengi sana wanaathirika sana na jambo hili ni kweli kabisa kwamba hawajaridhika sana na hatua ambazo tunaendelea kuzichukua.

Lakini kama Serikali na baada ya kutambua ukubwa wa tatizo hili, ndio maana unaona sasa mwelekeo wa utekelezaji wa mpango wa namna ya kuweza kukabiliana na jambo hili, ni ule wa kuondokana na kutegemea mno chanzo cha maji ambacho kwa miaka mingi kimekuwa ndio msingi wa upatikanaji wa umeme.

Mheshimiwa Spika, sasa katika mazingira tuliyonayo maji sasa sio *source* nzuri sana ambayo inaweza ikatupa uhakika wa umeme. Kwa hiyo, sasa tunajikita katika maeneo mengine kama vile mkaa wa mawe, tunajikita katika masuala mazima ya gesi, lakini hata kwa kutumia upopo tumeona ni jambo jingine ambalo tutalitumia ili tuweze kutatua tatizo hili kwa muda mrefu.

Sasa ni kweli kabisa kwamba kwa maana ya hatua za leo au kwa maana ya kupata umeme kwa asilimia zote leo, hilo ndilo jambo ambalo sasa unaona Serikali tumelivalia

njuga kwa kuchukua hatua mbalimbali ikiwa ni pamoja na uagizaji wa baadhi ya jenereta ambazo tunategemea ndani ya miezi minne, mitano, sita, zitakuwa zimeshafika, zitatupunguzia tatizo hili la ukataji au mgao wa umeme kwa kiasi kikubwa sana. Lakini mimi na wewe na Watanzania wote, suala si hili hasa kwamba leo mnatupa hiyo fursa, tunataka tuwe na uhakika kwamba kwa muda mrefu jambo hili sasa litapatiwa ufumbuzi amba ni wa kudumu.

Mheshimiwa Spika, na mimi nina hakika kwa hatua ambazo Waziri atapata nafasi ya kueleza kesho, kwa maana ya *long term programs* nadhani tumejipanga vizuri. Nataka niwahakikishie Watanzania kwamba Serikali iko makini, tutajitahidi kwa kadiri inavyowezekana kuhakikisha kwamba tatizo hili linapatiwa ufumbuzi wa kudumu?

MHE. FREEMAN A. MBOWE: Mheshimiwa Spika, namshukuru Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa majibu yake. Lakini tatizo la umeme sio la leo na kauli anayoizungumza Mheshimiwa Waziri Mkuu, ni kauli imeshawahi kuzungumzwa na Mheshimiwa Rais, mara kadhaa na kuwahakikishia Watanzania kwamba tatizo la umeme litatatuliwa. Ni kauli ambazo zinatolewa na Serikali kwa zaidi ya miaka minne mfululizo kwamba, Watanzania wavute subira. Na kwa maana hiyo imani ya Watanzania kuhusu uwezo wa Serikali hii kutatua tatizo hili, umekwisha. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, na sisi wengine kama Viongozi wa vyama vyva siasa tunafanya kazi kubwa sana Mheshimiwa Waziri Mkuu, kuwazuia wananchi wasiandamane kulilia maisha yao, kwa sababu umeme ni maisha yao. Sasa, Mheshimiwa Waziri Mkuu, maadam Serikali yako vilevile, imekiri na imetangaza kwamba umeme ni janga la Taifa. Jambo lolote linapotangazwa janga, linawekewa utaratibu maalum wa kijanga. Huwezi ukatangaza janga na watu walewale wakaendelea kufanya kazi kwa mtindo uleule ukasema hilo ni janga. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, sasa Mheshimiwa Waziri Mkuu, huoni ni muda muafaka wa Serikali kuunda Tume Maalum, ambayo inaweza ikatoa ushauri na msaada wa karibu kwa Serikali yako. Ikihusisha wadau mbalimbali wa masuala ya umeme ndani ya Serikali na ndani ya *Private Sector* na hata katika Mashirika ya Umma? Kutafuta namna ya kupata ufumbuzi wa pamoja wa Taifa, kutatua janga hili la Kitaifa?

Mkheshimiwa Spika, kuliko kuendelea kuamini kauli zilezile za watu walewale wa siku zilezile, wakiendelea kutupa kauli hapa ndani ya Bunge? (*Makofi*)

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Spika, namwelewa Mbewe, anachosema ni nini na Serikali nzima tunaelewa sana. Lakini mimi nataka nikuambie Mheshimiwa Mbewe, hatuhitaji Tume, jambo hili linaeleweka, tatizo linaeleweka. Kubwa ni kuona dhamira ya Serikali katika kujaribu kumaliza tatizo hili. Ndio maana mimi ninasema kwa hatua ambazo Serikali imeshajipanga kwa sasa, tatizo hili tutalishughulikia na litakwisha. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante. Waheshimiwa Wabunge, mtakapopata nafasi naomba msihutubie wenzenu, kwa sababu muda hautoshi. Sasa nitamwita Mchungaji Peter Simon Msigwa.

MHE. MCH. PETER S. MSIGWA: Mheshimiwa Spika, nikushukuru sana. Mheshimiwa Waziri Mkuu, swali langu.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Mheshimiwa Samuel Sitta, alipokuwa Spika la Bunge wa tisa, alipangishiwa nyumba na Serikali, iliyoko eneo la Masaki. Na nyumba hii Serikali, imekuwa inakadiriwa inalipa shilingi milioni 12 kwa mwezi. Na kwa kuwa, hivi karibuni Mheshimiwa Sitta, alisafiri kwenda India yeye pamoja na mwanzo wake na msaidizi wake kwa daraja la kwanza. Na kwa kuwa, nyumba ile aliyokuwa amepangishiwa ilikuwa ni kwa hadhi yake ya Uspika. Na kwa kuwa, Mheshimiwa Sitta, sio Spika ni Waziri wa Afrika Mashariki, Wizara ambayo ni ndogo.

Je, ni lini Serikali itamwamuru Mheshimiwa Sitta, aondoke kwenye hiyo nyumba ya Serikali, akajunga na Mawaziri wenzake kule Kijitonyama na wakati huohuo ikimzuwia asisafiri yeye pamoja na msaidizi wake kwa kutumia daraja la kwanza ili kuipunguzia gharama Serikali, zisizo na lazima? (*Makofi*)

SPIKA: Yaleyale, mnasema siku zote kwamba mimi ninaingilia! Maswali mengine, Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Msekwa, ni ma-Spika Wastaifu. Na wanahudumiwa na Bunge hili, wala Waziri Mkuu hawahudumii; sasa mtanipeleka kwenye Kamati za Kanuni ngapi sasa? Huyu ni Spika Mstaifu, Msekwa, na matibabu yote tutayagharamia sisi na watu wengine watagharamiwa na sisi. Kwa sababu, katika masharti ya Spika, hilo ni mojawapo ya sharti lake. (*Makofi*)

Huwezi kunipiga mimi swali la nyongeza Mheshimiwa.

MHE. MCH. PETER S. MSIGWA: Mheshimiwa Spika, samahani!

SPIKA: Mimi hunipigi swali la nyongeza, naomba ukae. Mheshimiwa Regia Estelatus Mtema.

MHE. REGIA E. MTEMA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa, Wabunge wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tumekuwa tukipewa fedha za mafuta pamoja na posho za siku 10 kila mwezi kwa ajili ya kwenda kuwatumikia wananchi kwa maeneo ambayo tunayawakilisha. Na kwa kuwa. Fedha hizi ni za walipa kodi wa Tanzania. Na kwa kuwa, mpaka sasa hakuna chombo ambacho kina-*monitor* matumizi sahihi ya fedha hizi. Na kwa kuwa, Watanzania wengi wanalamika kwamba baadhi ya Wabunge, wanaishi nje ya maeneo wanayoyawakilisha na hawaendi kwenye Majimbo yao.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri Mkuu, hautakubaliana nami kwamba umefika wakati sasa Serikali ya Tanzania iandae *performance appraisal* kwa ajili ya Wabunge, ili kuongeza uwajibikaji na matumizi sahihi ya fedha hizi?

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Spika, naomba nimjibu Mheshimiwa Regia Mtema, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Wabunge, tunatokana na vyama vyaa siasa fulani fulani. Wengine tunatoka *CUF*, wengine *CHADEMA*, wengine *CCM* na kadhalika.

Serikali ilichofanya ni kuweka utaratibu utakaomwezesha Mbunge huyo kutekeleza majukumu yake vizuri. Sasa kama wewe Mheshimiwa, pamoja na uamuzi mzuri huo wa Serikali, wewe hutimizi wajibu wako! Ni jukumu la chama chako na wewe mwenyewe na wapiga kura kukuwajibisha kwa kutotimiza wajibu. Kilichofanyika ndani ya Serikali ni kumwezesha huyu Mbunge, ili aweze kutekeleza majukumu aliyopewa na Taifa. (*Makofi*)

SPIKA: Mheshimiwa Regia, una swalii lingine?

MHE. REGIA E. MTEMA: Mheshimiwa Spika, ninalo kwa kuwa, sijaridhika na majibu ya Mheshimiwa Waziri Mkuu.

SPIKA: Hayo ndiyo majibu *internationally* lakini! (*Makofi/Kicheko*)

MHE. REGIA E. MTEMA: Mheshimiwa Spika, *okay!*

Mheshimiwa Spika, fedha hizi, zinatolewa na Serikali na ninatambua kwamba hata ruzuku kwenye vyama vyaa siasa zinakaguliwa na *CAG*, haviachiwi vyama vyaa siasa vijiendeshe vyenyewe.

Kwa hiyo, pamoja na hayo ni lazima pia Wabunge, Serikali iunde *Performance Appraisal* kwa ajili ya kuwa-*monitor* na sio kuachia vyama vyaa siasa. (*Makofi*)

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Spika, mimi naamini Wabunge wote ni watu wazima, wenyewe hekima, wenyewe busara; na sipendi kuamini kwamba wako Wabunge hapa, *irresponsible* kiasi hicho. Sasa kama wapo na viongozi wa vyama wa Wabunge hao wapo! Ndio maana nimesema ni jukumu la chama kuadhibiti, maana wao wameingia pale kwa kofia ya chama husika.

Sasa, usituingize katika gharama za kuunda chombo, kwenda kufuatilia mafuta ya Mbunge, aah, *we can't do that! Everybody is responsible* kiasi chakutosha. (*Makofi*)

MHE. MWANAMRISHO TARATIBU ABAMA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kumwuliza swalii Mheshimiwa Waziri Mkuu. Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa kuwa mmoja kati ya Waasisi wa Muungano, Mheshimiwa Marehemu Mzee Abeid Amani Karume, alisema, naomba kunukuu, alisema “*Muungano wetu kama koti na likikubana unaweza kulivua.*” Mwisho wa kunukuu.

Mheshimiwa Spika, na kwa kuwa, Muungano wetu una kero na malalmiko kutoka kwa pande zote mbili. Je, Mheshimiwa Waziri Mkuu, utakubaliana na mimi kwamba ule wakati ambao aliutabiri Mheshimiwa Karume, kwamba koti likikubana unalivua, ndio huu sasa umefika? Je, Serikali ya Chama cha Mapinduzi ya Zanzibar, ikifikia hatua hiyo,

Je, Serikali ya Jamhuri ya Muungano itakubali kutia Baraka zake ili nayo iweze kujiondoa katika muungano huu?

SPIKA: Mheshimiwa Waziri Mkuu, majibu. Burundi na Rwanda, wanataka Muungano! Leo ninyi mnataka nini! Haya, Mheshimiwa Waziri Mkuu.

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Spika, naomba nitoe maelezo mafupi sana kwa Mheshimiwa Mwanamrisho Abama, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Tanzania na Zanzibar, ni kweli ni nchi ambazo zimeungana. Yako matatizo ya hapa na pale katika Muungano huo. Na miungano mingine mingi Duniani nayo inafanana na sisi kwa matatizo mbalimbali. Kikubwa ni kuendelea kuzungumza hayo matatizo kwa lengo la kuimarisha Muungano siku hadi siku. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, na mimi ninataka niseme kwamba suala la Muungano hili, tusilione kama jepesi! Maana wakati mwagine naona tunazungumza kama tunakuwa na jazba hivi, lakini ni jambo linalotakiwa litazamwe kwa umakini mkubwa sana. (*Makofi*)

Muungano wetu umetujengea heshima kubwa sana kama taifa, Muungano huu umetuunganisha vizuri sana kati ya pande hizi kuna historia zinafanana, tuna watu wanaofanana, ni jambo jema. Yako manufaa mengi tu kutokana na Muungano huu.

Mimi napata faraja sana ninapoona Wazanzibari wako huku wamewekeza wamejenga majumba makubwa hawana wasiwasi wanaishi kwa raha tu.

Kwa hiyo ni kitu ambacho lazima kwa kweli tuchelee kukibeza ila kama yako mambo ni vizuri tuendelee kuyazungumza kwa lengo la kuimarisha jambo hili. (*Makofi*)

MHE. MWANAMRISHO TARATIBU ABAMA: Mheshimiwa Spika, ahsante pamoa na majibu ya Mheshimiwa Waziri lakini ningependa kumwuliza swali lingine la nyongeza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Waziri Mkuu huoni sasa wakati umefika kwamba Watanzania wa pande zote mbili kupewa fursa ya kupiga kura za maoni juu ya Muungano wao?

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Spika, sijui kama maana yake nini unaposema wakati umefika, mimi nachosema dada yangu ni kwamba bahati nzuri tuko katika hatua nzuri sana sasa, tunazungumza juu ya Katiba mpya. Fikra hiyo ya kwako kama ndiyo

fikra za waliyowengi, ni vizuri likatazamwa katika mfumo wa jitihada za kujaribu kuangalia Katiba Mpya hivi leo. Mimi rai yangu kwa Watanzania wote ni kuendelea kuwa waangalifu katika kutangaza suala la Muungano wa nchi hizi mbili.

Watanzania tuko milioni 44 na zaidi, Zanzibar milioni 1 na kitu, Muungano wowote ambao utajaribu kuziweka nchi hizi mbili katika mazingira ya kufanana, huo Muungano utakuwa mgumu sana kuutekeleza. Ndiyo maana pamoja na matatizo yaliyomo katika mfumo huu wa Muungano ambao mimi naamini ni mzuri sana, ni bora kuzungumza namna ya kumaliza hizo kero lakini mkaendelea kuwa na Muungano ambao unatambua na kuheshimu uwepo wa nchi ya Zanzibar hata kama ina watu wachache na udogo wake. (*Makofi*)

Kuja kuweka mfumo hapa wa Serikali ya Muungano ambayo inatambua nchi moja inatwa Tanganyika, nyingine Zanzibar, nyingine mnaita shirikisho tujaribu lakini matokeo yake mimi naamini hayatakuwa mazuri. Ndiyo maana nasema suala la kupiga kura kuwepo au kutokuwepo kwangu si hoja, Katiba inakuja wacha jambo hili lizungumzwe, tujisikie huru tuchangie itakavyoona inafaa. (*Makofi*)

MHE. AMINA MOHAMED MWIDAU: Mheshimiwa Spika, ahsante, kwa kunipa nafasi nami niweze kumwuliza Mheshimiwa Waziri Mkuu. Kwa kuwa sera za mahusiano ya kimataifa zimebadilika kutoka kuwa za kisiasa, kuelekea katika za kiuchumi na kibiashara zaidi mionganoni mwa mataifa na taasisi za kimataifa.

Je, ni kwa kiasi gani Serikali imejiandaa kuzifanya sera za Mashirikiano yetu kwenda sambamba na mabadiliko hayo?

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Spika, sina hakika kama nimemwelewa vizuri sana Mheshimiwa Amina Mwidau, lakini siasa na uchumi huwezi ukavitenganisha vyote vinakwenda pamoja kwa sababu uchumi utatanguliwa mara zote na siasa za namna moja au nyingine.

Lakini kwa upande wa Tanzania kwa maana ya mahusiano yake labda na nchi za nje na namna tulivyojipanga katika kujaribu kutumia fursa zilizopo nje kiuchumi ndiyo jitihada zote ambazo leo unaona tunazijenga, kuimarisha ushirikiano huo, lakini kubwa ni kuona fursa zilizoko katika nchi hizo na namna zinavyoweza kunufaisha taifa letu na sisi tuweze kukua na kuwa kama taifa jingine kubwa kiuchumi.

Kwa hiyo kama nimekuelewa vizuri, ninachowea kusema kwa kifupu ni kwamba tunajitahidi sana kujaribu kwenda na wakati.

SPIKA: Eeh! Mnataka kujielimisha zaidi.

MHE. AMINA MOHAMED MWIDAU: Mheshimiwa Spika, ahsante, nashukuru Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa majibu yako ni na swali moja la nyongeza. Kwa kuwa tumeshuhudia mionganoni mwa wafanyabiashara wengi wanaokuja kufanya biashara nchini mwetu ni *pet traders*, kama machinga wa Kichina ambao wako

Kariakoo. Wakati wenzetu kwa mfano kama China, unapotaka kwenda kufanya biashara nchini mwao ni lazima uweke benki dola 150,000 kwa mwaka mzima bila kuzigusa.

Je, Serikali haioni kuwa huu ni wakati muafaka kuleta Muswada Bungeni ambao utakaoweka masharti yatakayosaidia kuleta wafanyabiashara ambao siyo wababaishaji? (*Makofi*)

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Spika, mimi nafikiri swalí limechanganya mambo mawili, matatu kwa pamoja, ulikuwa unazungumza wafanyabiashara wadogo wadogo umewaita machinga wa kichina.

Sasa unataka Serikali ilete Muswada hapa lakini ambao unaondoa uwezekano wa wafanyabiashara wababaishaji, sasa haya ni mambo mawili kidogo tofauti. Ninachowea kukubaliana na wewe ni kwamba Serikali kwa hatua ambazo imeshaanza kuchukua tayari ni vizuri tukawa na mfumo unaotenganisha ni shughuli zípi mtu wa nje afanye anapokuwa hapa nchini kwetu, na zípi kwa kweli asiruhusiwe kufanya. Na hiyo ndiyo kazi moja ambayo sasa tunaifanya kwa ajili ya kutenganisha jambo hilo. (*Makofi*)

Pili, wafanyabiashara wanaokuja kufanya kazi hapa nchini kwetu, wanaokuja kufanya biashara na sisi, kwa sehemu kubwa huihitaji kuwa na kitu maalum kama hicho unachopendekeza, ni suala la taifa kama taifa sisi wenyewe kuwa makini na kuwa macho na wafanyabiashara wababishaji ambao hawana kitu *productive* kwa ajili ya manufaa ya taifa letu. Na hili naweza likasimamiwa likadhibitiwa kila mmoja katika nafasi yake. Maana wanapokuja hapa wana watu wao, hawaji tu hapa kuja kufanya hewani hapana, wanakuja kufanya biashara na Watanzania.

Kwa hiyo ni vizuri kila Mtanzania akawa macho ili asije akaingizwa mkenge, kwa kufanya biashara na mtu ambaye haaminiki, hana uwezo na hajui atapata nini mwisho wa safari.

SPIKA: Sasa nimwite Mheshimiwa Godbless Lema, tumekumiss sana Mheshimiwa Lema. (*Kicheko*)

MHE. GODBLESS J. LEMA: Mheshimiwa Spika, hata mimi nimekumiss. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, ninaomba kumwuliza Waziri Mkuu swalí lifuatalo; kwa vile Serikali inafanya jitihada nyingi kuongeza vyuo vikuu mbalimbali na hivi karibuni tumepokea ripoti kwamba vyuo vyetu vinatoa wanafunzi wengi kila mwaka ambao ni wataalam wa fani mbalimbali. (*Makofi*)

Katika soko la ajira, hasa katika mahoteli na makampuni mbalimbali unakuta kwamba ajira ambazo wangeweza kufanya Watanzania wenye utaaliam unaofanana, ajira hizo unakuta zinafanywa na watu kutoka mataifa mbalimbali.

Kwa mfano hasa katika mahoteli ya kitalii, especially katika jimbo langu unakuta kwamba kuna mtu ametoka hata India anakuja kufanya kazi ya kufuta vioo wakati kuna Watanzania wamesomea mambo kama hayo. Ni nini mkakati wa Serikali sasa wa kuweza kudhibiti uhaifu mkubwa kama huo katika ajira za Watanzania na kuweza kufanya watu wetu wakapata ajira nyingi?

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Spika, naomba kumjibu rafiki yangu Mheshimiwa Godbless Lema kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ajira za wageni zinatawaliwa na sheria na taratibu maalum, kutegemea na aina ya kazi ambayo huyu aliyeju ka kuwekeza hapa au anashughuli hapa anahitaji utaalalm wa namna fulani. Na hii zaidi ni kwa yale maeneo ambayo kazi zake ni zile za uwekezaji mkubwa.

Kwa kawaida idadi ya watumishi wa aina wanaohitajika huwa haizidi tano katika fani zile ambazo ndani hapa inaonekana hatujabobe a kwenye maeneo hayo.

Kama nilivyojibu swali la mara ya mwisho wakati namjibu Mheshimiwa Mbunge mwingine, kwa kazi kwa kweli nyingine zote jukumu letu ni kuhakikisha kwamba kazi zile ambazo Watanzania tunaweza ziachwe kwa ajili ya Watanzania. Kwa hiyo, Wizara ya Kazi, ndiyo kazi ambayo sasa tumesema waifanye kwa bidii ili waweze kuhakikisha kwamba si kila mtu anaweza akaleta mtu yoyote kwa ajili ya kufanya kazi hapa nchini. (*Makofii*)

Mheshimiwa Lema, kwa upande mwingine nataka niombe sana Watanzania mimi nazunguka sana, hata kwenye hoteli hizi nazunguka sana.

Watanzania lazima sasa tuwe watu tunaopenda kufanya kazi. Kwa sababu moja ya jambo ambalo nimepambana nalo nilipokwenda katika moja ya hoteli kule Ngorongoro, nilizungumza na Wakenya wale ambao wanasingimia hoteli pale. Wanasema tatizo lenu ninyi Watanzania sijui kwa sababu mko huku, mnavingizio vingi mno vya kutokuwepo kazini *on a day, today basis*.

Sasa hii inawaumiza, leo dada anaumwa, kesho umefiwa, kesho kutwa una mtoto sijui anaharisha na kadhalika. Hakuna mtu ambaye amewekeza hapa atakubali kupoteza muda wake kiasi hicho. Ndiyo maana wakati mwingine wanazimika kutafuta watu wa nje, maana anajua yule hana kisingizio, anakuja hapa anajua kazi ni kazi hakuna visingizio.

Kwa hiyo lazima na sisi tubadilike tuwe ni watu wa kupenda kazi, tuchape kazi, tuache kutumia muda wetu kwa mambo ambayo hayana tija, hiyo itatusaidia sana kujenga *credibility* ya nchi yetu. (*Makofii*)

MHE. RAJAB MBAROUK MOHAMED: Mheshimiwa Spika, ahsante, kwa mujibu wa tafiti za kitaalam inaonyesha kwamba Watanzania asilimia 33.4 wanaishi chini ya mstari wa umaskini. Vilevile asilimia 35 ya wananchi wa Tanzania wako katika tofauti ya vipato baina ya aliyenacho na yule ambaye hana kitu.

Serikali katika Bajeti yake ilitangaza kwamba bei ya mafuta itapungua, lakini hali sivyo ilivyo. Bei ya mafuta inazidi kupanda kila kukicha katika nchi hii, kupanda kwa bei ya mafuta kunazidisha umaskini katika nchi hii.

Mheshimiwa Waziri Mkuu naomba kuititia kwako utoe tamko rasmi la Serikali juu ya upandaji holela wa mafuta?

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Spika, naomba nitoe maelezo kwa ndugu yangu Mheshimiwa Rajab Mbarouk Mohamed, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali ilipotamka juu ya bei za mafuta ni kweli tulijua haziwezi kuteremka siku moja, kwa sababu tulijua yako mafuta tayari yatakuwa yameshaingizwa nchini na yanaendelea kutumika na uko utaratibu wake wa namna ya kufuatili kuona kila *consignment* inapoingia ndani ya muda gani, *consignment* ile itakuwa imefika kabla hamjaanza kuingiza mafuta mengine. Kwa kawaada ni siku 15, 30 mpaka 45 *consignment* moja inakuwa imekwisha.

Kwa hiyo na mimi nimelipata hilo kama ulivyolipata wewe, na mara nyingi inatokana tokana na hali ya wafanyabiashara kutaka kujinufaisha katika mazingira haya mapya. Kwa hiyo nimewaomba watu wa *EWURA* na nimemuagiza Waziri anayehusika pamoja na *TRA* wajaribu kufuatilia mafuta yote kwa ujumla tu, pamoja na mafuta ya taa tuone *consignment* zote ambazo zilikuwa zimeshaagizwa kabla ya tangazo lile la Serikali ili tuone tarehe ile ambayo wanassema kwa vyovyyote vile lazima *consignment* hizo zitakuwa zimekwisha, tuone kitakachojitokeza ni nini.

Ninataka niendelee kuomba Watanzania kwamba tatizo hili tunalipata sana kwa sababu wafanyabiashara wengine siyo waaminifu sana. Lakini tunajaribu tutalisimamia na tutaona wakati ule tunaweza pengine tukawa katika nafasi nzuri zaidi ya kutoa tamko ambalo linaweza likasaidia kuliko sasa, kwa sababu jambo hili nimeliulizia ni juzi tu baada ya kurudi, baada ya kuona hali bado ndiyo nikaelimishwa hivyo na mimi nikasema basi tungoje tuone matokeo yake. (*Makofifi*)

NAIBU SPIKA: Ahsante nimefanikiwa kuchukua dadika tano za hao Mawaziri wanapowasilisha hati zao mezani. Mheshimiwa Waziri naomba nikushukuru ahsante. (*Makofifi*)

Waheshimiwa Wabunge napenda pia niwapongeza kwa namna mlivyouliza maswali, ni kipindi cha Waziri Mkuu dakika 30 inatakiwa *live, short and brief* kusudi watu wote wawefeze kupata nafasi. Nimeshindwa kuwapa nafasi wawili tu, lakini wengine walikuwa nane, sita wamefanikiwa. Kwa hiyo Waheshimiwa Wabunge tuendelee kuwa na nidhamu wakati tunauliza maswali kwa furaha wote tunapata elimu wote na nchi

nzima inapata elimu. Mimi nawashukuru sana na nyinyi pia kwa kuuliza maswali vizuri. Tunaendelea, Katibu tuendelee na *Order Paper*.

MASWALI NA MAJIBU

Na. 233

Mashambulizi Dhidi ya Libya

MHE. HAROUB MOHAMMED SHAMIS aliuliza:-

Nchi yetu kupitia Serikali ya awamu ya nne imekuwa kinara wa usuluhishi wa migogoro mingi Barani Afrika:-

- (a) Je, Serikali ina msimamo gani juu ya mashambulizi yanayofanywa na nchi za Magharibi dhidi ya Libya?
- (b) Je, ni nini tathmini ya Serikali kwa Libya kushambuliwa kijeshi na Mataifa ya kigeni?

WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Haroub Mohammed Shamis, Mbunge wa Chonga, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, msimamo wa Serikali ya Jamhuri ya Muungani wa Tanzania ni kwamba haiungi mkono mashambulizi ya kijeshi yanayofanywa na nchi za Magharibi dhidi ya Libya. Msimamo huu unatokana na ukweli kuwa mashambulizi yanayofanywa na nchi za Magharibi dhidi ya Libya hayaafuati Azimio (1973) la Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa lililopitishwa kwa ajili ya kuwalinda raia wa nchi hiyo kutokana na mapigano kati ya majeshi ya Serikali na waasi.

(b) Mheshimiwa Spika, tathmini ya Serikali kuhusu mashambulizi ya nchi za Magharibi dhidi ya Libya ni kwamba mashambulizi hayo hayalengi kuwalinda raia wa Libya kama ilivyoidhinishwa na Baraza la Usalama bali yanalenga kuing'oa madarakani Serikali ya Libya inayoongozwa na Mhe. Muammar Gaddafi.

Mheshimiwa Spika, Tanzania inaamini kuwa mgogoro wa Libya unahitaji usuluhishi wa kisiasa baina ya pande hasimu badala ya kutumia nguvu za kijeshi pekee. (*Makofî*)

MHE. HAROUB MOHAMED SHAMIS: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali ya nyongeza, nina mawili ya nyongeza, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri.

Je, ni kwanini Serikali kupitia Umoja wa Afrika *AU*, usiende katika *United Nations*, na msimamo wa pamoja kupinga mashambulizi dhidi ya Libya?

Je, Serikali ya Tanzania inajitayarishaje na hali kama iliyoikumba Libya ambapo inaonekana ni sera ya mataifa makubwa kuyavamia mataifa kidogo kijeshi na kupora rasilimali zao baadaye kuweka vibaraka wao?

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA: Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, naomba kumjibu Mheshimiwa Shamis, maswali yake ya nyongeza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kuhusu *AU* kuwa na msimamo wa pamoja, tayari msimamo huo upo na umewekwa na kutolewa mara kadhaa, na *AU*, msimamo wake ni kama Watanzania kwamba suluhisho la mgogoro huu lazima liwe la kisiasa, na kwamba pande hasimu sasa lazima zikae kupata suluhu ya mgogoro huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la (b) sikulisikia vizuri.

SPIKA: Swali la pili hukumwelewa vizuri *okay*.

MHE. HAROUB MOHAMED SHAMIS: Mheshimiwa Spika, kwa ruhusa yako naomba nimweleze swali la pili, nasema Serikali yetu ya Tanzania imejitayarishaje, kuepukana na hali kama iliyoikumba Libya, ambapo inaonekana mataifa makubwa ni sera yao kuvamia nchi ndogo kijeshi, kuweka vibaraka wao na kupora rasilimali za nchi hizo?

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA: Mheshimiwa Spika, Tanzania katika sera yake ya mambo ya nchi za nje, inaungana na wale wote ambao wanaonewa na inaunga mkono juhudzi za watu kupigania uhuru wao, kupigania maslahi yao.

Tuweke wazi kwamba katika dunia ya leo ni nchi chache ambazo zinaweza zikasimama kijeshi kupigana na au kupingana na hayo mataifa makubwa.

Kwa hiyo bado tutaendelea kuungana mkono na nchi mbalimbali kupitia taratibu zilizopo za kimataifa ikiwemo *AU* na Umoja wa Mataifa katika maazimio ambayo yanaweza kupitishwa katika majukumu hayo.

MHE. ZUBERI K. ZITTO: Mheshimiwa Spika, imekuwa ni kawaida ya mataifa mabeberu kuvamia nchi ndogo za kiafrika kwa ajili ya rasilimali, na sisi ndani ya miaka mitatu ijayo tutakwenda kuwa nchi ambayo ina mafuta na gesi na tunaweza kabisa

tukaangukia katika hali ambayo inaikuta Libya leo. Kwa nini, Serikali yetu *hai-suspend diplomatic relations* na mataifa yote ambayo yanawapiga na kuwaua raia wa Libya?

NAIBU WAZIRI WA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA:
Mheshimiwa Spika, naomba kumjibu Mheshimiwa Zitto kama ifuatavyo:-

Hivi sasa mwelekeo wetu zaidi ni *engagement* na wale wote ambao mitizamo yetu inatofautiana kuliko kuwatenga. Kwa hiyo, njia rahisi zaidi ni kuendelea kushirikiana na kujadilikanu katika kutafuta suluhisho la matatizo mabalimbali na siyo kuwatenga wale ambao mitizamo ambayo iko tofauti. (*Makofi*)

Na. 234

Utekelezaji wa Mpango wa Kilimo Kwanza

MHE. RITA L. MLAKI (K.n.y. MHE. ZARINA S. MADABIDA) aliuliza:-

Asilimia 75 ya Watanzania ni wakulima wadogo wadogo wenye kilimo duni kwa mazao ya kilimo, ufugaji na uvuvi na sera ya Kilimo Kwanza imelenga kuboresha kilimo, ufugaji na samaki:-

Je, serikali ina mpango gani wa kuwashirikisha wakulima wadogo katika Mpango wa Kilimo Kwanza ili waweze kuwa na kilimo chenye tija katika kuinua kipato chao na cha Taifa.

WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Zarina S. Madabida, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, azma ya Kilimo Kwanza inatekelezwa kupitia Programu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo (*Agricultural Sector Development Program – ASDP*). Programu hiyo inatekelezwa katika ngazi ya Wilaya kupitia Mipango ya Maendeleo ya Kilimo ya Wilaya husika (*District Agricultural Development Plans – DADPS*).

Mipango hiyo hujumuisha miradi inayoibuliwa na wananchi kwa kutumia mbini shirikishi ya Fursa na Vikwazo kwa Maendeleo (*Opportunities and Obstacles to Development - O & OD*). Baada ya wananchi kuibua miradi, miradi hiyo huingizwa katika Mpango wa Maendeleo ya Kilimo wa Kijiji (*Village Agricultural Development Plans – VADPs*) ambayo hupitishwa na Mkutano Mkuu wa Kijiji na kuunganishwa na miradi mingine katika ngazi ya Kata na hatimaye kuingizwa katika DADPs kwa ajili ya utekelezaji.

Mheshimiwa Spika, miradi inayoibuliwa kwa utaratibu huo huwezeshwa kupitia ruzuku za DADPs zinazotolewa na Serikali ambazo ni pamoja na ruzuku za kujenga uwezo, huduma za ugani na uwekezaji.

Miradi inayoweza kunufaika na ruzuku hizo ni pamoja na ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji, majosho, malambo, barabara za vijijini, ufugaji bora wa mbuzi na kuku, ununuzi wa zana za kilimo kama vile matrekta madogo ya mkono, mashine za kusindika mazao, ujenzi wa masoko na maghala.

MHE. RITA L. MLAKI: Mheshimiwa Spika, kwanza nashukuru sana kwa majibu ya Mheshimiwa Waziri. Kwa kuwa, wakulima wadogowadogo wanapolima mazao wakati mwagine wanashindwa kusindika na yanaozea mashambani. Je, Serikali haioni umuhimu wa kuwasaidia wakulima hawa kuwajengea viwanda kama inavyosema Sera na kuwakabishi wakulima hawa na kuwatafutia masoko ili waweze kufaidi kilimo chao?

Serikali vile vile haioni umuhimu wa kuanzisha maghala kama inavyofanya katika zao la Korosho na ifanyike kwa mazao yote ambapo wakulima watakuwa wanapeleka mazao ya ziada ili waweze kuuza na Serikali iwaweke katika ghala la taifa na hiyo imesababisha katika Mkoa wa Kilimanjaro kutoroshwa kuperekwa Kenya kwa sababu wanakua hawana kwa kuyapeleka?

WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKIA: Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi ya kujibu swali la nyongeza la Mheshimira Rita L. Mlaki, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, mkulima mdogo mmoja mmoja hana uwezo wa kujenga viwanda lakini Serikali inafanya juhudini kubwa kuwashamasisha wakulima wajunge katika vyama vya Ushirika na vyama vya Ushirika vya kuweka na kukopa pamoja na vikundi vya wakulima ambavyo kuititia mikopo ya aina mbalimbali inayotolewa na Serikali vinaweza kuanzisha miradi midogo ya usindikajiwa vyakula na mazao mengine.

Serikali itaendelea kufanya hili ili kuwawezesha wakulima waweze kuongeza nguvu yao ya usindikaji. Aidha, nakubaliana na Mheshimiwa Rita Mlaki kwamba ni muhimu sasa tujiandae katika kufanya biashara ya mazao ya aina mbalimbali na hususani mazao ya chakula kwa kujenga maghala katika maeneo ambayo wakulima wameonyesha uzalishaji mkubwa wa chakula hasa katika mikoa kama Iringa, Mbeya, Ruvuma na Rukwa ili kuhakikisha kwamba wakulima walio na ziada wanapeleka mazao yao katika maghala hayo na mazao hayo yanauzwa kwa utaratibu wa stakabadhi ghalani. (*Makofi*)

Utaratibu huu ukiwekwa pia katika mikoa ambayo ina masoko makubwa ya mpakani itawezesha hatimaye kutuwezesha kuwa na *Commodity Exchange* ambayo itawasaidia sana wakulima katika kuuza mazao yao. (*Makofi*)

MHE. FREEMAN A. MBOWE – KIONGOZI WA KAMBI YA UPINZANI BUNGENI: Mheshimiwa Spika, kwa sababu kwa muda mrefu tatizo la kuuza nafaka

nchi za nje limekuwa linakabili taifa letu na imekuwa ni vigumu sana kudhibiti kutokana na ushawishi wa bei.

Je, Serikali haioni sasa ni muda muafaka kupiga marufuku kabisa uuzaji wa nafaka hasa Mahindi nje ya nchi lakini itoe ruhusu ya kuuza bidhaa za unga nje ya nchi kwa maana hiyo tuweze kuendeleza viwanda vyetu kwa kuweza ku- *add value* katika nafaka hii ya Mahindi?

WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKIA:- Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Freeman Mbowe kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba tuna tatizo la muda mrefu la kufanya biashara ya mazao na hasa nafaka na nchi za nje kwa sababu kwa muda mrefu biashara hii hufanywa na wafanyabiashara ambao wanakwenda mpaka shambani kwa mkulima kufanya majadiliano na kununua mazao wakati mwininge yakiwa shambani.

Mheshimiwa Spika, wiki iliyopita tulipiga marufuku kabisa uuzaji wa mazao ya chakula nje ya nchi kutokana na tatizo ambalo linajionyesha kwamba nchi yetu inaweza kuingia katika uhaba wa chakula. Hata hivyo, ninakubaliana na Mheshimiwa Mbewe kwamba katika kujitayarisha kuuza chakula nje ya nchi ni vizuri tuuze chakula ambacho kimeshasindikwa ili kuhakikisha kwamba tunapata biashara nzuri kutokana na jasho letu. (*Makofi*)

MHE. ALLY KEISSY MOHAMED: Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Nataka kumwuliza swali dogo Waziri wa Kilimo.

Tarehe 1 Julai, 2011 alipiga marufuku mazao kwenda nje naomba ahakikishie Bunge lako Tukufu na wananchi wa Mbeya, Iringa, Rukwa na Ruvuma kwamba atanunua mazao yote ya Mahindi na atangaze bei ili wakulima wafahamu maana yake mpaka sasa alivyotangaza tu Mahindi yameshaanza kushuka bei vijijini na mengine yameshaanza kuwaozea wananchi, inaonyesha hana huruma na wakulima.

Mkulima kama mkulima ni mazao yake binafsi ni kama vile mshahara wangu mimi nina haki ya kuutumia ninavyotaka na mkulima ni mazao yake asipigwe marufuku, aweze kuwasaidia wananchi wakauze Darfur na hata Somalia ili waweze kuokoka na hii adha ya kuwa wanyonge kila siku. (*Kicheko*)

WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKIA: Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, amri hii ya kuzuia chakula kisiende nje ni amri ya muda na imetolewa kwa muda wa miezi sita ili kuiwezesha Serikali kuangalia kwa undani na kuhakikisha kwamba taifa haliingii katika janga la njaa wakati tumezalisha chakula cha kutosha.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, Serikali imejiandaa kununua Mahindi kupitia kwenye shirika lake la *NFRA* Wakala wa Hifadhi ya Chakula ya Taifa na kupitia kwenye Bodi ya Nafaka na Mazao Mchanganyiko ili wakulima waendelee kupata soko kwa ajili ya mazao yao.

Mheshimiwa Spika, aidha, Serikali haizuii wananchi kununua Mahindi na kuyapeleka katika maeneo ambayo yana njaa kama mikoa ya Mwanza, Shinyanga, Singida na kadhalika.

Na. 235

Matatizo Yanayokabili Mashamba ya Mkonge

MHE. YUSUF ABDALAH NASSIR aliuliza:-

Maeneo ya mashamba ya Mkonge yamekumbwa na umaskini mkubwa uliokithiri licha ya kuwa na raslimali ardhi iliyo bora:-

(a) Je, ni lini Serikali itaingilia kati suala la mafao ya waliokuwa wafanyakazi wa Mkonge hasa shamba la Ngombezi?

(b) Je, ni lini Serikali itarejesha mashamba hayo chini ya umiliki wake, hasa baada ya kampuni ya *Katani Ltd.* kushindwa kuyahudumia ili kuyatoa kwa wananchi au kwa wawekezaji wengine wenyewe tija?

(c) Je, Serikali ina waahidi nini wananchi wa Korogwe waishio kwenye mashamba hayo katika kupunguza makali ya maisha zinazotokana na kutokuwepo kwa tija katika maeneo hayo?

WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Yusuf Abdallah Nassir, Mbunge wa Korogwe Mjini, kama ifutavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, shamba la Mkonge la Ngombezi ni moja kati ya mashamba matano yaliyokuwa yanamiliikiwa na kampuni ya *Katani Ltd.* kushindwa kuyaendesha. Mashamba mengine ni Hale, Magunga, Magoma na Mwelya.

Serikali kwa kushirikiana na Shirika Hodhi la Mali za Mashirika ya Umma yaani *Consolidated Holdings Corporation (CHC)* imekamilisha uchambuzi na uhakiki wa madeni ya wafanyakazi wastaafu wa iliyokuwa Mamlaka ya Mkonge Tanzania. Uchambuzi huo umeonesha kwamba wastaafu 10,701 wanadai jumla ya shilingi 2,187,873,955/= kama malipo ya mafao na nauli za kuwasafirisha wastaafu hao kwenda kwao. Uchambuzi huu umewasilishwa kwa Msajili wa Hazina kwa ajili ya malipo.

(b) Mheshimiwa Spika, baada ya mashamba kurudishwa Serikalini uliandaliwa utaratibu mpya wa kuyaendesa wa mashamba hayo. Chini ya utaratibu mpya, mkataba wa mauzo ya hisa kati ya Serikali, Bodi ya Mkonge Tanzania na Kampuni ya *Mkonge Group of Companies (MGC)* na *Katani Ltd.* Hati za mashamba zilikabidhiwa kwa Bodi ya Mkonge isipokuwa viwanda (korona) na maghala ya kuhifadhi Mkonge ambavyo viliachwa mikononi mwa *Katani Ltd.*

Hivi sasa, mashamba yote yanaendeshwa kwa mfumo wa kilimo cha mkataba kati ya *Katani Ltd.* na wakulima waadogo wa Mkonge chini ya skimu ya *Sisal Small Holders Out growers Scheme (SISO)* ambapo wakulima wameruhusiwa kumiliki hekta 1,900 ambapo kila mkulima anaweza kumiliki kati ya hekta 6 na 200.

(c) Mheshimiwa Spika, Serikali itapima mashamba yote ya wakulima mapema iwezekanavyo na kuwapatia hati miliki za mashamba ili waweze kuzitumia kwa kilimo na kujipatia mitaji na mikopo kutoka katika Taasisi za fedha ili kujenga uwezekano wa kuyaendeleza.

MHE. YUSUF ABDALAH NASSIR: Mheshimiwa Spika, ahsante. Pamoja na majibu ya matumaini ya Mheshimiwa Waziri nina maswali mawili ya nyongeza.

Kwa kuwa, ni kweli kwamba bei ya Mkonge sasa imepanda inakaribia dola 1000 kwa tani na kwa kuwa pia ni ukweli alithibitishia Bunge lako hili Tukufu kwamba *Katani Ltd.* walishindwa mashamba yale matano.

Je, Serikali haioni kwamba wakati umefika wa kuwanyang'anya hata zile Korona sasa na maghala pamoja na viwanda vilivyopo ili hatimye tuwape hawa *Out Growers?*

Kwa kuwa pia kumekuwa na unyonyaji mkubwa ambao wakulima wadogo wadogo wamekuwa wakiuzungumzia na hatimaye wengi kuzuia mkonge wao usivunwe.

Je, Serikali inawahakikishiaje wananchi kwa kuwalinda? (*Makofî*)

WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA: Mheshimiwa Spika, napenda kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Nassir, kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Wizara itafanya tathmini ya masuala haya ya kuwa na Korona pamoja na maghala pamoja na matatizo ambayo ameeleza Mheshimiwa Mbunge ili kuona ni kitu gani sahihi cha kufanya.

MHE. STEPHEN H. NGONYANI: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa majibu ya Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika, yaliyo mazuri.

Kwanza nataka nimshukuru Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kutusaidia kwa wakati chakula cha msaada sasa kimeanza kufika pamoja na kwamba hakitoshi, lakini ubarikiwe sana sana Mheshimikwa Waziri Mkuu.

Kwa kuwa, mashamba ya Mkonge ya Hale, Magoma, Magunga, pamoja na Mwelya yametelekezwa na *Katani Ltd.* na kwa kuwa, Mheshimiwa Rais alipokuja kwenye Jimbo langu aliahidi mashamba pori kufutiwa leseni zao.

Je, Serikali ina mpango gani wa kuyagawa mashamba yale kwa wakulima wadogo wadogo ili wananchi wangu wapate sehemu ya kulima mazao?

WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA: Mheshimiwa Spika, napenda kumjibu Mheshimiwa Stephen Hilary Ngonyani, swali lake la nyongeza, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inaendelea kuyaangalia mashamba haya na kuyapima upya ili kuyatayarisha kwa ajili ya kuwagawia wakulima ambao wanaweza kuyaendeleza kwa kuwa mashamba haya kama nilivyoeleza katika swalii la msingi yamekuwa hayatumiki na yamerudishwa Serikalini na kampuni ya *Katani Ltd. (Makofi)*

Na. 236

Mikopo ya Fedha za Zana za Kilimo kwa Wakulima

MHE. GODFREY W. ZAMBI aliuliza:-

(a) Je, ni kiasi gani cha fedha na matrekta kimekopeshwa kwa wakulima nchini hususan wale Wakulima wa Mbozi kwa Mwaka wa Fedha wa 2010/2011?

(b) Katika Bunge la Tisa Serikali iliahidi kuangalia upya masharti ya ukopeshaji ndani ya Benki ya *TIB* kwa wakulima; je, ahadi hiyo imefanyiwa kazi kwa kiasi gani?

WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA alijibu:-

Mheshimiwa Spika, ninapenda kujibu swalii la Mheshimiwa Godfrey Weston Zambi, Mbunge wa Mbozi Mashariki, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inatoa fursa kwa wakulima kupata mikopo yenye masharti na riba nafuu kupitia Mfuko wa Taifa wa Pembejeo za Kilimo na Benki ya Raslimali ya Tanzania (*TIB*), kupitia Dirisha Maalum kwa ajili ya kutoa mikopo ya kilimo.

Katika Mwaka wa Fedha wa 2010/2011, Mfuko wa Pembejeo ulitoa mikopo yenye thamani ya shilingi 3,615,768,556 kwa ajili ya ununuzi wa matrekta makubwa 96, matrekta madogo 19 na kukarabati matrekta makubwa manne.

Mheshimiwa Spika, aidha, hadi kufikia tarehe 18 Machi, 2011 Benki ya *TIB* ilikuwa imeidhinisha mikopo yenyе thamani ya shilingi bilioni 15.66, maombi mengine yenyе thamani ya shilingi bilioni 5.44 yalikuwa katika hatua za mwisho za uchambuzi.

Mheshimiwa Spika, kufikia tarehe 30 Mei, 2011, *TIB* ilikwishatoa mikopo ya matrekta makubwa 101 na matrekta madogo (*Power Tillers*) 82, kwa ajili ya waombaji wakiwemo Makampuni, Benki Jamii, SACCOS, Vyama vya Wakulima vya Ushirika na Watu Binafsi katika Mikoa ya Morogoro, Dodoma, Iringa, Mwanza, Kagera, Mbeya, Ruvuma, Arusha, Dar es Salaam na Mtwara.

Taasisi za Mfuko wa Pembejeo na *TIB* hazikutoa mikopo yoyote kwa wakulima Wilayani Mbozi kutokana na kutopata maombi yanayokidhi masharti nafuu yaliyowekwa ikiwa ni pamoja na kutokuwa na dhamana zinazokubalika.

Mheshimiwa Spika, katika Bunge la Tisa, Serikali iliahidi kuliangalia upya masharti ya ukopeshaji ndani ya Benki ya *TIB*, Sera ya Mikopo ya *TIB* na mwongozo wa ukopeshaji kupitia dirisha dogo la kilimo, inaelekeza kuwa njia rahisi ya kuwawezesha wakulima wadogo kupata mikopo ni kutumia Taasisi za Mikopo Midogo (*Micro Finance Institutions*), Benki Jamii, Vikundi vya Wakulima, SACCOS na Vyama vya Ushirika ambavyo vinawenza kukopa kutoka *TIB* na kuwakopesha Wanachama wake kwa masharti nafuu.

MHE. GODFREY W. ZAMBI: Mheshimiwa Spika, ninashukuru kwa kunipa nafasi niulize maswali madogo mawili ya nyongeza kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, ni dhahiri kwamba Wananchi wengi wa Tanzania na hususan wakulima hawapati mikopo mingi kupitia Mfuko wa Pembejeo wa Taifa, kwa sababu Mfuko huu unapewa kiasi kidogo sana cha fedha. Mimi ninao ushahidi wa majina ya waombaji wengi ambao wameomba mkopo kupitia Mfuko wa Pembejeo wa Taifa kule Mbozi, lakini wanapokwenda kwenye Mfuko wa Pembejeo wa Taifa, hawawezi kupewa mikopo kwa sababu mfuko unasema Serikali imetupa pesa kidogo: Je, ni lini sasa Waziri atawahakikishia Wananchi hawa wa Mbozi na wakulima wengine nchini kote ambao wamekopa kupitia Mfuko wa Pembejeo wa Taifa kwamba sasa Mfuko utapata pesa za kutosha ili hao waliokopa pia waweze kupata mikopo yao?

(b) Mheshimiwa Waziri anasema kwamba Mbozi hakuna wakulima waliofanikiwa kupata mikopo kwa sababu maombi hayakukidhi masharti nafuu yaliyowekwa na *TIB*; na kwa sababu anasema masharti hayo yalikosa dhamana zinazokubalika; ninaomba awaeleze hao waombaji masharti nafuu au dhamana zinazokubalika ni zifi ili wajue na waweze kuzikamilisha? Ahsante sana.

WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA: Mheshimiwa Spika, ninapenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya mkwe wangu, Mheshimiwa Godfrey W. Zambi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni vigumu sana kumweleza mkwe wako kwamba, umekosa mkopo kwa sababu huna dhamana ya kutosha. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, lakini ni kweli kwamba, Mfuko wa Pembejeo una mtaji mdogo na tunaendelea kuiomba Serikali ili iweze kuuongezea mtaji, kwa sababu Mfuko huu ni msaada mkubwa sana wa wakulima katika kuwapatia mikopo kwa ajili ya pembejeo za kilimo.

Mheshimiwa Spika, Wakulima wa Mbozi ambao wameshindwa kupata mikopo kwa sababu ya kukosa dhamana zinazostahiki, tunawaomba watumie Vyama vyaa Ushirika wa Kuweka na Kukopa na kutumia Vyama vyao vyaa Msingi vyaa Ushirika ili wapewe mkopo kupitia vyama hivyo na vyama hivyo ndiyo viwapatie wakulima wake mikopo hiyo kwa masharti yaliyo nafuu zaidi.

MHE. LUHAGA J. MPINA: Mheshimiwa Spika, ahsante.

Kwa kuwa toka mwaka jana Baraza la Mawaziri liliridhia Benki ya *TIB* kutoa mikopo ya uwekezaji na hapo hapo kanuni zilianza kuandaliwa; lakini mpaka sasa hivi kanuni zinazoiruhusu Benki ya tib kutoa mikopo ya uwekezaji hazijakamilika; nini kilichosababisha kanuni hizo kutokamilika na sasa ni lini zitaanza kutumika?

WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA: Mheshimiwa Spika, ninapenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Luhaga Mpina, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kama ninavyojuu na kama ninayo taarifa sahihi, Kanuni za *TIB* zipo tayari na zimekwishaanza kutumika. Pamoja na Kanuni hizi kuwa tayari na kuanza kutumika, Serikali ipo kwenye mchakato na hatua nzuri ya kuanzisha Benki ya Kilimo na ninategemea kabisa kwamba, benki hii itakapoanzishwa, mengi ya matatizo ambayo tunaulizana hapa ya mtaji kwa wakulima, yatakuwa yamepungua au kwisha kabisa.

Na. 237

Ahadi ya Kuongeza Upatikanaji wa Maji Safi na Salama

MHE. AMINA N. MAKILAGI aliuliza:-

Serikali iliahidi kuendeleza Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji ili kuongeza upatikanaji wa huduma ya maji safi na salama hadi kufikia 65% vijiji na 75% mijini ifikapo mwaka 2015:-

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kutenga fedha za kutosha katika Bajeti ya Mwaka 2011/2012 ili kuleta changamoto katika Sekta ya Maji nchini?

(b) Je, ni lini Serikali itaanza kutoa elimu ya uvunaji maji ili Wanancni waweze kuvuna maji na kupunguza tatizo la maji linalowakabili?

NAIBU WAZIRI WA MAJI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maji, ninaomba kujibu swalii la Mheshimiwa Amina Makilagi, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b), kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inaendelea kuboresha huduma ya maji safi na salama nchini kote kuitia Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji, iliyoanza kutekelezwa mwaka 2006/2007. Kuitia programu hiyo, Serikali imekuwa ikitenga fedha mwaka hadi mwaka ili kutekeleza malengo yaliyoainishwa katika Sera ya Kitaifa. Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya Mwaka 2010, inaelekeza kuongeza huduma ya maji safi na salama vijijini kufikia 75% na mijini 95% ifikapo mwaka 2015. Ili kufikia lengo hilo, katika Mwaka wa Fedha wa 2011/2012, Serikali imeongeza bajeti ya fedha za maendeleo ya Wizara ya Maji kutoka shilingi bilioni 216.2 mwaka 2010/2011 hadi kufikia shilingi bilioni 428.6, sawa na ongezeko la 98%. Ongezeko hilo litawezesha kutekelezwa kwa miradi mingi zaidi ya maji na hivyo Wananchi wengi kunufaika.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kuhamasisha matumizi ya teknolojia ya uvunaji wa maji ya mvua kuitia mapaa. Kati ya mwaka 2005 na 2010, Serikali ilijenga matanki ya mfano katika Taasisi za Umma, Shule, Zahanati na Vituo vya Afya. Jumla ya matanki 313 yamejengwa na mengine tisa kukarabatiwa katika Wilaya mbalimbali. Vilevile, Serikali kuitia Chuo cha Maendeleo na Usimamizi wa Maji, ilitoa mafunzo ya uvunaji wa maji ya mvua kwa Mafundi 18 kutoka Wilaya ya Kasulu, Karatu, Bunda, Lushoto, Kigoma, Shinyanga, Lindi, Liwale, Mtwara na Kilosa. Aidha, uhamasishaji wa matumizi ya teknolojia hiyo unaendelea kutekelezwa chini ya Programu ndogo ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Vijijini, ambapo Serikali kuitia Halmashauri itajenga matanki matatu ya mfano katika vijiji kumi katika kila Halmashauri. Wataalamu Washauri tayari wameajiriwa na watasimamia ujenzi na kutoa mafunzo kwa mafundi wawili katika kila kijiji na kutoa elimu ya matumizi ya teknolojia hiyo katika vijiji vyote kumi vyenye miradi.

Mheshimiwa Spika Halmashauri zimeagizwa kutunga Sheria ndogo, ambapo michoro ya nyumba za kisasa mijini na vijiji, itakuwa na miundombinu ya kuvuna maji ya mvua kuitia mapaa ya nyumba.

MHE. AMINA N. MAKILAGI: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Pamoja na majibu mazuri sana, yenye matumaini ya Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji, ninaomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza kama ifuatavyo:-

(a) Kwa kuwa Serikali imedhamiria kuitia Mradi wa Benki ya Dunia kufikisha maji katika vijiji kumi katika kila Halmashauri; na kwa kuwa Mradi wa Benki

ya Dunia wa Vijiji kumi umekuwa ukisuasua kwa sababu mbalimbali ikiwemo na Serikali kutofikisha fedha kwa wakati katika vijiji na halmashauri husika: Je, Serikali inatoa tamko gani la kufikisha fedha kwa wakati katika vijiji vinavyohusika?

(b) Kwa kuwa Serikali imeweka mipango mizuri sana ya kuhamasisha Wananchi waweze kuvuna maji kupitia nyumba zao wanazojenga na ambazo wamekwishazijenga: Je, Serikali sasa imetenga fedha kiasi gani kwa ajili ya kuzisaidia Halmashauri za Wilaya na hasa Madiwani na Wenyeviti wa Vijiji waweze kufanya kazi yao kikamilifu kuhamasisha Wananchi? Ahsante sana. (*Makofi*)

NAIBU WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Maji, ninaomba kujibu swalil ya nyongeza la Mheshimiwa Amina Makilagi, lenye sehemu mbili kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza, kwenye upande wa mradi kwenye vijiji kumi; Serikali imejipanga kutatua matatizo ambayo yamejitokeza katika awamu hii ya kwanza. Kwanza, tumesema Wizara itaaniszisha Kitengo Maalum ambacho kila siku kitafuatalilia utekelezaji wa mradi huu katika kila halmashauri, Kitengo ambacho hakikuwepo hapo awali. Kwa hiyo, tunahakikisha kasoro ndogo ndogo ambazo zimejitokeza tutazishughulikia.

Mheshimiwa Spika, katika sehemu ya pili ya swalil lake, ambalo anazungumzia uvunaji wa maji ya mvua, niseme tu kwamba, kwenye bajeti ambayo tutaiwasilisha hivi karibuni, tutaelezea kwa kina namna gani tutahamasisha namna ya kuvuna maji ya mvua katika nchi nzima.

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, ningetamani wote muulize maswali, lakini kwa kuwa Waziri hajasoma Hotuba yake, mtapata nafasi ya kuuliza kila kitu atakapoivasilisha.

MWONGOZO WA SPIKA

MHE. ALPHAXARD K. N. LUGOLA: Mheshimiwa Spika, Mwongozo wa Spika.

SPIKA: Mwongozo wa Spika, kuhusu kitu gani?

MHE. ALPHAXARD K. N. LUGOLA: Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 68(7) ambayo inasema; “Hali kadhalika Mbunge anaweza kusimama wakati wowote ambapo hakuna Mbunge mwengine anayesema na kuomba Mwongozo wa Spika kuhusu jambo ambalo limetokea Bungeni mapema ili Spika atoe usafanuzi kama jambo hilo linaruhusiwa au haliruhusiwi kwa mujibu wa Kanuni na Taratibu za Bunge na majibu ya Spika yatatolewa papohapo au baadae kadiri anavyoona inafaa.”

Mheshimiwa Spika, saa moja iliyopita, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Nishati na Madini, amewasilisha Randama za Makadirio na Mapato ya Matumizi ya Wizara yake ya Mwaka 2011/2012.

Mheshimiwa Spika, tarehe 4 na 5 mwezi huu, vyombo vya habari, hususan baadhi ya Magazeti viliwahabarisha Watanzania wakati tunahitaji kutatua mgao wa umeme ambao umekuwa ni sugu kwamba, Wizara ya Nishati na Madini, imeihonga Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini ili wakubali kuitisha mapendekezo yao.

Mheshimiwa Spika, uwasilishaji wa Randama ni ishara tosha kwamba, hapo kesho Hotuba ya Wizara itasomwa na Kamati ya Kudumu ya Bunge nayo pia itatoa taarifa hapa Bungeni.

Mheshimiwa Spika, katika mazingira ya namna hii, ninaomba Mwongozo wako kama taarifa ambayo inaonekana sasa imeshawishiwa inaruhusiwa kule twa hapa Bungeni katika kuishauri Serikali yetu juu ya masuala ya Nishati na Madini.

Mheshimiwa Spika, ninaomba mwongozo wako. (*Makofi*)

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, magazeti mimi ninavyoju, Waziri wa Habari yuko wapi; sijui yako zaidi ya mangapi? Kama Bunge hili litakuwa linaongozwa na Magazeti, tumekula hasara na wenyewe nimewaambia mimi kama Spika, wasiniulize nje kwa sababu wakiniuliza nje nitaandikwa vinginevyo halafu nitaanza kujitetea humu ndani, sipendi. Mimi ya kwangu wanishtaki humu humu na Wananchi wanania bayana ninachokisema na ninachoongea au sana sana wawaalize watendaji wangu, wakikosea nitakuja kuwasahihisha, maana mimi kubaki ninajitetea kila siku kwamba, Waandishi wameniandika vinginevyo, ninakuja kujitetea hapa hili litakuwa siyo Bunge. (*Makofi*)

Mahali pangu pa kufanya kazi ni humu na Kamati zangu zinawajibika ndani ya Bunge na siyo mahali pengine popote. Kwa hiyo, mimi sina taarifa yoyote wala ushahidi wowote kwamba, Kamati ilihongwa na kwa maana hiyo taarifa yao siyo halali. Wametumwa na mimi, wamefanya kazi ikatolewa taarifa hapa na ninyi mtaijadili kwa nguvu na uwezo wenu na ninyi msiwe mmehongwa mkaanza kujadili mambo waliyowatuma hao wanaowatuma, mjadili mambo ambayo yako hapa na hicho ndiyo ninakitegemea kesho. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, tunayo taarifa ya wageni; wapo wageni wa Mheshimiwa Prof. Makame Mbarawa, Waziri wa Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia, ambao ni Wataalam kutoka kule ofisini kwake. Hao ni Dkt. F. M. Turuka, Katibu Mkuu, Dkt. Makungu, Naibu Katibu Mkuu na wapo Wakurugenzi wa Wizara na Watendaji Wakuu wa Taasisi zote za Wizara yake, ninadhani wapo kwenye nafasi zao za kufanyia kazi.

Tunao wageni wa Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia, Mheshimiwa Charles Kitwanga, naye siye mwingine ni mke wake mpwendwa, Bi. Matrida Kitwanga, pamoja na familia yao. Yuko wapi Bi. Matrida? Aah, ulipaswa

kukaa kwa Spika pale. Eeh, wanatakiwa wakae pale kwa Spika. Ahsante sana Mama; na watoto wake si mnawaona hao?

Halafu tunao wanafunzi 40 kutoka Shule ya Sekondari Dar es Salaam, Ilala, wakiongozwa na Almaalim Sadiki Samuel Ikune. Wanafunzi walipo wasimame. Ahsante sana, someni kwa bidii, ndiyo mategemeo yetu sisi. Ahsanteni na kaeni.

Kuna wanafunzi tisa ambaa ni walemavu wa macho na Walimu watatu kutoka Shule ya Msingi Uhuru Mchanganyiko, wakiongozwa na Mwalimu Asha Jeta. Wako wapi hawa ndugu zetu? Aah, ahsante sana, tumefurahi kuwaoneni, karibuni sana. Ahsante Walimu kwa kuwaleta watoto kuja kusikiliza. (*Makofi*)

Tuna wanafunzi 20 kutoka Shule ya Sekondari ya Ilowela, Njombe, ile shule ya kwangu kule. Hii ni shule ya watu binafsi, lakini wameshirikiana na inafanya kazi vizuri sana kule vijijini, wakiongozwa na Mkurugenzi Mkuu wa Shule hiyo Bwana Erasto Haule. Wanafunzi walipo wasimame wote. Ahsante sana, ninafurahi kuwaoneni. Baada ya Msemaji wa Kambi ya Upinzani kumaliza, nitawaona huko nje. Karibuni sana na poleni kwa safari kutoka Njombe, kwani huko ni mbali sana. Mbona hamnishangilii ninyi Waheshimiwa? (*Kicheko*)

Ahsante sana, ninawashukuru sana, wanatoka mbali kwa kweli.

Kuna wageni wetu wengine kutoka Mfuko wa Hifadhi ya Jamii, Accra Ghana, kwa hiyo, tuna wageni kutoka nje ya nchi, kutoka Ghana. Wageni hawa wa Mfuko wa Hifadhi ya Jamii, nitawataja mmoja mmoja.

Yupo Director General of Social Security and National Insurance Trust, Ghana, Dkt. Francis Sapara and then we have the Chairperson of the Trust, Mr. Collin Esamahu. Some of the pronunciations may not be correct. Then we have the Public Relations and Marketing Manager, Mr. Joseph Gordon Meshack. Okay, thanks very much.

Tunae huyu wanasema Mkurugenzi Mkuu, Mamlaka ya Mifuko ya Hifadhi ya Jamii, huyu ndiye Mwenyeji wao, Miss Irene Isaka. *Okay! Then we have the Director General, Government Employees Provident Fund*, huyu ni mwenyeji wao, Mr. Daudi Msangi, ahsante.

Tunae mgeni mwengine tena ambaye ni Mkurugenzi wa *ITGEFP*, huyu ni wa Tanzania, Edgar Shambuso, ahsante sana. Halafu kuna Lightness Maliki, yeze ni Mkurugenzi wa Matekelezo SSRA. Matekelezo tena, Kiswahili kigumu hicho.

So in short we welcome you to our Parliament and Tanzania, and we hope you will have good time with your colleagues who are here. You are Welcome.

Waheshimiwa Wabunge, matangazo ya wageni ni hayo. Shughuli za kazi; Mheshimiwa John Mnyika, yeze ni Katibu wa Wabunge wa CHADEMA, anaomba

niwatangazie Wabunge wa CHADEMA kwamba, leo saa saba mchana, kutakuwa na kikao kwenye Ukumbi Na. 219; Wabunge wa CHADEMA mzingatie hilo.

Kuna tangazo lingine linasema, Wizara ya Nishati na Madini inawatangazia Waheshimiwa Wabunge wote kuwa, kutakuwa na Maonesho ya Shughuli za Wizara na Taasisi zake katika Viwanja vya Bunge kuanzia leo tarehe 14 hadi 18 Julai, 2011 pale nyuma, wametengeneza mabanda kwenye eneo letu la maonesho.

Waheshimiwa Wabunge, Mbunge mwenzetu Mheshimiwa Juma Nkamia, amefiwa na dada yake jana, aliyekuwa anakaa Mkoka Wilaya ya Kongwa, Mkoa wa Dodoma. Dada yake amefariki jana, mazishi yatafanyika leo huko huko Mkoka. Mwenzetu amefiwa na dada yake jana, ambaye anaitwa Bi. Aisha Kaita na wanazika leo. Tunaomba tumpe pole na tumtakie marehemu mahali pema peponi. (*Amin*)

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea.

MWONGOZO WA SPIKA

MHE. KABWE Z. ZITTO: Mwongozo.

SPIKA: Eeh! Mwongozo.

MHE. KABWE Z. ZITTO: Mheshimiwa Spika, ninaomba mwongozo wako, tumepata taarifa kwamba, ndani ya Bunge lako Tukufu kutakuwa na nafasi ambayo iko wazi. Kwa hiyo, ninaomba ulitaarifu Bunge kama tayari umepata barua ya Mbunge ambaye amejiuzulu na kama tayari umeitaarifu Tume ya Taifa ya Uchaguzi ili twende tukachukue Jimbo letu la Igunga.

SPIKA: Ukisikia watu wanasema ni wakati wa kupoteza nafasi wakati ndiyo huu. Jamani mimi nimeona kama mlivyoona ninyi, kwa hiyo na sisi tunazo taratibu zetu. Sisi tumeona kama mlivyoona nyinyi kwenye mitandao, kwa hiyo, ikifika wakati kuna utaratibu utakaofuata. Utaratibu ni kwamba, mimi nitaambiya na wanaohusika ama kama Mheshimiwa Rostam Aziz angekuwa ameniandikia ndiyo ningekuwa na taarifa, lakini sikuambiya ilikuwa Igunga sijui. Kwa hiyo, tutatoa taarifa wakati utakaokuwa mwafaka.

HOJA ZA SERIKALI

Makadirio ya Matumizi ya Serikali kwa Mwaka 2011/2012
Wizara ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia

WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA: Mheshimiwa Spika, kufuatia taarifa iliyowasilishwa leo ndani ya Bunge lako Tukufu na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu, Mheshimiwa Peter

Joseph Serukamba (Mb.), kuhusu Wizara ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia, ninaomba kutoa hoja kwamba, Bunge lako Tukufu, likubali kupokea na kujadili taarifa ya utekelezaji wa kazi za Wizara ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia kwa mwaka 2010/2011 na Malengo ya Wizara katika Bajeti ya mwaka 2011/2012. Aidha, ninaliomba Bunge lako Tukufu lipokee, lijadili na kuitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia pamoja na Taasisi zake kwa Mwaka wa Fedha wa 2011/2012.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote, ninapenda kuchukua fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kutujalia uhai na afya njema na kutuwezesha sisi kushiriki katika Mkutano huu wa Bunge unaojadili Bajeti ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, niruhusu pia niungane na Waheshimiwa Wabunge wenzangu, kumpongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, kwa kuchaguliwa tena kuongoza kwa muhula wa pili wa Serikali ya Awamu ya Nne. Pia, ninampongeza Mheshimiwa Dkt. Mohammed Gharib Bilal, kwa kuchaguliwa kwake kuwa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kuchaguliwa kwao kwa ushindi mkubwa ni ishara na imani ya Wananchi wa Chama cha Mapinduzi.

Mheshimiwa Spika, ninapenda kumpongeza Mheshimiwa Mizengo Kayanza Peter Pinda (Mb.), kwa kuchaguliwa kuwa Mbunge na kuteuliwa tena na hatimaye kuitishwa na Waheshimiwa Wabunge kuwa Waziri Mkuu kwa muhula wa Pili wa Serikali ya Awamu ya Nne. Nina imani kwamba, uongozi wao wa busara utaiwezesha nchi yetu kupata maendeleo makubwa katika Serikali ya Awamu ya Nne hasa katika kukuza uchumi na kutoa huduma bora kwa jamii kwa ajili ya ustawi wa Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, ninapenda kukupongeza wewe binafsi, Mheshimiwa Anne Semamba Makinda (Mb.), kwa kuchaguliwa kwako kuwa Spika ili kuliongoza Bunge letu Tukufu na hivyo kuwa mwanamke wa kwanza kuliongoza Bunge katika nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki. Kuchaguliwa kwako kunatokana na imani kubwa walijonayo Waheshimiwa Wabunge kwa kuzingatia uwezo, uzoefu na busara zako katika kulitumikia Bunge hili. Ninapenda pia kumpongeza Mheshimiwa Job Yustino Ndugai (Mb.), kwa kuchaguliwa kwake kuwa Naibu Spika.

Mheshimiwa Spika, ninaomba nitumie fursa hii pia kumshukuru sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa imani kubwa aliyonayo kwangu kwa kunteua kuwa Mbunge na pia kunipa dhamana ya kuiongoza Wizara ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia. Vilevile, ninapenda kumpongeza Mheshimiwa Charles Muhangwa Kitwanga (Mb.), kwa kuchaguliwa kwake kuwa Mbunge na hatimaye kuteuliwa na Mheshimiwa Rais kuwa Naibu Waziri wa Wizara ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia. Ninaomba niwahakikishie Viongozi wetu na Wananchi kwa ujumla kuwa, tutafanya kazi tuliyodhaminiwa kwa bidii na uadilifu mkubwa.

Mheshimiwa Spika, ninapenda pia kuchukua fursa hii, kuwapongeza Mawaziri na Naibu Mawaziri kwa kuteuliwa katika nyadhifa zao mpya. Aidha, ninapenda

kuwapongeza Waheshimiwa Wabunge wote, kwa kuchaguliwa kwao kuwawakilisha Wananchi katika Bunge hili. Ninaamini kuwa, kwa ushirikiano na Waheshimiwa Wabunge, tutaijenga nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, ninapenda pia kumpongeza Mheshimiwa Jaji Frederick Mwita Werema, kwa kuteuliwa kwake kuwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa muhula wa pili wa Serikali ya Awamu ya Nne. Kuteuliwa kwake kunathibitisha uwezo wake mkubwa katika masuala ya Sheria na imani kubwa aliyonayo Mheshimiwa Rais kwa utendaji wake ulio makini.

Mheshimiwa Spika, nitakuwa mchoyo wa fadhila kama sitawashukuru wafanyakazi wote wa Wizara yangu. Kipekee, ninapenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa wale wote walioniwezesha kutekeleza majukumu ya Wizara yangu kwa kipindi kilichopita na ambao wamewezesha kuandaa Mpango wa Mwaka wa Fedha wa 2011/2012 na kuboresha hoja yangu ambayo ninaiwasilisha katika Hotuba hii. Ninatoa shukrani zangu za pekee kwa Mheshimiwa Charles Muhangwa Kitwanga (Mb.), Naibu Waziri wa Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia, Dkt. Florens Martin Turuka, Katibu Mkuu, Dkt. Patrick James Makungu, Naibu Katibu Mkuu, Watendaji wote katika Wizara, Taasisi na Mashirika yaliyo chini ya Wizara.

Mheshimiwa Spika, kwa namna ya pekee kabisa, ninatoa shukrani zangu kwa Waheshimiwa Wabunge wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu chini ya Mwenyekiti wake, Mheshimiwa Peter Joseph Serukamba, Mbunge wa Kigoma Mjini (CCM), kwa ushauri na maelekezo yao. Aidha, ninapenda kumshukuru Mheshimiwa Prof. Kulikoyela Kanalwanda Kahigi, Mbunge wa Bukombe (CHADEMA), ambaye ni Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani kuhusu Wizara ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia, kwa ushirikiano wake na mchango wake katika kuiboresha hoja hii. Aidha, ninatoa shukrani zangu kwa Wananchi wote wa Tanzania, kwa mchango wao katika kutekeleza majukumu ya Wizara yangu.

Mheshimiwa Spika, kwa upendo mkubwa ninapenda kumshukuru mke wangu, Dkt. Unice Mbarawa na watoto wangu; Jennifer, Asia na Baraka, kwa ustahimilivu wao mkubwa waliouonesha, moyo walionipa na ushirikiano wa dhati katika kutekeleza majukumu yangu ya kila siku.

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia, ilikabitihwa dhamana ya kuhakikisha kwamba, Teknolojia ya Habari na Mawasiliano, Sayansi, Teknolojia na Ubunifu, vinachangia kikamilifu katika maendeleo ya nchi yetu. Pamoja na jukumu hilo, Wizara hii imepewa dhamana ya kusimamia Taasisi, Mashirika, Tume na Kampuni ambazo zinachangia juhudhi za Wizara katika kuyafikia malengo na matarajio ya Wananchi. Taasisi hizo ni Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam (*DIT*); Taasisi ya Sayansi na Teknolojia Mbeya (*MIST*); Taasisi ya Sayansi na Teknolojia ya Nelson Mandela - Arusha (*NM-AIST*); Tume ya Nguvu za Atomiki Tanzania (*TAEC*); Tume ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia (*COSTECH*); Shirika la Posta Tanzania (*TPC*); Kampuni ya Simu Tanzania (*TTCL*); Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (*TCRA*); na Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote (*UCAF*).

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia, katika kipindi cha Mwaka wa Fedha wa 2010/2011, imetekeleza majukumu na mipango yake kwa kuzingatia Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025, Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini Tanzania na Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya Mwaka 2010 – 2015. Aidha, Wizara inazingatia Sera ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia, Sera ya Taifa ya Bayoteknolojia, Sera ya Taifa ya Utafiti na Maendeleo, Sera ya Taifa ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano, Sera ya Taifa ya Mawasiliano ya Simu, Sera ya Taifa ya Posta pamoja na Sera na Sheria mbalimbali za Sekta ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia na miongozo mingine inayoongoza Sekta ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia na Serikali kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha wa 2010/11, Wizara ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia ilitengewa jumla ya Sh. 71,071,600,000. Kati ya fedha hizo, Sh. 26,590,690,000 zilitengwa kwa ajili ya matumizi ya kawaida, yaani mishahara na matumizi mengineyo na Sh. 44,426,910,000 kwa ajili ya matumizi ya maendeleo zikijumuisha fedha za ndani Sh. 42,426,910,000 na fedha za nje Sh. 2,000,000,000.

Mheshimiwa Spika, hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2011 jumla ya Sh. 21,927,092,337.84 zilikuwa zimetolewa na kutumika, ambazo ni sawa na asilimia 82.46 ya Bajeti ya Matumizi ya Kawaida iliyoidhinishwa. Aidha, kiasi cha Sh. 21,673,706,747 zilikuwa zimepokelewa kwa upande wa fedha za maendeleo. Kiasi hiki ni sawa na asilimia 49 ya fedha za Maendeleo zilizoidhinishwa na Wizara.

Mheshimiwa Spika, majukumu yaliyotekelezwa na Wizara ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia pamoja na Taasisi zake katika kipindi tajwa ni haya yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA): Serikali imeendelea kujenga Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano, ujenzi ambaao ulianza rasmi mwezi Februari, 2009. Awamu ya Kwanza ya ujenzi wa mkongo wa mawasiliano imekamilika na huduma za mawasiliano zimeanza kutolewa. Katika awamu hii, jumla ya kilometra 4,300 za Mkongo katika Mikoa 16 zimejengwa. Mikoa hiyo ni Dar es Salaam, Pwani, Morogoro, Iringa, Mbeya, Dodoma, Singida, Arusha, Manyara, Kilimanjaro, Tanga, Shinyanga, Mwanza, Tabora, Mara na Kagera.

Mheshimiwa Spika, Awamu ya Pili ya ujenzi wa Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano, inayohusisha ujenzi wa takriban kilometra 3,000 imeanza na inatarajiwu kukamilika mwezi Machi, 2012 (ndani ya kipindi cha miezi 18 kuanzia Agosti 2010). Hadi kufikia tarehe 30 Juni 2011, jumla ya kilomita 900 zilikuwa zimekamilika katika njia ya Dar es Salaam – Lindi – Mtwara; Songea – Njombe; Tunduma – Sumbawanga na Kigoma - Biharamulo.

Mheshimiwa Spika, uunganishwaji wa Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano kwenvye Mikongo ya Baharini ya *SEACOM* (ambao uliunganishwa mwezi Julai, 2009) na *EASSY* (ambao uliunganishwa mwezi Aprili, 2010), umeendelea kuboresha na kupunguza

gharama za mawasiliano ya simu na *Internet*. Kabla ya Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano kuwepo na kabla ya Mikongo ya Baharini kuunganishwa na Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano, gharama za simu kwa sekunde moja zilikuwa kati ya Sh. 2.50 na Sh. 3.00. Aidha, gharama za mtandao wa intaneti zilikuwa shilingi 12,400,000 kwa kiwango cha *2 mega bits/sec dedicated internet bandwidth*.

Hivi sasa, gharama ya simu kwa sekunde ni kati ya senti hamsini na shilingi moja na gharama za mtandao wa intaneti kwa kiwango cha *2mbts/sec* ni shilingi 3,620,000. Aidha, Vituo sita vya kuunganisha Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano na nchi jirani vilivyopo Rusumo (Rwanda), Kabanga (Burundi), Mtukula (Uganda), Namanga (Kenya), Tunduma (Zambia) na Kasumulo (Malawi) vimejengwa na viko tayari kwa ajili ya kuunganisha mawasiliano na nchi jirani. Hivi sasa, Vituo vya Kasumulo, Rusumo na Tunduma, vimeshaunganishwa kimawasiliano na Nchi za Malawi, Rwanda na Zambia. Uunganishwaji wa kimawasiliano kupitia Mkongo huu kwa nchi za Kenya, Uganda na Burundi kunasubiri ukamilikaji wa ujenzi wa miundombinu katika nchi hizo. Kimiundombinu, Tanzania ipo tayari.

Mheshimiwa Spika, Wizara inaratibu Programu ya kujenga uwezo wa rasilimali watu katika fani ya TEHAMA kwenye Taasisi za Serikali (*ICT HR Development Program*), kwa malengo ya kuimarisha na kuhamasisha matumizi ya TEHAMA kwa ajili ya maendeleo. Aidha, kupitia Mradi wa Ujenzi wa Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano, watumishi 268 wa Kampuni ya Simu Tanzania, ambayo imepewa dhamana ya kuendesha Mkongo wamepata mafunzo ya kusimamia na kuuendesha Mkongo huo.

Mheshimiwa Spika, Wizara imekamilisha tathmini ya uanzishwaji wa Mtandao wa Elimu na Utafiti (*National Education and Research Network-NREN*), utakaounganisha Vyuo Vikuu na vituo vya utafiti 27 katika Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano kupitia Mradi wa Sayansi, Teknolojia na Elimu ya Juu, unaofadhiliwa na Benki ya Dunia.

Mheshimiwa Spika, Wizara kwa kushirikiana na *International Telecommunication Union (ITU)*, inaratibu Miradi ya Maendeleo ya TEHAMA (*ICT Development Initiatives*) nchini hususan katika Sekta ya Elimu. Lengo ni kuunganisha shule za msingi, sekondari na vyuo katika Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano. Tayari shule mbili za msingi na tano za sekondari (wasioona) nchini zimenufaika na Mradi huu. Shule za Msingi zilizonufaika ni Buigiri (Dodoma) na Kizega (Singida). Aidha, Shule za Sekondari zilizonufaika na juhudi hizo ni Ilula (Iringa), Mpwapwa (Dodoma), Ilowola (Njombe), Tumaini na Lulumba (Singida). Aidha, vifaa vya TEHAMA, vyenye thamani ya kiasi cha Dola za Marekani \$ 113,100 vimefungwa katika shule hizo. Wizara imeratibu uunganishwaji wa vifaa hivi na kutoa mafunzo mafupi ya utumiaji wa vifaa. Vilevile, Mpango wa Kitaifa wa Kuunganisha Shule za Msingi, Sekondari na Vyuo katika Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano (*National Schools Connectivity Plan*), umeandalisha kwa ushirikiano wa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundis, Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii Ofisi ya Waziri Mkuu - TAMISEMI na *ITU* kwa kuzingatia viwango vya kimataifa

Mheshimiwa Spika, katika jitihada za Serikali kupeleka huduma za mawasiliano hadi vijiji, Serikali imeanzisha Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote (*UCAF*). Madhumuni ya Mfuko huu ni kusaidia juhudini za upelekaji mawasiliano ikiwa ni pamoja na kutoa ruzuku kwa wawekezaji watakaokuwa tayari kupeleka huduma za mawasiliano maeneo ya vijiji na baadhi ya maeneo ya mjini yasiyokuwa na mvuto kibashara. Hadi sasa Mfuko umeainisha vijiji 239 katika Mikoa 17 ambayo ni Dodoma, Arusha, Tanga, Morogoro, Pwani, Lindi, Ruvuma, Iringa, Mbeya, Singida, Tabora, Rukwa, Shinyanga, Kagera, Mara, Manyara na Kigoma. Aidha, vijiji 139 vimechaguliwa kwa ajili ya Mradi wa Majaribio (*Pilot Project*). Uhakiki wa maeneo mengine unaendelea.

Mheshimiwa Spika, hadi kufikia mwezi Juni, 2011, Kampuni 14 zilikuwa zimepewa leseni ya kutoa huduma za mawasiliano ya simu nchini. Uwepo wa Kampuni nyingi, umeleta ushindani mkubwa kwenye soko ambao umewezesha kushusha gharama za mawasiliano ya simu na kupanua wigo kwa watumiaji kuchagua mto huduma bora zaidi. Aidha, utoaji wa leseni kwa kampuni za simu umeboreshwa. Leseni zinazotolewa hivi sasa, zinazingatia mwingiliano wa teknolojia (*Converged License*) ili kurahisisha na kuvutia uwekezaji kwa watoa huduma.

Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza mabadiliko ya teknolojia za utangazaji kutoka Analogia kwenda Digitali, hadi sasa kampuni tatu zimepewa leseni ya kutoa huduma hiyo. Kampuni hizo ni *Agape Associates Ltd, Basic Transmission Ltd na StarMedia (T) Ltd*. Makubaliano ya kuzima mitambo ya Analogia kwa Jumuiya ya Afrika Mashariki (*EAC*) ni mwaka 2012 na kwa Jumuia ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika (*SADC*) ni mwaka 2013. Tanzania ni Mwanachama kwa Jumuiya zote mbili na hivyo inapaswa kuzingatia muda uliowekwa wa kufanya mabadiliko hayo.

Mheshimiwa Spika, ni muhimu Taifa kufanya mabadiliko haya kutohana na maendeleo ya kiteknolojia yasiyokwepeka yaliyofikiwa katika Sekta ya Utangazaji kote Ulimwenguni. Mabadiliko ya Teknolojia ya utangazaji yatalipatia Taifa mafanikio mengi. Miongoni mwa hayo ni pamoja na:-

(a) Fursa ya masafa ya ziada katika teknolojia ya digitali ikilinganishwa na ile ya analogia. Hivyo, kwa masafa yaliyolengwa kwa ajili ya Tanzania Kimataifa, wawekezaji wengi zaidi wataweza kuhudumiwa kwa masafa yaliyopo; hivyo kuongeza faida kiuchumi kwa kutoa fursa zaidi kwa wawekezaji na ajira zaidi;

(b) Huduma inayotumia teknolojia ya digitali ina ubora wa juu ikilinganishwa na ile ya analogia. Vilevile, teknolojia ya digitali ni ya kisasa ikilinganishwa na analogia ambayo inakaribia kufutika, hivyo mabadiliko hayakwezeki;

(c) Kurahisishwa zaidi kwa mfumo wa mawasiliano na hivyo kuwawezesha Wananchi wengi zaidi kupata taarifa mbalimbali mahali popote walipo na kwa kutumia vyanzo vingi zaidi vya habari na mawasiliano kama vile simu za mkononi na kompyuta; na

(d) Kutenganishwa kwa shughuli za utayarishaji wa vipindi vya Televisheni na shughuli za urushaji wa Matangazo hivyo kuongeza utaalamu katika utayarishaji vipindi na kuongeza nafasi za ajira.

Mheshimiwa Spika, kwa kutambua umuhimu wa sayansi na teknolojia nchini, Serikali imekamilisha Sera ya Taifa ya Bayoteknolojia na Sera ya Taifa ya Utafiti na Maendeleo. Mipango Mkakati wa Utekelezaji wa Sera hizo imeandaliliwa na kujadiliwa na wadau mbalimbali. Vilevile, Wizara imekamilisha rasimu ya Sera ya Taifa ya Teknolojia za Nyuklia na hivi sasa iko katika hatua za kuridhiwa na Serikali. Pia, Wizara imekamilisha rasimu ya Sera ya Taifa ya Sayansi, Teknolojia na Ubunifu, ambayo imetokana na kuhuishwa kwa Sera ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia ya Mwaka 1996. Sera hii inaainisha maeneo ya kipaumbele katika kuimarisha mchango wa sayansi, teknolojia na ubunifu katika kuchangia uchumi wa taifa. Aidha, Wizara kwa kushirikiana na Wadau mbalimbali, imeandaa Kanuni za Tatu za Matumizi ya Mionzi nchini.

Mheshimiwa Spika, Wizara imeendelea kusimamia matumizi ya fedha za utafiti na maendeleo. Hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2011 kiasi cha Sh. 19,494,651,700 kimetolewa na kuelekezwa katika maeneo ya kipaumbele kama ifuatavyo:-

(a) Kujenga uwezo wa watafiti; ambapo watafiti kutoka vituo vya utafiti na vyuo vikuu wapatao 202 wamegharimiwa kusoma shahada za uzamili na uzamivu katika vyuo vikuu mbalimbali hapa nchini;

(b) Uboreshaji wa miundombinu ya utafiti na vitendea kazi katika taasisi za utafiti; kwa kuanzia Wizara imegharimia ununuzi wa vifaa katika Taasisi ya Taifa ya Utafiti wa Magonjwa ya Binadamu (*NIMR*) – Kituo cha Tabora, Tume ya Nguvu za Atomiki (*TAEC*) na Taasisi ya Utafiti wa Tiba Asilia – Chuo Kikuu cha Muhimbili cha Sayansi za Afya;

(c) Uhamasishaji wa matumizi ya matokeo ya utafiti na uhawilishaji wa teknolojia;

(d) Kugharamia utafiti ambapo maombi (*proposals*) ya mwega yapatayo 360 yalipokelewa na kati ya hayo maombi, 106 yamepita hatua ya kwanza ya mchujo; na

(e) Kuratibu na kutathmini shughuli za sayansi na teknolojia nchini.

Mheshimiwa Spika, Wizara imeendelea kutekeleza Programu ya Uboreshaji wa Mfumo wa Sayansi, Teknolojia na Ubunifu kwa ushirikiano na Shirika la Kimataifa la Elimu, Sayansi na Utamaduni (*UNESCO*). Sekretarieti na Kamati ya Kitaifa ya Kusimamia Programu ilianza kazi tarehe 1 Aprili, 2010. Katika kipindi hiki yafuatayo yamefanyika:-

(a) Semina nne za uhamasishaji kwa wadau zimefanyika hadi kufikia mwezi Machi, 2011; na

(b) Wizara imeshaandaa andiko la awali (*background paper*), ambalo litatoa hali halisi ya mfumo wa sayansi, teknolojia na ubunifu ulivyo ili kuonesha maeneo yanayohitaji kuboreshwa. Hatua inayofuata ni kufanya mapitio kwa kutumia wataalam wa kimataifa ili kupata namna bora zaidi ya kuendeleza sayansi, teknolojia na ubunifu hapa nchi kulingana na *best practice*.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kusimamia Mpango wa Uanzishwaji wa Taasisi ya Sayansi na Teknolojia ya Nelson Mandela Arusha. Ukarabati na uboreshaji wa majengo yaliyopo Tengeru, eneo lililokuwa likimilikiwa na *CAMARTEC*, unaendelea vizuri. Ukarabati huo ulianza mwezi Agosti, 2010 na upo katika hatua za mwisho na majengo yatakabidhiwa ifikapo tarehe 10 Agosti, 2011.

Ukarabati huo unafanywa kwa fedha za mkopo wa shilingi bilioni 38.7 kutoka kwenye Mifuko ya Pensheni chini ya usimamizi wa *Pension Properties Limited*, baada ya Mkataba kusainiwa tarehe 22 Mei, 2010.

Mheshimiwa Spika, kwa sasa mchakato wa ununuvi wa samani na vitendea kazi unaendelea na tayari baadhi ya vifaa na samani vimefikishwa na kupokelewa na Taasisi hiyo. Aidha, mitaala ya mafunzo ya uzamili na uzamivu imekwishaandaliiwa na wafanyakazi wapatao 76 wamekwishaajiriwa. Masomo yanategemewa kuanza mwaka huu (2011/2012) katika fani zifuatazo: *Life Sciences and Bio-engineering (LSBE)*; *Mathematics Computational Science and Engineering (MCSE)*; *Information and Communication Science and Engineering (ICSE)*; *Hydrology and Water Resources Engineering (HWRE)*; *Environmental Science and Engineering (EnSE)*; *Materials Science and Engineering (MaSE)*; *Sustainable Energy Science and Engineering (SESE)*; na *Humanities and Business Studies (HuBS)*.

Mheshimiwa Spika, Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya Mwaka 2010 – 2015, ilieelekeza Wizara ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia kutekeleza yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, Sayansi na Teknolojia: Serikali kutenga kila mwaka kiasi kisichopungua asilimia 1.0 ya Pato Ghafi la Taifa (*GDP*) kwa ajili ya utafiti na Maendeleo (*R &D*), pamoja na Maonesho ya Matokeo ya utafiti. Katika kipindi cha mwaka 2010/2011, Serikali ilitenga jumla ya Sh. 30,746,000,000 kwa ajili ya utafiti. Hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2011 Serikali ilitoa kiasi cha Sh. 19,494,651,700. ambazo zimeelekezwa katika maeneo yafuatayo: -

- (i) Kujenga uwezo wa watafiti;
- (ii) Kuboresha miundombinu ya utafiti na vitendea kazi katika taasisi za utafiti na maendeleo;
- (iii) Kuhamasisha matumizi ya matokeo ya utafiti na uhawilishaji wa teknolojia;

(iv) Kugharamia utafiti na shughuli za maendeleo ya teknolojia zitakazotuwezesha kufikia malengo ya MKUKUTA II na Milennia; na

(v) Kuratibu na kutathmini shughuli za sayansi na teknolojia nchini.

Mheshimiwa Spika, katika kuchukua hatua za makusudi za kuiimarisha Tume ya Sayansi na Teknolojia ili kiwe chombo kinachowaunganisha watafiti na wagunduzi wote nchini ili waweze kukaa na kubadilishana uzoefu na kuwa na msukumo wa pamoja katika ujenzi wa msingi wa sayansi na teknolojia imara; Serikali imeanza mchakato wa kutunga sheria itakayosimamia masuala yote ya sayansi, teknolojia na ubunifu nchini (*Science, Technology and Innovation Act*). Kupitia mchakato huu, Sheria Na. 7 ya Mwaka 1986 iliyounada Tume ya Sayansi na Teknolojia itarejewa ili kuhakikisha majukumu ya Tume yanakidhi mahitaji ya sasa ya sayansi, teknolojia na ubunifu ndani ya mfumo wa kisheria.

Mheshimiwa Spika, kuishirikisha sekta binafsi katika kuchangia maendeleo na matumizi ya sayansi na teknolojia kwenye uzalishaji mali na utoaji wa huduma. Kulingana na Sera ya Ushirikishwaji wa Sekta Binafsi, Wizara imeandaa na kuainisha maeneo ya sayansi na teknolojia ambayo sekta binafsi inaweza kuwekeza. Maeneo hayo ni pamoja na eneo la usindikaji mazao ya kilimo na uzalishaji wa bidhaa za bayoteknolojia. Aidha, mfumo mpya wa sayansi, teknolojia na ubunifu unaoandaliwa utawezesha uanzishwaji wa taasisi za utafiti zisizo za serikali katika sekta mbalimbali za sayansi na teknolojia kama ilivyo kwenye mazao ya chai na kahawa, ambapo taasisi za jinsi hii zimeonesha kuwa na manufaa makubwa kwa Wananchi.

Mheshimiwa Spika, kuandaa programu mahususi ya wataalamu wa kada mbalimbali kama vile uhandisi, uganga wa binadamu na wanyama, madini, jiolojia na kilimo na kadhalika, watakaojaza nafasi ambazo ni muhimu na za lazima katika kuyafikia malengo hayo ya dira. Ili kukabili ana uhaba wa wataalam katika fani mbalimbali za sayansi nchini, Serikali imeendelea kupanua taasisi zinazotoa mafunzo katika fani mbalimbali za sayansi na teknolojia na kuanzisha taasisi mpya ikiwemo Taasisi ya Sayansi na Teknolojia ya Nelson Mandela Arusha, ambayo imeanzishwa mahususi ili kupambana na uhaba wa Wataalam katika fani za sayansi na teknolojia. Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam (*DIT*) na Taasisi ya Sayansi na Teknolojia Mbeya (*MIST*), zimeendelea kuongeza udahili wa wanafunzi, uanzishwaji wa programu mpya na kupanua zilizopo katika taaluma za uhandisi TEHAMA, Mazingira na nyinginezo. Aidha, Wizara inatekeleza mkakati wa kuhamasisha wanafunzi katika ngazi zote za elimu kusoma masomo ya sayansi ili kuhakikisha taasisi mbalimbali za mafunzo ya sayansi na teknolojia zinapata wanafunzi wenyewe viwango vizuri vya elimu na ujuzi. Pia, Wizara inaendelea kubuni mbinu mbalimbali za uhamasishaji ikiwa ni pamoja na kutoa tuzo za aina mbalimbali kwa wanafunzi wenyewe ufaulu wa juu katika masomo ya sayansi na teknolojia katika shule za sekondari na taasisi za elimu ya juu.

Mheshimiwa Spika, kufufua, kupanua na kuanzisha viwanda ili uzalishaji viwandani na kuongeza ajira ya wanasayansi. Wizara inaendelea kushirikiana na Wizara ya Viwanda na Biashara katika kufanya tafiti mbalimbali zinazoweza kukuza viwanda vyetu hapa nchini na kuhawilisha teknolojia mbalimbali zinazoweza kutumika katika

viwanda vyetu hapa nchini na hivyo kutoa ajira kwa wanasayansi na wanateknolojia na kuongeza Pato la Taifa.

Mheshimiwa Spika, kuimarisha shughuli za kuatamia teknolojia (*technology incubation*), kabla ya kuzipeleka sokoni. Wizara, kupitia Tume ya Sayansi na Teknolojia (*COSTECH*), imeanzisha utaratibu wa kutoa ushauri na kuatamia teknolojia za TEHAMA. Uatamizi huo umepangwa kuchukua muda wa miaka mitatu, muda ambao mgunduzi anatarajiwa kuwa na uwezo wa kuingiza teknolojia yake sokoni. Aidha, Tume ya Sayansi na Teknolojia kwa kushirikiana na wadau wengine, imekuwa ikiandaa mafunzo mbalimbali kupitia warsha na semina juu ya matumizi ya teknolojia mpya zinazotokana na utafiti na kusaidia kuzihawilisha kwa watumiaji.

Mheshimiwa Spika, kuandaa mazingira bora ya kusambaza teknolojia kwa watumiaji. Tume ya Sayansi na Teknolojia, kwa kushirikiana na Wajasiriamali na watumiaji mbalimbali wa teknolojia, imesambaza teknolojia zilizohakikiwa (*prototypes*) ili ziwafikie watumiaji wa mwisho. Teknolojia hizo ni pamoja na zile za majiko bora na mashine zinazoendeshwa kwa upemo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu kutumia vyombo vya habari kutoa taarifa muhimu za sayansi, teknolojia na ubunifu katika maendeleo ya kiuchumi na kijamii nchini; Wizara kwa kupitia Tume ya Sayansi na Teknolojia na Taasisi ya Teknolojia ya Dar es Salaam, zimeendelea kuandaa vipindi mbalimbali vya redio na runinga vinavyohusu masuala ya sayansi na teknolojia ili kuhamasisha Umma wa Tanzania kuongeza matumizi ya sayansi na teknolojia katika shughuli za uchumi na maendeleo Taifa. Aidha, Wizara na Taasisi zilizo chini yake, zinachapisha majorida kuhusu masuala mbalimbali ya sayansi, teknolojia na matokeo ya tafiti mbalimbali ili kuwaelemisha Wananchi umuhimu wa sayansi na teknolojia kwa matumizi ya kila siku. Vilevile, Wizara kupitia Tume ya Sayansi na Teknolojia, imeendelea kuhamasisha na kusaidia taasisi za utafiti na vyuo vikuu nchini kuanzisha na kuendeleza majorida ya kitaaluma.

Mheshimiwa Spika, kuwatambua wagunduzi wetu na kuwapa rasmi hakimiliki za ugunduzi wao. Wizara imeendelea kuwatambua na kuwahamasisha wagunduzi nchini. Wizara kupitia Tume ya Sayansi na Teknolojia, imekuwa ikiwasaidia wagunduzi hao kuboresha ugunduzi wao kwa kuwafadhili kwenye mafunzo ili wapate ujuzi zaidi katika fani zao. Aidha, Tume imeanzisha ofisi maalum inayojulikana kama *Tanzania Intellectual Property Advisory Services and Information Centre (TIPASIC)*, ambayo inatoa ushauri kwa wabunifu na wagunduzi. Katika eneo hili, Serikali imekuwa ikitoa tuzo maalum kwa wagunduzi na wabunifu ambao ugunduzi wao umedhihirika kuwa na mchango katika kutatta matatizo ya jamii. Tuzo hii hutolewa kwa wagunduzi binafsi, kikundi au Taasisi.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi kinachoanzia Julai, 2010 hadi Juni, 2011, Tume imepokea jumla ya maombi 19 kwa ajili ya Tuzo za Kitaifa za Sayansi na Teknolojia. Mchanganuo wa Tuzo hizi ni kama ifuatavyo: Tuzo ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia (*TASTA*) maombi 15, Tuzo ya Utafiti wa Mawasiliano na teknolojia (*NARST*) ombi moja na Tuzo ya Utafiti na Hifadhi na Uendelezaji wa Mazingira (*NAEM*) maombi

matatu. Vilevile, wagunduzi wameendelea kushauriwa kujandikisha *BRELA* ili kulinda ubunifu wao na kupata Hakimiliki kwa ubunifu wao. Aidha, katika kipindi kilichoanzia Julai, 2010 hadi Juni, 2011, jumla ya maombi 22 yalipokelewa *BRELA* ya wagunduzi na watafiti mbalimbali wanaoomba hataza. Kati ya maombi hayo, 13 ni ya kutoka Tanzania katika Taasisi za Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo na Kampuni Binafsi. Aidha, maombi tisa yametoka nje ya nchi.

Mheshimiwa Spika, Serikali kwa kutambua umuhimu na kazi nzuri wanayofanya watafiti nchini, mishahara ya watafiti walio ndani ya Serikali Kuu, hususan katika Sekta za Kilimo na Mifugo, imeboreshwa kuititia Waraka wa Watumishi wa Serikali Na. 5 wa Mwaka 2010, ambao uliana kutekelezwa kuanzia tarehe 1 Julai, 2010.

Mheshimiwa Spika, kufuatia kukamilika kwa Awamu ya Kwanza ya ujenzi wa Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano mwezi Juni, 2010, ili kuimarisha huduma za mawasiliano ya simu, mitandao na posta ndani na nje ya nchi ili kuifanya Tanzania kuwa kitovu cha mawasiliano Kikanda, Wizara kwa kushirikiana na *TTCL*, imeanzisha Kitengo Maalum cha Kuendesha na Kuendeleza Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano (*NICTBB Unit*). Kitengo hiki kimewezesha utoaji wa huduma za Mkongo kwa watumiaji mbalimbali katika awamu ya Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano uliokamilika. Hadi sasa Kampuni za mawasiliano za *Zantel*, *SimbaNet*, *TTCL*, *AirTel*, *MTN – Zambia*, *Malawi Telecom* na *MTN Rwanda*, zimeunganishwa na zinatumia huduma ya Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano.

Mheshimiwa Spika, kuititia ushirikishwaji wa Sekta Binafsi katika kutoa huduma za TEHAMA, Kampuni za Simu za mkononi za *Airtel*, *Tigo* na *Zantel* zimeanzisha umoja (*Consortium of Operators*), kwa nia ya kujenga miundombinu ya TEHAMA yenye uwezo mkubwa wa Kimawasiliano (*Broadband*) katika maeneo ya miji (*Metro Networks*) ili kufikisha huduma za Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano kwa watumiaji wa mwisho (*Last Mile Connectivity*). Kampuni hizo zitaanza kujenga miundombinu hiyo katika Miji ya Dar es Salaam, Arusha, Mwanza na Dodoma.

Mheshimiwa Spika, katika kuongeza matumizi ya Mkongo na miundombinu mingine ya mawasiliano, Serikali imeamua kuunda Tume ya Kuendeleza TEHAMA. Andiko la kuanzisha chombo hiki lipo katika hatua za kufanyiwa maamuzi na Serikali, baada ya kupata maoni kutoka kwa Wadau wa Sekta ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano.

Mheshimiwa Spika, Shirika la Posta Tanzania (*TPC*), linaendesha ofisi 253 zinazotoa huduma kamili za Posta, ikiwa ni pamoja na utumaji na ulipaji wa fedha na shughuli za uwakala kwa niaba ya taasisi nyingine. Aidha, ofisi 145 kati ya hizo zinatoa huduma ya usafirishaji wa nyaraka, vifurushi na vipeto vya haraka ndani na nje ya nchi (*EMS courier*). Pia, huduma za intaneti zinatolewa katika ofisi 26 za posta nchini ikilinganishwa na kituo kimoja kilichokuwepo mwaka 2000. Vilevile, Shirika limeanzisha huduma mpya ya kusambaza kwa haraka nyaraka, vifurushi na vipeto kwa Ofisi za Serikali, Kampuni Binafsi na Taasisi kuititia huduma inayoitwa *City Urgent Mail*.

Mheshimiwa Spika, Vituo vya Posta 104, vinavyotoa huduma za kawaida za Posta vinaendeshwa na wakala katika juhudzi za kushirikisha Sekta Binafsi katika kutoa huduma za posta. Aidha, vibali 2,878 vimetolewa kwa wafanyabiashara kuwa Wakala wa Shirika katika kuuza stempu na shajala za posta.

Mheshimiwa Spika, katika utoaji wa huduma za fedha, Shirika la Posta Tanzania limeendelea kutoa huduma ya kupeleka fedha za wateja mbalimbali. Katika mwaka wa 2010, kiasi cha shilingi bilioni 43.5 zimepelekwa kwa wateja kupitia mtandao huu ikilinganishwa na shilingi bilioni 46.4 katika mwaka 2009. Kupungua kwa kiasi cha fedha kinachotumwa kupitia mtandao wa Posta, kumesababishwa na mambo mengi. Miiononi mwa hayo ni pamoja na Kampuni za Simu za Kiganjani kutoa huduma ya kutuma na kupokea fedha na hivyo kuongeza ushindani kwa Shirika la Posta na Taasisi nyingine zitoazo huduma hiyo. Pia, mtikisiko wa Kiuchumi ulioikumba Dunia hivi karibuni, umedhoofisha huduma za kifedha zilizokuwa zinatolewa na taasisi mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, Shirika la Posta Tanzania, linatekeleza Mradi wa *Counter Automation*, ambao umeunganisha Makao Makuu ya Shirika na Posta Kuu za Mikoa kwa lengo la kuboresha huduma zinazotolewa na Shirika. Mradi wa *Counter Automation* umeliwezesha Shirika kutumia TEHAMA katika kutoa huduma mtandao kama vile:-

- Kutuma fedha kwa kutumia mtandao wa kompyuta (*Posta Cash*);
- Kufuatilia mwenendo wa nyaraka, vifurushi na vipeto vya haraka kwa kutumia mtandao wa kompyuta (*Computerized Track and Trace*);
- Kupokea na kulipa fedha kwa niaba ya taasisi zingine kama vile Baraza la Mitihani Tanzania (*NECTA*);
- Kuuza hisa na kulipa magawio ya kampuni zilizosajiliwa katika soko la mitaji; na
- Kuimarisha mawasiliano na mifumo ya habari ndani ya Shirika.

Mheshimiwa Spika, Shirika linashirikishwa katika kutekeleza Mradi wa *Super-Computer* unaoratibiwa na Taasisi ya Teknolojia ya Dar es Salaam na ambao umezinduliwa tarehe 27 Mei, 2011. Mradi huu utalinufaisha Shirika katika kuendesha Vituo vya Mawasiliano ya Jamii (*Community Information Centres*), vitakavyotoa huduma mtandao ya *Tele-medicine*, *e-Government*, *e-Health*, *e-Learning*, *Internet* na *e-Commerce*.

Mheshimiwa Spika, Kampuni ya Simu Tanzania (*TTCL*), imejenga na kupanua mtandao wa mawasiliano (*Backbone Network Services*), wenye ubora wa hali ya juu unaotumia teknolojia ya kisasa ya *Next Generation Network (NGN)*. Kupitia mtandao huu, *TTCL* imeweza kutoa huduma za mawasiliano ya simu, *data* na video kwa pamoja.

Huduma hii imesambazwa katika Makao Makuu ya Mikoa yote ya Tanzania. Vilevile, zaidi ya asilimia 70 ya Makao Makuu ya Wilaya imeshafikiwa na huduma hii.

Mheshimiwa Spika, Kampuni pia imejenga mtandao wa kisasa wa simu za kiganjani (*TTCL Mobile*), unaotumia teknolojia ya *Code Division Multiple Access (CDMA)*. Katika kutekeleza shughuli hii, *TTCL* imejenga mtambo wenyewe uwezo (*capacity*) wa kubeba simu 250,000 za sauti na simu 15,000 za *data (EVDO)*. Hadi sasa, jumla ya wateja wa simu za kiganjani wapatao 120,000 wameunganishwa kwenye huduma hii ikilinganishwa na wateja 6,390 mwaka 2006 waliouanganishwa wakati huduma hii ilipoanzishwa.

Mheshimiwa Spika, Kampuni ya Simu Tanzania imepanua mtambo wa *broadband fixed broadband services* kufikia njia 29,000 kutoka njia 19,000 zilizokuwepo kabla ya upanuzi huu mwaka 2006, hili ni ongezeko la asilimia 65. Upanuzi huu umewezesha utoaji wa huduma bora zaidi wa haraka wa simu na intaneti katika sekta mbalimbali za kiuchumi, kiutawala na kijamii, hususan serikalini, kwenye mabenki, mashirika ya umma na taasisi za kimataifa. Huduma zinazotolewa kupitia mtandao huu ni pamoja na ile ya huduma za kibenki kupitia huduma za fedha (*Automatic Teller Machines - ATM*) na malipo ya huduma za umeme kupitia utaratibu wa Lipa Umeme Kadiri Utumiavyo (LUKU), ambazo zimeunganishwa kupitia mtandao huu wa Kampuni ya Simu Tanzania.

Mheshimiwa Spika, vilevile, *TTCL* kwa kutumia teknolojia ya *Asymmetric Digital Subscriber Lines (ADSL)*, inayotumia mtandao uliopo wa nyaya za shaba imewezesha upatikanaji wa huduma za kisasa za *broadband* na intaneti katika Miji Mikuu yote ya Mikoa. Kupitia teknolojia hii, hivi sasa *TTCL* inatoa huduma ya *data (broadband services)* na ya intaneti kwa gharama nafuu zaidi.

Mheshimiwa Spika, *TTCL* imejenga njia kuu (*backbone*) za *Digital Microwave* kwa kuweka mitambo mipyä ya *microwave radio* katika njia kuu za Dodoma -Mbeya kupitia Iringa na Nyololo; Mwanza – Kigoma – Bukoba na Mwanza - Musoma. Pia, *TTCL* imeweka mitambo mipyä ya *digital microwave* kati ya Dar es Salaam – Morogoro – Dodoma; Morogoro – Mikumi ikihusisha Mji wa Kilosa; Dar es Salaam – Tanga – Arusha; Mbeya – Sumbawanga; Shinyanga – Kahama na Mtwara – Masasi – Nachingwea. Hali kadhalika, mitambo ya *digital microwave* imewekwa kati ya Dodoma na Arusha kupitia Babati kama njia mbadala ya mawasiliano kwenda na kutoka Arusha. Maboresho haya yameiwezesha *TTCL* kukidhi mahitaji ya wateja na watumiaji katika njia kuu hizi.

Mheshimiwa Spika, *TTCL* imeboresha njia za mawasiliano Mjini Dar-es-Salaam kwa kuweka *optic fibre cable* Kunduchi na Kawe. Hii imerahisisha uunganishwaji wa mtandao wa *TTCL* na ule wa mkongo wa baharini wa *SEACOM*. Kupitia uunganishwaji huu, huduma za *TTCL* zimeboreshwa kwa kiwango kikubwa. *TTCL* inakamilisha taratibu za kuunganisha mtandao wake na mkongo wa baharini wa *EASSy*.

Mheshimiwa Spika, Wizara iliwezesha kuanzisha vituo vya mawasiliano katika maeneo ya Mrijochini – Kondoa – Dodoma, Bagamoyo – Pwani, Kilolo na Ludewa - Iringa, Wete – Pemba, Hai – Kilimanjaro, Isaka – Shinyanga, Ikungi – Singida, Masota ‘A’ Tegeta – Dar es Salaam, Namtumbo – Ruvuma, Rarya – Mara, Karagwe – Kagera, Masasi – Mtwara na Mpanda – Rukwa. Vituo hivi vimekuwa vikitoa huduma mbalimbali za TEHAMA (nukushi, kudurusu, picha, simu) sanjari na kutoa mafunzo ya TEHAMA kwa Wananchi wa maeneo hayo.

Mheshimiwa Spika, Wizara inaendelea kuhamasisha uanzishwaji na utumiaji endelevu wa vituo hivi ili viwe chachu ya kuwaendeleza Wananchi kiuchumi, kielimu na katika upatikanaji wa huduma nytingine za maendeleo. Aidha, rasimu ya mwongozo wa uanzishaji na uendeshaji wa vituo hivi imeandaliwa. Mwongozo huu unalenga kuvifanya vituo hivi kuwa vituo vya taarifa mbalimbali zikiwemo za elimu, kilimo, afya na serikali na hivyo kuvifanya viwe gurudumu la kuchochea kasi ya maendeleo ya kijamii, kiuchumi na kiutawala. Ili kufanikisha mkakati huu, vituo hivi kumi vya mfano vimepangwa kujengwa katika maeneo mbalimbali ili viweze kutumika kwa kuigwa katika maeneo mengine.

Mheshimiwa Spika, Mfumo wa Anuani za Makazi na Simbo za Posta ni moja ya utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Posta ya Mwaka 2003. Kukamilika kwa Mradi huu kutafanya kila Mwananchi, biashara, kampuni na taasisi itambulike kulingana na jengo na eneo ilipo. Mfumo huu utarahisisha ufikishaji wa huduma na utendaji wa shughuli mbalimbali za kijamii, kiuchumi na kiusalamu ikiwa ni pamoja na zoezi zima la utoaji wa Vitambulisho vya Taifa.

Utekelezaji wa Mradi huu chini ya uratibu wa Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania, ulianza kwa majoribio katika Kata saba za Manispaa ya Arusha (Kaloleni, Kati, Sekei, Lovolosi, Orelioni, Unga Limited na Thembi) na kuendelea katika Kata saba za Manispaa ya Dodoma (Kiwanja cha Ndege, Uhuru, Makole, Viwandani, Uhindini, Tambukareli na Kilimani).

Mheshimiwa Spika, Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI), inawasiliana na wadau mbalimbali ili kuwezesha upatikanaji wa fedha kwa ajili ya utekelezaji wa Mradi huu nchini. Aidha, Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania, inaendelea kutoa mafunzo kuhusu mfumo huu mpya wa anuani kwa Watendaji wa Serikali za Mitaa na wadau mbalimbali kwa ajili ya kuutekeleza Mradi huu Kitaifa.

Mheshimiwa Spika, Wizara kupitia Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania, inasimamia Sheria na Kanuni mbalimbali za Mawasiliano ili kuhakikisha kuwa, watumiaji wa huduma za Mawasiliano wanapata huduma bora. Sheria ya Mawasiliano ya Kielektroniki na Posta (*EPOCA*), ilitungwa mwaka 2010 ili kuboresha matumizi ya simu, kuzuia matumizi mabaya ya simu za viganjani na mitandao, kudhibiti uchafuzi wa mazingira, kudhibiti ongezeko la gharama za huduma za simu pamoja na kutambua mifumo mipy ya teknolojia ya utangazaji.

Hivi sasa, Kanuni za Sheria hiyo zimeandaliwa na inatarajiwa kuwa, Kanuni hizo baada ya kujadiliwa na wadau katikati ya mwezi Julai, 2011 zitaanza kutumika baada ya taratibu nyingine stahiki kukamiliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Mwaka wa Fedha wa 2010/2011, Wizara yangu imeendelea kutekeleza ahadi ilizotoa Bungeni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, katika Sekta ya Mawasiliano, Wizara imeendelea na juhudzi za kuimarisha mtaji wa Kampuni ya Simu Tanzania na Shirika la Posta Tanzania. Kwa upande wa Kampuni ya Simu Tanzania, juhudzi zinaendelea za kuwezesha Kampuni hiyo kupata mikopo kwa ajili ya kuendeleza biashara. Hii ni pamoja na kufanya tathmini ya hali ya Kampuni hiyo kifedha na fursa za kibiashara ilizonazo kwa lengo la kubaini uwezekano wa kukopa fedha kibiashara. Aidha, imeandaa utaratibu wa kulipa madeni ya simu ya Wizara na asasi zake kwa kupeleka moja kwa moja *TTCL* fedha inazodai toka katika kasma za Wizara/Asasi husika. Pia, Serikali imelipa kiasi cha shilingi milioni 791 kati ya shilingi bilioni 7.2 ya madeni ya *TTCL* kwa Taasisi na Idara za Serikali katika kutekeleza azma hiyo.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Shirika la Posta Tanzania, Serikali imelipa deni la mkopo wa Benki ya Maendeleo ya Afrika Mashariki (*EADB*) kwa Shirika la Posta la kiasi cha USD 786,615.87. Aidha, kiasi cha shilingi bilioni mbili kimerejeshwa katika Shirika la Posta, ikiwa ni sehemu ya malipo ya wastaafu wa lililokuwa Shirika la Posta na Simu la Afrika Mashariki (*EAP&TC*) yaliyofanywa na Shirika kwa niaba ya Serikali ili kupunguza deni linalolikabili Shirika.

Vilevile, mchakato wa kuwezesha Shirika la Posta kutafuta wabia kwa ajili ya kuendeleza viwanja vya Shirika na rasilimali nyingine kama njia mojawapo ya kutatua tatizo la mtaji unaendelea.

Mheshimiwa Spika, Wizara inaendelea kukamilisha taratibu na TANESCO ili kutumia Mkongo uliopo katika nyaya za umeme kati ya Tanga na Pemba na Makambako na Njombe kwa ajili ya kuziunganisha Pemba na Songea kwenye Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano. Kwa utaratibu huo huo, Zanzibar pia itaunganishwa kwenye Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano baada ya TANESCO kukamilisha uwekaji wa nyaya mpya za umeme kati ya Dar es Salaam na Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, Wizara imeanza uhamasishaji na uendelezaji wa Wataalam wa TEHAMA (*ICT Professionals*) katika Taasisi za Serikali na Sekta Binafsi ili kujenga rasilimali watu nchini, itakayowezesha kutumia fursa na rasilimali za TEHAMA vizuri na kwa manufaa zaidi. Kwa upande wa Serikali, Wizara kwa kushirikiana na wadau wengine wa TEHAMA, imekamilisha Muundo wa Utumishi wa Wateknohama ambao tunaamini utatoa fursa mahususi katika kuendeleza watumishi wa fani hiyo ambao ina jukumu kubwa sana katika maendeleo ya nchi yetu katika zama hizi za TEHAMA.

Mheshimiwa Spika, Wizara imekamilisha Andiko-Dhana (*Concept Paper*) la Mradi wa Ujenzi wa Kituo cha Kitaifa cha Kutunza Kumbukumbu za TEHAMA

(*Megadata Centre*). Aidha, Wizara imekamilisha mchakato wa utambuzi wa maeneo ya kujenga vituo vya kuendeleza sayansi, teknolojia na ubunifu vinavyoitwa *Science and Technology and Innovation Parks*. Vituo hivi vitajengwa Arusha, Mwanza na Mbeya kama vituo vya majaribio. Aidha, Serikali imeanza kutekeleza utekelezaji Mradi wa Habari Jamii (*Information Society and ICT Sector Development*), kwa ushirikiano na Serikali ya Finland. Pamoja na kushughulikia masuala ya Sera za TEHAMA, Mradi huu utajielekeza pia katika kuendeleza ubunifu na kujenga uwezo wa kitaasisi wa kusimamia masuala ya teknolojia ya habari na mawasiliano.

Mheshimiwa Spika, Wizara imewapandisha vyeo watumishi kumi na moja wa kada mbalimbali kwa kuzingatia sifa na vigezo vilivyoko katika Waraka wa Maendeleo ya Utumishi wa Mwaka 2002, pamoja na kuwa na utendaji mzuri wa kazi kwa mujibu wa tathmini ya utendaji kazi (*OPRAS*).

Mheshimiwa Spika, Wizara imeratibu mafunzo mbalimbali ndani na nje ya nchi kwa kuwapeleka watumishi ishirini kwenye mafunzo ya muda mrefu; ambapo kati ya hao, watumishi kumi na sita wamehudhuria mafunzo ndani ya nchi na wanne nje ya nchi.

Mheshimiwa Spika, pamoja na uandaaji wa sera mbalimbali nilizozitaja hapo awali, Wizara imeandaa Mpango wa Utekelezaji wa Ilani ya CCM kwa kipindi cha 2010-2015 ambao umewasilishwa Ofisi ya Waziri Mkuu. Aidha, Wizara imeratibu na kukamilisha uandaaji wa Mpango Kabambe wa Maendeleo ya Sekta ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia (*Communication, Science and Technology Master Plan*) na pia kuendelea kufuatilia utekelezaji wa Miradi iliyo chini ya Wizara na Taasisi zake.

Mheshimiwa Spika, Wizara imeendelea kuhamasisha watumishi kujikinga na kuepuka maambukizi mapya ya UKIMWI, upimaji wa UKIMWI kwa hiari, matumizi ya dawa za kurefusha maisha kwa waishio na Virusi vya UKIMWI na kupunguza maambukizi ya UKIMWI kutoka kwa mama kwenda kwa mtoto. Aidha, Wizara imeendelea kuelimisha watumishi ili wale waliopata maambukizi waweze kujitokeza na kupatiwa huduma kwa mujibu wa Waraka wa Utumishi wa Serikali Na. 2 wa Mwaka 2006.

Mheshimiwa Spika, Wizara imeendelea kuratibu na kufanya ukaguzi wa matumizi ya fedha za Wizara na Taasisi zilizo chini yake kwa lengo la kuongeza ufanisi wa utendaji kazi na kuwa na matokeo mazuri na yenye tija kwa Taifa. Aidha, Wizara imeendelea kushirikiana na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali katika masuala yote yanayohitaji ushauri wa kisheria ikijumuisha masuala ya Mikataba, Miswada, Sheria Ndogo Ndogo, Kanuni na Mashauri mbalimbali yanayohusu Wizara au Taasisi zake. Vilevile, Wizara imeandaa taarifa ya mashauri yanayohusu Wizara au Taasisi zilizo chini ya Wizara kwa lengo la kuzifuatilia kwa karibu.

Mheshimiwa Spika, Wizara imeendelea kuelimisha umma na wadau mbalimbali kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara, ambapo nakala 5,000 za vipeperushi kuhusu Sera za Wizara, Ujenzi wa Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano, Ujenzi wa Taasisi ya Sayansi na Teknolojia ya Nelson Mandela-Arusha, uanzishwaji wa Mfuko wa

Mawasiliano kwa Wote, Tume ya Nguvu za Atomiki Tanzania, Vituo vya Mawasiliano pamoja na elimu kuhusu Dira, Dhima na Majukumu ya Wizara, vimeandaliwa na kusambazwa kwa wadau mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, katika kuwapata wazabuni wa kutoa huduma mbalimbali kwa mujibu wa Sheria ya Ununuzi Namba 21 ya Mwaka 2004, Kifungu Namba 35, shughuli zote za Ununuzi na Ugavi zimesimamiwa kwa kushirikiana na Wakala wa Ununuzi na Ugavi wa Serikali (*GPSA*). Aidha, ununuzi wa bidhaa na huduma umezingatia taratibu hizo.

Mheshimiwa Spika, Taasisi ya Teknolojia ya Dar es Salaam. Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam (*DIT*), ilidahili jumla ya wanafunzi 1,505 katika Programu za *IT Basic Certificate* (182), Diploma katika fani mbalimbali (825) na *Bachelor of Engineering* (498) na hivyo kufanya jumla ya wanafunzi wote katika mwaka 2010/2011 kuwa 2,555. Idadi hii ya wanafunzi ni ongezeko la asilimia 70 ikilinganishwa na mwaka 2009/2010. Aidha, baada ya mafunzo ya awali (*Pre-entry Training*) yaliyoendeshwa kuanzia mwezi Juni hadi Septemba, 2010, jumla ya wanafunzi 44 walifaulu na kudahiliwa kati ya wanafunzi wa kike 68 waliofanya mafunzo hayo.

Mheshimiwa Spika, Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam imepeleka wafanyakazi 20 katika masomo ya juu. Kati ya hao, wakufunzi ni 11 na wafanyakazi waendeshaji ni tisa. Wakufunzi wanne ni kwa ajili ya shahada ya uzamivu, sita ni kwa ajili ya shahada ya uzamili na mmoja shahada ya kwanza. Aidha, kati ya wafanyakazi tisa waendeshaji, mmoja anasoma shahada ya uzamivu, wawili shahada ya uzamili, mmoja shahada ya kwanza na watano stashada. Aidha, Taasisi imeendelea kugharimia wafanyakazi 48 wanaoendelea na masomo ya juu ndani na nje ya nchi.

Mheshimiwa Spika, awamu ya kwanza ya ujenzi wa Jengo la *DIT Teaching Tower* lenye madarasa, maabara na ofisi za wafanyakazi, umekamilika na Taasisi imekabidhiwa. Matayarisho ya nyaraka za Mshauri Mwelekezi wa ujenzi kwa ajili ya awamu ya pili yameanza. Kwa upande wa Kampasi ya Mwanza, matayarisho kwa ajili ya ukarabati wa majengo na miundombinu ya maji, umeme na mawasiliano ya iliyokuwa Taasisi ya Teknolojia za Ngozi Mwanza yanaendelea ili hatimaye iweze kutoa mafunzo katika taaluma ya ngozi katika ngazi mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, Taasisi imepata kandarasi kutoka *TANROADS* ya kufanya matengenezo taa za kuongoza magari barabarani Jijini Dar es salaam. Pia, Taasisi imepata kandarasi ya ujenzi na usimikaji wa taa za kuongoza magari katika makutano ya Barabara ya Nyerere na Msimbazi, Dar es Salaam.

Mheshimiwa Spika, Taasisi ya Sayansi na Teknolojia Mbeya (*MIST*), imeongeza idadi ya wanafunzi kutoka wanafunzi 1,242 Mwaka wa Fedha wa 2009/2010 hadi kufikia wanafunzi 1,757 kwa Mwaka wa Fedha wa 2010/2011, sawa na ongezeko la asilimia 41.5. Aidha, idadi ya wanafunzi wa kike imeongezeka kutoka wanafunzi 105 mwaka 2009/2010 hadi kufikia wanafunzi 162 kwa Mwaka wa Fedha 2010/2011. Hili ni ongezeko la asilimia 54.3.

Mheshimiwa Spika, idadi ndogo ya wanafunzi wa kike katika masomo ya Sayansi bado ni changamoto. Taasisi imeendelea kutoa mafunzo ya awali (*pre-entry training*) kwa wanafunzi wa kike katika masomo ya sayansi, uhandisi na teknolojia. Jumla ya wanafunzi wa kike 43, sawa na asilimia 122.9 ya lengo wamedahiliwa kwa kupitia mpango huo. Taasisi itaendelea na mpango huu ambaeo umeanza kuonesha mafanikio ili kuongeza idadi ya wanafunzi wa kike katika fani za Sayansi na Teknolojia.

Mheshimiwa Spika, Taasisi imefanikiwa kuanzisha mafunzo ya fani ya Sayansi na Teknolojia ya Maabara na mafunzo yanatolewa katika ngazi ya stashahada. Kwa mwaka wa masomo wa 2010/2011, jumla ya wanafunzi 51 wa fani hii wamedahiliwa. Kati ya wanafunzi hawa, 37 ni wanafunzi wa kiume na 14 ni wanafunzi wa kike.

Mheshimiwa Spika, ujenzi wa majengo mawili ya mabweni ya wanafunzi yenye uwezo wa kulaza wanafunzi 350 kila moja unaendelea vizuri. Hatua iliyofikiwa sasa ni kupaka rangi, kuweka mfumo wa umeme, kufunga vioo katika madirisha, kukamilisha mfumo wa maji taka pamoja na kuweka mazingira nadhifu kwa kupanda miti na bustani katika eneo linalozunguka majengo haya.

Mheshimiwa Spika, Taasisi imeendeleza uhusiano na Taasisi mbalimbali za Sayansi na Teknolojia. Katika kipindi cha mwaka huu, Taasisi imesaini hati ya makubaliano na *Lilongwe Technical College (LTC)* iliyopo nchini Malawi. Aidha, Taasisi ni Mwanachama wa Muungano wa Vyuo vya Ufundsi Katika Nchi za Jumuiya ya Madola (*Commonwealth Association of Polytechnics in Africa - CAPA*) na *African Network of Science and Technology Institution – ANSTI*. Taasisi hii ni muungano wa vyuo vinavyofundisha taaluma mbalimbali za sayansi na teknolojia katika Bara la Afrika yenye Makao Makuu yake Nairobi, Kenya.

Mheshimiwa Spika, Taasisi ya Sayansi na Teknolojia ya Nelson Mandela – Arusha (*NM-AIST*), katika kujipanga kuanza kutoa mafunzo mwaka 2011/2012 imeajiri watumishi 76. Kati ya hao, watumishi 26 ni wanataaluma na watumishi 50 ni waendeshaji. Aidha, Taasisi imeandaa rasimu ya *Charter* na miongozo mingine ambayo inasubiri kuundwa kwa Baraza la Taasisi na Kamati Kuu ya Taaluma (*Senate*) ili iweze kujadiliwa hatimaye kupitishwa.

Mheshimiwa Spika, Taasisi imeshirikiana na Taasisi na Vyuo Vikuu vya ndani na nje ya nchi katika kuandaa mitaala na kupanga mifumo ya maabara. Aidha, Taasisi imevitembelea baadhi ya vyuo maarufu vya Sayansi na Teknolojia katika nchi za Marekani, China, Korea, India na Saudi Arabia, ambavyo vimeonesha nia ya kushirikiana na Taasisi ya Sayansi na Teknolojia ya Nelson Mandela katika kufundisha na kufanya utafiti.

Mheshimiwa Spika, ili kupata maji kwa kiwango kinachohitajika, Taasisi imechimba visima viwili vya maji. Kisima kimoja kina uwezo wa kutoa maji kiasi cha mita za ujazo 33 kwa saa na kingine kina uwezo wa kutoa mita za ujazo 13 kwa saa.

Aidha, kazi ya kuongeza msongo wa umeme kutoka 11 kV na kuwa 33 kV kukidhi mahitaji ya Taasisi inashughulikiwa na *TANESCO*.

Mheshimiwa Spika, Tume ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia (*COSTECH*), ikishirikiana na wadau wa utafiti ilibainisha maeneo matano ya kipaumbele ya fedha za utafiti ili kuendeleza mikakati ya Kilimo Kwanza kama ifuatavyo:-

- (a) Utafiti utakaosaidia kupata njia bora ya kuhamasisha matumizi ya pembejeo za kilimo kwa watu wengi zaidi;
- (b) Utafiti utakaosaidia kuongeza thamani ya mazao ya Kilimo;
- (c) Utafiti wa kupata taarifa juu ya mnyororo wa thamani (*value chain*) wa mazao ya kilimo;
- (d) Kuhawilisha teknolojia zilizofanyiwa utafiti ili ziweze kutumika na watu wengi zaidi; na
- (e) Tafiti zitakazosaidia kujua ubora wa teknolojia.

Mheshimiwa Spika, Tume ilikaribisha mapendekezo ya tafiti ya awali (*research concept notes*) katika Sekta za Kilimo, Mifugo na Uvuvi kutoka katika Taasisi na Vyuo Vikuu nchini. Kupitia mwito huo, *Concept Notes* 360 zilipokelewa na baada ya kuchambuliwa na wataalamu, 106 zilipitishwa kwa ajili ya kutengeneza maandiko kamili ya tafiti (*Full Proposals*). Mchakato wa kupitia maandiko ya tafiti hizi umekamilika na kuingia hatua ya kuchagua tafiti zilizo bora kwa ajili ya kupatiwa mwega. Matokeo ya mchakato huu yatatangazwa kwa wanasayansi na watafiti kwenye vyombo vya habari hivi karibuni ili shughuli za utafiti ziweze kuanza.

Mheshimiwa Spika, Tume imetengeneza Mwongozo wa Kutoa Mwega (*Grants Manual*) na kuusambaza kwenye taasisi za utafiti, vyuo vikuu na wadau wengine. Pia, Tume imenunua programu ya kompyuta ili kuimarisha mfumo wa kupokea maombi kupitia mtandao wa kompyuta (*internet*). Aidha, Tume imeingiza kwenye Daftari la Hati Miliki aina ishirini za mazao mbalimbali yalizozalishwa na taasisi za utafiti wa kilimo na taratibu za usambazaji wake zinaendelea. Hati Miliki hizo ziko kwenye mazao ya kahawa, mahindi, maharage na soya.

Mheshimiwa Spika, Tume imetumia jumla ya shilingi bilioni 5.2 kufadhili wanasayansi 202 kutoka taasisi za utafiti na vyuo vikuu kwa ajili ya masomo kwenye ngazi ya uzamili (144) na uzamivu (58) katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (55), Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (116), Chuo Kikuu cha Sayansi za Afya cha Muhimibili (23) na Chuo Kikuu cha Ardhi (10).

Mheshimiwa Spika, Tume imefadhili ujenzi wa maabara katika Taasisi ya Taifa ya Utafiti wa Magonjwa ya Binadamu (*NIMR*) Tabora na kununua vipima mionzi (*radiation meter*) katika Tume ya Nguvu za Atomiki Tanzania (*TAEC*) na vifaa vya maabara kwa ajili ya Taasisi ya Utafiti wa Tiba Asilia ya Muhimbili (*Institute of Traditional Medicine*). Aidha, Tume imekusanya taarifa ya hali ya miundombinu na vitendea kazi katika taasisi za utafiti na vyuo vikuu ambapo taarifa hizi zitatumika katika kuboresha miundombinu na vitendea kazi katika taasisi na vyuo hivyo.

Mheshimiwa Spika, Tume imesajili miradi ya utafiti 273 ya watafiti kutoka katika nchi 25 za Amerika, Ulaya, Asia na Afrika wakishirikiana na watafiti wa hapa nchini. Miradi ya tafiti hizo imelenga katika maeneo ya afya, sayansi ya asili, sayansi jamii, wanyama pori, historia, uchumi na kadhalika. Aidha, Tume imeanza kusajili tafiti zinazofanywa na taasisi za utafiti nchini kwa kuanzia na Sekta za Kilimo, Mifugo na Afya.

Mheshimiwa Spika, Tume pia ikishirikiana na vyuo vikuu na taasisi za utafiti, imeanzisha mtandao unaouunganisha vyuo na taasisi hizi kurahisisha upatikanaji wa taarifa za utafiti baina yao na wadau wengine. Aidha, mtandao huu umeunganishwa na mtandao wa vyuo vikuu vingine vya Ulaya na Marekani kwa malengo ya kukuza mawasiliano na ushirikiano katika masuala ya utafiti baina yao.

Mheshimiwa Spika, Tume ikishirikiana na Benki ya Dunia, kupitia Mradi wa *Info Dev*, imeanzisha Atamizi ya TEHAMA (*ICT Incubator*) kwa ajili ya kukuza ujasiri amali katika Teknolojia ya Habari na Mawasiliano. Atamizi hii itatoa ushauri wa teknolojia, mafunzo ya biashara kwa wajasiri amali wanaokusudia kuanzisha kampuni za biashara ya TEHAMA ili waweze kujiajri wenye na pia wale wenye kampuni hizo kuweza kuongeza ufanisi na kupata teknolojia mpya.

Mheshimiwa Spika, Tume kwa kushirikiana na Shirika la Misaada la Sweden, imeanza kuratibu shughuli za Kongano (*Clusters*) 19 katika mikoa 12. Kongano zinazoratibiwa kwa utaratibu huu, zinajishughulisha na mambo ya uhandisi, usindikaji wa mazao na matunda, utalii, uchimbaji wa madini chini ya wachimbaji wadogo wadogo, kilimo cha mwani, uyoga, mihogo na wabunifu wa sanaa za mikono. Kongano zinawezesha wataalamu wa vyuo vikuu na vituo vya utafiti, kufanya kazi karibu na wajasiri amali katika kutoa mafunzo na katika upatikanaji wa teknolojia zinazoongeza ufanisi na uzalishaji wa wajasiri amali walio kwenye kongano hizo.

Mheshimiwa Spika, Tume ya Nguvu za Atomiki (*TAEC*), katika kutekeleza moja ya jukumu lake kuu, ilipima jumla ya sampuli 19,921 za vyakula na mbolea ambapo hakuna sampuli iliyoonekana kuwa na kiwango kikubwa cha mionzi. Vile vile, kaguzi 39 zilifanywa bandarini, mipakani na kwenye viwanja vya ndege katika sehemu za kuingia/kutoka (*entry/exit points*) nchini ili kuhakikisha kuwa waingizaji wote wa bidhaa za vyakula wanazingatia Sheria na Kanuni za Kinga ya Mionzi. Aidha, upimaji wa mionzi (*Personal Dosimetry*), ulifanywa kwa wafanyakazi 1,032, ambao ni sawa na asilimia 86 ya wafanyakazi waliolengwa kupimwa katika vituo 119 vilivyokaguliwa. Pia, mabaki 45 ya vyanzo vya mionzi yamekusanya kwa kipindi cha miaka mitano kati ya

2005 na 2010 na kufanya jumla ya mabaki yote yaliyokusanya na kuhifadhiwa na Tume kufikia 70. Katika Mwaka wa Fedha 2010/2011, chanzo kimoja kilikusanya kutoka Dodoma.

Mheshimiwa Spika, Tume iliratibu misaada kwa Taasisi nane za Kitaifa kupitia Miradi ya Kitaifa na Kikanda (*AFRA*), inayogharamiwa na Shirika la Kimataifa la Nguvu za Atomiki (*International Atomic Energy Agency*).

Mheshimiwa Spika, Tume imewapeleka wataalamu wawili kwenye mafunzo ya shahada ya uzamili na kuendelea kumsomesha mfanyakazi mmoja kwenye mafunzo ya shahada ya uzamivu. Mafunzo mengine ya kitaalamu yanaendelea kutolewa kwa kushirikiana na wadau mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, Tume iliendesa jumla ya semina 19. Kati ya hizo, semina tatu zilifanywa kwa watumiaji wa mionzi (*Radiographers*), semina saba zilikuwa za mafunzo ya ufundi, semina mbili kwa ajili ya wafanyakazi katika migodi, semina sita kwa ajili ya watumishi walio mstari wa mbele (hasa Polisi), katika kushughulikia dharura za mionzi na semina moja kwa ajili ya Baraza la Mazingira la Taifa (*NEMC*). Aidha, Tume imesimamia na kufanya utafiti katika Wilaya ya Namtumbo ili kuona athari ya madini ya urani kwa mimea, maji na mazingira. Pia, Tume kwa kushirikiana na Wizara imeandaa kanuni tatu zinazohusu uchimbaji wa urani, usalama wa usafirishaji wa vyanzo vya mionzi na ada mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha wa 2010/2011, Shirika la Posta Tanzania, limeongeza vituo vya posta nchini kutoka vituo 358 hadi kufikia vituo 372, sawa na ongezeko la asilimia 3.9. Pia, vibali vya kuuza stempu vimeongezeka kutoka vibali 2,878 hadi 3,064, sawa na ongezeko la asilimia 6.4. Aidha, Vituo vya Intaneti vimeongezeka kutoka 23 hadi 29, sawa na ongezeko la asilimia 26.

Mheshimiwa Spika, Shirika la Posta Tanzania, linaendelea kuongeza na kuimarisha matumizi ya TEHAMA katika huduma zinazotolewa na Shirika. Hadi sasa, Ofisi za Posta zilizounganishwa katika mtandao wa kielectroniki zimeongezeka kutoka ofisi 14 mwaka 2009 hadi kufikia 30 mwaka 2011, sawa na ongezeko la asilimia 114. Huduma nyingine za kielektoniki zinazotolewa ni pamoja na *Electronic Money Transfer*, *Track and Trace* na *Management Information Systems (MIS)*. Aidha, vituo saba vilivyouniganishwa ki-elektroniki kupitia Mradi wa *India – Tanzania Centre of Excellence in ICT* wa Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam, vinatarajia kuanza kutoa huduma mbalimbali za TEHAMA kuanzia mwezi Oktoba, 2011.

Mheshimiwa Spika, Shirika limefanya matengenezo ya majengo ya Ofisi za Posta Kuu za Dar es Salaam, Shangani, Chakechake, Mwanza, Singida na Musoma. Matengenezo hayo yamefanyika katika viwango tofauti.

Mheshimiwa Spika, Shirika limetoa mafunzo katika kozi mbalimbali kwa lengo la kuboresha huduma zake kama ifuatavyo: Uendeshaji wa posta watumishi (14); huduma

kwa wateja watumishi (60); TEHAMA watumishi (60) na utoaji wa huduma za posta kwa watumishi (80).

Mheshimiwa Spika, Kampuni ya Simu Tanzania (*TTCL*), imepitia upya Mpango Mkakati wake ili kujielekeza kuwekeza zaidi kwene huduma za Intaneti (*data*) ikilinganishwa na simu za kiganjani. Malengo ya Kampuni kwa upande wa simu za kiganjani yamepitwa upya ili kuongeza wateja kulingana na mahitaji ya soko la sasa.

Mheshimiwa Spika, *TTCL* inaendelea na uendeshaji wa sehemu ya Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano uliokamilika. Hadi sasa Kampuni kubwa za simu za ndani na nje ya nchi zimeunganishwa kwene Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano. Kampuni hizo ni *Airtel Tanzania, Simbanet, TTCL, Zantel, Malawi Telecom, MTN Zambia* na *MTN-Rwanda Telecom*.

Mheshimiwa Spika, Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (*TCRA*), imeandaa mikutano minne iliyowashirikisha watoa huduma ya utangazaji kuhusu mabadiliko ya mfumo wa utangazaji kutoka analogia kwenda digitali. Kwenye mikutano hiyo, majadiliano ya kina yamefanyika ili kukabiliana na changamoto zinazojitokeza katika utekelezaji wa kujenga miundombinu ya utangazaji wa mfumo mpya. Maandalizi ya Kampeni ya Kitifa ya kuhamasisha umma juu ya mabadiliko ya mfumo wa utangazaji yamekamilika na kampeni hizo zitaanza kwa nguvu zaidi katika Mwaka wa Fedha wa 2011/12.

Mheshimiwa Spika, Mamlaka imeanza kuratibu uandaaji wa Kanuni zitakazowataka watoa huduma za mawasiliano ya intaneti na maudhui (*Content*), kujiunganisha na *IXP* yoyote iliyo karibu nao. Madhumuni ya kuanzishwa kwa utaratibu huu ni kuimarisha usimamizi na uthibiti kwa watoa huduma za intaneti ili waweze kuzingatia maadili kulingana na kanuni zinazotolewa kwa utoaji wao wa huduma. Aidha, Mamlaka imenendelea kutoa elimu kwa watoa huduma za Mawasiliano ya intaneti na maudhui juu ya manufaa ya kujiunganisha na *IXPs*. Vilevile, Mamlaka imeanza kuratibu majadiliano na wadau juu ya kuziunganisha *IXPs* moja kwa moja kutumia Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano.

Mheshimiwa Spika, Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania, imenendelea kupokea na kutathmini maombi ya leseni na kutoa leseni kwa makampuni yaliyosajiliwa. Jumla ya Leseni 72 zilitolewa kuanzia mwezi Julai, 2010 hadi mwezi Juni, 2011. Mchanganuo wa leseni hizo ni kama ifuatavyo: Leseni ya kujenga miundombinu ya mawasiliano (*Network Facilities*) leseni tano; leseni ya kutoa huduma za mawasiliano (*Network Services*) leseni moja; leseni za huduma za ziada za mawasiliano (*Application Services*) leseni moja; leseni ya utangazaji (*Content Services*) leseni 13; leseni ya usafirishaji wa vifurushi katika miji ndani ya nchi (*Intercity Courier*) leseni mbili; leseni ya ufungaji na matengenezo ya vifaa vya mawasiliano (*Installation and Maintenance*) leseni 21; leseni ya uagizaji na usambazaji wa vifaa vya mawasiliano (*Importation and Distribution*) leseni 15; na leseni ya huduma za satelaiti (*V-SAT licences*) leseni 14.

Mheshimiwa Spika, Mamlaka imeendelea kuelimisha watumiaji wa huduma za mawasiliano kuhusu taratibu za kuwasilisha malalamiko yao kwa mamlaka pale ambapo hawakuridhika na huduma. Katika kutekeleza azma hii, jumla ya vipindi 18 vya televisheni na 26 vya redio vimerushwa hewani. Aidha, Mamlaka imeendesha semina za kuelimisha watumiaji wa huduma za mawasiliano katika Wilaya 14 (Rufiji, Kisarawe, Mkuranga, Kibaha, Bagamoyo, Namtumbo, Songea Mjini, Songea Vijijini, Nyasa, Lushoto, Mbanga, Karatu, Kiteto na Lushoto); Vyuo vitano (Ukutubi Bagamoyo, Maendeleo ya Wananchi Kisarawe, Maendeleo ya Wananchi Rufiji, VETA Songea na TEHAMA Ruhuwiko) na Shule za Sekondari nne za Makita (Namtumbo), Pamoja - Namtumbo, Namabengo na Sekondari ya Wavulana Songea.

Vile vile, Mamlaka imetua vipeperushi na machapisho mbalimbali yenye kuelimisha watumiaji. Kutokana na uelimishaji huu na milango kuwa wazi, Mamlaka imepokea na kuyashughulikia kikamilifu malalamiko 79 na kuyatolea maamuzi. Kati ya hayo, malalamiko matatu yamekatiwa rufaa.

Mheshimiwa Spika, Mamlaka inaendelea kusimamia Mradi wa Anuani Mpya za Makazi na Simbo za Posta (*Postcode Project*), ambao umeanza kutekelezwa katika Manispaa ya Arusha na Dodoma. Utekelezaji huu pia umehusisha utoaji wa mafunzo ya kutekeleza Mradi huu yaliyofanyika katika Majiji, Manispaa na Halmashauri za Mwanza, Tanga, Arusha, Dodoma, Moshi, Morogoro, Kigoma Ujiji, Lindi, Ukerewe na Tandahimba. Utoaji wa mafunzo hayo na uhamasishaji umefanyika pia Zanzibar. Mafunzo haya yalilenga kuwezesha Mamlaka za Serikali za Mitaa kutekeleza Mradi huu kupitia bajeti zao. Aidha, mipango inaendelea ili kutekeleza Mradi huu katika Jiji la Dar es Salaam na Manispaa ya Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, Bodi ya Mfuko imepitisha Muundo wa Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote (*UCAF*), kama unavyotakiwa kisheria na nafasi za kazi zimetangazwa. Mchakato wa ajira unategemea kukamilika mwezi Agosti, 2011.

Mheshimiwa Spika, Mfuko umebainisha maeneo yasiyo na mvuto kibiashara na kwa kushirikiana na Kampuni za Simu nchini, wameainisha maeneo ya kutekeleza Miradi kwa Majaribio (*Pilot Project*), kabla ya kuanza utekelezaji wa Miradi mikubwa. Aidha, zabuni kwa ajili ya kutekeleza Miradi ya Majaribio itatangazwa baada ya kupata ridhaa ya Benki ya Dunia ambayo inafadhili Miradi ya Majaribio.

Mheshimiwa Spika, Mfuko uko kwenye mazungumzo na Shirika la Posta Tanzania kuhusu uanzishwaji wa huduma za Posta katika maeneo ya vijijini na yasiyokuwa na mvuto kibiashara. Aidha, Shirika limeukabidhi Mfuko andiko la Miradi ya Mawasiliano ya Posta Vijijini kwa majadiliano ya utekelezaji. Mfuko unakamilisha taratibu za kulipitia andiko hilo kuwezesha utekelezaji.

Mheshimiwa Spika, kwa mwaka 2010/2011, pamoja na mafanikio yaliyopatikana, Wizara imekabiliwa na changamoto kadhaa ambazo zilichangia katika kutofikia malengo kulingana na mpango.

Mheshimiwa Spika, changamoto moja kubwa kwenye sekta hii ni shughuli za Utafiti na Maendeleo (*Research and Development – R&D*), kutotengewa fedha za kutosha. Upungufu huu wa fedha umeendelea kuathiri ufanisi wa shughuli za utafiti na maendeleo. Katika Bajeti ya Mwaka wa Fedha wa 2010/2011, zilitengwa shilingi bilioni 30 kwa ajili ya shughuli za utafiti. Hata hivyo, hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2011 Wizara imepokea kiasi cha shilingi bilioni 19. Ili kukabiliana na changamoto hii, Serikali na Asasi za Utafiti zimeendelea kutumia njia nyingine kufadhili utafiti, ikiwa ni pamoja na kushirikiana na Mashirika ya Nje na Sekta Binafsi kuchangia shughuli za utafiti. Aidha, Sera ya Taifa ya Utafiti na Maendeleo, iliyoanza kutumika, inabainisha vivutio kwa Sekta Binafsi kwenye utafiti ikiwa ni pamoja na Sekta hiyo kuthamini na kutumia matokeo ya utafiti.

Mheshimiwa Spika, uhaba wa wataalam katika nyanja mbalimbali umeathiri mafanikio ya sekta. Aidha, changamoto kubwa katika eneo hili ni pamoja na kuwa na idadi ndogo ya wataalam wa TEHAMA, ikilinganishwa na mahitaji, wataalam wengi watafiti kuwa wa umri mkubwa, wataalam kutokuwa na uelewa wa teknolojia mpya na uwiano baina ya wataalam mbalimbali (kama vile uwiano wa wahandisi na mafundi wa ngazi ya cheti na diploma) kutokuwa mzuri. Wizara, kupitia Sera ya Utafiti na Maendeleo, inaandaa mikakati ya muda mfupi na mrefu ili kupata ufumbuzi wa kudumu kukabiliana na changamoto hii.

Mheshimiwa Spika, Taasisi zinazohudumia Sekta ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia ziko katika hatua ya kujijenga ama katika hatua za kuanzishwa (kama vile Taasisi ya Sayansi na Teknolojia ya Taasisi ya Nelson Mandela na Taaluma za Ngozi cha Mwanza) au kuwa katika hatua ya kujipanua kukidhi mahitaji ya soko kama ilivyo kwa MIST na DIT, ambazo zinaongeza michepuo na udahili na hivyo kuwa na mahitaji ya miundombinu mipyä na kuongezewa bajeti zao. Aidha, bado lipo hitaji la kuzijenga taasisi hizi kuwa imara na kujenga nyingine ili kuharakisha maendeleo ya sayansi na teknolojia nchini. Kama ilivyo kwa shughuli za utafiti, njia ambayo Wizara imeendelea kutumia kukabiliana na changamoto hii ni pamoja na kubuni njia mbadala za kupata fedha ikiwa ni pamoja na kushirikisha wadau wa maendeleo kutoa misaada na pia mikopo ya ndani na nje ya nchi.

Mheshimiwa Spika, kwa ujumla, Wizara bado inakabiliwa na changamoto ya kupata fedha za kutosha ili kutekeleza majukumu yake ya msingi. Uhaba unajidhihirisha katika matumizi mengineyo na matumizi ya fedha za maendeleo. Uhaba wa fedha za Maendeleo umeathiri ujenzi wa Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano, ikiwa ni pamoja na ugomboaji wa vifaa bandarini vinavyohitajika katika kazi ya ujenzi.

Vilevile, utekelezaji wa Mradi wa Mfumo wa Anuani za Makazi na Simbo za Posta ambao una malengo yanayoendana na yale ya mradi wa utoaji wa Vitambulisho vya Kitaifa, nao umeathirika kutokana na uhaba wa fedha za maendeleo. Kukamilika kwa Mradi huu, kutaongeza uwezo wa Serikali katika ukusanyaji wa mapato, hususan kodi za majengo, jambo ambalo litaiiongezea Serikali uwezo wa kifedha na hivyo kuchochea kasi ya maendeleo ya nchi.

Mheshimiwa Spika, pamoja na changamoto nilizozieleza hapo juu, Wizara itajitahidi kutekeleza majukumu yake ili kuwezesha upatikanaji wa miundombinu bora itakayowezesha uendelezaji wa Sekta ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia nchini. Hatua hii itawezesha kuwa na jamii yenyе rasilimali watu wenye uwezo na maarifa ya kuibua vipaji vipyा na fursa mpya za kuleta maendeleo ili kuliondoa Taifa katika umaskini.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2011/2012 Wizara yangu kupitia Idara na Taasisi zake imejiwekea malengo mbalimbali kwa kuzingatia Mpango wa Maendeleo ya Taifa na Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi kwa mwaka 2010 – 2015 kama yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, katika nyanja za mawasiliano, Wizara itaendelea kushauri na kusimamia utendaji kazi wa Kampuni ya Simu Tanzania, Shirika la Posta Tanzania, Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania na Mfuko wa Mawasiliano kwa wote. Pia, Wizara itaendeleza juhudhi za kuwezesha upatikanaji wa mitaji kwa Kampuni ya Simu Tanzania na Shirika la Posta Tanzania.

Mheshimiwa Spika, ili kuongeza ufanisi, uratibu na kuchochea ubunifu na ujasiriamali katika eneo la TEHAMA, Wizara itaendeleza na kukamilisha mchakato wa kuanzisha Tume ya TEHAMA. Pamoja na mambo mengine, Tume hii itaratibu shughuli za maendeleo ya TEHAMA, taaluma na wataalamu wa TEHAMA, usalama na uhifadhi wa mazingira katika nyanja za TEHAMA. Vile vile, Wizara itaendelea kuratibu mpango wa kuanzisha na kuendeleza Vituo vya Mawasiliano ya Kijamii nchini kwa kushirikiana na wadau na Taasisi mbalimbali za Kitaifa na Kimataifa.

Mheshimiwa Spika, Wizara itasimamia uhuishaji wa Sera za Mawasiliano pamoja na kutunga sera mpya zinazokidhi mahitaji ya sasa ya sekta hii. Hii inatokana na ukuaji wa haraka wa Sekta ya Mawasiliano unaochochea mabadiliko ya mara kwa mara ya kiteknolojia, kiuchumi, kisasia na kijamii.

Mheshimiwa Spika, Wizara itaendelea kusimamia utekelezaji wa mradi wa ujenzi wa Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano na kufikisha huduma zake hadi Makao Makuu ya Mikoa na Wilaya zote nchini. Aidha, Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma, itaratibu uunganishwaji wa Wizara 15 na Taasisi 50 za Serikali kwa kutumia fedha kutoka Benki ya Dunia kupitia mradi wa *Regional Communication Infrastructure Project (RCIP)*. Vile vile, Wizara itakamilisha andiko la mpango wa kuziunganisha Hospitali za Rufaa, Mikoa teule na Wilaya kwa upande mmoja na Shule za Msingi na Sekondari katika Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano. Lengo ni kuimarisha matumizi ya mtandao katika utoaji wa huduma za afya, elimu na utawala bora.

Mheshimiwa Spika, Wizara itaendelea kuratibu maandalizi na kuchangia utekelezaji wa programu ya kuendeleza mifumo, viwango na huduma salama za TEHAMA (*IT Systems, Services and Cyber Laws Development Program*). Pia Wizara

itaendelea kuratibu utekelezaji wa programu ya kujenga uwezo wa raslimali watu katika TEHAMA na kujenga Jamii Habari ikiwa ni pamoja na kuweka mazingira mazuri ya kutumia huduma za TEHAMA.

Mheshimiwa Spika, Wizara itaendelea kusimamia na kuratibu shughuli za utafiti na maendeleo nchini, sambamba na uboreshaji na upanuaji wa Taasisi za Sayansi na Teknolojia. Aidha, Wizara imeanza kutekeleza programu ya mageuzi ya sayansi, teknolojia na ubunifu kwa kurejea sera na kuandaa mpango wa utekelezaji.

Mheshimiwa Spika, Wizara itaandaa andiko la programu ya matumizi ya teknolojia za nyuklia na kuendelea kuratibu na kusimamia matumizi ya teknolojia za nyuklia na mionzi. Lengo ni kupanua wigo wa matumizi salama ya teknolojia ya mionzi na nyuklia katika uzalishaji, nishati na uhifadhi wa mazao.

Mheshimiwa Spika, Wizara itaendelea kuajiri watumishi wapya na kuwapandisha vyeo watumishi wenyе sifa kwa mujibu wa Sheria ya Utumishi wa Umma Na. 8 ya Mwaka 2002, ikisomwa pamoja na marekebisho ya sheria ya Utumishi wa Umma Na.18 ya Mwaka 2007 kwa kuzingatia ikama na muundo wa Wizara. Pia, Wizara itasimamia masuala ya utawala bora kwa mujibu wa kanuni za maadili ya utendaji katika utumishi wa umma.

Mheshimiwa Spika, Wizara itaendelea kuhamasisha watumishi kujikinga na kuepuka maambukizi mapya ya UKIMWI, upimaji wa UKIMWI kwa hiari, matumizi ya dawa za kurefusha maisha kwa waishio na virusi vya UKIMWI na kupunguza maambukizo ya UKIMWI kutoka kwa mama kwenda kwa mtoto. Aidha, Wizara imeendelea kuhamasisha watumishi waliopata maambukizi kujitokeza ili waweze kupatiwa huduma kwa mujibu wa Waraka wa Utumishi wa Serikali Na. 2 wa Mwaka 2006.

Mheshimiwa Spika, Wizara itarejea Mpango Mkakati (*Strategic Plan*) ya mwaka 2008/2009 – 2011/2012 na kusimamia Mpango wa Utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi (CCM) 2010 - 2015 katika Sekta ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia. Aidha, itasimamia utekelezaji na ufuatiliaji wa miradi mbalimbali inayotekeliza ikiwa ni pamoja na ile iliyoko kwenye taasisi zilizo chini yake.

Mheshimiwa Spika, Wizara itaandaa chapisho la takwimu mbalimbali zinazotoa taarifa ya maendeleo ya Sekta ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia. Pia Wizara itaratibu na kuendesha zoezi la kupitia matumizi ya fedha za Sekta ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia kwa kulingana na majukumu ya Wizara.

Mheshimiwa Spika, ili kuendeleza na kuimarisha Sekta ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia, Wizara itaendelea kuimarisha ushirikiano wa kikanda na kimataifa ili kuchocha ukuaji wa sekta hizi nchini. Katika kutekeleza jukumu hilo, Wizara itakamilisha uridhiwaji wa mikataba mbalimbali ya kikanda na kimataifa inayohusu Sekta ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia.

Mheshimiwa Spika, Wizara itaendelea kutoa huduma za malipo kuitia mtandao wa malipo wa Serikali ambao unasimamiwa na Katibu Mkuu Hazina kuitia Mhasibu Mkuu wa Serikali kwa mujibu wa sheria, kanuni na taratibu za usimamizi wa fedha. Aidha, Wizara itaendelea kutoa taarifa za mwaka za hesabu za Wizara na kwa ajili ya ukaguzi na tathmini za wadau mbalimbali kwa mujibu wa sheria, kanuni na taratibu zilizopo.

Mheshimiwa Spika, Wizara itaendelea kukagua na kutoa taarifa za matumizi ya raslimali za Wizara na Taasisi zilizo chini yake kulingana na sheria, kanuni na taratibu zilizopo. Vile vile, Wizara itafuatilia utekelezaji wa ushauri uliotolewa katika taarifa za ukaguzi ili kurekebisha kasoro zilizojitokeza pamoja na kuongeza ufanisi wa utendaji kazi na kuwa na matokeo mazuri. Aidha, Wizara itaendelea kutoa elimu kwa umma kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara kwa kutumia njia mbalimbali ikiwa ni pamoja na vipeperushi, majorida, mabango, redio, luninga pamoja na magazeti.

Mheshimiwa Spika, Wizara itaendelea kusimamia Sera, miongozo na mikakati ya sekta ya *TEHAMA*, mawasiliano, sayansi, teknolojia na ubunifu. Vile vile, itasimamia na kuratibu uandaaji wa mikataba na uridhiwaji wa itifaki za kisekta. Aidha, itaandaa Miswada ya Sheria na sheria ndogo ndogo zinazoihusu Sekta ya Mawasiliano, *TEHAMA*, Sayansi, Teknolojia na Ubunifu kwa kushirikiana na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Pia itaendelea kushughulikia masuala ya madai na usuluhishi kwa mujibu wa sheria, kanuni, taratibu pamoja na mashauri mbalimbali yanayohusu Wizara na Taasisi zake.

Mheshimiwa Spika, Wizara itatoa mafunzo maalum kwa ajili ya kuelimisha watumishi juu ya Sheria ya Ununuzi ya Mwaka 2004 na kanuni zake za mwaka 2005 na kusimamia shughuli zote za ununuzi na ugavi. Aidha, Wizara itaandaa taarifa za ununuzi za kila mwezi na kutoa taarifa kwa Mamlaka ya Ununuzi wa Umma (*PPRA*) kwa mujibu wa Sheria.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2011/2012, Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam itadahili wanafunzi 1505 katika programu za *IT Basic Certificate* (182), *Diploma* katika fani mbalimbali (825) na *Bachelor of Engineering* (498), hivyo kuwa na jumla ya wanafunzi 3,028 ikiwa ni ongezeko la asilimia 19. Aidha, Taasisi itaendeleza wafanyakazi 15 katika masomo ya juu, wakufunzi nane na maafisa waendeshaji saba. Pia, Taasisi itaendelea kuhudumia wafanyakazi 48, wakufunzi 41 na maafisa waendeshaji saba walioko masomoni. Vile vile, Taasisi itaendesha masomo ya awali (*Pre-entry training*) ili kupata wanafunzi wa kike katika kozi ya ufundi sanifu (30) na uhndisi (25).

Mheshimiwa Spika, Taasisi itaanza kufundisha kozi mpya za Diploma za *Biomedical Equipment Engineering* 35, *Communication Systems Engineering* 35, *Multimedia Technology* 35 na *Information Technology* 35. Aidha, Taasisi itakamilisha taratibu za kuidhinishwa na kozi mpya za *Diploma* za *Electronic Equipment Maintenance*, *Geographical Information System* na *Mechatronics*. Kozi hizi huidhinishwa na Baraza la Elimu Tanzania (*NACTE*).

Mheshimiwa Spika, Taasisi itakarabati na kufunga mitambo katika vituo vitatu vya Habari Jamii vya mradi wa *Super Computer* vilivyoko Morogoro, Mtwara na Dodoma ili kukamilisha mradi wa *Super Computer*. Pia Taasisi itaendelea kuhudumia Kituo cha *TEHAMA (IT Centre of Excellence)* kwa kutoa mafunzo ya *TEHAMA*, kuhamasisha matumizi ya *Super Computer* na kutoa huduma za Tiba Mtandao (*Telemedicine*). Aidha, Taasisi itakamilisha awamu ya pili ya ujenzi wa jengo la *DIT Teaching Tower* kwa ajili ya madarasa, maabara na ofisi za wafanyakazi.

Mheshimiwa Spika, Taasisi itakarabati majengo na miundombinu ya Taasisi ya Teknolojia ya Ngozi Mwanza ili iweze kutoa mafunzo ya Diploma ya Teknolojia katika mwaka wa masomo 2011/2012. Aidha, Taasisi itafanya matengenezo ya nyumba tano za wafanyakazi wa Taasisi zilizoko Mbezi Kilongawima, Dar es Salaam.

Mheshimiwa Spika, Taasisi itaendelea kujitangaza ili kupata zabuni za kutengeneza na kuweka taa za kuongoza magari barabarani. Aidha, Taasisi itajitangaza na kuhamasisha matumizi ya *TEHAMA* kupitia miradi mbalimbali katika Taasisi.

Katika mwaka wa fedha 2011/2012, Taasisi ya Sayansi na Teknolojia Mbeya itaongeza udahili wa wanafunzi kutoka idadi ya wanafunzi 1,757 hadi kufikia wanafunzi 2,000 ikiwa ni ongezeko la asilimia 14. Pia itaanza kutoa mafunzo ya awali (*pre-entry training*) kwa wanafunzi wa kike kwa lengo la kudahili wanafunzi wa kike 50. Vile vile, Taasisi itaajiri watumishi wapya 21 ili kuendana na uhitaji wa raslimali watu unaotokana na kupanuka kwa Taasisi. Aidha, Taasisi itakamilisha uandaaji wa mitaala katika fani za Mekatroniki, Sayansi na Teknolojia ya Vyakula, Uhandisi Usalama, Uhandisi Mawasiliano na Uhandisi Madini.

Mheshimiwa Spika, Taasisi itaanza ujenzi wa jengo la maktaba litakalokuwa na uwezo wa kuchukua wanafunzi 2,000 kwa wakati mmoja. Pia itakamilisha ujenzi wa majengo mawili ya mabweni ya wanafunzi yenye uwezo wa kulaza wanafunzi 350 kila moja. Aidha, Taasisi itakamilisha tathmini ya fidia kwa wananchi wote waishio katika eneo ambalo lilitengwa kwa ajili ya shughuli za Taasisi.

Mheshimiwa Spika, kufuatia nia ya Serikali ya kupandisha hadhi Taasisi ya Sayansi na Teknolojia Mbeya kuwa Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia Mbeya, kama alivyoagiza Mheshimiwa Rais wakati wa usfunguzi wa Bunge la Kumi la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, nanukuu: “Tutaendelea kuipandisha hadhi Taasisi ya Sayansi na Teknolojia Mbeya kuwa Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia Mbeya.” Taasisi imetoa tamko rasmi kupitia Baraza la Chuo la kufanya mabadiliko ya Taasisi kuwa Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia. Maandalizi ya programu na miundombinu ya Taasisi itakayokidhi azma hii yataendelea kufanywa. Nia ya Serikali ni kuhakikisha kwamba mchakato wa kufanya Taasisi ya Sayansi na Teknolojia Mbeya kuwa Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia unakamilika kabla ya mwaka 2015.

Taasisi itaananza na kuendeleza uhusiano na Taasisi mbalimbali za Sayansi na Teknolojia kitaifa, kikanda na kimataifa. Aidha, Taasisi itafanya upembuzi yakinifu kwa ajili ya kuwezesha utekelezaji wa Mpango Kabambe wa Taasisi ili kuvutia uwekezaji na

ufadhili katika maeneo yafuatayo: ujenzi wa mabweni ya wanafunzi, nyumba za walimu, hoteli, migahawa, Kituo cha Afya, Kituo cha Mikutano na Kituo cha Huduma za Kibiashara.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2011/2012, Taasisi ya Nelson Mandela inatarajia kudahili wanafunzi 100 katika ngazi za uzamili na uzamivu. Pia, Taasisi itakamilisha uandaaji wa Mpango wa Matumizi ya Ardhi (*Land use Plan*) wa eneo la Taasisi lililopo Karangai. Aidha, Taasisi itajenga Kituo cha *TEHAMA (ICT Resource Centre)*, nyumba ya Makamu Mkuu wa Chuo, Kituo cha Afya na Maabara ya *bio-safety* katika Kampasi ya Tengeru. Taasisi itaongeza vifaa vya maabara kwa matumizi ya Mtandao wa *TEHAMA (Communication Network Services)*, vifaa vya maabara (*Laboratory Equipment*), vitendea kazi vya kompyuta (*Computers, printers, photocopiers and scanners*) na itanunua magari matatu kwa ajili ya matumizi ya Taasisi. Taasisi itaimarisha uhusiano na ushirikiano na vyuo pamoja na asasi mbalimbali ndani na nje ya nchi kwa lengo la kuendeleza Taasisi hii.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2011/2012, Tume ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia itaendelea kusambaza taarifa za matokeo ya utafiti kwa wadau mbalimbali ikiwa ni pamoja na watoa maamuzi ili zitumike katika kuandaa sera, sheria na mipango mbalimbali ya maendeleo. Aidha, Tume itaendelea kuratibu shughuli za utafiti nchini, ikiwa ni pamoja na zile zinazofadhiliwa na mfuko wa *MTUSATE*.

Mheshimiwa Spika, Tume itaendelea kugharamia tafiti ikiwa ni pamoja na uendelezaji wa rasilimali watu, kuboresha mazingira ya utafiti (miundombinu na vitendeakazi), miradi mipy ya utafiti na ile inayoendelea kulingana na vipaumbele vya Taifa. Tume itaanzisha atamizi mipy ya biashara na kilimo (*Agri-business incubator*) ili kukuza ujasiriamali na uwekezaji katika Sekta ya Kilimo, hususan usindikaji wa mazao. Pia Tume itaimarisha kongano (*clusters*) zilizopo ili ziweze kufanya vizuri zaidi na kutoa msukumo katika uanzishwaji wa kongano mipy.

Mheshimiwa Spika, Tume itaendelea kusimamia utaratibu wa usajili na kulinda hakimiliki za matokeo ya ubunifu kwa watafiti na wagunduzi nchini. Aidha, Tume itaendelea kubaini na kutambua wagunduzi na wabunifu wapya ili iweze kuwasajili na kuwaendekeza. Vile vile, Tume itaendelea kuelimisha umma kuhusu matumizi ya sayansi, teknolojia na ubunifu kupitia luninga, redio na machapisho mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, Tume kwa kushirikiana na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar (SMZ) itafungua ofisi Zanzibar kwa lengo la kupanua shughuli zake.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2011/2012, Tume ya Taifa ya Nguvu za Atomiki Tanzania, itaendelea kutoa na kuimarisha huduma za kinga ya mionzi ayonisha (*ionizing radiation*) kwa kukagua na kusimamia vituo 190. Pia itapima viwango vya mionzi (*Personnel Dosimetry Service*) kwa wafanyakazi 1,300 na kufanya ukaguzi wa vituo vinavyotumia mionzi isiyoayonisha (*non-ionizing radiation*) kwenye minara 20 kwa kushirikiana na Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania. Vile vile, Tume itapima vyanzo

vya mionzi katika sampuli 20,000 za vyakula. Tume itaimarisha upimaji wa mionzi kwenye vituo 26 ambavyo vimekuwa vikiendeshwa kwa ushirikiano na Taasisi nyingine.

Mheshimiwa Spika, Tume itatafuta na kukusanya mabaki ya vyanzo vya mionzi na kuyahifadhi katika maabara maalum (*Central Radioactive Waste Management Facility*) iliyoko katika eneo la Tume, Arusha. Vile vile Tume itaendesha Kituo cha Kupima Mionzi iliyoko kwenye mazingira chini ya mkataba wa *Comprehensive Nuclear Test-Ban Treaty of Nuclear Weapons* kwa kutumia Kituo cha Dar es Salaam (*Radionuclide Monitoring Station, (TZP-RN64), Dar es Salaam*). Aidha, Tume itatoa elimu kwa wananchi waishio maeneo yenyе madini ya urani ili kuwaongezea uelewa na kuweka hadhari pale panapostahili.

Mheshimiwa Spika, Tume itasimamia na kuratibu miradi ya kitaifa na kikanda (*AFRA*) katika taasisi nane za kitaifa inayogharamiwa na Shirika la Kimataifa la Nguvu za Atomiki (*International Atomic Energy Agency*) na kusimamia mchakato wa kuandaa miradi mipyä kwa kipindi cha mwaka 2012/2013. Aidha, Tume itaendelea kutoa mapendekezo ya tafiti mbalimbali kwa kushirikiana na wadau.

Mheshimiwa Spika, Tume imedhamiria kuendeleza ukaguzi katika migodi 40 ili kubaini hali ya usalama na kutoa tahadhari. Pia Tume itafanya utafiti katika migodi ya urani kwa nia ya kubuni na kutekeleza mbinu nzuri za kinga na matumizi salama ya uchimbaji na usafirishaji wa madini ya urani. Aidha, Tume itaendelea kutoa elimu kwa njia ya semina kwa wafanyakazi wa migodi, viwandani, kilimo, ujenzi wa barabara na Idara za *X-ray* hospitalini kuhusu madhara ya mionzi isipotumiwa vyema. Vile vile, Tume inatarajia kuanzisha ofisi za kanda kwa kuanzia na Mkoa wa Ruvuma (Namtumbo) na Visiwani Zanzibar ili kurahisisha utekelezaji wa majukumu ya Tume.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2011/2012, Shirika la Posta Tanzania litaendeleza na kuimarisha matumizi ya *TEHAMA* katika huduma zitolewazo na Shirika ikiwa ni pamoja na kuunganisha ofisi zote za Posta za Wilaya katika Mtando wa Kielekitroniki wa Posta. Aidha, Shirika litaendelea kueneza huduma za posta vijijini ili kukidhi matakwa ya leseni ya kutoa huduma za posta za msingi. Vile vile, Shirika linatarajia kuongeza vibali vya kuuza stempu, shajala pamoja na kuongeza vituo vinavyotoa huduma za *internet*.

Shirika litaendesha mafunzo kwa watumishi ili waweze kumudu matumizi ya teknolojia katika utendaji kazi. Mafunzo yatakayotolewa ni pamoja na kozi ya uendeshaji (watumishi 18), huduma kwa wateja (watumishi 72), *TEHAMA* (watumishi 90) na mafunzo ya awali ya huduma za Posta (watumishi 96).

Mheshimiwa Spika, Shirika pia litaendelea kutumia majengo yake na raslimali nyinginezo kibiashara na kukamilisha mchakato wa kutumia wabia kuendeleza viwanja vyake ambavyo havijaendelezwa. Aidha, Shirika litanzisha ujenzi wa Posta za Kibondo na Katesh. Vile vile, Shirika litafanya matengenezo majengo ya Posta mpya Dar es Salaam, Mwanza, Wete, Masasi na Muheza.

Katika mwaka wa fedha 2011/2012, Kampuni ya Simu Tanzania inatarajia kuongeza tija na ufanisi wa Kampuni hivyo kuongeza mapato kutoka shilingi bilioni 80 mwaka 2010 hadi shilingi bilioni 113 mwaka 2011. Aidha, Kampuni itaboresha makusanyo yanayotokana na huduma za simu zilizotolewa kwa wateja wake, ikiwemo Serikali kuu na taasisi zake. Lengo ni kukusanya angalau asilimia 94 ya mauzo ya kila mwezi husika.

Mheshimiwa Spika, Kampuni itaboresha huduma kwa wateja kwa kuweka mitambo (*switches*) ya Kisasa inayotumia teknolojia ya *Next Generation Network* kwa kuondoa mitambo ya simu ya zamani aina ya *NEAX*, *AXE10*, *DTS* na *GX 5000* iliyobakia. Pia, Kampuni itarekebisha njia za simu zilizoharibika pamoja na kuboresha huduma kwa wateja ili kukidhi mahitaji halisi ya kibashara ya simu na *data*. Aidha, Kampuni itaendelea kupanua mtandao wa *internet (Fixed and wireless Broadband)* kwenye Makao Makuu ya Mikoa na miji mikubwa yote Tanzania Bara na Visiwani kwa kujenga minara mipyä.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2011/2012, Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania itaanzisha rejesta (*Central Equipment Identification Register*) ili kudhibiti matumizi mabaya ya simu za viganjani nchini na nchi za Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Spika, Mamlaka itaendelea kuratibu utekelezaji wa kuhamia katika mfumo mpya wa utangazaji wa digitali (*Migration from Analogue to Digital Broadcasting*), kwa kutoa elimu kwa umma na kwa watoa huduma za utangazaji kwa mujibu wa kanuni na sheria husika.

Pia, Mamlaka itaendelea kuratibu ushiriki wa watoa huduma za mawasiliano katika ujenzi wa mitambo ya *internet (Internet Exchange Points)* na kuunganisha mitandao yao kwenye mtambo huo. Aidha, Mamlaka itashirikiana na Umoja wa Watoa Huduma za Mawasiliano wa Afrika Mashariki ili kufanikisha uunganishwaji wa *Internet Exchange Points* za Kenya, Uganda, Rwanda, Burundi na Tanzania kama ilivyoazimiwa na Umoja huo.

Mheshimiwa Spika, Mamlaka itaendelea kupokea na kutathmini maombi ya leseni, kutayarisha na kutoa leseni kwa makampuni yaliyosajiliwa. Pia, Mamlaka itaendelea kusimamia na kudhibiti ubora wa huduma za mawasiliano kwa kuyafanyia ukaguzi Kampuni zilizosajiliwa ili kuhakikisha kuwa huduma zinazotolewa zinakidhi viwango vilivyowekwa kwenye leseni zao.

Mheshimiwa Spika, Mamlaka itaendelea kuelimisha watumiaji wa huduma za mawasiliano kuhusu taratibu za kuwasilisha malalamiko yao kwa Mamlaka pale ambapo hawakuridhika na huduma walizopewa na mtoa huduma. Aidha, Mamlaka itaendelea kushirikiana na wadau wengine katika utekelezaji wa Mradi wa Kitaifa wa Anuani za Makazi na Simbo za Posta (*New Addressing System and Post Code Project*).

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2011/2012 Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote (*UCAF*) utaendelea kutathmini mahitaji ya huduma za mawasiliano katika

maeneo yasiyo na mvuto wa kibashara na kuanzisha miradi itakayohakikisha mawasiliano yanafika kwenye maeneo hayo kwa kushirikiana na wadau wa sekta. Pia, Mfuko utaanzisha Vituo vya Mawasiliano vya Jamii na kupeleka huduma za *internet* kwenye Shule za Serikali za Sekondari. Aidha, Mfuko utaendelea kushirikiana na wadau wa Sekta ya Posta kuhakiki mahitaji ya huduma za Posta vijiji.

Mheshimiwa Spika, Sekta ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia inaazimia kutekeleza Mpango wa Muda wa Kati na Muda Mrefu ambao umetilia mkazo programu ya kufanya mabadiliko ya mfumo wa mawasiliano, habari na utangazaji kutoka analogia kwenda digitali.

Mheshimiwa Spika, Wizara itaendelea kusimamia uanzishwaji wa mfumo mpya wa Anuani za Makazi na Simbo za Posta ambao una lengo la kurahisisha upatikanaji wa anuani kamili za makazi zinazoonyesha mitaa, majina ya majengo na uwekaji wa namba za nyumba. Mambo haya kwa pamoja yatawezesha upatikanaji wa anuani ya mwananchi na mfumo huu wa anuani za makazi na simbo za Posta utarahisisha utoaji wa huduma mbalimbali za kibashara na kijamii kama vile wakati wa dharura na uokoaji kama zimamoto, magari ya wagonjwa, maji, umeme, mawasiliano, ugawaji misaada, bima, ukusanyaji wa kodi mbalimbali za Serikali na ushirikishwaji wa wananchi katika shughuli za maendeleo. Mambo mengine yatakayoweza kufanya kwa urahisi kupitia utekelezwaji wa mradi huu ni pamoja na utambuaji wananchi kupitia Wakala wa Vizazi, Vifo na Ufilisi (*RITA*), uandikishaji wapiga kura, na utoaji wa vitambulisho vya mkazi kupitia Mamlaka ya Vitambulisho Tanzania (*NIDA*).

Mheshimiwa Spika, Wizara itaendelea kuimarisha usimamizi wa masuala ya mawasiliano na haki za watumiaji wa huduma na kuboresha mtandao wa simu za mezani na viganjani hadi vijiji. Aidha, Wizara itaendelea kukamilisha ujenzi wa Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano (*National ICT Broadband Backbone Infrastructure*). Pia, Wizara itaratibu na kusimamia uanzishwaji wa Vituo Vikuu vya Kumbukumbu (*Mega Data Centers*) pamoja na kuandaa Sera ya Usalama wa *TEHAMA*.

Mheshimiwa Spika, Wizara itaendelea kuratibu na kusimamia shughuli za utafiti nchini na kufuatilia upatikanaji wa fedha za utafiti na maendeleo toka ndani na nje ya nchi. Pia Wizara itaendelea na utekelezaji wa programu ya mageuzi ya sayansi, teknolojia na ubunifu. Vile vile, itasimamia na kuratibu uboreshaji na upanuaji wa Taasisi za sayansi na teknolojia nchini.

Wizara kupitia Tume ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia, itaendeleza jitihada za kuweka na kusimamia utaratibu wa usajili na kulinda hakimiliki za matokeo ya ubunifu kwa watafiti na wagunduzi. Aidha, itaendelea kuandaa na kuhuisha sera na sheria za sayansi, teknolojia na ubunifu pamoja na kukamilisha mkakati wa utekelezaji wa sera hizo.

Mheshimiwa Spika, napenda kutoa shukrani zangu za pekee kwa wadau na wahisani mbalimbali kwa michango yao katika maendeleo ya Sekta ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia. Wahisani hao ni pamoja na Serikali za Marekani, Sweden,

Norway, Finland, Uholanzi, Japan, Afrika Kusini, Jamhuri ya Korea ya Kusini, China na India. Mashirika wahisani ni pamoja na Umoja wa Mataifa, Jumuiya ya Madola, Shirika la Kimataifa la Nguvu za Atomiki, *KOICA*, *UNESCO*, *UNCTAD*, *UPU* na *ITU*. Mashirika haya yameonyesha nia ya dhati kusaidia maendeleo ya Sekta ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia. Wizara inaahidi kuendeleza ushirikiano huu. Aidha, naishukuru sekta binafsi kwa mchango wao katika kuendeleza Sekta ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia na hivyo kuongeza mchango wa sekta hii katika maendeleo ya nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, ili kuwezesha Wizara yangu kutekeleza mipango iliyojiwekea katika mwaka wa fedha 2011/2012, sasa naliomba Bunge lako Tukufu liidhinishe jumla ya Sh. 64,017,516,000/= kwa ajili ya matumizi ya kawaida na ya maendeleo. Kati ya fedha hizo Sh. 23,799,259,000/= ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida, yaani mishahara na matumizi mengineyo, ambapo Sh. 14,765,658,000/= ni kwa ajili ya mishahara na Sh. 9,033,601,000/= ni kwa ajili ya matumizi mengineyo na Sh. 40,218,257,000/= ni kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo. Kati ya fedha hizo za Maendeleo, Sh. 38,195,679,000/= ni fedha za ndani na Sh. 2,022,578,000/= ni fedha za nje.

Mheshimiwa Spika, mwisho kabisa, napenda kukushukuru wewe binafsi, Naibu Spika, Wenyeviti wa Kamati za Bunge pamoja na Bunge lako Tukufu kwa kunisikiliza wakati nikiwasilisha hotuba yangu. Aidha, napenda kutoa taarifa kuwa hotuba hii itapatikana pia katika tovuti ya Wizara ambayo ni www.mst.go.tz

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. (*Makofi*)

WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Spika, naafiki.

(*Hoja ilitolewa iamuliwe*)

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, katika Bunge la *SADC*, kama mnavyofahamu mpaka sasa hivi bado siyo Bunge ni *forum*. Sasa kuna utaratibu ambao unaendelea kufanyika kwamba liweze kuwa Bunge kamili kama vile ilivyo *East African Legislative Assembly*. Kwa hiyo, katika kufanya hivyo basi, kuna Kamati ya Mikakati ambayo imeundwa ikihusisha na Bunge letu la Tanzania, yaani Spika na Katibu wa Bunge. Kwa hiyo, ninaondoka sasa hivi, tutakwenda kesho kufanya kikao pale Johannesburg na kurudi keshokutwa. Kwa hiyo, ninaomba kwa sasa hivi Mwenyekiti, Mheshimiwa Jenista Mhagama aje anipokee. (*Makofi*)

Hapa Mwenyekiti (Mheshimiwa Jenista J. Mhagama) Alikalia Kiti

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, kabla hatujaendelea na kabla sijasahau, naomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati ya Uongozi wa Chama cha Mapinduzi kuwepo kwa kikao saa 7.00 na niwatangazie Wabunge wa Chama cha Mapinduzi wote kwamba kutakuwa na Kikao cha Kamati ya Wabunge wa CCM baada ya kuahirisha shughuli za Bunge usiku wa saa 2.00 leo usiku. Baada ya hapo naomba nimwite Msemaji wa Kamati iliyochambua hotuba ya bajeti hii ili aje kutoa maoni kwa niaba ya Kamati nzima.

MHE. RITTA L. MLAKI (K.N.Y. MWENYEKITI WA KAMATI YA BUNGE YA MIUNDOMBINU): Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naomba nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kusimama hapa katika Bunge hili kwa mara ya tatu mfululizo. Pili, niwashukuru wanawake wa Mkoa wa Dar es Salaam kwa kunichagua kwa kura nyingi na Baraza Kuu la UWT kwa kuniwezesha kuwa hapa siku hii ya leo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati ya Miundombinu, naomba nichukue fursa hii kukushukuru kwa kunipa fursa ili niweze kuwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu maoni ya Kamati yangu kwa Mujibu wa Kanuni ya 99(7) ya Kanuni za Bunge, Toleo la 2007 kuhusu utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia kwa mwaka wa fedha wa 2010/2011, pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha wa 2011/2012.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati yetu inasimamia Wizara tatu ambazo ni Wizara ya Ujenzi, Wizara ya Uchukuzi na Wizara ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia. Mimi na wanakamati wenzangu tunaitambua dhamana hii kubwa. Napenda kuwashakikishia Waheshimiwa Wabunge na umma wa Watanzania kwamba, kwa niaba yenu, kazi ya kupitia bajeti hizi tulizifanya kwa umahiri na umakini mkubwa na kufanikisha baadhi ya mabadiliko yenyi tija kwa maendeleo ya Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza natoa pongezi kwa Wizara ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia kwa maandalizi na mawasilisho mazuri yaliyofanywa na Wizara hii mbele ya Kamati kuhusu Mpango wa Makadirio ya Bajeti ya mwaka 2011/2012. Aidha, Wizara iliwasilisha pia Taarifa ya Utekelezaji wa Maagizo ya Kamati na Mipango ya Bajeti ya mwaka uliopita wa mwaka 2010/2011 na kazi zilizopangwa kufanyika katika Mwaka wa Fedha wa 2011/2012 ikiwa ni pamoja na maombi ya fedha kwa ajili ya kazi hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati wa kuchambua bajeti ya Wizara hii, Kamati ilipata fursa ya kujadili:-

- (i) Utekelezaji wa maagizo ya Kamati yaliyotolewa wakati wa kujadili Bajeti ya mwaka 2010/2011;
- (ii) Utekelezaji wa Malengo ya Wizara kwa mwaka 2010/2011 na malengo yanaoombewa fedha kwa mwaka 2011/2012; na
- (iii) Changamoto zilizojitokeza wakati wa utekelezaji wa majukumu kwa mwaka 2010/2011 na mikakati ya kukabiliana na changamoto hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka wa fedha wa 2010/2011 Kamati ilitoa maagizo 21 kwa ajili ya utekelezaji kwa kipindi cha mwaka huo wa fedha. Kamati inaishauri Serikali ipunguze urasimu katika utekelezaji wa majukumu yake, kwani kwa mwaka

mzima, utekelezaji wa maagizo mengi ulikuwa bado uko kwenye mchakato au juhudii ziliikuwa zikiendelea hata kwa masuala yaliyo ndani ya uwezo wa Wizara. Kamati inaendelea kushauri Wizara kwamba maagizo yote ambayo hayajatekelezwa yakamilishwe na taarifa ya utekelezaji wake utolewe kabla ya bajeti ijayo.

Ukusanyaji mapato katika mwaka wa Fedha 2010/2011, Wizara ilikadiria kukusanya jumla ya Sh. 1,900,000/= kama Mapato ya Serikali. Hadi kufikia tarehe 30 Aprili, 2011 Wizara ilikusanya jumla ya Sh. 19,658,751/= ambazo sehemu kubwa ya fedha hizo zilitokana na mauzo ya nyaraka za zabuni mbalimbali, mishahara isiyolipwa na marejesho ya masurufu ikiwa ni ongezeko la asilimia 1034.7 ya makisio kwa mwaka wa fedha wa 2010/2011.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tofauti hii kubwa sana kati ya makisio na makusanyo iliishtua Kamati. Kamati inashauri Wizara iwe makini zaidi katika kufanya makadirio ya makusanyo ya mapato.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2010/2011, Wizara ilitarajia kutumia jumla ya Sh. 71,017,600,000/=, kati ya fedha hizo Sh. 15,290,382,000/= ni kwa ajili ya mishahara na Sh. 11,300,308,000/= kwa ajili ya matumizi mengineyo. Hadi kufikia tarehe 30 Aprili, 2011 Wizara ilipata jumla ya Sh. 16,719,857,177/= kwa ajili ya mishahara na matumizi mengineyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha wa 2010/2011 ziliidhinishwa jumla ya Sh. 44,426,910,000/= kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli mbalimbali za maendeleo, kati ya Fedha hizo Sh. 42,426,910,000/= ziliikuwa ni fedha za ndani na Sh. 2,000,000,000/= ziliikuwa ni fedha za nje. Hadi kufikia tarehe 30 Aprili, 2011 jumla ya Sh. 6,582,019,319/= zilipokelewa. Kati ya fedha hizo Sh. 6,006,467,454/= ziliikuwa ni fedha za ndani na Sh. 575,551,865/= ni fedha za nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia imefanikiwa kutekeleza majukumu mengi ikiwemo machache haya yafuatayo:-

- Wizara imetekeliza maagizo ya Kamati licha ya kukabiliwa na uhaba wa fedha katika utekelezaji wa majukumu yake;
- Kuendelea kuratibu na kusimamia ujenzi wa Mkongo wa Taifa;
- Kuendeleza ujenzi wa Taasisi ya Teknolojia ya Dar es Salaam na Taasisi ya Sayansi na Teknolojia ya Nelson Mandela ya Arusha;
- Imeendelea na ujenzi wa Makao Makuu ya Tume ya Nguvu za Atomiki ya Tanzania; na
- Kuendeleza ukarabati wa jengo la Tume ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na mafanikio yaliyopatikana, zilikuwepo pia changamoto ambazo Wizara ilikutana nazo, ikiwa ni pamoja na:-

- Kuwa na mtiririko mdogo wa fedha za matumizi ya kawaida kwani mpaka tarehe 30 Aprili, 2011 fedha zilizopokelewa ni Sh. 6,789,264,717/= katika ya Sh.11,300,308,000/= zilizoidhinishwa;
- Shughuli za utafiti kutotengewa fedha za kutosha hali ambayo inaathiri ufanisi wa shughuli za maendeleo ya utafiti;
- Uhaba wa raslimali watu kwenye Sekta ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia. Aidha, wataalamu wengi waliopo wana umri mkubwa, kutokuwa na uwiano wa kada ya wahandisi na mafundi wa ngazi za cheti na Diploma ikiwemo wengi wao kutokuwa na uelewa wa teknolojia mpya;
- Ujenzi wa miundombinu ya kuendeleza Sekta ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia kuhitaji uwekezaji mkubwa na hivyo kuwa mzigo mkubwa kwa Serikali na wawekezaji;
- Uharibifu wa kukata nyaya za Mkongo wa Taifa katika maeneo ambayo nyaya hizo zinaonekana;
- Kutokuwa na mazingira ya kuibua na kuendeleza vipaji vya ubunifu na uvumbuzi kwa Watanzania pamoja na kutokuwepo kwa mfuko maalumu wa kuendeleza wagunduzi, wavumbuzi na vijana wenye vipaji; na
- Kukosekana kwa sheria/uratibu wa matumizi ya miundombinu kwa ajili ya watoa huduma za msingi za kijamii (*Public Utility Services*).

Kamati inaipongeza Wizara kwa kuiwekea mikakati mbalimbali ya kukabiliana na changamoto hizo, ikiwa ni pamoja na:-

- Kuvutia mashirika ya nje na sekta binafsi kuchangia na kudhamini shughuli za utafiti;
- Kupata fedha kupitia mikopo inayodhaminiwa na Serikali, hususan katika ujenzi wa miundombinu;
- Serikali kuweka sera shirikishi na kutenga fedha za kutosha kuendesha elimu kwa umma ili kushirikisha wananchi kulinda Mkongo wa Taifa; na
- Kushirikiana na wataalam pamoja na mkandarasi kukabiliana na vikwazo vinavyochelewesha upitishaji wa mkongo kwenye baadhi ya hifadhi za barabara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha zilizotengwa na Wizara ya Mawasiliano zimegawiwa kulingana na vipaumbele vya majukumu ya Wizara na Taasisi zake. Hivyo, fedha kiasi cha Sh. 64,017,516,000/= katika mwaka wa fedha wa 2011/2012 zinaombwa kwa ajili ya kutekeleza shughuli zifuatazo:-

- Ukamilishaji wa uanzishaji na uendeshaji wa Mfuko Maalum wa kufanikisha maendeleo ya huduma za mawasiliano kwa wote nchini;
- Utekelezaji wa miradi ya mawasiliano, Posta, Vituo vya Mawasiliano (*telecentres*) hususan sehemu za vijiji kwa lengo la kupunguza umaskini na kuongeza ajira;
- Kufanya upembuzi yakinifu na kufunga Mtandao wa Mawasiliano wa Elimu na Utafiti (*National Research and Education Network*) katika Vyuo Vikuu na Taasisi za Utafiti zilizoko Dar es Salaam na Zanzibar chini ya udhamini wa Benki ya Dunia;
- Kuratibu tafiti za kisayansi katika maeneo yenyе kipaumbele Kitaifa (kilimo na chakula, viwanda, nishati, maliasili na mazingira);
- Kuanzisha vituo vipyä vya Sayansi na Teknolojia, kuhuisha mfumo wa sayansi, teknolojia na ubunifu nchini kwa kushirikiana na *UNESCO*;
- Kuendelea na Ugazi wa Vituo vya Matumizi ya Mionzi isiyaoayonisha ikiwemo minara 70 ya simu za mikononi na radio;
- Kuendeleza ujenzi wa Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano, kuhamasisha na kuratibu matumizi yake hadi kufikia ngazi ya mtumiaji;
- Kuendeleza uanzishwaji wa anwani za makazi na simbo za Posta amba una lengo la kurahisisha upatikanaji wa anuani kamili za makazi zinazoonyesha mitaa, majina ya majengo na uwekaji wa namba za nyumba; na
- Ujenzi wa Kituo cha Kutunza Kumbukumbu za *TEKNOHAMA (MEGADATA CENTRE)* kitakachoimisha mawasiliano ya kimtandao ya ndani na nje ya nchi na kulingizia mapato Taifa kutokana na huduma zitakazotolewa na kituo hiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ilivyoeleza kwenye hotuba ya Waziri, katika mwaka wa fedha wa 2011/2012 Wizara ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia inakadirisha kuwa na matumizi ya Sh. 64,017,516,000/= ambapo Sh. 23,799,259,000/= ni kwa ajili ya matumizi ya kawaada na Sh. 40,218,257,000/= ni kwa ajili ya maendeleo. Kati ya hizo Sh. 38,195,679,000/= ni fedha za ndani na Sh. 2,022,578,000/= ni fedha za nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maoni na ushauri wa Kamati baada ya kuujadili Mpango na Bajeti hiyo kwa kina, Kamati inatoa maoni na ushauri ufuatao:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaipongeza Wizara kwa kupanga kutekeleza miradi ya maendeleo kwa kutumia fedha nyingi kutoka vyanzo vya ndani. Pesa zilizotengwa kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ni jumla ya Sh. 40,218,257,000/= ambapo

fedha za ndani ni Sh. 38,195,679,000/= ikiwa ni 94.9% ya makadirio na Sh. 2,022,578,000/= ni pesa kutoka vyanzo vya nje ambayo ni 5.1% tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uzoefu umeonyesha kuwa fedha nyingi zinazoahidiwa na wafadhili huwa hazitolewi kwa wakati, na wakati mwingine hazitimii au kutotolewa kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inatoa pongozi za dhati kwa Wizara ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia kwa makadirio haya ambayo fedha zilizombwa kwa ajili ya miradi ya maendeleo ni nyingi kuliko za matumizi ya kawaida. Huu unapaswa kuwa mfano wa kuigwa kwa Wizara na Taasisi zote za Serikali katika upangaji wa bajeti.

Kamati inasikitishwa na kupungua kwa bajeti ya Wizara hii kwani kwa mwaka wa fedha wa 2010/2011 ilipangiwa kiasi cha Sh. 71,017,600,000/. Hata hivyo, pamoja na kushuka kwa thamani ya shilingi na kupanda kwa gharama ya maisha, bajeti ya Wizara hii kwa mwaka 2011/2012 ni Sh. 64, 017,516,000/= na hivyo kushuka kwa 9.85% ya bajeti iliyopita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati haikuridhishwa na utekelezaji wa miradi ya maendeleo iliyokusudiwa kutekelezwa mwaka 2010/2011, kwani mpaka mwezi Aprili, 2011, miradi nane kati ya 14 iliyokusudiwa kutekelezwa ilikuwa hajapatiwa kiasi chochote cha fedha na iliyopatiwa fedha ilipatiwa kiasi kidogo sana. Jumla ya fedha iliyokusudiwa kwa ajili ya maendeleo ilikuwa ni Sh. 44,426,910,000/= iliyokuwa imetolewa mpaka Aprili, 2011 ni Sh. 6,582,019,319/= sawa na 14.8% tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuzingatia Sheria ya Ununuzi wa Umma ya Mwaka 2004 hata kama fedha yote ilitolewa katika kipindi kilichobaki, miradi iliyopangwa haingeweza kutekelezwa ipasavyo. Ni matumaini ya Kamati kuwa mwenendo huu wa utekelezaji wa miradi hautajirudia tena katika bajeti ya mwaka 2011/2012.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inasikitishwa na utaratibu uliopo wa kutoshughulikia kikamilifu changamoto zinazoikabili Wizara hii kwani nyingi kati ya changamoto zilizowasilishwa mbele ya Kamati yangu pia ziliwasilishwa kwenye Kamati iliyopita wakati wa kujadili bajeti ya mwaka 2010/2011. Huu ni upungufu wa kutochukua hatua madhubuti kukabiliana na changamoto na hata zile zisizohitaji fedha kuzitattua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaendelea kuishauri Serikali kukamilisha mapema mradi wa anuani mpya za makazi na simbo za Posta. Wizara ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia ishirikiane kwa karibu na Wizara ya Mambo ya Ndani na TAMISEMI, kwa vile mradi huu ukikamilika, utasaidia kufanikisha utoaji wa huduma mbalimbali za kibashara, kijamii pamoja na utekelezaji wa mradi wa vitambulisho vya uraia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali iendelee kuimarisha Shirika la Posta nchini, pamoja na mambo mengine iipatie mtaji utakaowezesha kuweka mitandao ya kompyuta (*internet*) katika utoaji wa huduma zake ili kuhimili ushindani unaotokana na mabadiliko ya teknolojia. Shirika pia lifanye juhudhi ya kutangaza huduma zake ili wananchi wazielewe na kuzitumia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaishauri Serikali ifanye juhudhi za makusudi za kuikwamua Kampuni ya Simu Tanzania (*TTCL*) kifedha na kiutendaji kwa kuipatia mtaji wa kutosha. Aidha, Wizara, Idara na Taasisi za Serikali zilazimishwe kulipa madeni yao yote yapatayo shilingi bilioni 6.3/= . Kama kweli nchi yetu inataka maendeleo, lazima Watanzania tuwe na mtazamo wa kibashara. Haipendezi kuona kuwa Wizara, Idara na Taasisi za Serikali hazilipi madeni ya kupiga simu wakati kila mwaka katika bajeti zao kuna kasma za kugharamia matumizi ya simu na huduma nyingine zitolewazo na *TTCL*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, inashangaza kuona kuwa makampuni yakibinafsishwa, Wizara na Taasisi hizo zinaanza kulipia huduma zinazotolewa na makampuni hayo kwa wakati na kwa ukamilifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaishauri Serikali isifikirie kuibinafsisha *TTCL*, badala yake ipewe mtaji wa kutosha ili isimamiwe na kuendeshwa na Watanzania kwa kuwa kuna utaalami, miundombinu na mtandao wa kutosha. Aidha, raslimali zote za Kampuni hii zitumike kibashara bila kuingiliwa na mamlaka za Serikali ikiwemo kutoa maamuzi bila urasimu usio wa lazima. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa kukamilika kwa mkongo wa mawasiliano nchini kutasaidia sana kuongeza ufanisi katika Sekta ya Mawasiliano, na kwa kuwa Mkongo huo bado haujakamilika, Kamati inaishauri Serikali kuongeza juhudhi za makusudi ili mradi huo ukamilike. Aidha, kutokana na umuhimu wa mkongo huu na gharama kubwa iliyotumika kuujenga Kamati inaishauri kuwe na ulinzi rasmi ikiwemo kushirikisha wanavijiji katika maeneo ulikopitia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa namna ya pekee, Kamati yangu inayapongeza Makampuni ya Simu za Mikononi kwa jitihada zao za kupanua huduma za mawasiliano ya simu hadi vijiini. Makampuni ya simu yamechangia kuboresha maisha ya Watanzania kwa kutoa ajira kwa maelfu ya Watanzania, kwa ajira ya moja kwa moja au kwa kupitia biashara zinazotokana na huduma za simu, pia kudhamini shughuli mbalimbali za maendeleo. Kutokana na umuhimu wa sekta hii kwa maendeleo ya nchi yetu, Kamati inaishauri Serikali ioanishe tozo zote zinazopaswa kulipwa na makampuni ya simu kwa Halmashauri badala ya hali ya sasa ambapo kila Halmashauri inajipangia yenyewe kiasi cha kuleta mkanganyiko kwa wawekezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, kutokana na kazi kubwa zinazofanywa na makampuni haya na umuhimu wake kiuchumi, kijamii na kisiasa, Kamati inaendelea kuishauri Serikali kuangalia uwezekano wa kupunguza kodi na tozo mbalimbali, ambazo zinachangia kumwongeza mteja wa mwisho gharama za kutumia simu za mkononi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2006 sheria ilitungwa ili kuanzisha mfuko wa mawasiliano kwa wote (*Universal Communication Access Fund*) kwa kushirikiana na sekta ya binafsi kwa lengo la kuongeza upatikanaji wa huduma za mawasiliano maeneo mbalimbali vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, Kamati inasikitishwa na ucheleweshaji wa uanzishwaji wa Mfuko huo kwani tangu mwaka 2006 mpaka mwezi Februari, 2011 watendaji bado walikuwa wanajipanga. Kamati inashauri kwamba mfuko huu uanzishwe mapema na uelekezwe kwenye maeneo yenye uhitaji ambako kwa sasa hakuna mawasiliano ya simu za mkononi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inashauri Serikali ishawishi Makampuni ya Simu kuondoa gharama za kupiga simu kati ya mtandao mmoja na mwingine (*interconnection charges*). Kuondoa gharama hizi kutawapunguzia Watanzania gharama za kutumia simu na kutembea na simu zaidi ya moja, kuwa na *sim cards* zaidi ya moja. Kamati inashauri makampuni ya simu yashindane kwa bei zao, kwa mawanda (*scope*) ya mitandao yao mpaka vijijini, ubora wa mitandao, huduma bora kwa mteja (*customer care*) na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, juhudhi zifanywe kuhakikisha upatikanaji wa umeme wa kuaminika kwani minara ya simu inatumia umeme. Maeneo mengi vijijini hayana umeme na mijini kuna tatizo la kukatika kwa umeme mara kwa mara. Hali hii inasababisha kuwepo kwa matumizi ya jenereta jambo ambalo lina gharama kubwa na kusababisha makampuni kushindwa kuboresha huduma zao kwa wateja sawasawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa kuna Watanzania wenyе vipaji vya ugunduzi, kwa mara nyingine Kamati inashauri Serikali ifanye juhudhi za makusudi za kuhamasisha ugunduzi huo kwa kutunga sera maalum na sheria ili kuhakikisha kuwa bidhaa zinazogunduliwa (*prototypes*) zinatengenezwa kwa wingi kwa ajili ya matumizi ya wananchi. Hii itaokoa fedha za kigeni ambazo zingetumika kuagiza bidhaa hizo kutoka nje ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, wanataluma wa Taasisi za Teknolojia za Dar es Salaam (*DIT*) na Mbeya (*MIST*) waliweza kutengeneza taa za kuongozea magari barabarani, lakini hawajapewa fursa ya kuzalisha kwa wingi kwa ajili ya matumizi ya barabara zetu. Aidha, Jeshi la Wananchi wa Tanzania wameweza kutengeneza magari yaliyopewa jina la “Nyumbu”, lakini bado hakuna uhamasishaji na uwezeshwaji wa kutosha kuwatia moyo wagunduzi hao ili kuzalisha bidhaa hizo kwa wingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Mkutano wake wa Tatu, Bunge hili liliridhia Azimio la Itifaki ya Sayansi, Teknolojia na Ubunifu ya Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika. Ibara ya 2(h) ya Itifaki hii inaelezea azma ya kutambua, kuthamini na kukuza vipaji na teknolojia ya wazawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inasisitiza kuwa elimu ya Sayansi iimarishe wе katika Shule za Msingi pamoja na Sekondari; ikiwa ni pamoja na kuwepo kwa Waalimu wa masomo ya sayansi na kujengwa kwa maabara ili kuwaandaa vijana kwa ajili ya masomo ya sayansi. Aidha, wanafunzi bora wa sayansi wagharamiwe masomo hayo kwenye Vyuo Vikuu bora duniani ili kupata wataalam waliobobea katika fani ya sayansi na teknolojia ya mawasiliano badala ya mtindo wa sasa wa kuwapa zawadi za fedha za vyeti. Ili kuweza kutekeleza azma hii, Kamati inashauri uanzishwe mfuko maalum wa **TEKNOHAMA**.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, elimu ya sayansi haitakuwa na maana iwapo wagunduzi wetu hawatiwi moyo na kupewa fursa ya kuonyesha ugunduzi wao na vipaji vyao. Kuna mwelekeo kuwa Taasisi zilizowekwa kwa ajili ya kukuza sayansi ikiwemo *COSTECH* zina mtazamo kuwa wagunduzi lazima wawe ni wasomi wenye shahada za Vyuo Vikuu. Kamati imefanya utafiti na kugundua kuwa baadhi ya wanasayansi wakubwa duniani hawakuwa na elimu ya juu bali ugunduzi wao ultokana na vipaji walivyozaliwa navyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, James Watts aliyegundua *steam engine* miaka ya 1660 hakuwa na elimu ya Chuo Kikuu, Guglielmo Marconi mgunduzi wa *wireless telegraph* miaka ya 1900 ambayo matokeo yake ni redio tunazotumia sasa, pia hakuwa na elimu hata ya Sekondari, Orville na Wilbur Wright (hawa walikuwa ndugu wa familia moja) walikuwa na elimu ndogo sana na walikuwa ni mafundi baiskeli, na ndio waliogundua ndege mwaka 1903, Mikhail Kalashnikov aliishia elimu ya Sekondari lakini ndiye mgunduzi wa aina 17 za silaha ndogo ndogo ikiwemo AK 47 mwaka 1947.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa nchini kuna wagunduzi wengi sana, lakini kila wanapowasiliana na mamlaka husika ili kuelezea ugunduzi wao hawaungwi mkono wala kutiwa moyo kwa vitendo na hivyo kuwakatisha tamaa. Ukitaka kujua hali halisi, tembelea maonyesho mbalimbali yakiwemo ya Nane Nane, Saba Saba, *SIDO* na kutazama kipindi cha Sanaa na Ubunifu kinachotangazwa na Kituo cha Televisheni cha *TBC*. Kamati inashauri Serikali ichukue hatua madhubuti kwa kupokea na kuendeleza ugunduzi bila kujali elimu ya mgunduzi ili kuwepo kwa Wizara hii na taasisi zinazohusika na masuala ya sayansi na teknolojia kuwe na maana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nchi zilizoendelea, ugunduzi wa kisayansi unafanywa na Majeshi, Vyuo Vikuu na Taasisi za Sayansi na Teknolojia na unapewa kipaumbele. Kamati inaendelea kuishauri Serikali kuweka mazingira mazuri na kuzijengea uwezo wa kifedha Taasisi zetu, kujenga maabara za kisasa zenye vifaa na mashine za kutosha, kuwawezesha Wahandisi na Wataalam wetu kufanya kazi zao za kiutafiti, kujenga karakana zenye sifa na viwango, kwani katika Taasisi zetu, majengo mengi, vifaa na mashine nydingi zilizopo ni chakavu na zimepitwa na wakati. Aidha, Kamati inashauri kuwa vyuo vinavyotoa elimu ya ufundi kama vile ngazi ya Fundi Mchundo viendelee kuwepo ili kukidhi mahitaji ya kuwa na mafundi wa kufanya kazi chini ya wahandisi kwa uwiano unaohitajika kitaalamu badala ya hali ya sasa kuwa vyuo vyote vilivyokuwa vinatoa mafundi mchundo vinataka kugeuzwa kuwa Vyuo Vikuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alitoa agizo la kutenga asilimia moja ya pato ghafi la Taifa kwa ajili ya shughuli za utafiti. Aidha, alipotembelea Wizara hii, tarehe 23 Machi, 2011 alielekeza kuwa Mwaka wa Fedha wa 2011/2012 zitolewe shilingi bilioni 100 kwa ajili ya shughuli za utafiti. Hata hivyo, pamoja na maelekezo hayo katika bajeti hii zimetengwa Sh. 25,968,769,000/. Hii ni kinyume na maagizo ya Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaendelea kusisitiza kuwa shughuli za utafiti zipewe kipaumbele kwa kutengewa fedha za kutosha. Kwa kawaida shughuli za utafiti huchukua muda mrefu na zinahitaji fedha nyingi. Kwa sababu hiyo, makampuni binafsi huwa yanasa kujingiza kugharamia tafiti ambazo hazina manufaa ya haraka kwao. Hivyo, Kamati inaendelea kusisitiza kuwa Serikali ichukue jukumu la kugharamia shughuli za utafiti bila kutegemea michango ya makampuni na watu binafsi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna taarifa za kugunduliwa kwa madini ya urani (*uranium*) katika maeneo mbalimbali nchini na kwamba uchimbaji wa madini hayo unaanza hivi karibuni. Kwa kuwa madini haya yanahitaji uangalifu mkubwa na usalama wake usipozingatiwa athari zake ni kubwa sana kwa afya ya watu na viumbe wengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na unyeti wa suala hili, Kamati inashauri itungwe sheria na kanuni za uchimbaji na matumizi ya madini haya ili shughuli hiyo iweze kuleta manufaa katika maendeleo ya nchini yetu. Ifahamike kuwa mionzi ya madini haya na nishati ya nyuklia ni suala linalotatiza dunia kwa sasa na mataifa yaliyoendelea yanafanya juhudhi ya kutafuta nishati mbadala ili kuepuka au kupunguza matumizi ya nishati inayotokana na nyuklia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kushughulikia uchimbaji wa madini haya, kuwe na uhusiano wa karibu baina ya Wizara ya Nishati na Madini na Tume ya Nguvu za Atomiki ili kuratibu shughuli za uchimbaji na uhifadhi salama wa madini ya urani. Aidha, kuwepo na maandalizi ya kutosha ya wataalamu wa nguvu za Atomiki ili kuhakikisha usalama wa madini hayo na uandaaji wa mikataba mizuri yenye maslahi kwa Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kwenda na wakati katika ulimwengu wa sayansi na teknolojia hasa katika masuala ya *TEKNOHAMA*, Kamati inashauri Ofisi ya Bunge na Wabunge waanze kutumia mfumo wa kompyuta katika kufanya mawasiliano na kupeana nyaraka mbalimbali. Mfumo huu utapunguza Wabunge kubeba nyaraka nyingi badala yake nyaraka zitatumwa kwenye mtandao na kuwawezesha kusoma humo au kuzichapisha zile anazozihitaji tu. Gharama ya kuingia katika mfumo huu ni ndogo kwani kila Mbunge anahitaji kutumia Dola za Kimarekani 1500 kwa miaka mitano ambazo zitapunguza gherama za machapisho kwa Ofisi ya Bunge na Serikali kwa ujumla. *We must now walk the talk. (Makof)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, maombi ya fedha kwa mwaka wa fedha 2011/2012 ili Wizara ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia iweze kutekeleza majukumu yake kwa mwaka 2011/2012, inaomba iidhinishiwe jumla ya Sh. 64,017,516,000/. Kati ya hizo,

fedha za Matumizi ya Kawaida ni Sh. 23,799,259,000/=. Aidha fedha za Bajeti ya Maendeleo zinazoombwa ni Sh. 40,218,257,000/=, kati ya hizo Sh. 38,195,679,000/= ni fedha za ndani na Sh. 2,022,578,000/= ni fedha za nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati yangu ilipitia na kujadili kwa kina Makadirio ya Bajeti ya Wizara hii na kupitia kifungu kwa kifungu na kuridhika nayo na sasa naliomba Bunge lako Tukufu likubali kujadili na kupitisha maombi hayo yenye jumla ya Sh. 64,017,516,000/= kwa ajili ya matumizi ya kawaida na maendeleo kwa mwaka wa fedha wa 2011/2012.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, Kamati yetu inaamini kwa dhati kabisa kwamba Sekta ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia ndiyo mhimili wa maendeleo na uchumi wa kisasa tunaotaka kuujenga. Hapa nchini sasa hivi, simu ya mkononi siyo tu kwa ajlii ya kuzungumza, bali ni benki ya kuhifadhi na kutuma fedha, ni kiungo cha kuingia kwenye mtandao wa *internet*, na kiungo cha kupata taarifa mbalimbali, ikiwemo bei za mazao, milipuko ya magonjwa na mambo mengineyo muhimu kwa ustawi wa maisha ya Mtanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mawasiliano ni uwezeshaji muhimu kama ilivyo mitaji. Mawasiliano ni kivutio cha uwekezaji. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa msingi huo, kama nchi yetu inataka kupiga hatua ya maendeleo kwa haraka, ni lazima mawasiliano yapatikane kwa watu wote na kwa gharama wanayoweza kuimudu. Kwa sasa, hali siyo hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuhitimisha, napenda kukushukuru wewe binafsi kwa kunipa nafasi hii ya kuwasilisha Taarifa ya Kamati yangu mbele ya Bunge lako Tukufu. Aidha, nawashukuru pia Mheshimiwa Prof. Makame Mnyaa Mbarawa - Waziri wa Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia, Mheshimiwa Charles Muhangwa Kitwanga - Naibu Waziri wa Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia, Dkt. Florens M. Turuka - Katibu Mkuu wa Wizara ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia pamoja na Wataalam wote wa Wizara hii na Taasisi zilizo chini yake kwa ushirikiano wao ambao umeiwezesha Kamati hii kutekeleza majukumu yake na kuwasilisha Taarifa hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba pia niwashukuru Wajumbe wenzangu wa Kamati hii kwa busara zao, hasa kwa kutekeleza kazi za Kamati kwa umahiri na umakini mkubwa. Ushirikiano wao na kujituma bila kuchoka kwa kupitia na kuchambua mpango na Makadirio ya Bajeti ya Wizara hii na hivyo kufanikisha Taarifa hii ambayo kwa niaba yao naiwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu. Naomba niwatambue kwa kuwataja majina kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Peter J. Serukamba – Mwenyekiti na Mheshimiwa Anne K. Malecela –Makamu Mwenyekiti. Wajumbe walikuwa ni Mheshimiwa Saidi Amour Arfi, Mheshimiwa Lolesia J. M. Bukwimba, Mheshimiwa Herbert J. Mtangi, Mheshimiwa Juma S. Juma, Mheshimiwa Ritta Mlaki ambaye ndiye mimi hapa, Mheshimiwa Ritta E. Kabati, Mheshimiwa Innocent E. Kalogeresi, Mheshimiwa Rosweeter F. Kasikila,

Mheshimiwa Raya I. Khamis, Mheshimiwa Mkiwa A. Kimwanga, Mheshimiwa Moses J. Machali, Mheshimiwa Salvatory N. Machemli, Mheshimiwa Mohamed Habib Juma Mnyaa, Mheshimiwa Eng. Ramo M. Makani, Mheshimiwa Regia E. Mtema, Mjumbe, Mheshimiwa Rajab Mbarouk Mohammed, Mheshimiwa Faith M. Mitambo, Mheshimiwa Mtutura A. Mtutura, Mheshimiwa Suleiman Nassib Omar, Mheshimiwa Henry D. Shekifu, Mheshimiwa Grace S. Kiwelu, Mheshimiwa Haroub Muhammed Shamis, Mheshimiwa Ahmed Mabkhut Shabiby, Mheshimiwa Jeremiah S. Sumari, Mheshimiwa Rukia K. Ahmed, Mheshimiwa Prof. Juma A. Kapuya na Mheshimiwa Prof. Kulikoyela K.Kahigi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa, nachukua fursa hii pia kumshukuru Katibu wa Bunge - Dkt. Thomas Didimu Kashillah, Katibu wa Kamati - Ndugu Angumbwike Lameck Ng'wavi kwa kuihudumia Kamati ipasavyo na kufanikisha maandalizi ya Taarifa hii kwa wakati. Aidha, nawashukuru Watendaji wote wa Ofisi ya Bunge kwa ushirikiano wao mzuri wa kuiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi mkubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa, shukrani za pekee ziwaendee Wapigakura wangu wa Jimbo la Kigoma Mjini kwa kuniamini na kunichagua tena kuwa Mbunge wao kwa miaka mitano ijayo. Nawaahidi kuwa nitaendelea kuwatumi kia kwa uaminifu na uadilifu mkubwa ili kwa kushirikiana nao tuweze kuleta maendeleo katika Jimbo la Kigoma Mjini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati ya Bunge ya Miundombinu, naomba kuwasilisha na ninaunga mkono hoja. (*Makofi*)

MHE. PROF. KALIKOYELA K. KAHIGI - MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI KWA WIZARA YA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nachukua fursa hii kuwasilisha maoni na mapendekezo ya Kambi ya Upinzani kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia 2011/2012, kwa mujibu wa Kanuni za Bunge, Kanuni ya 99(7) Toleo la Mwaka 2007.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, na kwa heshima kubwa, naushukuru uongozi wetu wote wa Kambi Rasmi ya Upinzani chini ya Mheshimiwa Freeman Aikael Mbowe, Naibu wake Mheshimiwa Kabwe Zuberi Zitto - Mnadhimu wa Kambi Mheshimiwa Tundu Lissu, pamoja na Wabunge wenzangu wote kwa imani yao kwangu na kwa ushirikiano mkubwa wanaonipa katika kutekeleza wajibu wangu wa Kibunge na huu wa Uwaziri Kivuli. Nawashukuru pia wanachama wenzangu ambao hawasiti kunitia moyo katika kutekeleza majukumu yangu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru pia wewe kwa kunipa wasaa huu kutoa maoni ya Kambi ya Upinzani ili kufanikisha lengo letu la kukomaza demokrasia ya kweli katika nchi hii na kuchochea maendeleo ya haraka kwa Watanzania wote. Kadhalika, nakutia moyo uendelee kuongoza kwa busara, weledi na uelekevu Bunge hili la Kumi

lenye changamoto lukuki, na nakutia moyo uendelee kuliongoza kwa busara, weledi na uelekevu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawashukuru wananchi wa Jimbo la Bukombe kwa imani waliyonayo kwangu na ushirikiano ambao wameendelea kuuonyesha. Ninawaahidi kwamba nitaendelea kuwatumikia kwa dhati kama nilivyowaahidi. Mwisho, nawashukuru mke wangu, Selina Tibagololwa na wanangu Kwelukilwa, Kekutogwa, Kwesiga na Kwizigizya, kwa uvumilivu, moyo wa upendo na uelewa walioonyesha wakati wote nikiwa katika majukumu ya kuwatumikia wananchi. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, namaliza utangulizi huu kwa kuwapongeza Waziri wa Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia – Mheshimiwa Prof. Makame Mnyaa Mbarawa, Naibu Waziri - Mheshimiwa Charles Muhangwa Kitwanga na timu yao ya wataalamu mahiri kwa kazi nzuri ambayo wameifanya kwa kuandaa hotuba yao. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nafasi ya Sayansi na Teknolojia katika maendeleo ya nchi, Kambi Upinzani inataka kusisitiza kuwa tofauti kubwa kuliko zote ya kimaendeleo baina ya nchi zilizoendelea na nchi ambazo zinaendelea hukutwa katika mambo mawili:-

- Ubora na Uelevu wa Elimu ya Sayansi na Teknolojia na uimara wa Vyuo na Taasisi za kisayansi; na
- Kiwango cha usambaaji na utumiaji wa sayansi na teknolojia katika maeneo mbalimbali ya maisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi huanza kupiga hatua za kimaendeleo inapokamilisha zoezi la kuhawilisha sayansi na teknolojia katika maeneo mbalimbali ya uchumi na maisha, mijini na vijijini, na kuanza kufanya ugunduzi katika maeneo mbalimbali ambayo yanalenga utatuzi wa matatizo yanayowakabili wananchi wake. Bila kufanya hivyo, maendeleo hayafiki mbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia ina shughuli kuu mbili:-

- Kukuza Teknolojia ya Mawasiliano katika vipengele vyake vyote; na
- Kukuza Sayansi na Teknolojia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukuzaji unaosemwa hapa unajumuisha usambaaji kote nchini. Maendeleo katika nyanja hizi hadi sasa yanatia moyo, lakini bado kuna changamoto nyingi. Hapa nitagusia baadhi ya changamoto hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto kubwa inayoikabili Sekta ya Sayansi na Teknolojia ni uhauwilishaji wa matokeo ya Sayansi na Teknolojia hasa kufika vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sayansi, Teknolojia na Ubunifu eneo la sayansi na teknolojia linazo taasisi na vituo vyatufitit vyatufitit umma takriban 90, ambavyo vinashirikishwa na Tume ya Sayansi na Teknolojia. Taasisi na vituo hivi hushirikisha Sekta ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi, Viwanda na Nishati, Maliasili, Afya, na Vyuo Vikuu. Kuna Sera, Sheria, Kanuni na Taratibu mbalimbali ambazo zinaelekeza utendajikazi katika taasisi na vyuo hivi. Kwa hakika bado kuna changamoto nyingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja ya majukumu ya Idara ya Sayansi, Teknolojia na Ubunifu, ni kuratibu shughuli za utafitit na maendeleo nchini na kuratibu utekelezaji wa Programu ya Mageuzi ya Sayansi, Teknolojia na Ubunifu. Kambi ya Upinzani hairidhishwi na hali halisi ya utekelezaji wa majukumu haya, kwani matokeo yake hayaonekani katika maisha ya kila siku ya wananchi. Bado Taifa letu liko nyuma katika uhawilishaji au usambaaji wa matunda ya sayansi na teknolojia na pia ubunifu wa kiteknolojia ikilinganishwa na Mataifa mengi duniani. Tumeshindwa hata kueneza na kutumia maarifa na ujuzi wa kiteknolojia ambaao tayari tunao.

Mheshimiwa Spika, nitoe mfano. Nchi yetu ina tatizo kubwa la nishati ya umeme, ni asilimia 14 tu ya Watanzania ndio wanaotumia nishati ya umeme. Hali ni mbaya zaidi vijijini wanakoishi karibu asilimia 80 ya wananchi wote ambako ni asilimia 2.5 tu ya wananchi ndiyo wanaotumia nishati ya umeme. Wakati tatizo la umeme likiwa kubwa kiasi hicho, bado Serikali kuitia wataalam wake haijaweza kueneza kwa mpangilio matumizi ya nishati mbadala, rahisi na nafuu za umeme kama *biogas* na nishati ya umeme wa juu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati wakulima wetu, wafugaji na wavuvi, wanataabika kwa kukosa zana na vifaa bora vyatufitit kutendea kazi na kuboresha uzalishaji wao na hivyo kukosa masoko ya uhakika ya kuuza wanachozalisha au kikitengeneza, wakati wananchi wengi hususan wa vijijini wanaishi katika makazi duni yasiyokuwa na nishati bora ya kuendeshea maisha yao ya kila siku. Hali halisi inaonyesha kuwa Vyuo vyatufitit Ufundu, Taasisi za kiteknolojia na wataalam wetu wanayo maarifa, ujuzi na ugunduzi muhimu wa kiteknolojia yanayoweza kabisa kurahisisha kazi na kuongeza ubora na thamani ya mazao na bidhaa mbalimbali zinazozalishwa na wananchi, lakini ujuzi na wataalam huo hautumiki kwa sababu haujaenezwa kwa wananchi.

Mheshimiwa Spika, katika maoni ya Kambi ya Upinzani kuhusu Azimio la Kuridhia Itifaki ya Sayansi, Teknolojia na Ubunifu ya Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika katika Mkutano wa tatu, tulisema kuwa uhawilishaji wa sayansi na teknolojia ni kiungo dhaiyu katika shughuli za ukuzaji sayansi hapa nchini. Uhawilishaji ambaao umekuwa ukifanywa na taasisi au watu mbalimbali haukupangwa, ni wa kubahatisha tu. Ni muhimu Serikali ikatambua hilo na kuandaa mipango ya kulishughulikia kwa mpangilio mzuri na makini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sayansi na Teknolojia Shuleni/Vyuoni, Kambi ya Upinzani ilitoa rai kwa Serikali kwa mwaka uliopita wa fedha kuwa pamoja na kuongeza udahili kwa wanafunzi wanaodahiliwa kusomea masomo ya sayansi, udahili huo uende uambatane na huduma zinazohitajika zikiwemo madarasa ya kutosha, maktaba zenye

vitabu, maabara zenyenye vifaa vya kutosha, karakana zenyenye vifaa vinavyokidhi kwa mafunzo na viwango vinavyokubalika katika karne hii ya sayansi na teknolojia. Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali kutoa majibu kama ilizingatia ushauri huo na hatua za kimaendeleo zilizofikiwa mpaka sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sekta ya Mawasiliano inayosimamiwa na Mamlaka ya Udhibiti wa Mawasiliano ya Tanzania (*TCRA*), na inayohusisha Shirika la Posta (*TPC*) na Kampuni ya Simu Tanzania (*TTCL*) na makampuni ya simu za mikononi za kigeni, ni sekta inayopanuka haraka sana. Tayari Serikali imeshaandaa sera, sheria na kanuni zake, na utaratibu wa leseni mbalimbali ambavyo hutumika katika usimamizi wa shughuli katika sekta hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2011/2012, Wizara, pamoja na mambo mengi mengine, inalenga kushughulikia miradi ifuatayo kama ilivyoelezwa na Waziri:-

- Kutekeleza Mradi wa Kitaifa wa Anwani za makazi na Simbo za Posta;
- Kutekeleza mageuzi kutoka analogia kwenda digitali katika teknolojia ya utangazaji hadi ifikapo Desemba, 2013;
- Kuratibu uanzishaji na uendelezaji wa vituo vya mawasiliano ya kijamii;
- Kusimamia Kampuni ya Simu Tanzania, Shirika la Posta Tanzania, Mamlaka ya Udhibiti wa Mawasiliano Tanzania na Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote;
- Kutafuta mitaji kwa Kampuni ya Simu Tanzania na Shirika la Posta Tanzania kwa sababu yako hoi;
- Kukuza ubunifu katika Sekta ya Mawasiliano kwa wajasiriamali wadogo wadogo;
- Kuanzisha Tume ya *TEHAMA*; na
- Kuendelea na ujenzi wa Mkongo wa Mawasiliano wa Taifa ili kuunganisha Makao Makuu ya Mikoa na Wilaya, Shule za Msingi na Sekondari zote nchini, Vyuo Vikuu na Vituo vya Utafiti, hospitali zote nchini, na Wizara 15, Taasisi 50 za Serikali, na Vyuo Vikuu na Vituo vya Utafiti 27.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inaihimiza Wizara iyape kipaumbele mambo yafuatayo ili yakamilike mwaka 2011/2012:-

- Wizara ikamilishe ujenzi wa Mkongo wa Taifa ili vikwazo vya kimawasiliano vilivyokuwepo viishe kabisa, na Taifa liwe limeunganishwa kwa Mkongo;
- Wizara itafute mitaji ya kutosha ili Kampuni ya Simu Tanzania na Shirika la Posta Tanzania viweze kuijendesha bila matatizo;

· Tume ya *TEHAMA* ianzishwe, pamoja na kurekebisha Sera ya *TEHAMA* ya mwaka 2003;

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani pia inaihimiza Wizara iongeze kasi katika miradi ifuatayo:-

- Mradi wa Kitaifa wa Anwani za Makazi na Simbo za Posta uharakishwe kwani matatizo mengi yahusuyo ulipaji kodi, vitambulisho, usalama, huduma za mawasiliano, bima, na kadhalika, yatapungua sana au kuisha, na Taifa litakuwa la kisasa;
- Kasi iongezwe katika Mradi wa Vituo vya Mawasiliano kwa sababu ni maeneo machache tu yaliyo na vituo hivyo. Wizara ishawishi sekta binafsi, hasa mashirika ya huduma za simu za mkononi, ili yashiriki kikamilifu katika mradi huu; na
- Wizara iandae mpango mkakati wa kukuza ubunifu katika Sekta ya Mawasiliano.

Mheshimiwa Spika, simu ya mkononi imeleta mapinduzi katika uhabarishanaji, yaani ufikishaji na usambazaji wa taarifa baina ya watu vijijini na mijini, hali ambayo haikuwepo kabla ya ugunduzi wa simu za mkononi. Jambo la kufurahisha ni kwamba hivi sasa simu hizi zinatumika sana vijijini. Kwa wengi, ni nyenzo ya kupata/kutoa habari ambazo haziwezi kupatikana/kutolewa kwa haraka kwa njia nyingine katika mazingira ya vijijini, ambako hakuna umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, idadi ya watumiaji wa simu za viganjani hapa nchini iliongezeka kutoka 17,469,486 mwaka 2009, hadi kufikia watumiaji 20,983,853 Desemba, 2010. Idadi ya watumiaji wa huduma za tovuti (*internet*) iliongezeka kutoka watumiaji 4,378,392 mwaka 2009 hadi kufikia watumiaji 4,956,000 mwaka 2010. Hadi Desemba, 2010, jumla ya namba za simu za mkononi 19,000,000 zilikuwa zimesajiliwa hapa nchini. Taarifa hii ni kwa mujibu wa *TCRA*.

Mheshimiwa Spika, takwimu hizi za Serikali zinaonyesha wazi kuwa takriban nusu ya Watanzania kwa sasa wanamiliki simu za mkononi na hivyo wanaweza kuwasiliana kwa kutumia simu. Ni wakati muafaka sasa simu hizo zikawa chanzo cha kuweza kupata taarifa muhimu kwa ajili ya kuweza kuongeza uchumi na kukuza kipato kwa wananchi wetu. Ili kuhakikisha kuwa hilo linafanyika, tunaitaka Serikali, kwa kushirikisha Wizara mbalimbali Wizara hii, Wizara ya Afya, Wizara ya Kilimo na Mifugo, na kadhalika, iandae mpango wa kutoa taarifa muhimu kuhusu shughuli za kiuchumi vijijini. Sambamba na hilo, Serikali iyashawishi makampuni ya huduma za simu yaandae utaratibu wa kutoa taarifa hizo.

Mheshimiwa Spika, mpango huu tunaopendekeza umelenga kuwapa wakulima na wafugaji maarifa muhimu ili waboreshe uzalishaji. Ili kufanikisha mpango huu, Kambi ya Upinzani inapendekeza mambo yafuatayo yafanyike:-

- (i) Serikali, kupitia Wizara husika, ianze kutengeneza taarifa mahsusini kuhusiana na kilimo pamoja na ufugaji wa kisasa, na taarifa hizi ziwe ni kwa wakulima kuweza kujua mbinu mbalimbali za kuweza kukuza kilimo na mifugo yao.
- (ii) Taarifa hizi ziwe na mambo yafuatayo: dalili za magonjwa mbalimbali kwa mimea na mifugo, dawa za kuweza kutibu maradhi /magonjwa hayo, taarifa za masoko ya mazao ya ndani na nje, taarifa za hali ya hewa, na taarifa nyingine. (*Makofit*)
- (iii) Taarifa hizi zitumwe kwa Makampuni ya simu, ziingizwe kwenye mfumo wao, kisha zisambazwe kwa watumiaji wa simu za mkononi. Taarifa hizi zinaweza pia kuhusu eneo la afya, elimu na maeneo mengine ambayo yanaweza kuwasaidia wananchi.

Kambi ya Upinzani inaamini kuwa jambo hili linawezekana kama likipangwa vizuri. Kwa hiyo, simu ya mkononi inaweza kuwa mojawapo ya nyenzo ya kuwaelimisha wananchi. Mpango kama huu umetekelizwa China, na kwa taarifa tulizo nazo, umeonyesha mafanikio.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uuzwaji wa makampuni ya simu. Mojawapo ya matatizo ambayo Serikali inapaswa kuyashughulikia kikamilifu ni ukwepaji wa kodi wa makampuni ya simu yanayouzwa bila Serikali kupata kodi. Mathalani, kampuni ya *Celtel International* ilifungua kampuni huko Netherlands (*Celtel Tanzania BV*) ambayo ndio inamiliiki *Celtel Tanzania Limited*. Kama tunavyofahamu *Celtel* iliuzwa kwa kampuni ya Zain na baadaye kwenda Airtel. Serikali haikupata chochote katika mabadiliko haya ya wamiliki. Kufuatana na mikakati ya kiumiliki, kila mara kampuni hii ilipouzwa Serikali haikuweza kukusanya kodi yake na fedha ilikuwa nyingi. Kwa mfano, kwenye mauzo ya Zain kwenda Airtel, Serikali ingeweza kukusanya dola za Kimarekani 312 milioni. Hata uuzwaji wa Kampuni ya Vodacom ya Afrika Kusini kwenda kwa Kampuni ya Vodafone ya Uingereza hajjawekwa wazi kama Serikali ilipata chochote kutokana na uuzwaji huu. Makampuni haya yanafanya biashara humu nchini na kuuziana biashara bila Serikali kuingilia kati na kukusanya mapato.

Mheshimiwa Mwenyekiti, majibu ya haraka ya Serikali yanaweza kuwa kwamba Sheria zilizopo haziruhusu kutoza kodi au kuingilia kati uuzwaji wa kampuni au kuwa wakiweka njia za kuyatoza kodi makampuni haya inaenda kinyume na Sera za Taifa za Kuvutia Wawekezaji. Kambi ya Upinzani, inaishauri Serikali kufanya mabadiliko ya Sheria mapema iwezekanavyo ili iwe inatoza kodi makampuni yanapouzwa. Hatua hii itasahihisha kosa ambalo lilifanyika mwanzoni tulipoanza Sera ya kuruhusu sekta binafsi kushiriki katika biashara ya mawasiliano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (*TCRA*). Pamoja na mafanikio ya kusajili watumiaji wa simu za mkononi yaliyoainishwa kwenye Taarifa ya Hali ya Uchumi ya mwaka 2010 kuhusu Mamlaka, Kambi ya Upinzani inatoa rai kwa Mamlaka kuwa makini zaidi na uratibu wa masuala ya mawasiliano hasa kipindi hiki ambacho kuna ongezeko kubwa la watumiaji wa simu za mikononi na ongezeko la idhaa

za redio za watu binafsi ambazo zinaanzishwa kwa malengo tofautitofauti. Kuna kila haja Mamlaka kuhakikisha kuwa maagizo wanayoyatoa yanatekelezwa na makampuni ya simu na vituo vya redio ili kufanya Mamlaka kuwa na nguvu ya kuratibu mawasiliano nchini kuendana na tamaduni zetu na taratibu zilizopo. Wakiukaji wa tamaduni na taratibu hizo waadhibiwe kama wanavyostahiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Makampuni ya simu na huduma za fedha. Taarifa ya Hali ya Uchumi iliyowasilishwa na Waziri wa Fedha hapa Bungeni ilionyesha kuwa idadi ya Watanzania wanaotumia simu za mkononi imeongezeka mwaka hadi mwaka. Pamoja na ongezeko hilo, Kambi ya Upinzani ina mambo kadhaa ambayo inabidi Serikali iyatolee maelezo. Mambo haya ni pamoja na:-

- Gharama kubwa zinazotozwa na makampuni hayo kwa watumiaji.
- Makampuni kuendesha kamari kwa watumiaji na kuwatoza fedha nyingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, je, Serikali inaratibu vipi gharama hizi na kamari ambazo zinazotozwa na makampuni hayo ya simu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kuwa Serikali ilishatoa agizo kwa makampuni haya kuacha kuweka gharama nafuu nyakati za usiku, lakini ukweli ni kuwa bado hali hiyo inaendelea na agizo hilo halijatekelezwa. Serikali inapaswa kufuatilia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, matumizi ya huduma za fedha kwa kutumia mitandao ya simu yameongezeka sana katika siku za karibuni. Hivi sasa kuna huduma za M-PESA, ZAP, Z-PESA na TIGO PESA na inawezekana na nyingine zimeshaanza leo asubuhi au hata zitaanza kesho. Pamoja na kuwepo kwa Sheria zinazoratibu masuala ya kifedha nchini, mathalani Sheria ya Benki Kuu ya mwaka 2006, Sheria ya Benki na Taasisi za Fedha ya mwaka 2006 na pia Sheria inayounda Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania, bado hakuna uratibu wa moja kwa moja unaolenga kuyasimamia na kuyaongoza makampuni haya ya simu katika kutoa huduma kwa wateja wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni ukweli usiopingika kuwa uchumi wa kati unajengwa kwa watu wengi kushiriki katika taasisi za kawaida za benki, lakini kwa Tanzania ni asilimia chache sana ya watu ambao wanapata huduma hizi. Hili limepelekea kuongezeka kwa watumiaji wa huduma za kielektroniki za kutuma na kupokea fedha zinazotolewa na makampuni ya simu. Tumeshuhudia hata huduma za jamii na taasisi zingine za Kiserikali kama *TANESCO* na *DAWASCO* kuanza kutumia makampuni ya simu badala ya benki. Kambi ya Upinzani inashauri Serikali ama kutunga Sheria au kufanya marekebisho ya Sheria zilizopo ili ziweze kuratibu matumizi haya ya huduma hii ya fedha kwa kuwa inawezekana kabisa Serikali inashindwa kupata mapato kwa sababu tu hakuna Sheria inayoelekeza hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali kadhalika tunaishauri Serikali kutoa maelezo kama Mamlaka ya Mawasiliano imeshaanza kuchukua hatua ya kuratibu huduma hizi za fedha kwa njia ya mitandao ya simu. Ninavyofahamu, katika Sheria inayounda Mamlaka hii, hakuna kipengele kinachoyaruhusu moja kwa moja makampuni haya kutoa huduma hizi

za pesa. Hata hivyo, Mamlaka ina uwezo wa kutunga Kanuni zinazoratibu huduma hizi na kumlinda mteja kwa kuwa hata Sheria ya Ushahidi, Sura ya 6, pamoja na kufanyiwa marekebisho ili kukidhi haja ya ushahidi wa kielektroniki, bado ina upungufu mkubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA). Kambi ya Upinzani katika hotuba zake mbalimbali za nyuma, toka 2009/2010 - 2010/2011, imekuwa ikiitaka Serikali iweke mkakati wa makusudi wa kuhakikisha kuwa matumizi ya TEHAMA (*ICT*) yanatiliwa mkazo na kuhakikisha mitaala inaandaliwa na kutekelezwa hatua kwa hatua, pamoja na kuhakikisha umeme vijijini unapatikana. Pamoja na agizo la Rais kuanza mpango wa kutumia Teknolojia ya Mawasiliano katika kutoa elimu nchini, bado tunaona kuwa agizo hili litaendelea kuwa ni ndoto tu kama utekelezaji wake hautapangwa vizuri na kwa makini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Shirika la Posta Tanzania. Ingawa Shirika hili bado ni muhimu likiwa ni Shirika linalobeba bendera ya nchi, lakini Taarifa ya Hali ya Uchumi ya mwaka 2010 ilibainisha kuwa Shirika hili liko hoi bin tabani. Shirika lina upungufu ufuatao:-

- kupungua kwa kusafirishwa kwa vifurushi ndani ya nchi kulikotokana na kuongezeka kwa ushindani wa makampuni ya binafsi.
- ukosefu wa nyenzo za magari ya kukusanya vifurushi.
- kupungua kwa utumaji wa fedha ndani ya nchi kwa njia ya haraka.
- Utumaji wa telegramu umepungua.
- Uuzaji wa stempu nao umepungua.
- Ushindani kutoka kwa makampuni ya simu.
- utumaji wa ujumbe wa haraka wa barua-pepe.
- utumiaji wa mitandao ya M-PESA na kadhalika kutuma fedha badala ya posta. Yote haya yameathiri Shirika la Posta kiasi kwamba siku hizi liko hoi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani imebaini kuwa hata Kamati ya Bunge ya Mashirika ya Umma iligundua kuwa Shirika hilo limekuwa likijiendesa kwa hasara na linakabiliwa na madeni yenye thamani ya zaidi ya shilingi bilioni 2.1. Hali hiyo imesababisha hata wafanyakazi wa Shirika hilo kuanza kukosa mishahara, hivyo kuishi katika mazingira magumu sana. Aidha, hali hiyo imesababishwa na utendaji duni wa Shirika hilo na hivyo kuendelea kudidimia katika ufanisi, hali hiyo haiwezi kuvumiliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya upinzani inaunga mkono pendekeso la Kamati ya Bunge ya Mashirika ya Umma la kumwagiza Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (*CAG*) kufanya uchunguzi maalumu wa madeni yote ya Shirika la Posta yakiwemo ya rasilimali za viwanja na nyumba za shirika hilo. Kambi ya Upinzani, inaitaka Serikali kufanya hivyo mapema ili kuokoa fedha nydingi za umma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani inahoji Serikali imechukua hatua gani kuhusu ushauri tuliofa katika hotuba yetu ya mwaka jana kuwa Serikali ifanye maamuzi ya haraka kulinusuru Shirika hili kwa kulipa Mtaji na Dhamana ya Serikali (*Government Guarantee*) ili Shirika liweze kupata mikopo toka Taasisi za Fedha na kuweza kujiendesha kwa ufanisi pamoja na kufanya ukaguzi maalumu wa kifedha ili kuongeza ufanisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Alama na Anuani za Posta, Kambi ya Upinzani inaendelea kusisitiza kuwa ina mashaka sana juu ya mafanikio ya mpango huu kuanza katika miji iliyopangwa yaani Arusha na Dodoma, haitatoa picha halisi kuhusu maeneo mengine ambayo hayajapangwa hususani Jiji la Dar es Salaam. Kambi ya Upinzani inahoji kuhusu maendeleo ya mradi huu, gharama zilizotumika na tungependa kuona mpangomkakati wa mradi huu kwa Taifa zima. Kadhalika, kama Serikali inataka kufaulu katika maeneo mengi, ingefaa kuanzia katika Jiji gumu la Dar es Salaam ili ijifunze namna ya kushughulikia changamoto mbalimbali, hasa kutokana na ujenzi holela unaoendelea, ambao unaweza kufanya uwekaji wa anuani hizi kuwa mgumu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tume ya Sayansi Tanzania (*COSTECH*). Kambi ya Upinzani iliridhia kwa dhati kabisa Itifaki ya Sayansi, Teknolojia na Ubunifu ya Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika (*SADC*) ili kukuza ushirikiano, maendeleo, uhawilishaji na umahiri wa sayansi, teknolojia na bidaa/ubunifu/ugunduzi katika Mkutano wa Tatu wa Bunge. Tunapenda kusisitiza kuwa Tume ya Sayansi na Teknolojia ina jukumu kubwa la kutekeleza Itifaki hiyo. Katika kutekeleza hilo, Kambi ya Upinzani tunaishauri Serikali iendelee kuipa fedha ya kutosha Tume ya Sayansi na Teknolojia ili iweze kuratibu masuala mbalimbali ya sayansi nchini kwa ufanisi. Hata hivyo, tunaitaka Serikali kuitia upya Sera ya Sayansi na Teknolojia ili kuhimili changamoto mbalimbali za sayansi zilizopo kwa sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaelewa umuhimu wa Tume hii ya Sayansi na Teknolojia, lakini tunaomba kuelezwu kwa kina ni suala gani linaloonekana lililofanyika kwa bajeti ya maendeleo iliyotengwa kwa mwaka wa fedha 2009/2010 shilingi milioni 200 kama fedha za ndani na fedha za nje shilingi milioni 321.2, mwaka 2010/2011 shilingi bilioni 30.2 fedha za ndani na fedha za nje shilingi milioni 596.9. Mwaka huu shilingi bilioni 25.97 fedha za ndani na shilingi milioni 875.95 fedha za nje. Kambi ya Upinzani kabla ya kuidhinisha kiasi kingine kikubwa cha fedha kama kinavyoombwa na Serikali kwa ajili ya maendeleo kwenye Kitabu cha Miradi ya Maendeleo, *Volume 1V*, Fungu 68, Kasma 6345 cha zaidi ya shilingi bilioni 26.8, tungependa kupata taarifa ya kina ya jinsi *COSTECH* walivyotumia fedha za mwaka jana na ni miradi gani ilifanyiwa kazi na iko katika hatua gani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ubunifu/ugunduzi ni miiongoni mwa mambo ambayo hayakupangwa vizuri hapa nchini. Katika taratibu za Tume ya Sayansi na Vituo vingine vya Utafiti, hakuna namna ya kumsaidia na kumuendeleza mgunduzi/mvumbuzi ambaye ameonyesha uwezo wa kufanya hivyo. Wapo wagunduzi/wavumbuzi wengi ambao wameshaonyesha uwezo wao katika sehemu mbalimbali za nchi lakini hakuna taarifa

kama walitambuliwa na kuendelezwa na Tume hii. Tume iandae utaratibu wa kuwatambua wagunduzi, si wale tu walio katika Vyuo Vikuu au Taasisi za Utafiti, bali hata wale ambao hawakupata bahati ya kupata elimu ya juu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tume ya Nguvu za Atomiki. Zipo taarifa za kuwepo kwa wawekezaji wakubwa wanaofanya utafiti na uchimbaji wa *urani* (*uranium*) katika Hifadhi ya Selous (Mkuju, Namtumbo - Songea). Taarifa hizo zinasema kwamba wananchi wanaokaa maeneo hayo hawakushirikishwa na baadhi ya wananchi wameshaanza kuathirika kutokana na madini hayo ya urani. Tunashauri Serikali iiagize Tume ya Nguvu za Atomiki iende ifanye utafiti kuhusu hatari iliyopo katika machimbo ya urani ili kupata ukweli na kutoa ushauri juu ya hatua za kuchukua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi sasa Tume ya Nguvu za Atomiki imeshafanya kazi nzuri. Kambi ya Upinzani inakumbushia ushauri uliotolewa mwaka wa fedha uliopita kuwa wafanyakazi wa Tume hii wapewe Posho ya Mazingira Hatarishi (*Risk Allowance*) na Bima ya Mazingira Hatarishi. Tutaomba maelezo ya Serikali kama tayari imeshazingatia ushauri huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Kambi ya Upinzani, naomba kuwasilisha. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Nakushukuru sana Mheshimiwa *Professor* na kwa kweli leo tumetambua hata majina ya watoto wako kwa kweli ni kiboko, tunakushukuru sana kwa kuwasilisha taarifa hiyo. (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa *Professor* kwenye hotuba yake maeneo mengine alikuwa anaruka, naomba *Hansard* irekodi hotuba nzima kama ilivyowasilishwa asubuhi Bungeni.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hilo, naomba sasa tuendelee na hatua inayofuata na hiyo ni ya uchangiaji wa jumla. Ninayo orodha ya majina ya wachangiaji watatu ambao hawajawahi kuchangia hotuba ye yote hapa ndani hata mara moja na hao ni kama wafuataao. Wa kwanza ni Mheshimiwa Rajabu Mbarouk Mohamed, wa pili Mheshimiwa Pudenciana Kikwembe na wa tatu ni Mheshimiwa Dtk. Maua Abedi Daftari. Kwa hiyo, naomba Mheshimiwa Rajabu Mbarouk aanze, Mheshimiwa Pudenciana Kikwembe ajiandae na Mheshimiwa Dkt. Maua Daftari atafuatia.

MHE. RAJABU MBAROUK MOHAMED: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi hii ya kwanza kuweza kuchangia katika Wizara hii ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia.

Kabla sijaanza kuingia ndani katika bajeti hii, nataka nifuate kwanza wosia wa kaka yangu, Mheshimiwa Mfutakamba na hii nataka nimueleze Waziri kwamba ‘kikia cha mbuzi hufyagia pale kinapolala’, lakini vilevile ni *forward message* ambayo nimeipata kwa Watanzania walio katika Visiwa viwili vya Ugunja na Pemba kwa Mheshimiwa Waziri kwamba ‘kawaida ya mwanaume huitwa bwana kwao’. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianzie na suala la *TTCL* pamoja na Posta katika Kisiwa cha Pemba. Mtanielewa, katika Tanzania yetu hii, Pemba ni eneo pekee yake ambalo hadi leo halina jengo la ofisi za *TTCL*. Likifuatiwa na Mikoa mipyä ambayo imeanzishwa sasa hivi, labda na Lindi na Lindi iko sababu maalum, jengo walikuwa nalo wameamua kulikodisha na wao wakakodi jengo lingine. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la wafanyakazi, wafanyakazi walioko katika Kisiwa cha Pemba wako katika hali mbaya. Shirika la *TTCL*, Posta Pemba hawana vitendea kazi, hawana ofisi hasa *TTCL* wanakodi sasa hivi, hawa watu hata kiwanja ambacho wanakimiliki wao wenyewe hawana. Kwa hiyo, nataka niiombe Wizara iliangularie suala hili kwa dhati na namwomba Waziri atakapokuja kufanya majumuisho yake aniambie ni lini ujenzi wa Ofisi ya *TTCL* Pemba utaanza. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile hawa Watendaji walioko Pemba mbali ya kwamba hawana vitendea kazi, usafiri hawana, lakini na mafao yao kwa kweli yanabidi yaangaliwe upya hasa kutokana na mazingira mazima ya utendaji wao kazi katika Kisiwa cha Pemba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la Mkongo wa Taifa, nampongeza Mheshimiwa Waziri kwa kuiona Pemba na kwa kukiona Kisiwa cha Unguja katika kuunganishwa na Mkongo wa Taifa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, navyofahamu mimi kwamba Mkongo ule umepitia katika *cable* ya umeme ambayo imetoka Tanga kwenda Pemba, ile *fibre* iko ndani yake. Sasa ile *fibre* mmiliki, ina maana ni Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar au Shirika la Umeme la Zanzibar. Namwomba Mheshimiwa Waziri ajaribu kuisaidia *TTCL* Pemba, atazame uwezekano wa kuingia mikataba na wamiliki wa hii *cable* ili Mkongo huu *TTCL* waweze kuutumia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa niende katika suala zima la sayansi na teknolojia. Kabla ya hapo, nataka nimpongeze Mheshimiwa Waziri kwa jinsi alivyoweza kusimamia suala zima la mawasiliano, lakini wakati huohuo nimpe pole kwa upande wa pili wa sayansi na teknolojia. Wizara imekwenda vizuri na inashikana na mwelekeo mzuri kwa upande wa mawasiliano na hii nafahamu kwamba inatokana na kwamba sekta binafsi zimejingiza zaidi katika suala zima la mawasiliano. Kwa hiyo, uwekezaji wa Serikali pale ni mdogo, ndiyo maana ukakuta sekta hii ya mawasiliano imekwenda vizuri lakini tuingie katika sekta ya sayansi na teknolojia. Nchi zote ambazo zimeendelea, zimeendelea kutokana na kujiiamarisha katika suala zima la sayansi na teknolojia, leo hii bila ya sayansi na teknolojia hakuna maendeleo katika nchi yoyote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa kuna changamoto kubwa. Nataka nilizungumzie hili kiundani kwanza kwa kuangalia bajeti nzima ya Wizara na hii inaonesha ni namna gani Serikali yetu haijawa *committed* katika suala zima la sayansi na teknolojia. Tumesikia Mheshimiwa Waziri kapangiwa bajeti ya shilingi bilioni 64 ambayo ni pungufu ya asilimia 9.8 ya bajeti iliyopita. Sasa kama lengo letu ni kwenda katika Mpango wetu wa Maendeleo hatuna budi hili kuliangalia upya. Tunampa mzigo Waziri,

tutakuja kumlaumu, lakini kwa sababu tu tumeshindwa kumpa nyenzo na yeze aweze kutekeleza majukumu yake kama itakavyotakiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna uvumbuzi na utafiti, hiki ni Kitengo ambacho kwa kweli kinahitaji kupewa nguvu ya ziada, lakini bahati mbaya katika bajeti yetu ya mwaka huu, sehemu hii haikuweza kutengewa fedha za kuonesha kweli Serikali ina dhamira ya kujikwamua au kuleta mapinduzi ya kimaendeleo katika nchi hii. Katika bajeti iliyopita, Kitengo hiki kilipangiwa shilingi bilioni 30, bahati mbaya hazikuweza kupatikana, cha ajabu ni kwamba safari hii wametengewa chini ya hapo, hatujui hali itakuwaje. Kwa kweli hii hali haionyeshi mwanga mzuri wa mbele tunakokwenda. Wengi tunasema kwamba Serikali hii ni Serikali sikivu, lakini kimtazamo wa uhalisia Serikali yetu iko kinyumenyume. Nina maana ya kuzungumza hilo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Rais ni Kiongozi wa Taifa, ni mtu ambaye anakubalika na ni mtu ambaye anakubalika Kimataifa. Ameweza kutoa agizo mara mbili kwa Wizara, lakini vilevile Mheshimiwa Rais alikutana na Marais wenzake katika SADC na wakakubaliana. Katika makubaliano yale akatakiwa Mheshimiwa Waziri alete pendekezo la kuiomba Bunge kuridhia *Protocol* ya Sayansi na Teknolojia katika uvumbuzi. Katika *Protocol* ile ambayo Rais alichukua jukumu na kukubali inasema kwamba lazima *one percent* ya *GDP* ya nchi itumike kwa ajili ya kuimarisha sekta nzima ya sayansi na teknolojia hususani katika ubunifu. Rais alipotembelea katika Wizara hii alitaka zitengwe shilingi bilioni 100 kwa sababu Rais alijua umuhimu wake lakini cha ajabu leo tunaambiya zimetengwa shilingi bilioni 25. Mheshimiwa Waziri bado unafanya nini katika Wizara hiyo hujajiuzulu mpaka leo? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri tunakuamini ni msomi, leo unapewa shilingi bilioni 25 wakati Rais wako amesema upewe shilingi bilioni 100! *Protocol* umetuletea, ukatuomba hapa Wabunge jamani ridhieni na tukakubali kukuridhia. Leo mnatuaibisha katika uso wa Kimataifa? Hili hatukubaliani nalo. Sisi wengine tutabeba bango kwa kweli kuwataka wananchi waikatae Serikali inayoongozwa na CCM ili wakipe madaraka Chama cha CUF kiweze kuleta mageuzi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, inashangaza kama tuna lengo kweli la kuleta mapinduzi ya kimaendeleo, leo Rais anatoa agizo, Watendaji hawalifuati. Tuna haja gani ya kuwepo? Nakuomba Mheshimiwa Waziri utakapokuja kutoa ufanuzi wako, hili suala utapatie maelezo ya kina, bila ya hivyo tutatoa zaidi ya shilingi. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sitaki nichukue muda mwangi ili na wenzangu waweeze kuchangia. Siungi mkono hoja hii hadi hapo nitakapopata maelezo ya kina, ahsante. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Nakushukuru sana Mheshimiwa Rajab Mbarouk Mohamed. Sasa hiyo ya kutoa zaidi ya shilingi, leo itakuwa kali. (*Kicheko*)

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na wale waliochangia mara moja kama nilivyosema, Mheshimiwa Pudenciana Kikwembe, halafu atafuatiwa na Mheshimiwa

Dkt. Maua Abeid Daftari, halafu tutaangalia muda wetu tuendelee na orodha ya wale ambao tayari wameshachangia mara moja.

MHE. PUDENCIANA W. KIKWEMBE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi hii na mimi niweze kuchangia.

Kwanza kabisa, napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuwezesha Waheshimiwa Wabunge wote tulipo humu ndani kupumua mpaka sasa hivi. Pili, napenda pia kumshukuru Mheshimiwa Waziri kwa hoja yake nzuri na maelezo mazuri aliyojatoa pamoja kuonyesha nguvu yake ya namna ya kuenda sambamba na maendeleo ambapo sasa hivi tumo ndani ya utandawazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, napenda kuongelea kwanza kuhusu suala la gharama kubwa zinazotozwa na makampuni mbalimbali ya simu kwa watumiaji nikimaanisha wananchi wa kawaida. Pili, nitaongelea suala la ugunduzi na ubunifu kwa wananchi walioko vijijini hususani Mkoa wa Rukwa na Katavi. La tatu, napenda kuongelea suala la wizi kwa kutumia mitando.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na gharama, imeonekana kwamba makampuni mengi yamekuwa yakitoza gharama mbalimbali kwa namna yanavyojipangia bila kuangalia mtumiaji kwa kipato anachokipata. Napenda nimshukuru Mheshimiwa Waziri kwa kuonyesha hilo na pia napenda nitoe ushauri katika mpango ujao wa Wizara. Labda kwa kuangalia ni namna gani ambavyo Serikali kwa kuitia Kampuni Mama inayosimamia mawasiliano inaweza ikajipanga na kuangalia namna ya kutatua tatizo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, tunaweza tukawa na Shirika na Kampuni Mama ambayo inaweza ikasimamia makampuni haya mengine, kukawa na kiwango kimoja kutoka mtandao mmoja kwenda mtandao mwengine. Kwa sababu imeonyesha kwamba hata watumiaji wa simu, mara nyingi anabipu au anasema niongezee salio, ni kwa sababu anaona gharama kutoka mtandao mmoja kwenda mwengine ziko juu. Kama tungekuwa na kiwango kimoja cha gharama kwa nchi nzima haijalishi, hizi kampuni zinaweza zikawa na kadi zao kwa gharama zao, mtumiaji anaweza akachagua, ni mtandao gani, kwa gharama zipi na *unit* zipi anazoweza akatumia kutokana na pesa anazoweza kuwa nayo na kununua ile kadi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, usimamizi huo utakuwa mzuri kwa kumlinda mtumiaji ambaye ni mlipa kodi wa mwisho. Hii inaweza ikapunguza pia kwa wafanya biashara ambao wanakwenda nje ya nchi, kwa mfano wanaenda China, Korea sasa hivi watu wanakwenda, kwa ajili ya kwenda kuomba kutengenezewa simu za bei rahisi za *line* mbili. Sasa hivi kuna simu za *line* tatu mpaka nne. Hii yoe ina maana tunaongeza soko kwa nchi zingine badala ya sisi wenyewe kupunguza matumizi. Naomba Mheshimiwa Waziri kama anaweza akalichukua kama wazo ambalo kwa kutumia timu yake ya Wataalam wanaweza wakalifanyia utafiti na wakaona ni namna gani linaweza likatusaidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, napenda kuongelea suala la ubunifu na ugunduzi. Hili suala linaonekana sanasana ukiwa Chuo Kikuu labda Mhadhiri au nani amegundua

kitu fulani ndiyo anapewa kipaumbele lakini kuna watu ambao wanaweza wakatumia ile miti akatengeneza pikipiki au baiskeli. Kwa mfano, kuna kijana Sumbawanga mwaka jana aliwahi kutengeneza trekta kwa kutumia mabaki ya pilipiki. Sasa watu kama hawa katika jamii wana vipaji. Nafikiri Wizara kupitia Tume ya Sayansi inaweza kabisa ikawainua watu hawa wakaweza kujikwamua katika maisha yao na si maisha yao kama wao, familia na hata Taifa kwa ujumla kwa maana kwamba tutakapomwezesha yule mtu aidha kwa kumpeleka vyuo vya VETA au Vyuo vingine vya Ufundu, tukamwezesha kwa mitaji aidha kwa kupitia mashirika yetu ya *SIDO* na mashirika mengine yanayofanya kazi kama *SIDO*, tunaweza kabisa tukaokoa kundi zima la vijana na watu ambao wanakuwa na ujuzi ila kwa sababu moja au nyngine ujuzi wao hauonekani. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri naomba hili pia muweze kuliangalia kwa undani zaidi kwa sababu lengo ni kupunguza umaskini na kuwawezesha wananchi kujikwamua kiuchumi na kupambana na hali ya maisha ambayo inakwenda kwa kasi kwelikweli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine napenda kuongelea suala ambalo limeibuka hivi sasa. Sidhani kama wengine wako *aware* nalo, mimi kwa namna moja au nyngine limenitokea. Kumekuwa na watu ambao kwa kushirikiana na hao wenye makampuni, aidha makampuni ya pesa yakijiita M-Pesa ama kupitia *Internet* kwenye *e-mails* wamekuwa wakiwatumia watu mbalimbali, aidha kwa kutumia, sasa sielewi wanapata wapi namba za Wabunge au namba za watu wengine wanajifanya kama wapigakura, wanaomba pesa. Cha kushangaza, unaweza kukuta hii pesa kweli kabisa unaituma, labda mimi naituma pesa yangu kwa Mheshimiwa Kahigi pale, lakini mbaya zaidi Mheshimiwa Kahigi yuko Tabora lakini ile namba unaweza ukakuta mtu aliyeko Dar es Salaam ndiyo ame-*draw* hiyo pesa na haya makampuni ya simu yote yanakupa *information* na unaipata. Pale unaporudi Polisi kwa mfano, unaelezea suala hilo, wao wanakuambia hii ni aina ya *cyber crime*. Sawa lakini je, linatatuliwaje tatizo hili maana linawenza likamkumba mwananchi wa kawaida? Nimekutana na wapigakura wengi wakilalamika kwamba pesa zao unakuta aidha mtu wa Morogoro ndiyo ka-*draw*, mtu wa Dar es Salaam, ye ye yuko Mpanda, atafuatiliaje pesa yake hiyo? Hiyo yote ni matatizo ya mawasiliano. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Waziri aweze kuliangalia suala hili kwa undani na kwa mapana zaidi. Kwa sababu huu wizi si hapa tu, hata mtu yuko Nigeria anaweza akakuibia hapa, mtu yuko Afrika Kusini anaweza akakuibia wewe uko Canada. Kwa hivyo, hivi vitu vinakua kwa kasi kutokana na maendeleo ya sayansi na teknolojia. Kwa hiyo, naiomba Wizara na Serikali itenye fungu hata kama ni la dharura, kwa sababu hii hali hatuwezi kusema kwamba tunaisubiri, ni kitu ambacho kinaendelea na kipo. Itenye fungu kwa ajili ya wataalamu wake waweeze kuangalia ni namna gani wanaweza kulishughulikia suala hili kabla halijawa sumu na likawapata wahanga wengi zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi naipongeza sana kazi aliyoifanya Mheshimiwa Waziri pamoa na Wizara yake na wataalam wake wote na pia nafurahi kwamba kwa kasi na kwa kiwango kikubwa Mheshimiwa Waziri ameonyesha ni namna gani anavyokwenda sambamba na mabadiliko ya sayansi na teknolojia na kwa namna gani anavyoweza kukimbizana na ulimwengu huu wa utandawazi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kunipa nafasi hii. Ahsante sana.
(*Makofi*)

MWENYEKITI: Nakushukuru sana Mheshimiwa Pudenciana kwa mchango wako. Waheshimiwa Wabunge, naomba sasa nimwite Mheshimiwa Dkt. Maua Daftari.

MHE. DKT. MAUA A. DAFTARI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi nichangie mada hii. Mimi nitachangia kwa kifupi tu kwa sababu nami ni mdau wa Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, napenda niwashukuru wapigakura wangu wote walionisadia kunipa kura na kunifikisha hapa. Napenda niwaahidi kwamba nitaendelea kuwatumikia. Kupitia kwao nichukue nafasi hii, nilishukuru Shirika la Marekani kwa kuniunga mkono katika kusaidia miradi mbalimbali ya Mkoa wangu karibu shilingi milioni 300. Nashukuru sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, ingawaje Mheshimiwa Spika hayupo, napenda nimshukuru na nimpongeze kwa uteuzi wake na namuahidi kumpa ushirikiano. Zaidi nawashukuru Waheshimiwa Wabunge nyote kwa kunipa kura nyingi na kuwa mwakilishi wenu katika Kamisheni ya Tume ya Bunge hili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichangie katika maeneo yafuatayo:- Kwanza Mkongo wa Taifa, baadaye mawasiliano ya simu za mikononi, tatu, utafiti na watafiti, nne, Tume ya Mionzi ya Nyuklia na tano udhibiti wa uingizaji wa kompyuta zilizopitwa na wakati hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kila kilio kina mwenyewe. Tumemshukuru sana Mheshimiwa Waziri kwa kazi nzuri aliyoifanya yeye na wataalam wake lakini kupitia kwake niwashukuru waliomtangulia kwa kazi nzuri na misingi walioijenga katika kuiunda Wizara hii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkongo wa Taifa umefika maeneo mengi na katika maeneo ulikofika, nafikiri sasa ni wakati muafaka Mkongo huo ukatumika ipasavyo ili uwasadie wananchi kuwaokoa na kuwaondoshea dhiki mbalimbali. Mkongo wa Taifa sasa umefika maeneo ya mipakani kote. Napenda sana kuona kule ambako nimekutembelea, Mhepei-Songea, Tunduru na maeneo mengine ya mpakani na Msumbiji kwamba Mkongo huo sasa unafika pale na wananchi wa eneo lile wanaweza kuzungumza na wenzao wa Msumbiji vizuri sana. Kwa hivyo, napenda nisisitize kwamba Wizara ichukue juhudi ya kuelimisha Taasisi, Wizara, Mashirika juu ya matumizi ya Mkongo huu. Pia katika sekta mbalimbali tunayo nafasi kubwa lakini hatujaitumia. Kwa mfano, sekta ya elimu, itumie Mkongo kwa kuunganisha mashule, ili kusaidia kufundisha na kupunguza tatizo la upungufu wa Walimu, itaziba pengo hilo na tuna nafasi ya kujisomea sisi wenyewe *through distance learning*. Katika sekta ya utalii, hivi sasa nimesikia kutajengwa barabara, hata iwe ya moramu katika mbuga za wanyama, naomba itakapojengwa barabara hii twende sambamba na kuweka miundombinu ya Mkongo ili wakati tukifanya marekebisho makubwa ya kuwafikishia mtandao huu wale wenye hoteli

za kitalii basi na wao wafaidike. Kwa kufanya hivi, tutasaidia sana sekta ya utalii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine nasema sasa ni wakati muafaka wa kusomesha watu katika kupiga vita masuala ya *cyber crime*. Mkongo huu uendane na taaluma ya kuwafundisha wataalam, namna ya kudhibiti wizi utokanao na Mkongo. Tusipofanya hivyo, tutakuja kujikuta mabenki makubwa yanaibiwa kwa kupitia Mkongo huu na mambo mengine yanayotokana na Mkongo huu yatafanyika. Kwa hivyo, nawaomba wenzangu wanaohusika wafanye shughuli hizi ipasavyo na mapema ili kesho na keshokutwa tusijetutia kuwa na Mkongo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la pili ambalo napenda nilichangie ni mawasiliano ya simu za mkononi. Mawasiliano ya simu za mikononi yamesaidia sana jamii mijini na vijijini. Yamerahisisha maisha yetu kwa kiwango kikubwa sana. Leo hii kwa kutumia simu ya mkononi tunalipa bili zetu za umeme, za maji na mambo mengine mengi lakini tunaweza kuwapelekea ndugu zetu pesa kwa kutumia mifumo mbalimbali ya pesa ambayo nafikiri inadhibitiwa na Wizara ya Fedha lakini nataka niseme kwamba makampuni haya lazima twende nayo sambamba kwa sababu ni makampuni ya kibashara, wanapenda kuwekeza pale ambapo tija ipo. Kwa maana hiyo, kama hamkusukumana, mkawafikisha vijijini, vijiji vingine vilivyobakia havitapata huduma hizo. Kwa hiyo, niwaombe wenzangu wa Wizara kama tulivyokuwa tunahangaika sisi wenzenu kwenye Mikoa, kwenye Wilaya mbalimbali kufuatilia, msichoke, mfuatilie. Tunajua makampuni yote yana *roll* na *plan* zao lakini na wao wana *priority* zao vilevile, mfuatilie ili tija iweze kupatikana na wananchi wa vijijini nao wapate huduma zinazohitajika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika sekta hii, nataka niulize, siku nyingine nikipokea simu kutoka nje, nazikuta zina namba za simu aidha za *Tigo* au *Voda*, siyo ile simu yenewe ambayo ninapigiwa, nashindwa kuelewa kuna kitu gani hapa, kuna *technic* gani inayotumika? Mimi hii sekta nimejifunza, isije ikawa labda hapa katikati kuna mchezo unachezwa na makampuni hayo? Naomba sana Mheshimiwa Waziri muwafuatilie wenzetu katika hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nisisitize la mwisho katika simu za mikononi. Kuna *foundations* mbalimbali, *Vodacom Foundation*, kuna na Tigo lakini mara nyingi wanasadidhisho hapa hapa mjini tu. Hebu kule vijijini watazame kuna watoto yatima mbalimbali na wao wafikiriwe. Kuna watoto amba wanakosa pesa za karo, wazazi wao wameshindwa kuwapeleka shule baada ya kufaulu, naomba sasa waelekee kule kwa sababu mawasiliano yao yamesambaa nchi nzima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema, nataka nichangie kwa ufupi tu eneo la utafiti na watafiti. Mwaka jana tulihangaika sana kutafuta hela ya utafiti licha ya juhudhi na ahadi za Mheshimiwa Rais na hatimaye kwa dakika ya mwisho tukapata hela za utafiti ambazo kama alivyosema mwenzangu, hazikutosha na hazikutolewa zote. Nisema naipongeza Serikali angalau kwa kuonesha njia kwamba hili jambo lina umuhimu wake. Naelewa Wizara, kupitia *COSTECH*, inayo mipango thabiti ya kuboresha eneo hili, sasa

naomba basi zile *centre* zetu ambazo zina hali mbaya sana, hazina vifaa vyatutafiti, waendelee basi kuwasaidia ili ziweze kuboreka vizuri. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine zaidi ni watafiti wengi sana wamekataa tamaa kutokana na kwamba wamekaa muda mrefu bila kupata fedha za kutosha za kufanya kazi zao ambazo ni ujuzi waliosomea. Tuwaombe basi wenzetu mnaosimamia hili, mkikazana, sadaka ni yenu lakini msipokazana hii hela haitatoka na watafiti hawatafaidika. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, watafiti wengi wanaendelea kuwa katika *age* za kustaafu. Nadhani sasa ni wakati muafaka wa kuingiza damu mpya katika sekta hii ya utafiti ili iweze kujiimarisha zaidi. Ukikuta wengine wana miaka 60, 50, 55, tufanye jitihada za makusudi kabisa tupate watafiti vijana. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine nalotaka nichangie ni lilewalilochangia wenzangu, uchimbaji wa madini ya *uranium*. Watu wengi wanafanya utafiti hivi sasa na kule kwa ndugu zangu wa Namtumbo, wameshaona dalili ya kupata *uranium* ya kutosha na wengine katika kuchukua *samples* hakuna tahadhari za kutosha, naomba sana ili tusije tukaingia katika tatizo zito, suala hili wakabidhiwe Watu wa Mionzi, walismamie ipasavyo kwa kushirikiana na Wizara yetu ya Nishati na Madini. Nakuomba Mheshimiwa Waziri, ikiwezekana hiyo Sera ambayo tayari sisi tuliiacha pale, iletwe kwa haraka, ipitishwe ili tuwe na mwongozo wa kusimamia eneo hili. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho nalotaka kuzungumzia ni udhibiti wa uingizaji wa *computer* zilizotumika. Sasa hivi kuna miradi mingi ya kwa *used computers*, *used computer* zinaingia chungu nzima nchini! Nyingine hazifai hata kwa matumizi yetu lakini kwa sababu bado hatujashika hatamu katika udhibiti wake, zinaingia katika maeneo yetu mengi sana. Sasa tatizo naloliona mimi ni namna ya *ku-dispose* hizi *computer*, zina tabu sana. Kwa hivyo, tunawaomba wenzetu wote aidha *TCRA* na Wizara ya Elimu, ambapo *computer* nyingi zinakuwa *consumed* kule, basi walismamie ipasavyo suala hili na kama mtu anataka kutupa msaada kwa ajili ya shule na sisi kwetu *computer* hazina kodi, ni kwa nini atuletee *used computer*? (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba na naomba nisisitize anayetupa msaada basi atupe msaada wa *computer* mpya. Asiondoshe takataka kwake kwenye nchi yake akaleta takataka Tanzania. Naomba sana kusisitiza hilo kwa sababu baadaye itakuwa ni *disaster* kwetu kuziondisha hizi *computer*! Kama mmeangalia muda mfupi uliopita au miezi miwili iliyopita, *computer* hizi zinatupwa mpaka kwenye mitaro ya maji! Ni hatari na watoto wanacheza mle, wanatoa vipande wanavyovitaka mle ndani ya *computer* kwa ajili ya shughuli zao! Naona ni hatari, naomba sana kusisitiza, suala hili lipewe uzito unaofaa. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niliona kwa wale wenzetu wa Uingereza, wana mradi mmoja unaitwa *Trace and Tracking*. Wamefanya mradi huu ku-*trace computer* ambayo walishaitoa kwenye *system* miaka nenda miaka rudi, wakai-*trace* wakaikuta iko Ghana na

wakaitoa kule, lakini walipita nyumba kwa nyumba. Kama inawezekana na sisi kuwatafuta hawa watu, tukaona namna gani wanaweza kutusaidia ku-*trace* hizi *computer* ambazo tayari ni *absolutely* hazifai kabisa kwa matumizi yetu, tukaanza kuzitoa mapema kabla matatizo hayajawa makubwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema, mimi ni mdau wa Wizara hii. Naomba niunge mkono Wizara hii asilimia 100 kwa 100 na kuwatakia Mawaziri utekelezaji mwema wa majukumu yao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuunga mkono hoja. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Nakushukuru sana Mheshimiwa Dokta Maua Daftari na hasa kwa kukumbuka vile vijiji vya Mhepei na Muhukulu, katika Jimbo la Peramiko. Nakushukuru sana. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, ile orodha ya wachangiaji waliochangia mara moja imeisha, sasa tunaingia kwa Waheshimiwa Wabunge, waliochangia mara mbili na nitamwita Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu, atakuwa mchangiaji wetu wa kwanza.

MHE. MUSSA Z. AZZAN: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Nachukua nafasi hii kwanza kumshukuru Mwenyezi Mungu, Mwingi wa Rehema, aliyenipa fursa kusimama tena hapa mbele ya Bunge hili Tukufu na kuwashukuru wananchi wangu wa Ilala, kwa kunichagua tena kuja hapa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, nawapongeza *TICRA* lakini katika kuwapongeza, nina habari yao vilevile ambayo inakuja. Kazi ya *TICRA* sio ya kusajili namba za simu au ku-*endorse* namba za simu au kutoa leseni ya kufanya shughuli za mawasiliano nchini mwetu, *TICRA* ni lazima waje na *mindset* mpya ya *revenue watch*. Kutizama ni namna gani nchi yetu itanufaika na mapato ya watumiaji simu nchini mwetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, watu waliosajiliwa kwa uhakika kabisa, wanaotumia simu nchini mwetu, ni watu zaidi ya 22,000,000. Katika watu hawa 22,000,000 kila mmoja wao ana uhakika au kuweza kuchangia shilingi 200/= kwa siku kwenye pato la Taifa, zikipitia kwenye makampuni haya ya simu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, shilingi 200/= kwa kila mteja wa makampuni haya ni shilingi bilioni nne na milioni mia nne kwa siku moja, ni shilingi bilioni 132 kwa siku 30, ni shilingi trilioni moja na bilioni mia nane themanini na nne kwa mwaka mmoja. Hii pesa, inaondoka na hawa watu wa simu na Serikali yetu inakosa haki ya mapato haya. Kilimo Kwanza lakini mimi ninasema Kodi Kwanza. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni namna gani tunaweza tukazikusanya pesa hizi? Kuna kitu kinaitwa *Call Accounting Monitor*. Nchi nyingi sasa hivi zimefunga mtambo huu, mtambo huu unasaidia ku-*monitor incoming calls* na simu zinazopigwa nje. Inakuwa ina *a remote Manager* ambayo ina-*generate additional revenue* kwa Serikali kwa ku-*monitor* matumizi ya simu ambayo makampuni haya ya simu hawatoi taarifa hizi

kwenye Serikali au kwenye vyombo au taasisi za kukusanya mapato nchini mwetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, yapo malalamiko. Dakika moja inayochajiwa na kampuni ya simu, inakuwa tofauti na dakika moja ya saa ambayo unayo wewe! Kwa maana makampuni haya kama hakuna chombo kinacho-*monitor* gharama za dakika moja, iko hatari ya sekunde 25 kwa watu 22,000,000 kuwa zinaliwa na makampuni haya na wateja wanakosa kupata *value for money* wanayolipia ili waweze kupata mawasiliano. Sasa mimi nataka kujua ni lini Wizara itafunga mtambo huu, *Call Accounting Monitor*, ili tuweze kujua makampuni haya yana-*generate* shilingi ngapi na haki ya Serikali ipatikane wapi? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, najua, makampuni haya yana ugumu wake, makampuni haya yana *lobby* sana. Kuna kipindi uliletwa Muswada hapa wa kufanya Watanzania wamiliki makampuni haya kwa kununua hisa na Muswada ule ultoka kwenye *Order Paper!* Muswada ule ukaja ukayeyuka, hakuletwa tena kwenye Bunge hili! Hawa wananchi wa kawaida tutawa-*empower* vipi tukiwa na mwenendo kama huu wa watu kukubali kuingizwa mkenge, kutokukubali Watanzania kumiliki makampuni haya? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumekuwa *very soft* na masuala ya Kodi Kwanza. Mimi naomba, Waziri leo bajeti yako itapita na naiunga mkono kwa 100%, lakini nataka kujua, nataka kuambiwa mtambo huu utafungwa lini? Ethiopia wamefunga, Uganda wamefunga na sisi tusiogope makampuni haya! Hilo moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndio maana tunapata matatizo ya dola, shilingi yetu kuanguka kwa sababu pesa zinazotolewa nje na makampuni haya za kununua dola hizi ni nyingi mno kuliko mapato ambayo tunayapata ndani ya nchi. Ndio maana pesa yetu siku zote inayumba kutokana na mapesa mabilioni na matrilioni yanapelekwa nje na hakuna *investiment* yoyote makampuni haya yanayoifanya nchini mwetu! Hebu tuambiwe leo kuna kampuni gani ya simu imejenga jengo katika nchi hii? *I stand to be corrected* kama wapo! Wote wanakodi! Ukishakodi, kwanza huongezi ajira za watu, ukishakodi hakuna *return* za *investiment*! Kwa hiyo, *investiment* za hapa wanachokifanya wao ni kuweka minara tu! Ndio nini? Mitambo na *software* ambayo wanakujanayo wakiamua kuondoka, wanaondoka nayo! Hii sio *fair*! Wizara lazima muingilie, Kodi Kwanza! Kama hamkulismamia hili, tutaendelea kuitwa shamba la bibi, tutaingizwa mkenge na kila siku watu watakuja wanachuma, wanaondoka, wanaondoka na mahela, wanaondoka na *revenues*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kujua *monitor* hii itafungwa lini ili kwanza tuongeze mapato katika nchi yetu. Shilingi Trilioni moja na bilioni mia tano kwa kila mtu kuchangia shilingi 200/= kwa siku! *Imagine* wanapata shilingi ngapi kwa watu ambao, kuna watu najua mimi wako zaidi ya 4,000,000 nchi hii wanatumia gharama za simu, sio chini ya 50,000/= mpaka 100,000/= kwa siku! Kwa hiyo, nataka kupata maelezo hayo. Lazima tu-*dislodge* watu kama hao wanao-*benefit* mambo haya na Watanzania wengi

wakawa ndio wanaotumika kuwatahirisha watu na Serikali ikakosa mapato yake. Kwa hiyo, naomba nipaye maelezo haya. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala la *Celtel*. *Celtel* walinunua *shares TTCL*, 120,000,000 wamelipa 60,000,000. Milioni 60 wakageuza biashara ya kusema tunafanya mahesabu, nimeambiwa na *I stand to be corrected*, katika milioni 60 waliyotoa ni dola 5,000 tu! Waziri, utaniambia kama ni kweli au si kweli! Hizi ni habari ambazo mimi nimezipata, kwa hiyo, unaweza ukaniirekebisha. Kama ni hivyo nitafuta hiyo, lakini nimeambiwa walizotoa ni dola 5,000. Inakuwaje tunamruhusu mtu anafanya biashara miaka mitano, halipi deni, anauza kampuni, inaingia *Zain*, *Zain* inauza kampuni inawapa *Airtel* na mambo kama hayo, kwa hiyo, kila mtu *business as usual!* (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, haiwezekani vitu kama hivi! Ni lazima tuwe *serious* kwenye Kodi Kwanza! Ni lazima tubane haya makampuni, hayawezi *ku-operate, packup and go!* Serikali ianzishe simu yake yenewe. Vietnam, mpaka leo wanayo *V-Tel*, wanafanya wenewe! Kwa hiyo, mimi nataka nipaye maelezo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kodi Kwanza, narudia tena. Upo mtindo na nimelalamika sana, nimekwenda mpaka katika kampuni ya simu, upo mtindo wa kueletewa *message*, mpaka ligi za timu za kichina, mimi za nini timu za kichina? Kuniambia Ngwang'ngwengwe imemfunga sijui Chung'chongul 3 – 2, mimi inanihu kitu gani? Ukienda kuwaambia, unaambiwa wanafuta, hawafuti! Ukiaka kuna timu Spain inaitwa Hecuris sijui mara Galatasaray, ya nini mimi na hizi zote ni gharama! Ukiifungua ile *massage*, tayari wanakutoza pesa! Sasa watu wangapi kama mimi tunaingizwa kulipa pesa vitu ambavyo hatuna *interest* navyo? Kwa hiyo, nataka nipaye majibu hayo vilevile. (*Makof/Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine la kulitizama ni *package* ya makampuni haya kwa wanafunzi. Nimekwenda *Vietnam*, nimekuta kuna *package* nzuri sana za kusaidia wanafunzi. Mwanafunzi anapewa fursa ya kulipa gharama ndogo tu kwa siku ili aweze kufanya mawasiliano na wanafunzi wenzake katika mambo mbalimbali ya masomo yao. Sasa hii ni *incentive* ambayo makampuni haya yanafikiria yatoe kwa wanafunzi wa Vyuo vya Juu na Wanafunzi wa Sekondari na wanafunzi wa Elimu ya Katikati ili na wao waweze kupata fursa hizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja yangu kwa leo, nazungumzia tu masuala haya ya simu na hasa kwenye *revenue watch*. Naomba Waziri, tunakuamini na Naibu wako na Katibu Mkuu wako, suala la kuweka mtambo huu wa *monitor*, ni suala la maslahi ya Taifa. Ni lazima sasa tujitegemee, ni lazima sasa tubane *leakage* ya *revenue* ambayo nchi hii inapoteza kwa siku. Shilingi Trilioni moja, bilioni mia tano, zingepunguza matatizo yote haya, makelele ya Wabunge haya yanepungua na hii ndio njia ya kutafuta pesa. Tunapoteza pesa kwenye madini na leo tunapoteza pesa kwenye makampuni ya simu! Makapuni haya yana ujanjaujanja wa kuitapita hapa na hapa na kufanya mambo yao yaende na mambo mengine muhimu ya Serikali yasiweze kufanikiwa. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maneno haya machache, nilisema leo mimi nitachangia masuala haya ya *Call Accounting Monitor*, ina umuhimu sana katika nchi yetu, ina umuhimu sana katika kukusanya mapato. Naiomba sasa Serikali, mimi sina haja ya Shilingi yako Mheshimiwa Waziri, sitazuia mshahara wako, kachukue pesa zako, katumie na mkeo vizuri tu, wala usipate tabu, isipokuwa mimi nataka unipe majibu ya *Call Accounting Monitor*, lini utaifunga na lini itaanza kufanya kazi? (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maneno haya, naunga mkono hoja. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Zungu, kwa kweli hilo ulilomaliza nalo ndio la msingi haswa na Mheshimiwa Waziri amelisikia. (*Kicheko*)

Waheshimiwa Wabunge, naomba nitoe tangazo moja. Mheshimiwa Januari Makamba, Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Nishati na Madini, anaomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini, kuwa leo tarehe 14 Julai, 2011, kutakuwa na kikao cha Kamati kuanzia saa 7.00 mchana katika Ukumbi Namba 231. Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge, Wajumbe wa Kamati hiyo, baada ya kusitisha shughuli hizi, mnaombwa mkahudhurie kikao hicho.

Waheshimiwa Wabunge, bado tuna majina ya wachangiaji ambao wamechangia zaidi ya mara moja, sasa baada ya kikao hiki tutawasiliana kwanza na Mawaziri. Jana tuliedelea na mchango jioni kwa sababu Wizara ilikuwa na Waziri mmoja sasa tunao Mawaziri wawili, lakini *any way* tutaangalia kwa saa ile moja watakayoitumia, kwa sababu wanatakiwa wagawane muda wao ndani ya Ofisi, tutaona kama tunaweza kuongeza wangapi.

Anayefuata ni Mheshimiwa Faith Mitambo, atafuatia Mheshimiwa Dokta Mwanjelwa, Mheshimiwa George Simbachawene, Mheshimiwa Moses Manchali, kwa hiyo, tutaangalia tutafanya nini. Baada ya kuyasema hayo, naomba sasa nitumie nafasi hii kusitisha shughuli hizi za Bunge mpaka saa 11.00 jioni.

(*Saa 6.58 mchana Bunge lilisitishwa mpaka saa 11.00 jioni*)
(*Saa 11.00 Bunge lilirudia*)

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge habari za jioni, tunaendelea na ratiba yetu kama tulivyokuwa tumeiacha mchana wakati tukisitisha shughuli za Bunge.

Waheshimiwa Wabunge nilisema hapa tumbakia na wachangiaji kadhaa, ambao walikwishachangia mara moja, basi naomba nimwite Mheshimiwa Faith Mitambo, achangie na baada yake tutaanza kusikiliza hoja kutoka kwa Mawaziri.

MHE. FAITH M. MITAMBO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii. Nianze tu kwa kumpongeza Waziri wa Mawasili, Sayansi na Teknolojia, kwa hotuba yake nzuri na kwa kweli katika hotuba yake kuna mambo mengi mazuri sana, iwapo yatatekelezeka, basi yatakuwa ni yenye manufaa makubwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nayashukuru pia Makampuni ya Simu ya *TIGO*, *VODACOM* na *AIRTEL* kwa kazi nzuri wanayoifanya. Kwa kweli yametusaidia kwa kiasi cha kutosha kutupatia mawasiliano huko katika vijiji vyetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi binafsi naendelea kuyaomba sana Makampuni ya Simu ya *TIGO*, *VODACOM* na *AIRTEL*, ni kweli Wilaya ya Liwale, wametuletea minara. Lakini minara hiyo bado haitoshi, pamoja na mawasiliano yaliyopo sasa lakini bado watu wanapanda kwenye miti, wanapanda kwenye vichuguu, wanatembea umbali mrefu kwa ajili ya kutafuta mahali ambapo mawasiliano haya yanapatikana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kampuni ya *VODACOM*, Wilaya nzima ina minara miwili tu, mnara mmoja uko katika Kijiji cha Kiangara, ambao unasaidia kuunganisha mawasiliano kutoka Nachingwea kwenda Liwale na mnara wa pili uko Mjini Liwale na ndio huu pekee unaoweza kufanya kazi na ambao unaleta mawasiliano zaidi zaidi kwenye mji ule tu. Kwa maana hiyo, eneo zima karibu robo tatu ya eneo la Wilaya hii halina mawasiliano ya kampuni ya *VODACOM*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kampuni ya Simu ya *TIGO*, nayo ina minara mitatu, nawashukuru juzi juzi wametuongezea mnara mmoja lakini mnara waliouweka pale, mnara ule haufanyi kazi naendelea kuiomba Kampuni hii ya *TIGO* irudi tena pale, iweze kufanyia kazi mnara ule ili uweze kufanya kazi na kwa hiyo, kutuongezea mawasiliano ya kutosha katika Wilaya ile. Mpaka sasa hivi pia Kampuni ya *TIGO* imeweza kusaidia mawasiliano katika Wilaya hii kwa robo tu na kuacha robo tatu ya Wilaya nzima, haina mawasiliano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mtando wa *AIRTEL* nao una *sites* mbili tu, *site* moja iko katika Kijiji cha Kiangara, ambao pia una-*pick* mawasiliano kutoka Nachingwea na kuyafikisha Liwale. *Otherwise* mjini kuna mnara mmoja tu na kwa hiyo, kufanya mawasiliano katika Wilaya ile vilevile kuwa kwa asilimia 25 tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wilaya ya Liwale ina fursa nyingi za kiuchumi na kiatalii pia, Wilaya hii inazalisha sana zao la korosho, ufuta, mtama na mazao mengine. Wilaya hii ina fursa ya utalii katika hifadhi ya wanyama ya Selous (*Selous Game Reserve*) na vilevile sasa hivi ina fursa ya biashara ya madini. Kwa hiyo, ni Wilaya ambayo ina mafao ya kutosha na nina imani kabisa kwamba makampuni yakiwekeza ndani ya wilaya hii, hayatapata hasara. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Chama cha Msingi cha Umoja, Wilayani humo imeweza kujenga godauni kubwa na chama hicho cha msingi kinaendelea kuweka mazingira mazuri kwa ajili ya mnada wa korosho katika msimu ujao. Lakini korosho hizo zinapatikana uko vijijini na ambako sasa hakuna mawasiliano, katika kipindi hicho matajiri na wafanyabiashara wengi tunategemea watafika kwa ajili ya ununuzi huo wa korosho na kwa hiyo, ningefikiria kwamba tungehitaji mawasiliano mazuri ya kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo la kukosa mawasiliano katika Wilaya hii na hasa huko vijiji kumesababisha pia hata wagonjwa na akinamama wajawazito wanaohitaji kujifungua kukosa msaada na huduma na hivyo wakati mwininge kupoteza maisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili linatokeaje, kuna vijiji ambavyo viko zaidi ya kilomita 70 kutoka mjini ambako hospitali ya wilaya ipo na *ambulances* zipo. Inapotokea kwamba kumetokea mgongwa wa dharura ambaye anahitaji kufikishwa hospitali ya Wilaya ya Liwale ndipo tatizo linapotokea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jamaa wa mgongwa huyu analazimika kusafiri nusu ya kilomita hizo kama 35 kwenda kufuata sehemu ambapo mtandao aidha wa *TIGO* au *VODACOM* unafika au *AIRTEL* unafika. Kwa kufanya hivyo, muda mwininge unapotea na kwa maana hiyo badala ya kumwokoa mgongwa na yule mama mjamzito unakuta mgongwa huyu anapata madhara makubwa au anapoteza maisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichukue nafasi hii kuishukuru Kampuni ya Simu ya *AIRTEL* kwa kunikubalia kuongeza *sites* nydinge saba katika Vijiji vya Lilombe, Mihumu na Likombola, Makata, Miruwi, Barikiwa, Nduruka na Nahoro. Niwaombe tu ndugu zangu sasa wa *AIRTEL*, watu kule wana shida, kwa kuwa mmekubali kutuongezea hizo *sites* nydinge saba, basi *process* hizi nydinge zinazoendelea ni vema mngeziharakisha ili watu hawa waweze kupata mawasiliano hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niliahidiwa mara ya kwanza kufikia mwezi wa sita *sites* hizi saba zitakuwa zimewashwa, mwezi wa Sita umefika, *sites* hazijawashwa na baadaye nikaahidiwa tena kufikia mwezi wa nane, *sites* hizi saba zitawashwa, ni mategemeo yangu kwamba sasa mwezi wa nane, hautapita, *sites* hizo angalau nusu zitakuwa zimewashwa. Hivyo basi, tunaomba sana mtujengee kabla ya mwezi huo kwisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa niongelee kuhusu Mfuko wa Mawasiliano kwa wote, *UCAF*, mpango huu wa *UCAF* ni mzuri sana na nina imani utasaidia kwa kiasi kikubwa kueneza huduma hizi za mawasiliano vijiji kote. Niombe Serikali kwamba mpango huu sasa ungeanza mara moja na nimesikia kwamba kuna maeneo ambayo yamepangiwa kufanyiwa *pilot studies*, basi ikiwezekana naomba na mimi Wilaya yangu muiingize kwenye *pilots study* hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *logistics* za kuanzisha mpango huu wa *UCAF*, zimechukua muda mrefu mno tangu mwaka 2006 hadi 2011, bado tuko kwenye *logistics* tu, ni lini sasa mpango huu unategemea kuanza wakati watu wanaendelea kupata shida za mawasiliano?

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika bajeti ya mwaka ujao, Mheshimiwa Waziri wa Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia, tunategemea atatueleza habari njema za kuanza kazi kwa mpango huu wa *UCAF* na siyo kuendelea na *logistics* tena.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niongelee sasa ujenzi wa minara, maeneo ya watu binafsi, ujenzi wa minara katika maeneo ya watu binafsi umeleta matatizo sana na hasa Wilayani kwangu ningependa kuyashauri makampuni ya simu ni vyema minara hii ikajengwa katika maeneo ya Serikali za Vijiji ili kuviwezesha vijiji kupata mapato. Sifahamu vizuri ni utaratibu gani unatumika mtu anatoka Dar es Salaam anakwenda kununua eneo kijijini na eneo lile analonunua ndipo pale pale watu wa Kampuni hizi za Simu wameshapima na kuona kwamba hapa ndipo patakapostahili kuweka mnara. Kwa hiyo, mtu anatoka Dar es Salaam anakwenda kule Liwale Kijijini, anakwenda anasema nataka eneo kununua ili niweke famasi, badala yake baada ya siku chache unakuta minara inachomekezwa pale na ikishajengwa malipo yote sasa yanakwenda kwa yule mtu binafsi badala ya malipo yale kuingizwa katika Serikali za Vijiji na kwa kufanya hivyo Serikali za Vijiji zinakosa mapato. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba Waziri wa Mawasiliano, naziomba kampuni ikibidi kujenga minara katika vijiji ni vema basi uangalie na mkubaliane na Serikali za Vijiji mjenge minara ile katika maeneo ya Serikali za Vijiji, ili pesa zile ziweze kuingia kwenye Mifuko ya Vijiji na ziweze kusaidia kazi nyingine. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nikushukuru kwa kunipa nafasi, naunga mkono hoja. Ahsante sana. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Faith, Waheshimiwa Wabunge. Nilisoma orodha ya Waheshimiwa Wabunge wanenye, lakini kama tutawapa nafasi hawa Wabunge hatutapata nafasi ya kutosha ya kuingia kwenye vifungu na ili kuingia hasa kwenye dhima hii ya bajeti yenyewe. Kwa hiyo, nadhani tuishie hapo.

MICHANGO KWA MAANDISHI

MHE. ENG. ATHUMANI R. MFUTAKAMBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, Jimbo la Igalula ni kubwa kieneo sawa na Mkoa wa Kilimanjaro. Lina kata kumi, kati ya hizo Kata tatu tu zina mawasiliano ya simu za mkononi. Tunaomba Wizara yako Mheshimiwa Profesa Mbarawa utuombee Kampuni za Simu *Airtel*, *Vodacom*, *TIGO* na *ZANTEL* watuletee minara katika Kata ambazo hazina huduma hizi kabisa. Kata hizo ni Goweko, Loya, Miyanze, Kigwa, Lutende, Kizengi (Mwakadala) na Tura (Nkongwa, Munyu). Watumiaji ni wengi na wanazidi laki tatu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tutashukuru kupata huduma hizi mapema iwezekanavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mionzi ya Gama itumike kuongeza uhai wa matunda, mboga na nyama ili kuongeza muda (*Shelf life*) ili wakulima wafaidike kwenye kilimo kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Afrika ya Kusini na sehemu nyingine duniani wanahifadhi matunda kwa kuyapitisha kwenye mionzi bila kuathiri ubora na kuweza kuyatumia hata baada ya mwaka pia chakula kingine na kuondoa (*post harvest losses*) upotevu wa mazao na vyakula vingine. Je, COSTECH wametafiti ili matunda mbalimbali Igalula (maembe, mapera, ntalali, matikiti maji na kadhalika) na sehemu nyingine ili matunda yasipotee na Pato la Taifa kuongezeka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawasilisha.

MHE. DKT. FESTUS B. LIMBU: Mheshimiwa Mwenyekiti, napongeza juhudu kubwa na nzuri inayofanywa na Wizara kuendeleza Sekta ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia. Napenda kujikita kwenye suala la upatikanaji wa huduma ya Mawasiliano ya kimtandao (*mobile*) katika Tarafa ya Ndagalu. Jimbo la Magu, hususan katika Kata za Kabilia na Shishani na Ng' haya kiasi. Tarafa hii ina tatizo na kero kubwa ya mawasiliano ya simu za mkononi. Niliuliza swali kuhusiana na hoja hii katika Bunge hili lakini sikupata majibu toshelezi kutoka kwa Waziri wa Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia baada ya Waziri wa Nishati na Madini kujibu swali langu la nyongeza kwa niaba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kujua (kwa niaba ya wananchi wa maeneo husika walijotuma) ni lini sasa Wizara itahamasisha kampuni husika kupeleka huduma hii katika eneo husika. Izingatiwe pia ukubwa wa eneo husika ambalo linazalisha mazao ya biashara na chakula kwa wingi, kuna mifugo mingi, idadi kubwa ya watu wenye uwezo wa kumiliki na kutumia simu za mkononi na ina shughuli nyingi sana za kibiashara. Naomba sana tupatiwe huduma hii mapema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

MHE. HEZEKIAH N. CHIBULUNJE: Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza hotuba nzuri ya makadirio ya matumizi ya Wizara iliyowasilishwa na Mheshimiwa Waziri leo hii ambayo naiunga mkono.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda pia niwapongeze sana viongozi wakuu wa Wizara amba ni Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Naibu Katibu Mkuu kwa umahiri mlionao katika utekelezaji wa majukumu ya Wizara hii muhimu. Nawapongeza sana na nawatakia kila la kheri katika utekelezaji wa majukumu yenu na Mungu awatangulie kwa yote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na mipango mizuri na mikakati iliyoainisha kwenye hotuba ambayo inatoa matumaini makubwa ya kuleta mapinduzi katika Sekta ya Mawasiliano, naomba niwasilishe mchango wangu kwa njia ya ombi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimkumbushe Mheshimiwa Waziri kuhusu Makampuni ya Simu ya *TIGO*, *VODACOM* na *Airtel* (*Zain*) ambayo yalikwishafanya utafiti wa kupeleka huduma za mawasiliano ya simu katika Vijiji vya Kata za Dabalo, Membe na Zajilwa katika Jimbo langu la Chilonwa. Utafiti huo ulifanyika miaka mitatu iliyopita na wananchi katika maeneo hayo wanasubiri kwa hamu sana kujua nini kitafuata na ni lini watapatiwa huduma ya mawasiliano ya simu. Naomba Makampuni hayo

angalau watoe ratiba ya utekelezaji ili kuwapa imani wananchi wangu wa Jimbo la Chilonwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa baadhi ya vikwazo vikubwa kwa Makampuni ya Simu kufikisha huduma ya mawasiliano katika maeneo mbalimbali nchini ni miundombinu ya barabara pamoja na idadi ya wananchi. Vikwazo hivyo kwenye Jimbo langu la Chilonwa kwa hivi sasa havipo. Maeneo mengi ya Tarafa za Itiso na Chilonwa yana idadi kubwa ya watu wenye uwezo wa kudumu kugharamia huduma za simu za mkononi. Vile vile mtandao wa barabara katika maeneo mengi ya Jimbo langu la Chilonwa ni ya uhakika. Je, Serikali inaweza kunipa matumaini ya kuharakisha kuwafikishia huduma ya mawasiliano ya simu wananchi wa vijiji vyote vya Tarafa za Chilonwa na Itiso?

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kuipongeza Wizara kwa kazi nzuri inayofanyika, naomba maombi yangu hayo mawili yapewe kipaumbele na wananchi wangu wapewe majibu angalau ya kuwepo matumaini ya kupatiwa huduma ya mawasiliano ya simu za mkononi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

MHE. SUSAN A.J. LYIMO: Mheshimiwa Mwenyekiti, mawasiliano ni njia mojawapo inayoweza kuwaleta wananchi maendeleo, hivyo kupunguza gharama zisizo za lazima kwa mfano, hivi sasa simu za kiganjani zimesaidia sana kupunguza gharama za usafiri, wizi na kadhalika. Simu sasa zinatumika ku- *transfer* fedha, kulipa umeme, maji na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na mafanikio haya, bado kuna changamoto nyingi katika sekta hii ikiwa ni pamoja na bajeti ndogo sana, kukosekana kwa tafiti mbalimbali ambazo zingesaidia sana katika kuongeza teknolojia mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo lingine kubwa ni rasilimali watu. Wote tunatambua umuhimu wa tafiti na Wizara hii kuitia Tume ya Sayansi na Teknolojia. Wataalam ni wachache sana, hivyo kufanya Tanzania isisonge mbele katika sekta hii kwa kasi inayostahili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mkongo wa Taifa utasaidia kupunguza gharama za *internet*, hivyo kufanya wananchi wengi zaidi kutumia huduma hii muhimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Vyuo vya Ufundu nchini ni vichache na vinavyotoa *Certificates, Diploma* ni vichache sana. Pamoja na ujenzi wa Chuo cha Nelson Mandela ambacho kitatoa *Degree* na hata za Uzamivu *PhD* ni dhahiri kitaendeleza sana teknolojia hapa nchini, hivyo kupata wataalam wazuri. Hivyo, sekta hii katika rasilimali yetu itakuwa imeboreshwa ha hivyo kutoa mchango wake vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

MHE. DIANA M. CHILOLO: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutumia nafasi hii kwa njia ya maandishi kuwapongeza Mheshimiwa Profesa Mbarawa Waziri na Mheshimiwa Kitwanga, Naibu Waziri, Katibu Mkuu wa Wizara ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia pamoja na watendaji wote walioshiriki kuandaa bajeti hii nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijaanza kutoa mawazo yangu kuhusu bajeti hii, napenda kutamka rasmi kuwa naunga mkono bajeti hii na nawatakia mshikamano, afya njema na maisha marefu ili waweze kutekeleza azma yao ipasavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuishukuru Serikali kwa juhudzi zake za kuwashimiza wawekezaji wa simu mbalimbali za mkononi kujenga minara maeneo mbalimbali nchini yakiwemo maeneo ya Mkoa wa Singida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na juhudzi hizo bado kuna maeneo ambayo hayana mawasiliano ya simu za mkononi *Airtel*, *Vodacom*, *Tigo* na *Zantel*. Kwa kuwa maendeleo ya wananchi yanategemea sana mawasiliano naiomba Serikali kuwasiliana na wawekezaji kujenga minara ya simu maeneo yafuatayo:-

Wilaya ya Manyoni; Kata ya Sanza, Iseke Nkonko na Mitundu. Wilaya ya Ikungi, Kata za Mgungira na Mwaru. Wilaya ya Iramba; Kata ya Mtekenti na Wilaya ya Mkalama; Kata za Mwangeza na Nkinto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono uamuizi wa Serikali wa kukataza wananchi kukata miti kwa ajili ya kuchoma mkaa na kukata kuni. Naishauri Serikali kuhakikisha imetoa elimu ya nishati mbadala ili Watanzania waelewe na waweze kuanza kutumia. Ni ukweli usiofichika Watanzania bado hawajui nishati mbadala ya kutumia kwa mapishi ya nyumbani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumalizia mchango wangu kwa kurudia kuunga mkono hoja hii mia kwa mia nikitegemea maelezo juu ya mchango wangu.

MHE. GREGORY G. TEU: Mheshimiwa Mwenyekiti, juhudzi ya Serikali ya kuunganisha au kuwa na mawasiliano na mikoa yote ya Tanzania (kwa awamu) kwa kupitia Mkongo wa Taifa. Gharama za zoezi hili ni kubwa sana hasa kwa usambazaji wa nyaya za mawasiliano kote zinakotakiwa kufika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, je, Wizara haioni kwamba usambazaji wa nyaya hizi hapo baadaye zitakapoanza kuharibika na kuzeeka, Wizara haioni kwamba gharama za kuchimba tena itaigharimu Serikali fedha nyingi sana. Kwa nini Wizara isitumie utaratibu wa kutumia *wireless* badala ya nyaya zilizopitwa na wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mawasiliano ni sehemu muhimu ya kuleta maendeleo katika nchi yetu, hususan kwenye Mikoa, Wilaya na Majimbo yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jimbo la Mpwapwa linayo maeneo yafuatayo yanayohitaji mawasiliano, mahitaji haya ni ya muda mrefu, naomba Wizara iangalie uwezekano wa kuweka mawasiliano katika maeneo haya ambayo yana kiu na mawasiliano katika Jimbo la Mpwapwa, Kata ya Matomondo maeneo ya Mlembule, Mwenzele, Chisalu, Tambi, Mbori Makutupa na Kata ya Mima ikiwemo Mima yenyewe, Sazima, Mkanana, Igoji, Iwondo na Chitemo.

MHE. JEROME D. BWANAUSI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nikushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia kwa maandishi. Nimpongeze Mheshimiwa Waziri wa Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia kwa hotuba yake nzuri, nianze kwa kuchangia katika eneo la upatikanaji wa mawasiliano ya simu za mkononi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nipongeze juhudini za Serikali za kushirikiana na Mashirika mbalimbali ya mawasiliano kama vile *VODACOM*, *TIGO*, *ZANTEL*, *AIRTEL* na kadhalika katika kuwafikia wananchi wa vijiji katika mawasiliano ya simu za mkononi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba Mheshimiwa Waziri aendelee kuwasiliana na Mashirika haya ili wananchi wa Jimbo langu la Lulindi Wilaya ya Masasi katika Kata za Chiwata, Mkundi, Mkululi na Mnavita yanapitwa na huduma hii ya simu za mkononi. Naomba Mheshimiwa Waziri wakati wa majumuisho yake awaeleze wananchi kuwa watapata huduma hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika maeneo mengi, wale wananchi waliosoma masomo ya sayansi wanakata tamaa kutokana na vipato vya kuwa duni ukilinganisha na wale waliosoma masomo ya sanaa. Hii ndiyo sababu kuna upungufu mkubwa wa Walimu wa Sayansi na katika masomo ya Hisabati, hivyo, naiomba Serikali itoe tamko ya kutoa motisha kwa wale wanaosoma masomo haya ili iwe kivutio.

MHE. STEPHEN H. NGONYANI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwa na matatizo mengi. Mawasiliano kwenye Majimbo Tanzania na tatizo la kuweka vipaumbele kwenye sehemu zenyetumeme ndio wanaweka nguzo za mawasiliano kwani kwenye Jimbo langu hakuna hata mawasiliano ya simu. Mawasiliano yapo tu barabara kuu toka Dar es Salaam kwenda Arusha na sehemu chache. Kwenye Jimbo langu kuna Kata 20, Vijiji vyenye Serikali 118 na Vitongoji 2,020 na Matawi lakini Kata zaidi ya kumi hazina mawasiliano, Kata ya Bungu, Dindira Mali, Mpale, Kizara, Mkalamo na Mwehishimiwa. Naibu Waziri wa Mawasiliano ameahidi ikifika mwezi wa Tisa inakuwa na mawasiliano, Mheshimiwa Waziri naomba usemi huu ujue hayo uyajue. Mheshimiwa Waziri suala la Mawasiliano limekuwa kero kubwa sana kwenye Jimbo hasa ukizingatia kuwa mazao ya chakula na mifugo yanatoka kwenye Jimbo langu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mheshimiwa Waziri anipatie majibu mazuri.

MHE. MARIAM N. KISANGI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Kamati ya Miundombinu, Wadau wa Wizara pamoja

na Serikali yangu ya Chama cha Mapinduzi kwa kazi kubwa ya kusukuma gurudumu la maendeleo. Mungu Ibariki Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nichangie katika upande wa mawasiliano kwa ujumla. Tunashukuru sana kwa Serikali kutuletea wawekezaji katika upande wa mawasiliano ya simu jambo ambalo lilikuwa limetutesa sana miaka ya nyuma. Lakini sasa hali ni nzuri watu wanawasiliana kwa muda wowote kwa njia rahisi japo ni gharama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasikitika kuona pamoja na kazi ya mawasiliano. Makampuni ya simu za mikononi yanauzu fedha zaidi ya mawasiliano. Makampuni ya *Vodacom*, *Tigo* na *Airtel* yote yanatoa huduma za *M-Pesa*. Wasiwasi wangu ni huduma hizi za kifedha Serikali inafaidika vipi? Lakini pia tukiangalia huduma hii ni msaada kwa wananchi waliopo vijijini. Simu za mikononi zimesaidia kutuma ada za watoto wao na wao wenye kipatiwa misaada kutoka sehemu mbalimbali kuititia simu za mikononi. Pamoja na huduma hiyo kusaidiwa lakini sana inatolewa ovyo hata chini ya mti. Hali hii si nzuri kwa sababu fedha za Tanzania nayo ina heshima yake, hivyo inastahili kuthaminika na kupewa hadhi yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niishauri Serikali yangu, huduma hii itolewe kwa kufuata masharti au vigezo ambavyo Makampuni hayo yatatoa na Serikali ifuatilie. Pia iangalie umuhimu wa jambo hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa heshima na taadhima, naunga mkono hoja. Ahsante sana.

MHE. LIVINGSTONE J. LUSINDE: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Wizara hii iongezewe fedha, hatuvezi kuwa na maendeleo ya kisasa na kushindana na Mataifa mengine yanayoendelea kwa kasi kama bajeti ya Wizara hii itaendelea kushuka kila mwaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati wa kampeni ya mgombea Urais Mheshimiwa Jakaya Kikwete alipofika Tarafa ya Mpwayungu wananchi walimwomba awasaidie kujengewa minara ya simu za mikononi na Mheshimiwa Rais alikubali. Je, ni lini Wizara yako itatekeleza ahadi hiyo ya Mheshimiwa Rais? Tena ikumbukwe Tarafa hiyo yenye Kata tano na Vijiiji 20 haina mawasiliano kabisa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana na naunga mkono hoja.

MHE. SAID M. MTANDA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nampongeza Mheshimiwa Waziri wa Sayansi na timu yake kwa kazi kubwa wanayoifanya, nampongeza sana Mheshimiwa Waziri kwa hotuba yake. Naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kuunga mkono hoja ninamwomba Mheshimiwa Waziri wakati wa ufanuzi aniambie mambo mawili yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kiasi gani cha fedha kimetengwa katika bajeti hii kwa ajili ya Utafiti na hii ni katika kutekeleza Ilani ya Uchaguzi Ibara ya 71(a) inayosema na nanukuu: “Kutenga kila mwaka kiasi kisichopungua asilimia 1.0 ya pato ghafi la Taifa (*GDP*) kwa ajili ya utafiti, maendeleo na maonyesho ya matokeo ya utafiti”

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Jimbo la Mchinga tunaishukuru Serikali kwa kutuunganisha na mtandao wa simu. Naiomba Serikali sasa ituambie ni lini sasa Vijiji-Miji vya Mvuleni, Mipingo, Rutamba na Kiwawa vitapata huduma ya simu?

MHE. ANGELLAH J. KAIRUKI: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchukua fursa hii kuchangia bajeti hii. Kwanza kabisa, nielezee masikitiko yangu kuhusiana na hali ya kifedha ya Shirika la Posta hususan mtaji wa kujiendesha kibiashara. Upungufu wa fedha unaolikabili Shirika la Posta unalissababishia shirika kushindwa kujiendesha kwa kutokuwa na nguvu ya kifedha kimtaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitendo hiki cha ukosefu wa fedha za kuwawezesha kujiendesha kibiashara, kunalisababishia pia shirika hili kushindwa kuwaongezea wafanyakazi wake mishahara kwa kipindi kirefu cha zaidi ya miaka 13.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Menejimenti ya shirika hili pia imekuwa haiwakilishi mafao (michango) ya hifadhi ya jamii (*PPF* na *NSSF*) kwa muda mrefu na hali hii imekuwa ikisababisha ucheleweshaji wa malipo pindi mfanyakazi anapostaafu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile uongozi wa Menejimenti wa Shirika la Posta haufanyi vikao na wafanyakazi, jambo linalopelekea wafanyakazi hawa kutokushirikishwa katika maamuzi ili waweze kutoa mawazo yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa muda mrefu Shirika la Posta limekuwa na utaratibu wa kuwapa nyumba za kuishi wafanyakazi wake au kuwapa pesa ya kulipia pango. Hata hivyo, katika miezi ya karibuni wafanyakazi wametangaziwa kuondoka katika nyumba hizo kwa maeleo kwamba zinatakiwa kupangishwa. Suala hili linasikitisha sana kwani wafanyakazi hawa hawana haki ya kuishi katika nyumba hizo na kwamba mishahara yao ni midogo sana, hivyo hawawezi kumudu ongezeko la kodi hiyo. Aidha, kwa nyakati tofauti, Shirika la Posta limekuwa likiwakata fedha za kodi ya nyumba kwa kiwango kikubwa na kusababisha mfanyakazi kutopata mshahara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishauri Serikali ifanye maamuzi ya makusudi ndani ya taasisi zake, ili tamko au uamuzi utolewe ambapo kazi zote za usafirishaji wa barua na vifurushi zitafanya na Shirika letu la Posta. Kwa kufanya hivi, shirika hili litajengewa uwezo wa makusudi na kwamba litaweza kushindana na makampuni mengine. Hili ni shirika letu hivyo hatuna budi kulisiaidia ili liweze kufanya kazi kwa tija na liweze kuzalisha zaidi na hivyo kuchangia katika uchumi wa Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa katika majumuisho ya Wizara, tamko hili liweze kutolewa ili azma hii ianze kutekelezwa. Aidha, uamuzi huu utawezesha

kuboresha maslahi ya wafanyakazi wa Shirika la Posta ambao kimsingi, wamekuwa na maslahi na mazingira duni ya kufanya kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa pia kufahamu Serikali ina mkakati gani katika kuhakikisha mfumo wa anuani za makazi na simbo za posta unakamilika lini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawasilisha.

MHE. CLARA D. MWATUKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuzungumzia juu ya barabara. Barabara nyingi zina matuta ambayo alama zake hazionekani kwa urahisi au kwa mbali. Matokeo yake madereva hustukia wangali wamelipanda tuta, hali hiyo hupelekea kutokea ajali. Hivyo, ni vema Wizara husika ichukue hatua za makusudi kuhakikisha alama zinaweka mbali kidogo na tuta ili madereva wachukue tahadhari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile sehemu zenyenye ubovu kama vile mashimo au daraja haziwekwi alama ya hatari hadi patokee ajali kubwa ndipo alama ziwekwe. Pengine inaweza hata kama pametokea ajali, lakini pakaachwa kwa kipindi kirefu huku ajali zikiendelea. Hivyo, ni jukumu la Wizara husika kuchukua hatua kushughulikia hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, daraja la Mto Mbwinji-Nangoo daraja ambalo liliharibiwa na mafuriko ya 1990. Sehemu hii imetokeza ajali kubwa kubwa lakini hadi leo daraja hili bado halijafanyiwa kazi. Hata hivyo, alama za kuonyesha hatari imewekwa pale pale ambapo madereva hustukia wangali wameshafika na wangali wamekwishaingia ajalini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni ombi langu kuwa Wizara itashughulikia daraja hili kwa manufaa ya wananchi wanaotumia njia hii ya Mtwara – Masasi au Lindi – Masasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile barabara hii kutoka Kijiji cha Nangoo – Ndanda, pana mashimo yanayosababishwa na mvua. Mashimo hayo pia husababisha ajali kwa vile kuna alama zinazoashiria hatari mbele. Kambi la ujenzi lipo Ndanda ambapo ni katika eneo hilo. Wanaona mashimo hayo ambapo yapo sehemu ambayo haihitajiki gari kwa kufika hapo. Hivyo naomba sehemu hizi zishughulikiwe ili kuepusha ajali zisizo za lazima.

MHE. RICHARD M. NDASSA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hotuba ya Waziri, nawapongeza watendaji wote na viongozi wa taasisi zilizo chini ya Wizara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkongo wa Taifa nashukuru umefika Mwanza kati ya Mikoa 16 kwa kilomita 4,300. Mheshimiwa Waziri kuitia kwako naomba mkongo huo wa Taifa uwafaidishe wananchi wangu wa Ngudu, Sumve na Malya, maeneo hayo yanahitaji sana huduma hiyo ya mawasiliano. Mheshimiwa Naibu Waziri anayafahamu vizuri sana maeneo hayo na umuhimu wa kupata huduma hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niyashukuru sana Makampuni ya simu za mikononi *Airtel*, *Vodacom*, *Tigo* na *TTCL* na *Zantel* kwa kutoa huduma za simu katika Jimbo langu, nayaomba mashirika haya kuongeza usikivu kwenye minara (*buster*) kwani kuna wakati mwingine usikivu huwa hafifu kumfanya mtumiaji kutowasiliana vizuri. Nashauri *Tigo*, *Airtel* waongeze nguvu kwenye mapokezi ya minara yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyoanza *Fibre Optic* katika maeneo ya Ngudu, Sumve na Malya ni muhimu, ningependa kujua utaratibu ili kupata huo Mkongo wa Taifa tufanyeje?

MHE. GAUDENCE C. KAYOMBO: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza namshukuru sana Mungu aliyetujalia kufanya mambo makubwa ya mafanikio katika eneo hili. Pili, nimshukuru Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu na Wafanyakazi wote wa Wizara hii kwa utendaji mzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu kwa ujumla ni kwamba, kuwe na mkakati bora wa kuwatambua na kuwasomesha vijana ili tuwe na wataalam nchini katika eneo hili.

Wizara ituongoze au iongoze Serikali namna ya kutumia vema maendeleo ya teknolojia ili kuleta ufanisi na kupunguza gharama kama vile hapa Bungeni (*paper work*) karatasi ni nyingi sana zinaweza kupunguzwa kwa kutumia *soft copies*. Katika Wizara mbalimbali mambo ni hivyo hivyo. Serikali ikianza wote tutafuata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jimbo la Mbinga Mashariki ni Jimbo tajiri na watu wana fedha lakini Makampuni ya Simu hayajawekeza. Maeneo mengi bado yana matatizo ya mawasiliano ya simu na *internet*. Maeneo hayo ni kama vile Kata yote ya Ukata, Mpepai, Litumbadyosi, Mkako, Nguria, Nyoni, Nyangayanga, maeneo ya Maguu, Litembo na Mbui. Nitafurahi iwapo Wizara itawakumbusha wahusika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Makampuni ya Simu za Mkononi, gharama zao bado ni juu na mara nyingi motisha wanazozitoa zina madhara ya maadili kama simu bure masaa ya usiku.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawasilisha.

MHE. HAWA A. GHASIA: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Sayansi na Teknolojia kwa hotuba nzuri na viwango.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumpongeza Naibu Waziri Mheshimiwa Charles Kitwanga (Mawe Matatu), Katibu Mkuu Dokta F. Turuka (Mwalim wangu), Naibu Katibu Mkuu na watendaji wakuu wote wa Wizara kwa kazi nzuri wanayoifanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jimbo la Mtwara Vijiji ni mionganini mwa Majimbo ambayo mtandao wa simu za mikononi ni mdogo sana, naiomba Wizara kuwezesha Kata za Kitaya, Chawi, Kiyanga, Dihimba, Mnima, Makurunga, Namtumbuka, Mtiniko,

Mtimbwilimbwi na Njengwa kuwa na mawasiliano ya uhakika kwa kuwa mawasiliano ni kitu muhimu sana kwa wakati tulionao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

MHE. AL-SHAYMAA J. KWEGYIR: Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi sasa kuna Kampuni mbalimbali za Simu zilizopo nchini mwetu, Serikali haioni kuwa Kampuni hizi zinaidhulumu kodi kwa kiasi kikubwa kwa kuwa anaendesha shughuli, wanaauza na baadaye wanaondoka zao wakiwa wametuibia kodi zetu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna Watanzania wana vipaji maalum, Serikali iwe na mpango maalum wa kuwatambua na kuendeleza vipaji walivyo navyo.

MHE. MARGARET SIMWANZA SITTA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kuwe na utaratibu wa kuwatambua Watanzania wenye vipaji maalum ili wapewe msaada wa kuendeleza vipaji vyao hasa katika uvumbuzi wa zana mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, je, nchi yetu haidhulumiwi kodi kwa Kampuni mbalimbali za Simu zinazoingia nchini, kuendesha shughuli zao, kuuza na kisha kuondoka? Hasa upande wa kodi.

MHE. DKT. SEIF S. RASHID: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kupata nafasi ya kuchangia kwa maandishi. Naanza kwa kupongeza hotuba ya Mheshimiwa Waziri na naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kuunga mkono hoja, naomba niishauri Serikali kuboresha mawasiliano ndani ya Bunge ili liwe la mfano kwa Taifa katika matumizi ya kisasa ya teknolojia kwa kufanya yafuatayo:-

- (a) Mfumo wa uwasilishaji wa taarifa zote za maandishi Bungeni uwe wa kielectroniki ili kuachana na machapisho yenyen gherama ambazo hazina ulazima;
- (b) Ndani ya Jengo la Bunge kuwepo na *wireless internet connection*; na
- (c) Kila Mbunge apewe *laptop/palmtop* ambayo atakuwa anatumia akiwa Bungeni kwa kupokea mawasiliano yote ya maandishi *electronically*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na pongezi kwa kuboresha juhudhi za mkongo wa Taifa na mawasiliano kwa niaba ya Warufiji, naiomba Serikali kuunganisha Vijiji vya Wilaya ya Rufiji ambavyo hadi sasa havina huduma ya mawasiliano ya simu, Vijiji hivi ni pamoja na Nambunju, Tapika, Ndundunyikanza, Nyaminywili, Kipo, Kipugira, Mtanza, Msoma na Siasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Serikali pamoja na kazi nzuri inayofanya ishawishi na kuwezesha mashule mengi zaidi ili iweze kutumia masomo kwa njia ya masafa hasa shule za sekondari zikiwemo shule ya sekondari ya Mkongo Rufiji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishawishi Serikali kuona umuhimu wa kununua kompyuta kwa kila Kata ambayo itatumika katika kuweka kumbukumbu za watu, taasisi za Serikali na maendeleo ya kupashana habari na mfumo wa kuboresha utoaji wa huduma za ofisi mbalimbali za Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru na naunga mkono hoja.

MHE. RACHEL M. ROBERT: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchangia katika Wizara ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia mambo machache kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza napenda kuishukuru Serikali kwa kuona umuhimu wa mawasiliano kwa wananchi wake na kuruhusu wawekezaji wengi na tofauti kuja kuwekeza katika sekta hii. Ni jambo jema kabisa kwani tumeona Makampuni mengi ya Simu yakifanikisha hili na kufanya maisha ya Watanzania kuwa mepesi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumejitokeza baadhi ya Makampuni ya Simu ambayo yamekuwa yakifanya mambo sivyo. Suala la kuweka minara yao kwenye mashamba ya wananchi hasa maeneo ya vijijini linaonekana haliko sawa. Nasema haliko sawa kwa sababu nina ushahidi wa kutosha, Kampuni ya Simu ya *Zantel* imeweaka mnara wake katika Kijiji cha Maganzo kilichopo Kata ya Maganzo, Wilaya ya Kishapu, Mkoani Shinyanga katika shamba la mzee mmoja, jina lake nalihofadhi na kufanya makubaliano na mzee huyo kumlipa kiasi cha shilingi za Kitanzania 2,000,000, (milioni mbili tu) kwa mwezi lakini mpaka leo tokea mwaka 2008, hajalipwa hata senti moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Wizara ifanye utaratibu wa kuhakikisha maeneo ya wananchi yaliyowekewa minara, wamiliki wa ardhi wanalipwa kulingana na mikataba walioingia kati ya Makampuni hayo. Serikali pia ichunguze makampuni ambayo yanadhulumu wananchi ili yachukuliwe hatua sitahiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha na ikiwezekana nipatiwe majibu.

MHE. OMARI R. NUNDU: Mheshimiwa Mwenyekiti, nachangia kuhusu kuzindua ubunifu wa vijana wa Kitanzania. Ubunifu na utundu wa kivumbuzi wa vijana wadogo ambao wanatayarishwa barabara vina mchango muhimu na wa pekee katika kuiendeleza nchi ili kuleta mapinduzi ya viwanda na teknolojia. Pendekezo langu ni kuanza kuiga wanavyofanya nchi nyingine kama Jamhuri ya Korea, Japan, Malaysia na Singapore ambazo zimepiga hatua hivi karibuni. Hivyo vijana wetu wadogo wapewe chachu za kubuni na kutengeneza vifaa vya michezo kama vile *robotics* za mashindano ya ndondi, mbio za magari na kadhalika badala ya kumaliza kiu yao ya teknolojia kwa kucheza *computer games* bila ya kuja michezo hiyo imebuniwa vipi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

MHE. NASSIB SULEIMAN OMAR: Mheshimiwa Mwenyekiti, napendekeza Shirika la *TTCL* libinafsishwe. Sababu ni kwamba, shirika hili linahitaji fedha nyingi za kuwekeza. Pili, si vizuri tena Serikali kuendelea kuendesha mashirika, ni vizuri mashirika yakamilikiwa na sekta binafsi. Sababu ya mwisho ni kuwa bado tunakumbuka wizi wa fedha na vifaa uliokuwa ukifanywa na shirika hili katika miaka ya 1980/1990, watu wakipelekewa bili kubwa za simu zilizokuwa hawajazipiga. Ushauri ni kuwa serikali iendelee kuwa na *share* lakini uendeshaji uachwe kwa sekta binafsi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchangia kuhusu kodi kutokana na simu zinazopigwa na simu za mikononi kule Zanzibar. Serikali hutoza kodi kwa simu zote zinazopigwa nchini. Mashirika manne makubwa yana *operate* Zanzibar nayo ni *Zantel*, *Tigo*, *Vodacom* na *Airtel*. Kodi yote inayokusanywa Zanzibar huwa haipelekwi katika Serikali ya Zanzibar, *Zantel* pekee ndiyo inayolipa kodi kwa Serikali ya Zanzibar. Namwomba Waziri aeleze suala hili katika majuisho yake. Pia aeleze kodi kiasi gani Serikali ya Zanzibar inadai.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda pia kuchangia kuhusu mkakati wa Shirika la *Tigo* kutaka kuliua Shirika la simu la *Zantel*. *Tigo* imeshusha bei zake kwa kiwango kikubwa sana kwa azma ya kuliua Shirika la *Zantel*. Hii ni kwa sababu Shirika la *Zantel* lina wateja wengi sana Visiwani Unguja na Pemba. Bei zilizowekwa na *Tigo* ni chini ya *Break even cost*. Azma ya hatua hii ni kuwachukua wateja wote wa *Zantel*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara inachukua hatua gani kudhibiti suala hili? Lazima pawekwe sheria kudhibiti vitendo hivi. Naomba Waziri atoe maelezo juu ya tatizo hili.

MHE. AMOS G. MAKALLA: Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Jimbo la Mvomero kuna tatizo kubwa la mawasiliano ya simu. Kata ya Kanga na Vijiji vinne ambayo ni Vihinda, Kanga Mziha na Difinge. Kata hii yote hakuna mawasiliano ya simu za mkononi. Nilikuwa naomba kata hii pamoja na kata ya Kinda, Luale, Pemba, Kibati na Tarafa ya Ngeta yapatiwe ufumbuzi wa kujengewa minara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna wakati Mheshimiwa Waziri alinionesha orodha ya Vijiji vilivyo Jimboni Mvomero vitakavyofaidika na Mfuko wa Mawasiliano kwa wote (*UCAF*) katika orodha hiyo viro Vijiji vya Msolokelo, Pemba, Salawe na Digalama. Mheshimiwa Waziri wakati wa kujibu hoja naomba majibu au maelezo ni lini mpango huu utaanza kutekelezwa na je, idadi ya vijiji nilivyovitaja ni sahihi? Aidha, niliwhali kuandika barua ya kuomba Mheshimiwa Waziri ayashawishi Makampuni ya Simu kujenga minara, Kata ya Kaga, Kinda, Maskati na Luale. Je, maombi hayo yamefikia hatua gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja.

MHE. LUHAGA J. MPINA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa mtandao wa simu (*Airtel*) iliyoko Makao Mkuu ya jimbo la Kisesa – Meatu katika kata ya Mwando ya umeshindwa kumudu na kuhimili mawasiliano ya simu za mkononi katika jimbo zima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, je, Serikali kwa kushirikiana na Makampuni ya Simu itajenga mnara ili kuzipatia mawasiliano kata za Mwabuna, Mwasengela, Tindabuligi na Sakasaka pamoja na vijiji vya Mwandu Itinje, Mwagai Isangijo na Semu katika Bajeti ya mwaka huu 2011/2012?

Mheshimiwa Mwenyekiti, picha ya jitihada za Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete ya kukutana na Mwenyekiti wa Kampuni la *Microsoft*, Bwana Bill Gate kwa nini hotuba yako haijamtambua na kumpongeza Bwana Bill Gate kwa niaba ya kampuni yake kukubali kuja nchini kututengenezea *programmes* mbalimbali na kutuunganisha katika mfumo wa kompyuta?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali/Wizara imekuwa ikiripoti tatizo la uelewa mdogo wa wananchi juu ya umuhimu wa sayansi na teknolojia katika uzalishaji na katika utoaji wa huduma za kijamii. Hatua gani zimechukuliwa kuhakikisha kuwa ufahamu wa maarifa haya umewafikia wananchi? Ni vijana wangapi wamepelekwa kusoma maarifa maalum katika nchi za nje zinazotoa *unique skills* katika ngazi za *Degree, Masters na Phd*? Sayansi na teknolojia imesaidiaje upatikanaji wa nishati mbadala kama umeme wa jua (*solar*) na *biogas*?

Mheshimiwa Mwenyekiti, je Serikali itasaidia vipi Shirika la *International Child Support (ICS)* ambalo limekuwa na utaratibu wa kufunga *solar* vijiji sambamba na kupeleka wanawake wawili toka kila kijiji kuwapeleka India kwenye mafunzo ya kufunga (*installation*) na kufanya matengenezo zinapoharibika na hivi sasa wanawafungia *solar* na kuwatengenezea wanakijiji wenzao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania ni kati ya nchi 19 za Afrika zinazotekeleza mpango wa *AST II*, na tayari Shirika la *SIDA* limetoa *USD 2.9* milioni, Tanzania imepata fedha kiasi gani katika mgao huo?

MHE. GOODLUCK J. OLE-MEDEYE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Mheshimiwa Profesa Makame Mnyaa Mbarawa kwa kuteuliwa kuongoza Wizara hii muhimu, pia napongeza Mheshimiwa Charles Kitwanga, kwa kuteuliwa kuwa Naibu Waziri wa Wizara hii. Aidha nawapongeza sana, Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri wa Wizara kwa kuiongoza Wizara kutekeleza kwa dhati Ilani ya Uchaguzi ya CCM mwaka 2010, sera za sekta na sheria zinazosimamia sekta zilizo chini ya Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawapongeza kwa dhati watendaji wakuu wa Wizara na Taasisi zilizo chini ya Wizara. Natambua maendeleo makubwa yaliyopatikana katika nyanja za mawasiliano ya simu yaliyowezesha Taifa kuvuka malengo yaliyowekwa kwenye Dira ya Taifa ya mwaka 2025. Hii naamini imetokana na sera nzuri na sheria za sekta hiyo. Vile vile kanuni, misingi na miongozo mizuri ya udhibiti ndio sababu kubwa

za mafanikio haya. Nawapongeza sana uongozi wa *TCRA* na viongozi wa Makampuni ya Simu nchini kwa kufanya kazi kwa ushirikiano mzuri hivyo kufikia lengo la kutoa huduma kwa gharama nafuu kwa wananchi wetu. Nashauri Serikali iendelee kuboresha mazingira ya udhibiti wa sekta ili kuendeleza ushindani chanya kati ya watoa huduma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, anwani mpya na *symbol* za Posta, naipongeza Serikali kwa kutambua umuhimu wa kuwa na anwani za makazi na *symbol* za Posta ili kurahisha utoaji huduma za mawasiliano wa Posta, shughuli za Kiserikali na utoaji huduma za uokozi na usalama kwa wananchi mijini na vijijini. Hata hivyo nasikitika sana kuona kwamba mradi huu muhimu umetengewa fedha kidogo sana ukilinganisha na mahitaji halisi, nashauri kuwa Serikali itafute fedha na kuwekeza kwenye mradi huu kwani bila kufanya hivyo juhudhi za Serikali kuboresha ukusanyaji kodi na hivyo kuongeza mapato yake hazitofanikiwa bila kutambua wanakoishi walipa kodi. Aidha, maandalizi ya vitambulisho vya Taifa kabla ya kukamilisha mradi huu itakuwa ni kupoteza fedha hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote (*UCAF*) mahitaji ya huduma za mawasiliano vijijini hususani kwenye taasisi ikiwemo shule, zahanati na kadhalika yamekuwa yakiongezeka sana. Wawekezaji binafsi hawataweza kuwekeza ili kukidhi mahitaji halisi kwani lengo la kupata faida ni kipaumbele kwao. Kiasi cha fedha zilizotengwa kwenye Bajeti ya Serikali kwa ajili ya mfuko huu hazitoshi. Ni vizuri Bajeti zijazo mfuko utengewe fedha za kutosha ili iweze kutekeleza majukumu yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu sayansi na teknolojia – Taasisi ya Nelson Mandela. Naipongeza sana Serikali kwa kazi nzuri iliyofanyika kukarabati majengo yaliyokuwa ya *CAMARTEC* na kujenga mengine mapya na kuweka vifaa muhimu. Kwa vile lengo ni kujenga *campus* kubwa ya Taasisi hii huko Bwawani/Karangai, naishauri Serikali ianze kuandaa mipango na mikakati ya kutekeleza mpango wa kuweka miundombinu ikiwemo barabara, maji na umeme. Kwa kuzingatia tabia iliyozuka hivi karibuni ya uvamizi wa maeneo/mashamba yaliyo wazi nashauri kuwa Taasisi ijenge uzio kuzunguka shamba walilopewa huko Bwawani ili kuepusha uvamizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Taasisi za Teknolojia Dar es Salaam, Mbeya na Arusha naipongeza Serikali kwa maboresho yanayoendelea kufanyika kwenye Taasisi hizi ili ziweze kutekeleza majukumu yao. Ingawa Serikali imetambua vilivyo umuhimu wa utafiti kwa maendeleo ya Taifa letu, bado Taasisi hazijawezeshwa kufanya utafiti kwa vitendo. Nashauri wanafunzi wanaofanya utafiti kama sehemu ya masomo yao wawezeshwe kwa kupatiwa fedha na wafanye utafiti kwa kushirikiana na watoa huduma/wazalishaji bidhaa kwenye sekta zinazohusika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawasilisha na naunga mkono hoja.

MHE. EUGEN E. MWAIPOSA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuchukua fursa hii ya kuchangia hotuba ya Wizara hii kwa maandishi kwa kumpongeza Waziri na Serikali kwa jumla kwa hotuba nzuri na yenye matumaini makubwa kwa Watanzania.

Pamoja na uzuri wa hotuba ya Wizara nimeona ni vema nichangie katika mambo yafutayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, gharama za mawasiliano kwa simu za mkononi bado gharama za mawasiliano zinazotozwa na makampuni ya simu ni kubwa haswa ukizingatia umuhimu wa mawasiliano katika maendeleo ya Taifa letu. Makampuni haya yameweza kusambaza huduma hii hadi vijijini lakini vipato vya wananchi wa vijijini ni vidogo kiasi kwamba wanakuwa na uwezekano mdogo sana wa kumudu gharama za mawasiliano zinazotolewa na makampuni hayo. Nashauri Serikali iendelee kuwashauri makampuni haya ili yapunguze gharama zake ili kuwawezesha wananchi wengi zaidi kutumia teknolojia hii ya mawasiliano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la huduma ya kifedha, katika miaka ya hivi karibuni makampuni ya simu yameanza kutoa huduma ya kutuma fedha, kuhifadhi fedha katika simu na hata kulipia baadhi huduma za kijamii kwa kutumia mtandao wa simu. Pamoja na kuwa huduma hii imepunguza sana usumbufu wa wananchi kwenda kupanga foleni katika mabenki ili kutumia fedha au kulipia huduma mbalimbali nina wasiwas kama makampuni haya yamepewa kibali cha kisheria kinachoruhusu kufanya biashara hii ya fedha. Hata hivyo kwa kuwa huduma hii imependwa na wananchi wengi na wanaitumia kwa wingi kampuni hizi zinapata faida kubwa na kisheria sijui Serikali imejijenga VIPI kupata mapato ya biashara hii ya fedha inayotokana na makampuni haya. Hata hivyo kama huduma haitawekewa taratibu nzuri inaweza kudhoofisha shughuli za mabenki yetu nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha ushauri huu na naomba Serikali iufanyie kazi.

MHE. SAID SULEIMAN SAID: Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ni mojawapo ya Wizara ya Muungano, lakini jambo linalonisikitisha ni kuwa huleta maendeleo zaidi ya 90% kwa upande mmoja wa Muungano upande wa Tanzania Bara, kwa mfano, Mkongo wa Mawasiliano kwa upande wa Tanzania Bara umeshafikishwa kwenye Makao Makuu za Wilaya na mikoa mingi wakati kwa upande wa Zanzibar ambayo ipo karibu na kituo kikuu cha mapokezi au cha uunganishi kilichopo Dar es Salaam, mkongo huu haujafika. Hata kwa Pemba ambako ile *main cable* iliyopeleka umeme Pemba ambayo tayari imeambatanishwa na mkongo wa mawasiliano (*optic fibre*) haujaunganishwa na Mkongo wa Taifa na mawasiliano kwa hivyo ninaomba Wizara iharakishe kuunga mkongo huu na kufikisha mkongo huu wa mawasiliano kwenda katika Makao Makuu yote ya Wilaya na mikoa ya Pemba pamoja na kuziunganisha zile nafasi muhimu na Makampuni ya Simu yaliyoko Pemba, Hospitali ya Chake Chake, Hospitali ya A. M. Mko, Hospitali ya Micheweni, Hospitali ya Wete, *Public Health Laboratory* iliyoko Wawi Chake, shule zote za sekondari na ofisi kuu za Wizara zote zilizoko Pemba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine naomba kujua Zanzibar inafaidika VIPI na mapato yanayotokana na Makampuni ya Simu yaliyosajiliwa Tanzania Bara na mapato yanavyotoka na matumizi na mawasiliano ya sekta ya anga. Taasisi na majengo yote ya

Wizara hii yapo upande mmoja tu wa Tanzania Bara, naiomba Wizara ijenge na kuweka Taasisi zote upande wa pili Zanzibar. Ahsante.

MHE. NAMELOK E. M. SOKOINE: Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. Kwanza naipongeza Wizara ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia kwa kazi nzuri na kubwa wanayoifanya kujitahidi katika kuhakikisha mawasiliano yanapatikana katika nchi yetu. Nitachangia katika mambo mawili katika Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la mradi wa Vitambulisho vya Taifa, mradi huu uende sambamba na kupatiwa anuani mpya ambazo zitakuwa na namba ya nyumba na *symbols* za Posta, kwa kufanya hivi ni rahisi kuwa na *data* zote za mmiliki wa kitambulisho ila pia itarahisisha kutoa huduma, kama kuna mgonjwa ni rahisi kutoa maelezo.

Suala lingine ni kuwa kuna gharama kubwa kupiga simu kutoka kampuni moja kwenda nyingine mfano, kwenda *Tigo* au *Zain*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu kwa kampuni hizi zitoe gharama hizo ziwe kama ilivyo kwa nchi nyingine ambapo hakuna *charges* kama hizo hii pia itatuondolea kero za mtu mmoja kutembea na simu zaidi ya moja ili kukwepa gharama toka mtandao mmoja kwenda mwengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, narudia kupongeza Wizara ya Sayansi na Teknolojia kwa usajili wa kadi za simu kwa kiasi kikubwa imesaidia sana kupunguza uhalifu uliokuwa unafanywa kwa kutumia simu ambazo zilikuwa hazijasajiliwa, pia nawapongeza kwa kuanzisha huduma za *M-Pesa*, *Zain-Pesa* na *Tigo-Pesa*, pia kwa kuweza kulipia gharama za umeme na maji kwa kutumia simu. Napendekeza Wizara hii iongezewe fedha ili huduma za mawasiliano ziweze kufika nchi nzima.

MHE. GODFREY W. ZAMBI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naipongeza Serikali kupitia Wizara hii, Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na wengine wote waliohusika na uandaaji/utayarishaji wa Bajeti hii na kuiwasilisha hapa Bungeni. Napenda kuchangia katika maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la Mkongo wa Mawasiliano wa Taifa, naipongeza sana Serikali kupitia Wizara hii kwa hatua nzuri zilizofikiwa katika ujenzi wa Mkongo wa Taifa. Tanajua kutohana na taarifa ya Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania hadi sasa mkongo umefika katika mikoa 19 na wilaya 59. Ombi langu ni kwamba Wizara ifanye jitihada ili mikoa na wilaya zilizobaki ziweze kufikiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, faida kubwa za mkongo ni kupunguza gharama kubwa za mawasiliano ya simu, *internet* na kadhalika, hali hii itafanya watu wengi kumudu gharama za simu na *internet* na hivyo kuchangia Pato la Taifa, kupitia kodi na hivyo kukuza uchumi wa nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhsuu Vyuo vya Sayansi na Teknolojia, tunavyo vyuo muhimu sana vya Sayansi na Teknoloji katika nchi yetu ambavyo ni *Dar es Salaam Institute of Technology*, *Mbeya Institute of Science and Technology* na *Mandela Institute of Science and Technology*. Vyuo hivi ni muhimu sana katika kuzalisha wataalamu wa masuala ya sayansi na teknolojia fani ambayo kwa sasa ni muhimu sana katika maendeleo ya Taifa lolote duniani. Hata hivyo, kwa masikitiko makubwa sana vyuo hivi hasa *DIT* na *MIST* vinapewa/vinatengewa pesa kidogo na hivyo kufanya mipango yake mingi kutofanikiwa sana. Aidha, kiwango cha udahili kuwa cha chini sana. Serikali, nashauri itenge pesa za kutosha kwa vyuo hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kujua ni lini jengo la *Teaching Tower* la *DIT* litakamilika maana naona pesa inayotengwa kwa ajili ya jengo hilo ni kidogo sana. Nataka pia kujua ni lini *MIST* itatoka katika hadhi ya *MIST* na kupewa hadhi ya Chuo Kikuu. Suala la kuanza kutoa shahada nalifahamu, ila nataka kujua Chuo Kikuu lini? Kumbukeni kwamba hiyo ilikuwa ni ahadi ya Baba wa Taifa Mwalimu Nyerere.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawasilisha na naunga mkono hoja.

MHE. AUGUSTINO L. MREMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, napongeza hotuba nzuri iliyotolewa na Waziri wa Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia. Naunga mkono hoja yake. Naomba nipayendekeze yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, itungwe sheria na kanuni za uchimbaji na matumizi ya madini ya Urani (*Uranium*) kutokana na madini haya kuhitaji uangalifu na usalama mkubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfumo wa kompyuta uanzé kutumika katika Bunge ili Wabunge waanzé kutumia teknolijia ya *TEKNOHAMA* wakati wa kufanya mawasiliano na kupeana nyaraka mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, shilingi bilioni 25 zilizotengwa kwa mwaka 2011/2012, kwa ajili ya tafiti hazitoshi. Napendekeza ushauri wa Rais wa kutoa 1% ya Pato ghafi la Taifa au shilingi bilioni 100 zitolewe ili kugharamia shughuli za utafiti. Nashauri isibinafusishwe kampuni ya *TTCL* bali ipewe mtaji wa kutosha ili isimamiwe na kuendeshwa na Watanzania wenye kwa kuwa tayari wana utaalamu, miundombinu na mtandao wa kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri Serikali ishawishi Makampuni ya Simu kuondoa gharama za kulipia simu kati ya mtandao mmoja na mwengine.

MHE. DAVID Z. KAFULILA: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri kwa hotuba yake ya leo hasa kuhusu namna ambavyo sayansi na teknolojia inavyoweza kusukuma uchumi katika medani na kilimo, biashara na ajira. Naomba kupatiwa majibu kuhusu masuala yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kampuni za Simu za *Vodacom* na *Zain* zimekuwa na minara isiyofanya kazi katika Kata za Sunuka, Sigunga na Buhinga Jimbo la Kigoma Kusini kwa zaidi ya miaka minne bila mafanikio. Maeneo haya ni miji yenye wakazi wengi sana na kuna shughuli za kilimo, uvuvi na biashara. Ni muhimu nielewe nafasi ya Wizara katika makampuni haya hususani kampuni ya *Zain* ambayo Serikali yetu ni mbia. Nasema haya kwa sababu mpaka sasa nusu ya eneo la wilaya ya Uvinza hakuna simu. Hii ni pamoja na Kata za Sigunga, Sunuka, Buhinga na Kalya. Kata zote hizo zipo Ukanda wa Ziwa Tanganyika ambayo kwa sasa inafikika kwa barabara nzuri kabisa. Naomba Serikali iwapatie majibu wakazi wa kata hizi ni lini watapata mawasiliano ya simu. Naomba sana Serikali/Wizara yako imsaide katika tatizo hili kwani ni kilio cha wakazi wa wilaya hii ya Uvinza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujua mchango wa Wizara hii katika kuisaidia Serikali kufahamu mapato halisi hasa ya Makampuni ya Simu Tanzania ambayo mpaka sasa kuna taarifa kwamba hatujawa na teknolojia ya kutuwezesha kujua mapato halisi ya kampuni hizi na hivyo tunapoteza mapato mengi ambayo tungeyapata kupitia kodi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ajili ya kuboresha sayansi na teknolojia, nashauri Taasisi zinazosimamia vyuo vya elimu ya juu zipangwe upya. *TCU* na *NACTE* zitazamwe upya. Nadhani tungeweka Vyuo Vikuu vyote Tanzania vingewekwa chini ya *TCU* na *NACTE* ibaki inasimamia vyuo vya ngazi ya *diploma* na *certificates*. Hii itasaidia kuboresha viwango vya elimu za vyuo vikuu vyote kwa kuwa vitakuwa chini ya *regulatory authority* moja na pia *NACTE* ingeweza kuboresha *skills* na teknolojia ngazi za chini kabisa (*primary certificate*), kati kwa maana ya *advanced certificates* na *diploma*. Hii itasaidia kujenga mfumo ambao kada za chini na kati zitakuwa chini ya mamlaka moja na hiyo urahisi wa kusimamia viwango. Nasisitiza kwamba *skills* za chini na kati zina mchango mkubwa sana katika kujenga uchumi na ajira.

MHE. AMINA ABDALLAH AMOUR: Mheshimiwa Mwenyekiti, nachukua nafasi hii kwanza kuipongeza hotuba ya Bajeti ya mwaka 2011/2012. Kwanza nina suala dogo kabla sikuanza kuchangia hii hotuba nalo ni huduma za mawasiliano za *Zantel*, *Celtel*, *Tigo* huwa leseni zao wanapata kwenye Wizara ya Mawasiliano lakini siku hizi *Zantel*, *Tigo* na nyinginezo hizi sasa wamejikita kwenye huduma za fedha za kutuma na kupokea pesa kama mabenki na Benki huwa wanapata leseni zao *BOT*. Je, haya Mashirika ya Simu yanapotoa huduma za kifedha hutumia leseni hiyo hiyo ya mawasiliano au wanachukua na leseni nyingine ya *BOT*? Nimefarijika sana kusikia kwamba Tume kwa kushirikiana na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar itafungua Ofisi Zanzibar kwa lengo la kupanua shughuli, kwa hivyo naomba hiyo Ofisi ifunguliwe kwa haraka sana ili tuweze kwenda sambamba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Shirika la Simu (*TTCL*) ipo katika hali mbaya na la kusikitisha sana kuwa hili ni Shirika la mwanzo Tanzania na hii leo limekuwa ni la mwisho na hii n nikutokana madeni mengi wanayodai makampuni na wananchi wa kawaida kutokana na hayo naiomba Serikali isaidie Shirika la *TTCL* kwa kuwawezesha ili waweze kulifufua hili shirika au kulinusuru hili shirika lisije likafa kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu simu za mkononi, nianze kuzipongeza Kampuni zote za simu kwa huduma zake nzuri na punguzo lao na kila siku wanabuni mbinu mbadala ya kuweza kumuwezesha mwananchi wa kawaida kutumia simu lakini hawa ni wawekezaji na huwa wanapata msamaha wa kodi kwa muda wa miaka mitano, naiomba Serikali iwaangalie vizuri.

MHE. HAMAD RASHID MOHAMED: Mheshimiwa Mwenyekiti, matumizi mazuri ya rasilima – mkongo. Pamoja na kuwepo kwa Mkongo wa Taifa, lakini pia Mashirika kama *Tanesco, Railway* wanayo miundombinu ya *fibre optic* ambayo haitumiwi kikamilifu. Ni vyema Wizara ikazijua na kuzitambua rasilimali hizi na kujua namna zinavyoweza kutumika vyema (*maximum utilization*) vinginevyo thamani halisi ya rasilimali hizi haitofikiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la urasimu katika kutoa huduma, dhana nzima ya teknolojia ni kupunguza urasimu, gharama na kuongeza ufanisi. Taasisi za Wizara zingetegemewa kuwa mfano wa kutoa huduma kwa wadau wake, lakini hali halisi sivyo ilivyo hivyo kuondoa dhana nzima ya Taifa letu kuingia katika karne ya utandawazi. Ni vyema Wizara ikasimamia Taasisi zake ili zitoe huduma kwa wadau wake kwa kiwango cha kuridhisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu kuwatambua wagunduzi, ni vyema Waziri akaeleza idadi na aina ya ugunduzi uliofanywa na kwa kiwango gani ugunduzi huo unalisaidia Taifa ama kiuchumi au kitaaluma. Ni vyema Waziri akatueleza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, matumizi ya *TEKNOHAMA* katika manunuzi, Serikali kutumia 82% ya Bajeti yake katika manunuzi, matumizi ya manunuzi kwa njia ya mtandao inazipunguzia Serikali kama za *line* 30% ya gharama ya manunuzi. Wizara isaidie *PPRA* katika kufanya utafiti namna ambavyo mtandao utatumika katika *E-Procurement* kwa ngazi za mikoa na Taifa ili kupunguza rushwa, wizi, ununuzi bidhaa dhaifu na kupandishiwa bei.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wizi katika matumizi ya simu, Wizara kwa kuititia Taasisi zake ifanye utafiti juu ya namna ya wizi unaofanywa na mabingwa wa matumizi ya mtandao. Benki nyingi, *TRA* ni miongoni mwa waathirika wa wizi huu. Aidha, Wizara ifanye uchunguzi wa namna ya kampuni za simu inavyowaibia wateja kwa kubana mawimbi na kuwakata katika muda wa matumizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mapato ya Kampuni za Simu katika mchango wa Pato la Taifa, Makampuni ya Simu mbalimbali na kutoa huduma pia zinaweza kutoa mchango mkubwa katika mapato yake kwa kulipa kodi stahiki kwa Serikali. Namtaka Waziri aeleze kwa kipindi cha miaka mitatu makampuni yamechangia kiasi gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la kuunganisha matumizi ya minara, Wizara kwa kuititia Taasisi zake iratibu na kupunguza ujenzi wa minara na izishauri Kampuni za Simu kuunganisha matumizi ya minara yao.

MHE. JOSEPHINE T. CHAGULLA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa wema wake wa upendo wake mkubwa kutuwezesha sisi sote leo kuwa hai na wenyе afya ya kutosha ni kitu cha kumshukuru sana. Aidha, napenda kumpongeza Rais wa Tanzania Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, kwa kuchaguliwa kwake kuwa Rais katika awamu ya pili. Pia nampongeza sana Waziri wa Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia pamoja na timu yake yote ya Wizara kwa kazi nzuri sana wanayoifanya. Pia naipongeza hotuba hii pamoja na Bajeti husika ya Wizara ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nitajikita kwenye usajili wa simu pamoja na mafanikio ya kusajili watumiaji wa simu za mkononi yaliyoainishwa kwenye taarifa ya hali ya uchumi ya mwaka 2010 kuhusu mamlaka haya, lakini naona bado kuna mapungufu sana. Matumizi ya simu za mkononi imeleta mabadiliko katika nchi yetu, mawasiliano yamerahisishwa sana hadi vijijini. Niombe Serikali iweze kuangalia upya gharama za uendeshaji kwa watumiaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu mradi wa *TEHAMA*. Naipongeza sana Wizara kwa jitihada zake za mradi wa ujenzi wa Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano na kufikisha huduma zake hadi Makao Makuu ya Mkoa na Wilaya zote nchini. Aidha, napongeza sana Wizara ya Sayansi na Teknolojia ndio muhimili wa maendeleo na uchumi wa kisasa tunaoutaka kuujenga. Hapa nchini sasa hivi simu ya mkononi sio tu kwa ajili ya kuzungumza bali ni Benki ya kuhifadhi na kutumia fedha na ni kiungo cha kupata taarifa mbalimbali ikiwemo bei za mazao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hivyo naunga mkono hoja.

MHE. RITTA E. KABATI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijaanza kutoa mchango wangu, nichukue nafasi hii kumpongeza Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na watendaji wote wa Wizara kwa hotuba yake aliyoiwasilisha hapa Bungeni. Nianze na pongezi zangu nyingi kwa Wizara hii hasa kwa ujenzi wa Mkongo wa Taifa. Pia ujenzi wa Taasisi ya Teknolojia ya Dar es Salaam, Taasisi ya Teknolojia ya Nelson Mandela Arusha na ujenzi wa Jengo la Tume ya Taifa Makao Makuu ya Nguvu ya Atomiki Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na pongezi hizo lakini kuna mambo ambayo Wizara ingetakiwa kuzingatiwa na Wizara na hasa kuwa na mkakati wa kutoa elimu ya umma. Kuna uelewa mdogo sana wa wananchi kuhusu sayansi na teknolojia yanavyohusiana moja kwa moja na maendeleo ya uchumi wa nchi yetu hivyo elimu zaidi inahitajika kwa umma kuititia vyombo vyahabari kwa Serikali na wawekezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, siyo siri bila sayansi na teknolojia nchi hii maendeleo yetu hayatakwendwa popote na tutaendelea kuwa nchi maskini, nchi isiyokwenda na wakati. Jambo lingine ni kutokuwa na mkakati madhubuti wa uibuaiji na uendelezaji wa vipaji vyahabari kwa Watanzania pamoja na kutokuwepo kwa mfuko maalum ya kuendeleza wagunduzi, wavumbuzi na vijana wenye vipaji kwa ufanisi zaidi ili kuleta

uzinduzi. Pia Serikali ingelazimisha Wizara zote za Serikali zitumie huduma ya vifurushi kutumia shirika hili ili kusaidia pia mzunguko wa pesa za Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho ningeomba pia Wizara iwe na mkakati madhubuti wa vivutio kwa vijana wa kike kupenda kusoma masomo ya sayansi ili kuwapo na uwiano baina ya vijana wa kike na wa kiume. Masomo ya sayansi ni magumu sana, ningeshauri Serikali wanapofanya mitihani ya mwisho na kufeli warejee na mitihani yao ya mazoezi kwa sababu watoto wanaweza kufeli sababu ya woga au wasiwasi wa mitihani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeshuhudia vijana wetu wengi sana wakivumbua vitu vingi sana ambavyo suaona mkakati wowote wa Serikali katika kuwasaidia ili uvumbuzi wao uwe na tija kwa Taifa na kuwatia moyo vijana wetu. Jambo lingine ambalo ningependa kulichangia ni pamoja na mradi wa anuani za makazi. Ni imani yangu kuwa kama zoezi hili litakamilika lingeweza sana kulisaidia Shirika hili la Posta. Lakini mradi huu umekuwa hadithi isiyokuwa na mwisho, niombe Serikali sasa iweke mkakati wa kuanza kwa huu mradi, ni imani yangu utaleta tija kwa wananchi na nchi hii kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Shirika la Posta halitaimarika kama halitakuwa na mkakati madhubuti wa kukabiliana na mabadiliko ya teknolojia ili kuhimili ushindani mkubwa kutokana na kuwepo na makampuni yanayofanya biashara kama hili na kwa ufanisi mkubwa. Nashauri Serikali ilisaidie Shirika hili ili liweze kujidesha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuunga mkono hoja.

MHE. IGNAS A. MALOCHA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nachukua nafasi hii kuipongeza hotuba hii na kuunga mkono. Naomba kuchangia hotuba hii kwa kueleza tatizo lililopo katika Jimbo langu baadhi ya kata na vijiji kukosa mtandao wa mawasiliano ya simu za mkononi japokuwa kuna minara ya *Vodacom* na *Airtel* kuwepo umbali wa kilomita 25 au 30 toka minara hiyo ilipo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kata hizo ni kata ya Milepa katika vijiji vya Milepa, Kisa na Msia, Kata ya Mfinga katika kijiji cha Mfinga na Kata ya Kaoze katika vijiji vya Kianda, Ilonda, Chombe, Tururu na Kirando. Katika vijiji hivyo ni tatizo kubwa wananchi hulazimika kupanda juu ya miti ya miembe, vichuguu au kuvizia mtandao katika maeneo fulani fulani. Eneo hili ni eneo lenye watu wengi na ni maeneo maarufu kwa kilimo cha mpunga, ufuta, mbaazi, ulezi na kadhalik, pia ufungaji na uvuvi katika Ziwa Rukwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na jitihada zote nilizofanya za kumuona Mheshimiwa Waziri na kumuomba kwa kumuandikia barua bado sijapata jibu la uhakika. Hivyo kupitia majumuishi ya hotuba ya Mheshimiwa Waziri naomba kupatiwa majibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huduma ya *TBC* Mkoa wa Rukwa ni tatizo kubwa. Naomba atoe ufanuzi wa tatizo hili katika Mkoa wa Rukwa na kutoa utatuzi wake. Narudia, naomba Serikali kutatua matatizo haya ni kero kubwa mno.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kupata ufanuzi nitaunga mkono hoja. Naomba majibu.

MHE. SALOME D. MWAMBU: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naomba kuipongeza Wizara na Mheshimiwa Waziri, wafanyakazi wote wa Wizara kwa juhudi wanazofanya kuhakikisha shughuli zinaenda kwa njia zote, mfano kutafuta fedha za kuendeleza utafiti. Utafiti ndio uti wa mgongo wa Taifa lolote. Hata nchi tajiri zilizoendelea huhakikisha fungu kubwa la utafiti linatengewa fedha, shilingi bilioni 30 walizopewa mwaka 2010/2011 hazikutosha. Tena mwaka huu zimepungua Wizara imepewa shilingi bilioni 19.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mawasiliano ya simu za mikononi bado ni tatizo kubwa kwenye maeneo mengine hususani Wilaya ya Mkalama Jimbo la Iramba Mashariki hadi sasa hivi kata 12 bado hazina mawasiliano ya simu za mikononi ya uhakika. Kata hizi ni Miganga, Nduguti, Sumanga, Mwangeza, Mwanga, Ilunda, Matongo, Mpambala, Nkinto, Msingi, Kikonda na Kinyangiri. Pamoja na kuandika barua kama alivyonishauri Mheshimiwa Waziri mwezi Februari, 2011 sikupata jibu, juhudi ziligonga mwamba. Namuomba Mheshimiwa Waziri awajibu wananchi lini watapata mawasiliano haya ya simu za mikononi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ihakikishe inasambaza haraka mawasiliano ya *TEHAMA*, ili tuweze kupunguza wanafunzi wetu kufeli mitihani. *Internets* zifungwe haraka wilayani na shule za *A-Level*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niunge hoja mkono kwa 100% nashukuru kwa kazi nzuri waliyofanya. Ahsante.

MHE. ALI KHAMIS SEIF: Mheshimiwa Mwenyekiti, miaka miwili iliyopita Tume ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia ishirikiana na wadau wengine na walipewa jukumu la kuitafiti nishati mbadala ya kupikia kutohana na makaa ya mawe. Utafiti huo mpaka leo haujatoa matokeo mazuri na bado Watanzania wanategemea misitu kwa 92% kwa ajili ya kupata nishati ya kupikia aidha ya mkaa au kuni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia hotuba ya Waziri katika ukurasa 45 na 46 kifungu 28 Tume hii imeweka tafiti tano ndizo zenye msisitizo na ndizo zitakazoteklezwa. Nionavyo mimi mfano utafiti wa Kilimo Kwanza hautakuwa kwa ajili ya kukidhi nishati ya kupikia. Tendo la uhitaji wa misitu kwa wingi utasababisha uhaba wa mvua na vyanzo vya maji hukauka, bila maji hakuna kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamuuliza Waziri huu utafiti wa uhaba wa mawe kwa ajili ya kupikia umefikia wapi? Nchi yetu hivi sasa ipo katika matayarisho ya

kuchimba Urani (*Uranium*). Je, Wizara imejipanga vipi kukabiliana na changamoto na athari ya uchimbaji wa madini ya Urani, hii ni hatari sana kama uchimbaji wake haukudhibitiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, inavyoonesha Kampuni ya Simu Tanzania na Shirika la Posta Tanzania bado mitaji yao haitoshelezi. Hali hiyo inasababishwa na nini wakati mashirika hayo yanafanya kazi zao kibashara? Ipo haja mashirika hayo yaangaliwe upya miundo yao na namna wanavyofanya biashara zao. Mtindo wa Serikali kutolipa gharama za simu wanazotumia uachwe na malimbikizo ya madeni yalipwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukurasa wa 36 kifungu 64 kinaelezea suala zima la Zanzibar kuunganishwa na Mkongo wa Taifa. Je, mkongo huo unategemea kuunganishwa hivi angalau Mheshimiwa Waziri anieleze mwezi na mwaka gani? Katika maelezo ya awali ya huko nyuma tuliambiwa uwepo wa Mkongo wa Taifa utapunguza kwa kiasi kikubwa gharama za simu za mkononi. Ninaelewa kuwa mkongo huo haujaenea nchi nzima lakini hizo sehemu ambazo mkongo umeshafika kuna tahfifu gani ya gharama za simu za mkononi? Ahsante.

MHE. AUGUSTINO M. MASELE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaunga mkuu hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia kwa namna alivyowasilisha taarifa yake kwa kiwango kinachokubalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la mawasiliano ni nyenzo muhimu katika harakati zote za maendeleo, sote ni mashahidi ni kwa jinsi gani hivi sasa mawasiliano yaliyoleta mapinduzi ya hali ya juu ya upashanaji habari kupitia mitandao ya simu, mitandao ya tovuti pamoja na barua pepe kumeifanya dunia kuwa ni kijiji kidogo ambapo taarifa nyingi muhimu zenye mwelekeo wa kurahisisha maisha ya wananchi zinapatikana kwa wakati muafaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi sasa shughuli za kibashara zinafanyika kwa wepesi kabisa ambapo wafanyabiashara hivi sasa wanaweza kuagiza bidhaa kwa njia ya simu na mitandao ya tovuti na barua pepe bila ulazima wa mhusika kulazimika kusafiri yeche. Hali hii imepunguza kwa namna ya pekee usumbufu usiokuwa wa lazima uliokuwepo hapo mwanzo ambapo wafanyabiashara wanalazimika kusafiri kufuatilia bidhaa sehemu mbalimbali bila kufahamu kama bidhaa zipo sokoni na zinapatikana kwa bei gani. Kwa kila hali kuboreshwa kwa mawasiliano nchini kumeboresha maisha ya Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huduma za malipo iliyokuwa ikifanywa kwa njia ya benki hivi sasa zinafanyika kwa njia ya simu kama vile *M-pesa*, *Tigo Pesa* ambapo malipo ya ankra za umeme, maji na kadhalika na usafirishaji wa pesa unaafanyika kwa urahisi kabisa. Upanuzi wa Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano umekuwa na mchango mkubwa katika kupunguza gharama za mawasiliano ya simu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la sayansi na teknolojia katika ulmwengu huu lina umuhimu wa pekee maana hapa ndipo mapinduzi halisi ya ufanisi na ustaarabu wa

maendeleo katika sekta mbalimbali za kijamii zikiwemo afya, kilimo, viwanda, biashara na kiulinzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hili ni jukumu la Serikali kuhakikisha kuwa kunakuwepo na fedha za kutosha ili kuiwezesha Wizara na nchi kwa ujumla kuweza kupata teknolojia za kisasa kutoka nje ya nchi. Ikibidi kuzinunua kwa maslahi ya nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania likiwa ni Taifa changa lina wajibu wa kipekee wa kuwekeza kwa kiwango kikubwa katika sekta hii muhimu ili kuwa na muono mpana katika kuwekeza katika utafiti kwa kushirikiana na Mataifa mengine yaliyopiga hatua katika nyanja husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania yenye nguvu inategemea ni kiwango gani inawekeza katika sekta hii ya sayansi na teknolojia. Mataifa mengi yenye nguvu za kiuchumi na hata kijeshi yaliwekeza kwa kiwango kikubwa katika sayansi na teknolojia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

MHE. RAJAB MBAROUK MOHAMMED: Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara hii ni Wizara ya Muungano, lakini muundo mzima wa uongozi hauonyeshi kuwa Wizara hii ni ya Muungano ambapo viongozi wote hususan Wakurugenzi, Wakuu wa Idara na wa vitengo.

Nakuomba Mheshimiwa Waziri unipatie maelezo yafuatayo; ni Wazanzibari wangapi ambao wanaendesha Idara/Vitengo katika Wizara hii? Kuhusu ajali za barabarani, Wizara ya Sayansi na Teknolojia ina jukumu kubwa la kusaidia wananchi na kulishauri Taifa juu ya teknolojia ipi ya kutumia ili kudhibiti ongezeko la ajali za barabarani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni hivi karibuni Kampuni ya *U-track* imekuja na teknolojia yake mpya ya kuweka kifaa kinachonakili mwenendo wa gari. Hata hivyo bado teknolojia hii haijaweza kupunguza tatizo hilo. Ni dhahiri kwamba teknolojia hii ni mradi ambao hauleti tija ila kuongeza gharama kwa watumiaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, je, Mheshimiwa Waziri una taarifa gani kuhusu teknolojia hii na ni hatua gani Wizara yako imechukua ili kuridhia kutumika kwa teknolojia hii?

Kuhusu Bajeti ya mwaka 2011/2012 Mheshimiwa Waziri, ni ukweli usiofichika ya kwamba Bajeti uliyopangiwa ni ndogo hata hivyo matumizi ambayo yanaonekana hayana ulazima, yamekuwa na fedha nyingi kuliko maeneo ambayo ni muhimu mfano Wizara imepanga kutumia shilingi milioni 759 kwa safari za ndani na nje, shilingi milioni 126 kwa *hospitality*, shilingi milioni 176 kwa matengenezo ya magari na shilingi bilioni 1.2 kwa kulipia posho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Idara ya *ICT Subvote 2002 – Item 410700 (Feasibility Studies, Project preparation and design)*, haikutengwa fedha, je, Mheshimiwa Waziri atakuwa tayari kupunguza matumizi hayo ili angalau kitengo hiki kipatiwe fedha?

MHE. KOMBO KHAMIS KOMBO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nachukua nafasi hii kuchangia hotuba ya Wizara ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia kama ilivyowasilishwa katika Bunge lako hili Tukufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara hii ni mionganoni mwa Wizara zinazohusiana na mambo ya Muungano. La kusikitisha zaidi, tunapotetea haki za Zanzibar ndani ya mambo ya Muungano wanatokea wengine kutukejeli, kutudharau na hata kutuona maadui dhidi ya Muungano. Kinachotendeka ndani ya Serikali ni kutuwekeea Mawaziri kutoka Zanzibar kwa mambo ya Muungano kama njia ya kutufunika macho wazanzibar tuone kwamba Mawaziri wanatoka Zanzibar kumbe ni sawa na chambo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, takribani maafisa wote wa Wizara hii ambaeo ni wa nafasi za juu ni wa upande wa Tanzania Bara. Tujiulize, hivi hakuna watu ambaeo wana uwezo wa kushikilia nafasi hizo isipokuwa nafasi ya Uwaziri tu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia ni chombo muhimu sana katika ulimwengu huu wa karne ya 21 ya Sayansi na Teknolojia. Hata hivyo Serikali ina haki na wajibu wa kuelewa yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, karne ya 21 ni karne inayoendana na masuala ya utaalamu huo. Nchi yetu leo imefikia hatua ya kuijiedeleza kielimu kipitia mitandao, hata hivyo uendelezaji wa elimu hiyo ya kutumia mitandao imekuwa ya viwango vya chini na duni kutokana na umuhimu wa jambo hilo katika sekta husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia imeweza kuifanya dunia kuwa kijiji kwani ni maeneo machache ambayo hayana mawasiliano ya simu na mitando mingine. Hata hivyo kutokana na Sayansi na Teknolojia, wananchi walio wengi wameweza kuijiedeleza kielimu kipitia mitandao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na Wizara hii nina ushauri ufuatao:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa kuna Wizara hii ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia na kwa kuwa kuna makampuni kadhaa ya mawasiliano: Je, Wizara hii imechukua hatua gani juu ya kuhakikisha kwamba makampuni haya yanafanya kazi zake kwa ufanisi na kutoa pato kwa Taifa bila kuwepo kwa ubadirifu wowote?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Mashirika haya huwa yanaweka minara ya mawasiliano katika sehemu mbalimbali ya nchi yetu na kwa kuwa baadhi ya sehemu nyingi hazijapata mawasiliano licha ya kwamba wananchi walio wengi wana simu za mikononi: Wizara itachukua hatua gani kuhakikisha kwamba Minara ya mawasiliano ya mashirika ambayo ni mengi lakini hayajafika katika baadhi ya maeneo ya Tanzania yanafika katika maeneo mengine?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kila chenye faida hakikosi kuwa na hasara. kwa maana hiyo, Wizara ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia ina wajibu wa kuunda timu ya wataalamu ambayo itachunguza ni kwa kiasi gani minara ambayo imejengwa karibu sana na makazi ya wananchi wetu kwamba haitafika mahali ikaweza kutusababishia madhara kwa wananchi wetu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukizingatia kwamba nchi yetu kwa upande wa Bara kuna sehemu ambazo ni za minyanyuko (milima) ambayo tunaweza kupata mawasiliano kwa masafa marefu na maeneo hiyo ya milima hayana wakazi, sasa basi kwa nini Wizara haitaki mashirika hayo ya simu kutumia maeneo hayo kuweka minara yao ili kupunguza athari ambazo zinaweza zikaja kututokea hapo baadaye.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni matumaini yangu kwamba Wizara hii itafanya kazi kuhakikisha kwamba wananchi wa Tanzania wataondolewa na matatizo ya mawasiliano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba Mheshimiwa Waziri awatake wahusika wa mashirika ya simu nchini kuweka viwango sawa kwani unapopiga simu katika shirika moja kumpigia mtu aliye katika shirika linguine, fedha zinakatika kiasi ambacho inakatisha tamaa. Je, kwa nini hawaweki viwango sawa hasa ukizingatia kwamba mashirika hayo yapo Tanzania lakini na watumiaji pia ni Watanzania? Kwa nini wasiweke makato hayo kwa simu za nje ya nchi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, namalizia kwa kusema kwamba penye nia pana njia. Tukiwa makini tutafanya Taifa lenye ubora katika karne ya 21 ya Sayansi na Teknolojia ya kweli.

MHE. HAROUB MUHAMMED SHAMIS: Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla ya yote, napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu (S.W) kwa kunipa afya njema, elimu na uelewa na kuniwezesha kushika kalamu kuandika machache kuchangia Wizara hii kwa manufaa ya nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda pia kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa mawasiliano, Sayansi na Teknolojia Prof. Makame Mnyaa Mbarawa kwa hotuba yake nzuri na ya kitaalamu. Napenda pia kumpongeza Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete kwa kuuona uwezo alionao Prof. Mnyaa na ndiyo maana akamkabidhi Wizara hii muhimu. Ama sasa “upele amepewa mwenye kucha”, kwani Prof. Mnyaa ni mtaalam aliyebolea kwenye sayansi na teknolojia na ni mchapakazi mahiri na makini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mawasiliano, sayansi na teknolojia ni kitu muhimu sana kwa maendeleo ya nchi yoyote katika ulimwengu wa sasa. Inasikitisha kuwa Serikali hilo hajjaliona au inalitazama kwa makengeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ufinyu wa bajeti wa Wizara hii na hizo kidogo pia hazitolewi kama zilivyoidhinishwa na Bunge. Hiyo ni ushahidi kuwa Serikali inapuuza

maendeleo ya mawasiliano, sayansi na teknolojia. Mwezi Aprili, 2011 Bunge hili liliridhia Itifaki ya Sayansi, Teknolojia na Ubunifu ya *SADCC*; azimio la mwaka 2008.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na yote hayo, Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alitoa kauli ya kuboresha Sekta ya Utafiti kwa kuwapatia shilingi bilioni 100. Lakini jambo la kushangaza, zimetengwa Shilingi billioni 25 tu. Hii ni aibu kwa nchi inayopambana kutaka maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo la uduni mkubwa wa bajeti utalemaza ari na morali ya watafiti wetu, kwani utendaji wa *COSTECH* pamoja na urasimu mkubwa ilionao kwa kuruhusu kazi za kitafiti inataka pia mtafiti atoe 10% gharama ya utafiti wake ndiyo *proposal* yake ya utafiti ipitishwe. Hili ni tatizo na linawakatisha tamaa watafiti wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ugunduzi na vipaji katika Sayansi ni lazima Serikali isimamie na kusaidia vipaji kuendelezwa. Kuna tabia ya Serikali kuwapuuza wagunduzi wetu wenyе vipaji (wasiokuwa na elimu ya juu). Hili ni tatizo. Historia inatueleza, fundi wa banskeli ndiye mgunduzi wa ndege (*Aeroplane*), elimu yake ilikuwa ni ya kiwango cha chini, mgunduzi wa redio pia hali kadhalika hakuwa na *degree*. Kilichofanyika ni Serikali zao kuthamini ugunduzi wao, kuwawezesha, kuuboresha na kuwathamini. Waswahili wanasema, “Mdharau kwao Mtumwa.” Tuanze kujithamini na ndiyo tutathaminiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Nashukuru na Mwenyezi Mungu atubariki sote.

MHE. DKT. WILLIAM AUGUSTAO MGIMWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nachukua nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri wake pamoja na wafanyakazi wa Wizara yake kwa kazi yao nzuri. Pamoja na pongezi hizi, naomba nichangie kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, nafahamu kwamba Wizara yako imekamilisha Sera ya Taifa ya Bayoteknolojia na Sera ya Taifa ya Utafiti na Maendeleo, Sera ya Taifa ya Teknolojia za Nyuklia na kwamba sasa mnashughulikia rasimu ya Sera ya Taifa ya Sayansi, Teknolojia na Ubunifu. Katika hili, nashauri Wizara ishirikiane na Wizara ya Elimu vizuri ili kuhakikisha kwamba:-

(a) Ubora wa ufundishaji wa masomo ya *Science* unakuwepo kuanzia Shule za Sekondari mpaka Vyuo Vikuu. Hili linawezekana ikiwa tu miundombinu ya Elimu, (Walimu, vitabu, maabara, nyumba za walimu pamoja na mabweni) vitakuwepo;

(b) Taasisi za Utafiti zinaimarishwa katika nyanja zote za sayansi zitakazosaidia kuboresha shughuli za uchumi nchini;

(c) Kuhuishwa rasmi ubunifu wa nyanja mbalimbali katika mifumo rasmi ya ufundishaji na utafiti.

(d) Utaratibu uwepo wazi wa kutangaza matokeo ya tafiti mbalimbali za kisayansi na ushawishi wa kutumia matokeo ya tafiti hizo (*Application of Research Findings*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, jukumu la kujenga uwezo wa watafiti ni muhimu sana, lakini inasikitisha kwamba bajeti ya Wizara inapungua badala ya kuongezeka ili majukumu hayo yatekelezeke. Je, Wizara ina mikakati gani kulikabili hili?

Mheshimiwa Mwenyekiti, napongeza sana uundwaji wa Mfuko huu wa Mawasiliano kwa wote (*UCAF*). Napendekeza bila kubagua, tupewe orodha ya Wilaya na maeneo ya sehemu za vijiji ambapo mfuko huu utajikita kutoa huduma hii. La sivyo, napendekeza mfuko huu ulenge kutoa mawasiliano vijiji vyote Tanzania.

MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuipongeza Wizara kwa kazi nzuri na kasi yake katika kuhakikisha matumizi ya Teknohama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na pongezi zangu kwa Wizara, kwa ujumla, napenda kutoa ushauri kwa Serikali ili wananchi wote wa Tanzania wafaidi matunda ya uhuru na upashanaji habari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkoa wa Rukwa umekuwa na matatizo makubwa sana ya kupata habari katika maeneo mengi. Usikivu wa redio ya Taifa (*TBC*) haupo na maeneo ambayo yapo, basi ni ya taabu sana. Mfano halisi wa maeneo ambayo redio ya Taifa haisikiki hususan Kata zilizopo mwambao wa Ziwa Mkowe, Sopa, Matai (Makao Makuu ya Wilaya mpya) Katete, Mwazje Legezamwendo, Mwimbi, Ulumi na Jimbo lote kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Wizara itambue kwamba Mikoa yote pembezoni imekuwa *disadvantaged* katika mambo mengi ya kimaendeleo, hivyo rai yangu kwa Wizara ihakikishe kwamba Mikoa hii haiendelei kuachwa nyuma kwa kunyimwa fursa ya kupata mawasiliano na hasa kwa kupitia redio yao ya Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mawasiliano ya simu za mkononi kwa Jimbo la Kalambo ni ya taabu kweli. Naomba Wizara ichukue hatua za makusudi kuhakikisha kwamba mawasiliano yanapatikana na yale maeneo ambayo mawasiliano yanapatikana kwa taabu yaboreshwe ili kuwe na tija.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara imetua ahadi kwamba maeneo yote ambayo mawasiliano ya simu za mkononi hayapo watahakikisha kwamba ufumbuzi unapatikana kwa muda mfupi itekelezwe, maana tumewaaahidi wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

MHE. PAULINE P. GEKUL: Mheshimiwa Mwenyekiti, tafiti nyingi zianzishwe kuhusu vyombo vya usafiri mfano, magari, pikipiki, trekta na mashine za viwandani vinginevyo tutakuwa *dumping area* ya nchi nyingine. Ni jambo la aibu, miaka 50 ya nchi yetu hatuna viwanda kama hivyo wakati tuna raslimali nyingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, simu za mkononi nyingi zimekuwa za kichina na fanyeni huo mfumo wa Uingereza wa *tress and tracking* kuzikataa sisi kama nchi simu ambazo zinazwa madukani lakini hazina *quality*. Wananchi wengi wameibiwa fedha zao kwa kununua simu ambazo ukizichaji hazina hata siku moja na zimeshakata moto. Hizi simu zipigwe marufuku.

Mheshimiwa Mwenyekiti, gharama za simu ziunganishwe kwa kampuni zote, *rate* zilingane kwa kila mtandao ili kuondoa usumbufu wa wananchi kubeba simu mbili mpaka tatu. Gharama zikilinganishwa, usumbufu utapungua kwa wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vinginevyo ni Wizara nyeti, hivyo iijitahidi kufikisha huduma zake kwa wananchi, *next time* waongezewe fedha, kwani bilioni 71 hazitoshi kwa Wizara hii hasa suala zima la utafiti.

MHE. DAVID E. SILINDE: Mheshimiwa Mwenyekiti, katika maeneo mengi ya vijijini kama vile Tarafa ya Msangano, Kata ya Chiluluno katika Jimbo la Mbozi Magharibi hakuna mitandao ya simu ya aina yoyote, hivyo kuifanya jamii yetu kuendelea kutumia njia za zamani kufanya mawasiliano. Hii inaathiri sana utendaji kazi hasa katika kupata taarifa na wakati matukio ya uhalifu yaktokea wananchi wanashindwa kupata msaada kwa wakati. Hivyo basi, naiomba Serikali iliangalile hili upya kwa kupeleka mitandao ya simu vijijini na maeneo mengine ya jimbo la Mbozi Magharibi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika maeneo mengine ya vijiji katika Shule nyingi hasa za Misingi na Sekondari wanafundishwa masomo ya TEHAMA kwa Shule za Misingi na ‘*Computer*’ kwa Sekondari katika dhana ya nadharia. Sasa Serikali inaweza kutueleza ni lini tatizo hili litakwisha na wananchi kupata masomo kwa vitendo “*practical*” ili kukabiliana na changamoto zinazoendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali yetu imeshindwa kuwa wabunifu na wavumbuzi katika suala la mawasiliano na ndiyo maana leo kampuni yetu ya *TTCL* inakufa. Hivyo basi, Serikali inaweza kutueleza ni nini imeweza kugundua katika masuala ya mawasiliano?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

MHE. SABREENA H. SUNGURA: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda na mimi kuchangia hoja hii kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika suala zima la mawasiliano napenda kuchangia katika matumizi ya simu za mkononi, lakini ningependa kushauri zifungwe sheria kwa

kuwa tumekuwa tunakatwa pesa nyingi bila tija katika mawasiliano. Zitungwe regulations zitakazowajibisha pale ambapo pesa itakatwa bila *reasonable cause*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la habari ya simu za mionzi ni *sensitive*, mimi binafsi limenitokea mwaka 2010 tarehe 24 mwezi wa Desemba saa 10.15 jioni kutoka number +339. Hili ni tatizo kwa kuwa mimi binafsi lilitaka kunichomoa roho, tunaomba mamlaka ichunguze.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango mwingine ni katika suala zima la *email trafficking*. Hili ni tatizo sugu, watu wengi wana-interfere *email* zetu na hata kufikia kutapeli kupitia *email* za wenzao. Hili ni tatizo, lazima litafutiwe ufumbuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hayo machache, Naomba kuwasilisha.

MHE. SALUM KHALFAN BARWANY: Mheshimiwa Mwenyekiti, ili nchi iweze kupiga hatua katika maendeleo yake, ni lazima ijikite katika sayansi na teknolojia. Nchi ambazo zimeendelea zinafikia maendeleo yake katika kusimamia kwa karibu zaidi katika sayansi na teknolojia. Ni vyema sasa Taifa letu kama nchi ikajiandaa katika kuwaandaa wananchi hasa vijana wetu katika *School* zetu tukajenga mfumo imara na madhubuti katika taaluma ya sayansi. Aidha, masomo ya sayansi katika mitaala hayajashughulikiwa kikamilifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jengo la *TTCL* limekodishwa kwa shughuli nyingine na wao *TTCL* wamegharimika kukodisha kwa gharama kubwa zaidi ya wao walivyokodi hilo jengo wanaloofanya kazi. Hayo ni matumizi mabaya ya pesa za Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na ushindani mkubwa wa makampuni ya kutoa huduma za simu za mkononi, lakini bado gharama zake zipo juu kwa kiasi kikubwa. Ni vyema Serikali ikakaa na makampuni hayo na kuona gharama hizo zinapungua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Watanzania wengi wana ubunifu wa asili wa uvumbuzi wa kisayansi lakini Serikali bado haijaona umuhimu wa kutumia vipaji vyta wananchi wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna watengenezaji wa bunduki aina ya gobole ambao kwa miaka mingi tunao watu wenyewe uwezo wa kutengeneza hivyo vifaa. Ni muhimu kuvi boresha kisasa katika maana ya kisayansi. Kinyume chake, wenyewe uwezo na ujuzi huo huonekana ni wasaliti na mvunja sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaweza kuanza na hawa katika fani mbalimbali na watu hawa wenyewe utaalam wa aina hiyo wapo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

MHE. MOZA ABEDI SAIDY: Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, namshukuru *Allah Subhana huwataala* kwa kutujaalia afya njema. Nampongeza

Mheshimiwa Spika, Naibu Spika na Wenyeviti kwa kulimudu Bunge letu Tukufu na kuliongoza pamoja na changamoto za hapa na pale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nami nichangie machache kuhusu Wizara hii. Maendeleo ya nchi hupiga hatua inapokamilisha kuhalilisha sayansi na teknolojia katika maeneo mbalimbali ya uchumi na maisha mijini, vijiji na vitongoji katika nyanja hizi japo inatia moyo pamoja na changamoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa sayansi na teknolojia huchukua Sekta ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi, Viwanda, Nishati, Maliasili, Afya na Vyuo Vikuu pamoja na sera na sheria, bado changamoto za kiutendaji zipo. Nikianza na shule/vyuo kwa wanafunzi wanaodahiliwa, vifaa vya sayansi havifiki kwa wakati mashuleni, maabara ziwepo mashuleni na hasa ukizingatia Serikali inahitaji kuona umuhimu wa somo hili nchini. Basi iwajibike ipasavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa raslimali watu *TEHAMA* kuendeleza ujenzi wa mkongo wa mawasiliano wa Taifa ili kuunganisha Mikoa, Makao Makuu ya Mkao, Wilaya Shule ya Msingi/Sekondari nchini, hospitali zote na kadhalika, kwa kuwa wahitaji ni wengi, Serikali ingeliangalia Makao Makuu ya nchi Tanzania Dodoma na Wilaya zake, hasa Kondoa Kaskazini Wilaya mpya Chemba hakuna mawasiliano. Sehemu nyingi ndani ya wilaya hizi Vijiji na Vitongoji na hata Kata kwa Kata baadhi, hasa ongezeko la watu kuwa kubwa na hitaji halikidhi sehemu kubwa la eneo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa mawasiliano ni maendeleo ya nchi Serikali ione umuhimu simu za kiganjano na umeme ufikie kule ambapo hakuna kabisa zaidi ya makao makuu ya wilaya na sehemu za karibu na hapo kama vile Kondoa Kaskazini wilaya ya Chemba Serikali ifike wakati ione umuhimu wa kuwapelekea mawasiliano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ifikie wakati iunganishe Makampuni haya ya simu za mkononi, ziungane kuwa na bei moja kwani imekuwa gharama kubwa kwa mtumiaji. Hakuna sababu ya kuwa na bei tofauti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali iangalie tozo hizo za kwenye Halmashauri ndizo zinazosababisha wawekezaji kufikia bei ya mtumiaji kuwa gharama kwa mtandao mwingine kwenda mwingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza Wizara kwa kuanzisha *TEHAMA*, raslimali watu na kujenga mashule na kweli wananufaika. Ningependa kuishauri Serikali na Wizara kujenga Shule ya walemaru wakiwamo walemaru wa ngozi, kwani nao ni moja ya jamii inayohitaji huduma hii hasa hapa Mkoani Dodoma kwani tayari tumeona walemaru wakishirikiana na kuanzisha karakana yao ya kutengeneza balskeli za miguu mitatu. Hivyo wangetengewa shule na kupatiwa walimu wenye ujuzi wangefanya vizuri zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishauri Wizara kule ambapo bado, basi waangalie maeneo ambayo bado. Naipongeza Wizara, tena naunga mkono hoja.

MHE. JOHN P. LWANJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeomba minara maeneo yafuatayo:-

- (a) Mwamagembe & Kintanula (barabara ya Itigi – Chunya);
- (b) Itigi – Kitaraka – Kazikazi – Tabora;
- (c) Kata ya Ipande Tarafa ya Itigi; na
- (d) Kata ya Idodyandole, Jimbo la Manyoni Magharibi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na maombi haya ya muda mrefu, bado hatujapata huduma hii muhimu. Masharti/*requirements* za maeneo haya kupatiwa huduma za simu za mikononi yametimizwa, kwa mfano Mwamagembe, wengi ni matajiri kutokana na kilimo cha tumbaku na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkongo wa Redio Tumaini uliofungwa mji mdogo wa Itigi, umeingilia redio nyingine zote. Hakuna redio zinazosikika zaidi ya redio hiyo moja. *TBC* ambayo ni Redio ya Taifa haisikiki kabisa, inasikika maeneo ya Manyoni, Kamenyanga na mjini tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitapenda kupata maelezo au majawabu kwa hoja hizi mbili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawasilisha.

MHE. SYLVESTER M. MABUMBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, napenda kumpongeza Waziri mtoa hoja, Naibu Waziri na watendaji wa Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Wizara hii inashughulikia mambo yote ya mawasiliano, sayansi na teknolojia, napenda kuchangia hoja zangu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika sekta hii ya mawasiliano naiomba Serikali kupitia Wizara hii ihakikishe kwamba makampuni ya simu ambayo kwa hakika yanapata faida kubwa (*super abnormal profits*) kutokana na biashara ya simu za mikononi, yanachangia ipasavyo kwa njia ya kodi. Siku hizi karibu makampuni yote ya simu yanachezesha michezo ya bingo kwa namna ambayo yanawaibia kwa hadaa Watanzania. Mchezo wa bingo unaochezesha na makampuni haya naomba Serikali yetu ipige marufuku kabisa. Naomba Serikali michezo inayochezeshwa na Vodacom, Airtel, Zantel na Tigo ipigwe marufuku kwa sababu inawaibia sana wananchi wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba Mheshimiwa Waziri atuambie iwapo michezo hiyo inayoendeshwa na Makampuni hayo kama yanatangaza mapato yanayopatikana katika kila mchezo au *promotion* inayoendeshwa, ni kiasi gani kinalipwa Serikalini? Pia naomba gharama za mawasiliano kwa njia ya simu zishushwe ili kupunguzia mzigo wananchi wanapowasiliana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, napenda kuzungumzia Sekta ya Sayansi. Naiomba Serikali iwasaidie walimu wanaofundisha masomo ya sayansi ili tuweze kupata wataalam wengi katika eneo hili, sayansi iweze kuchangia maendeleo katika nchi yetu na sayansi ichangie katika uvumbuzi katika sekta mbalimbali katika nchi yetu. Naomba sana Serikali iwekeze katika sekta hii ili ichangie katika kilimo, afya na masuala yote ya kiuchumi na kijamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda pia nizungumzie Sekta ya Teknolojia. Maendeleo ya sayansi na teknoloji yasadie katika uvumbuzi. Naiomba Serikali yetu iongeze bajeti yake katika Vyuo vya Sayansi na Teknolojia. Nashauri tuwe na vituo vinavyoitwa “*Scientific Incubeters*,” yaani vituo ambavyo watoto watakuwa wakijifunza masuala ya teknolojia mbalimbali kwamba kwenye vituo hivi pawekwe vifaa ambavyo watoto watavitumia kuendeleza maarifa na mafunzo. Vituo kama hivi niliviona wakati wa ziara yangu Tokyo na Osaka, Japan.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Serikali ianzishe utaratibu wa kufundisha wanafunzi katika ngazi ya *Primary, Secondary* na elimu ya juu kwa kutumia Kompyuta kama inavyofanya nchi ya Rwanda. Wakati huu ni wa Sayansi na teknolojia. Tunao Watanzania ambao wamejaliwa vipaji mbalimbali ambavyo wameweza kutengeneza umeme unaotumia upepo, wameunda silaha, redio na kadhalika. Hawa wote nashauri Serikali yetu iwatambue, iwaratibu na iwave kila aina ya msaada wanaohitaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi naamini kwamba hata nchi zilizoendelea, zilianza na wavumbuzi au wabunifu wadogo wadogo ambao Serikali zao ziliwasaidia na kuwaendeleza ndio maana leo hii wanaunda ndege, magari, mali, silaha na mambo mengine mengi. Hawa wote hawakuzaliwa na vitu hivyo, bali walianza taratibu na Serikali zao ziliwasaidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, naomba nizungumzie uingizwaji wa bidhaa za *electronic* ambavyo viko chini ya kiwango. Wizara hii naomba isaidie kuelimisha wananchi namna ya kuvitambua vitu kama hivi ambavyo vinarudisha nyuma maendeleo ya Watanzania kwa kununua vitu ambavyo havina ubora/viwango lakini vinauzwa kwa bei kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

MHE. CAPT. JOHN Z. CHILIGATI: Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, nampongeza Mheshimiwa Waziri na Wasaidizi wake kwa hotuba nzuri yenye mwelekeo sahihi wa kuboresha masuala ya sayansi na teknolojia hapa nchini. Pamoja na pongezi hizi, ninayo maoni na maombi yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nashukuru kazi iliyofanywa na makampuni ya simu za mkononi ya kusambaza mawasiliano hapa nchini, mijini na vijiji hivi sasa takribani Watanzania milioni 20 wamefikiwa na huduma hii. Pamoja na kazi hii nzuri, bado kama Watanzania wengi hawajafikiwa na huduma hii kwa mfano katika Wilaya ya Manyoni, Tarafa nzima ya Nkonko yenye vijiji zaidi ya 20 na wananchi 10,000 kuna

minara miwili tu (*Voda na Airtel*) ya simu. Naomba Wizara izihamasishe kampuni za simu kuongeza minara Tarafa ya Nkonko. Kampuni za *Voda na Airtel* wamefanya *Market Survey*, soko lipo kubwa, lakini bado hawaanza kujenga minara licha ya ahadi za mara kwa mara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri kwamba Shirika la *TTCL* lihamasishwe kuongeza juhudhi, ubunifu na ujasiri wa kupanua huduma zao. Eneo la vijijini bado halina ushindani na kuna wateja wengi mno. Nashauri waelekeze huduma vijijini kwani watapata biashara nzuri na pia watakuwa wamepeleka ukombozi kwa Watanzania waishio vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, natamka kwamba naunga mkono hoja hii. Ahsante.

MHE. DKT. ANTONY G. MBASSA: Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa fursa ya kuwepo mahali hapa na kupata fursa ya kuchangia hoja hii muhimu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchukua fursa hii kupongeza juhudhi na jitihada mbalimbali zinazofanywa na Serikali katika kuboresha sayansi na teknolojia katika nchi hii, ikiwa ni pamoja na mawasiliano ya njia ya simu, redio, *fax* na *internet* na hii ikijumuisha juhudhi za kufanikisha Mkongo wa Taifa ambao utarahisisha mawasiliano hayo hapa nchini kwetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maendeleo ya nchi yoyote yanategemea ukuaji wa sayansi na teknolojia. Leo hii hapa nchini msukumo wa kuendeleza sayansi na kuendeleza uvumbuzi uliopatikana umekuwa mdogo mno. Kuna vijana wameweza kuunda vyombo vya kunasa mawimbi ya sauti au redio, wapo lakini Serikali haiwaendelezi wala kuwajali katika suala la kuendeleza ujuzi na upeo wao. Serikali ijali kazi yao na kuwapa motisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la mawasiliano ya redio ni ya muhimu sana katika nchi yetu. Zamani ilikuwepo Redio Tanzania na baadaye *TBC* na sasa hivi kuna vituo vingi vya redio, lakini masafa ya redio hizi hayafiki baadhi ya maeneo na hususan redio kongwe ya *TBC*, huko vijijini hakuna umeme na wengi hawana *television*, hivyo bado wanahitaji kupata habari, na redio ndicho chombo muhimu sana cha kufikisha mawasiliano haya. Napenda kuishauri Serikali kuongeza masafa ya redio ya *TBC* na ikiwezekana hata bei ya seli kavu nayo ipunguzwe ili wananchi wapate mawasiliano haya ya matangazo ya redio.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la kukua kwa teknolojia halikosi madhara yake. Kuna kundi kubwa sasa linafanya uhujumu kwa kuititia teknolojia hii. Kuna watu wanaiba fedha au wanatapeli kwa kutumia sayansi hii. Kuna matukio mengi ya wizi yametolewa taarifa benki na Polisi. Naomba Serikali ifanye mikakati ya dhati kuhakikisha wizi huu unakomeshwa na wahusika wanaadabishwa kwa kosa hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la wawekezaji wa huduma za makampuni ya simu ni la msingi kuangaliwa sana. Kampuni hizi zimewekeza sana hasa ujenzi wa minara huko vijiji, kumekuwepo na mikataba mibovu isiyo na tija kwa Serikali za vijiji hivyo. Aidha, ni mikataba ambayo imewekwa kinyemela na haina suala la uwepo wa usimamizi wa kisheria. Naomba Serikali ipitie upya mikataba hii na kuweka uwiano wa mapato kwa minara inayojengwa huko vijiji ili tuwainue hata wananchi kipato chao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, naomba makampuni haya ya simu yasadie katika kuboresha huduma za jamii huko vijiji na siyo mijini tu. Kimsingi, kuna zaidi ya watumiaji milioni 20. Naomba Serikali iangalie faida wanayokusanya watu hawa, nini wanachosaidia katika jamii kulingana na kile wanachozalisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia Serikali ifanye mikakati ya dhati ya kuhakikisha kuwa simu hizi na *Computer* zinazoletwa nchini hazihatarishi maisha ya mwananchi. Hakuna elimu inayotolewa kwa wananchi kuhusu madhara ya vyombo hivi kwa wananchi na: Je, yakitokea ni nani anayewajibika kulipia madhara ya athari hizi? Naomba Serikali inijibu kutokana na hili.

MHE. RIZIKI OMAR JUMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianze mchango wangu kwa hoja hii kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri na timu yake ya wataalam kwa namna walivyojipanga vizuri kulingana na hotuba yao nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mawasiliano ya Posta na Simu ni ya Muungano na kwa upande wa pili wa Muungano, yaani Visiwa vya Zanzibar haionekani kwamba kuna dhamira ya dhati ya kuboresha mawasiliano ya Posta hasa kule Pemba. Posta hizo zilizopo zimekaa kama magofu tu, hazina nyenzo zozote za kufanyia kazi zaidi ya visanduku vya barua tu. Hata hao wafanyakazi wamesahauliwa. Unapotuma pesa kwa njia ya Posta unaweza ukachukua zaidi ya siku mbili hazijapatikana. Je, kulikoni? Tunaomba hili lisawazishwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado kuna tatizo la matumizi mabaya ya simu. Pamoja na usajili wa namba unaofanywa, bado kuna baadhi ya watu wanatumia simu kwa kuwashambulia wengine, na ukitoa taarifa kwa wahusika wanakwambia hayo ni mambo ya kibinagsi. Je, usajili huu wa namba ulikuwa na maana gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kampuni ya Simu ya *TTCL* inaonekana kushindwa kutoa huduma kutokana na madeni mengi wanayodai kwa mashirika mbalimbali na kuwasababishia kutokuwapelekea huduma nzuri. Je, kwanini haibinafsishwi basi?

MHE. AGGREY D. J. MWANRI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya wananchi wa Jimbo langu la *SIHA* naomba kumpongeza Mheshimiwa Prof. Makame Mnyaa Mbarawa kwa hotuba nzuri na ya kuvutia ambayo ameitoa asubuhi hii hapa Bungeni. Pongezi sana Mheshimiwa Waziri. Aidha, nampongeza Mheshimiwa Charles Muhangwa Kitwanga - Naibu Waziri wa Wizara hii kwa kazi nzuri anayoifanya katika Wizara ya kumsaidia Prof. Mbarawa kwa ufanisi wa hali ya juu. Hongera sana Mheshimiwa Kitwanga (Mawe matatu) kwa kazi nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ombi langu katika Wilaya ya Siha ni kwamba ninayo maeneo katika Wilaya ya Siha ambayo mpaka sasa usikivu wake ni hafifu sana. Naomba tusaidiwe minara katika maeneo ya Mese, Kirisha, Miti Mirefu, Mowo-Njamu Kyaboo, Kandashi, Lekrimuni, Ngaritati, Donyomoruak na kadhalika, maeneo ambayo ni muhimu sana katika uzalishaji wa mazao ya biashara na chakula, mifugo na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, namkaribisha Profesa na Mheshimiwa Naibu Waziri katika Wilaya ya Siha ili wajionee wenyewe maeneo niliyoyataja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

MHE. AMINA ANDREW CLEMENT: Mheshimiwa Mwenyekiti, Shirika la Posta ni shirika mama katika teknolojia ya simu, lakini shirika hili kila siku zinapokwenda linazidi kudidimia. Naiomba Wizara kuliangalia kwa kina ili lisije likafa kabisa kwani linasaidia sana hasa kwa upande wa kusafirisha mizigo nje ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu teknolojia ya Simu, simu za mikononi bado zina ghamra kubwa kwa kukatwa pesa zisizo halali. Kuna wakati hata hujakopa hiyo mikopo wala hujajiunga na *music* unakuta umekatwa pesa bila sababu. Naomba Wizara ilifanyie kazi suala hili ili pesa zetu wateja zisipotee bure.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

MHE. LOLESTIA J. M. BUKWIMBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na watumishi wote wa Wizara kwa kazi nzuri wanayoifanya. Sekta ya Mawasiliano ni muhimu sana katika ukuaji wa uchumi katika nchi yetu. Kupitia mawasiliano, wananchi wanao uwezo wa kufanya biashara kwa urahisi na kuboresha kipato chao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimefurahi kuwepo kwa mfuko wa mawasiliano kwa wote (*UCAF*) unaolenga kupeleka mawasiliano katika maeneo yasiyo na mvuto wa kibiashara hasa vijijini. Ninaomba kupitia mfuko huu, Serikali iangalie namna ya kuboresha mawasiliano hasa maeneo ya vijijini. Katika Jimbo la Busanda, kuna baadhi ya Kata za Nyamalimbe, Bujula, Kamena, Nyamigota na Nyachiluluma kuna mawasiliano hafifu kabisa na hii hukwamisha maendeleo katika maeneo haya. Kwa kupitia mfuko huu, ninaomba Serikali iweke kipaumbele katika kuboresha mawasiliano katika maeneo haya muhimu sana ndani ya Jimbo langu. Hiki ni kilio kikubwa sana kwa wananchi wa maeneo niliyoyataja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana na naunga mkono hoja.

MHE. ROSWEETER F. KASIKILA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, nimshukuru Mwenyezi Mungu, kwa uhai, afya na pia kwa kuniwezesha kuwa hapa leo. Nimshukuru Waziri wa Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia, Mheshimiwa Prof. Makame

Mnyaa Mbarawa na timu yake kwa kuandaa na kutuletea sisi Wabunge bajeti ya Wizara yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hotuba ni nzuri na yenyewe kuleta matumaini kwa Watanzania wengi walio mijini na vijijini pia. Hapa nchini sasa hivi simu ya mkononi siyo tu kwa ajili ya kuzungumza bali ni Benki ya kuhifadhi na kutuma fedha, ni kiungo cha kuingia kwenye mtandao wa *Internet* na kiungo cha kupata taarifa mbalimbali ikiwemo bei za mazao mbalimbali, milipuko ya magonjwa katika maeneo mbalimbali, ajali na majanga mbalimbali yanayotokea hapa nchini, kuchangia michango ya fedha katika Taasisi mbalimbali kama Chama cha Mapinduzi na kadhalika kwa ustawi wa Mtanzania, mawasiliano mazuri ni kivutio cha uwekezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa msingi huo kama nchi yetu inataka kupiga hatua ya maendeleo kwa haraka, ni lazima mawasiliano ya uhakika yapatikane kwa watu wote vijijini na mijini na kwa wakati wote na kwa gharama wanayoweza kuimudu, kwa sasa hali siyo hivyo. Ili Wizara ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia iweze kutekeleza majukumu yale ipasavyo kwa mwaka 2011/2012, iidhinishiwe fedha kama zilivyoombwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni rai yangu kuwa mawasiliano hasa ya simu na mtandao (*network*) yangeboreshwa Mkoa wa Ruvuma hasa Sumbawanga Vijijini na Nkasi ambayo ipo mbali na Makao Makuu ya Mkoa wa Rukwa. Wilaya ya Nkasi katika Tarafa za Wampembe na Tarafa ya Kate mawasiliano ni duni sana katika Tarafa ya Wampembe yenye Kata za Wampembe, Ninde na Kala lakini pia Tarafa ya Kate yenye Kata za Kate, Sintali na Kipande.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uzoefu unaonyesha kuwa wawekezaji wa simu za mkononi Vodacom, Airtel, Tigo na kadhalika huwa hawawekezi katika maeneo ambayo idadi ya watu ni wachache. Hivyo basi, naiomba Serikali iweke jitihada za makusudi kuwapa mawasiliano ya uhakika wakati wote na mahali pote kwa maeneo hasa ambayo hayanufaiki na wawekezaji. Wananchi wa Rukwa – Nkasi wanayo haki ya kuwasiliana na Watanzania wengine popote walipo, ili nao waweze kutumia simu zao za mkononi kama Benki, kuweka na kutuma fedha, kuweza kujua bei ya mazao mbalimbali hapa nchini, waweze kujua matukio mbalimbali mazuri lakini mabaya pia yanayotokea hapa nchini na duniani kote kwa njia ya *Internet*. Mawasiliano – Wilaya ya Nkasi yakiboreshw, itawasaidia wananchi kuondokana na adha ya kuparamia miti na vichuguu kutafuta mtandao, hata wanapokuwa wanataka huduma ya dharura kama vile, *Ambulance*, Zima Moto, wavuvi kuvamiwa na maharamia na majambazi kuvamia wananchi na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

MHE. SUSAN L.A. KIWANGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchangia katika maeneo kadhaa ili nitoe ushauri katika Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu kuimarisha Shirika la Posta na Simu, Shirika hili ni Shirika Mama ndani ya nchi yetu na kwa miaka ya nyuma lilikuwa na ufanisi mkubwa kwa kuwa ndilo lilikuwa Shirika pekee la simu hapa nchini. Kutokana na kukua kwa teknolojia Duniani, ni kweli kwa sasa linahitaji liende na wakati kwa kuboresha huduma zake hasa huduma ya simu (*TTCL*) ziwe za kisasa zaidi kama ilivyo kwa makampuni ya Artel, Tigo na Vodacom ili kuongeza kipato. Hivi sasa *TTCL* linazidi kupoteza umaarufu na wateja kwa kukosa ubunifu wa kisasa. Hivyo iko haja ya kuwatumia vijana wetu (wataalamu) ambao wameajiriwa kwenye mashirika mengine ya simu za mikononi ili kuliweka Shirika la *TTCL* kisasa zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara hii iandae mpango maalum wa kuibua na kutambua vipaji vya Watanzania katika nyanja mbalimbali ambavyo vinapotelea vijijini bila msaada wa Serikali. Mfano, Wilayani Kilombero, kijiji cha Lipangalala alitokea kijana ambaye alitengeneza Kituo cha Mtangazo ya Redio kilikuwa kinasikika ndani ya Kata ya Ifakara, mara iliposikika alitishwa na kupigwa marufuku kufanya hivyo badala ya kumsaidia na kukuza kipaji hicho. Hivyo wakati umefika kutambua vipaji na kuvikuza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la sayansi na teknolojia ni muhimu sana katika kuharakisha maendeleo ya nchi. Wakati umefika sasa Wizara hii kushauri Wizara ya Elimu, Sheria na Katiba kuwa na Kitengo Maalum cha kupeleka habari kwa njia ya ujumbe mfupi wa simu za mikononi zitakazotoa elimu ya Katiba na Sheria zinazohusu moja kwa moja maisha ya kila siku ya wananchi kwa kuwa Watanzania wengi 74% waishio vijijini hawana Katiba, hawaijui na hivyo kuwaacha na kushindwa kudai haki zao au kuvunja Katiba bila kujua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara hii iandae vijarida vya lugha rahisi na kuvisambaza mashulenii kuanzia shule za msingi, sekondari na vyuo. Wizara hii ifuatilie mashulenii iwapo elimu hii hutolewa vizuri katika mashule hapa nchini na Walimu wa Sayansi ili ishauri Wizara ya Elimu badala ya hali ya sasa kuwa mbaya kwa Walimu wa Sayansi katika shule.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara hii iande na ituambie mpango madhubuti wa sasa na baadaye wa kisayansi katika uharibifu wa mazingira na athari zinazoweza kulikumba Taifa kutokana na uchimbaji wa mafuta, *Uranium*, Chuma, Gesi na Madini, aina zote nchini na jinsi ilivyojiandaa kukabiliana nayo kwa nchi yetu imeshaanza kuchimba madini hayo.

MHE. RASHID ALI ABDALLAH: Mheshimiwa Mwenyekiti, sina budi kumshukuru Mheshimiwa Waziri kwa hotuba yake. Pia sina budi kuwapongeza wale wote waliosaidia kufanikisha hatua hizi. Mchango wangu mimi unalenga zaidi kuhusu teknolojia ya mawasiliano ya simu za viganjani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, usajili wa simu za viganjani una kasoro kubwa sana. Kasoro hizi huifanya jamii kutokuwa na udhibiti wa simu zao. Usajili wa simu sio tu ule

wa *Lines Registration*, lakini ni vyema kuwepo na usajili wa simu yenyewe *system*, hii itaondoa wizi uliokithiri kwa wananchi pia kutaondoa upotoshaji wa majina bandia ya msajili. Mheshimiwa Waziri nakuomba sana kulifkiria hili kwani linaleta athari kubwa sana kwa wananchi (Tanzania).

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni kutoa nafuu juu ya matumizi ya ndani na yale ya nje. Kwa mfano *local calls* kuwe na malipo maalum kwa mwezi hata kama utatumia kiasi gani lakini simu za nje kuwe na *features* maalum za kujiunga na gharama ziwe za kufahamika pale unapopiga simu za nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine naloomba tuwe na *system* nzuri za uendeshaji shughuli zote za *computers* hasa maeneo yenyewe kutoa taaluma za elimu ili kuwezesha jamii inayokuja kujikita zaidi katika mabadiliko ya sayansi na teknolojia. Tujenge utamaduni wa kukuza uchumi kwa kuyawekea makampuni ya simu mikakati yenyewe maslahi kwa Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru, naomba kuwasilisha.

MHE. MARTHA M. MLATA: Mheshimiwa Mwenyekiti, natoa shukrani kwa kupata nafasi hii ili nami niweze kuchangia kwa njia ya maandishi. Pia nampongeza Waziri, Naibu Waziri pamoja na timu nzima ya Watendaji wakiongozwa na Katibu Mkuu wa Wizara na Wakuu wa Taasisi za Wizara hii. Hotuba yao ni nzuri na ina mwelekeo wa kutekelezeka hasa katika miradi ya maendeleo. Mungu awasaidie watimize yale yanayotarajiwa. Naomba nitoe maoni yangu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, baadhi ya magazeti yamediriki kuingilia mawasiliano ya simu ya watu fulani wakiwemo wanasiasa na kuchapisha magazeti, lakini *TCRA* imekuwa haichukui hatua kwa wahusika ikiwemo kampuni za simu. Tumeona nchi zingine zikichukua hatua pamoja na kuyafungia. Kwa mfano, juzi yalitokea Uingereza kufungiwa kwa gazeti la *News the World*. Je, ni kwa nini *TCRA* hawachukui hatua? Tunaomba sana Serikali iiongezee nguvu na ipewe uwezo wa kuchukua hatua, vinginevyo hali hiyo ni ya kuingilia uhuru wa mtu na pia ni udhalilishwaji na ni kukiuka haki za binadamu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa vyombo vingi vya habari yaani TV, Radio na simu za mikononi vimkuwa vikilipia na kutumia kazi za sanaa kama muziki, filamu na kadhalika, je, *TCRA* ina habari au takwimu zozote zinazoonyesha kuwa ni kiwango gani sanaa hizo zimetumiwa? Je, ni kiasi gani kimepatikana kwa mwaka 2010/2011 na wanaohusika wamefaidikaje na ni wangapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa kazi nyingi za wasanii zimekuwa zikiibiwaa na watu kuititia *computer* na kadhalika na hata studio. Je, Tanzania haioni kuwa ni jukumu lake sasa kuweka utaratibu wa kudhibiti wizi huo kuititia mitandao na kuona namna ya kushirikiana na *TRA*, *COSOTA* ili kulinda kazi za wasanii zisiibiwe na hatimaye kuliingizia Taifa pato kubwa na kwa msanii mwenyewe? Tafadhali naomba

sana majibu katika eneo hili ili nisije toa shilingi yangu bure kwani mimi pia ni mdau wa sanaa hii na tunaibiwa sana kwa njia ya mtandao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkoa wa Singida kwa sasa umeendelea sana na wengi wana simu za mkononi hadi vijiji, pia barabara zimefunguka za vijiji katika kufikia *centre* za mahitaji muhimu. Tatizo kubwa ni mtandao, mfano katika Wilaya ya Iramba maeneo ya Urughu, Tarafa ya Ndago, Mwangeza, Nkungi zote ziko Iramba Mashariki, tena Nkungi kuna Hospitali kubwa sana, tatizo hakuna mtandao. Naomba sana maeneo yale yaangaliwe na kupelekwa mnara utakaosaidia kwani mtu kama ana mgonjwa popote, anaweza kuita Taxi au msaada wowote na kama nilivyosema njia (barabara) sio tatizo. Tafadhal sana naomba jibu kwa maeneo haya muhimu yaani Iramba katika Hospitali ya Nkungi, Mwangeze na Urughu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hayo, naunga mkono hoja.

MHE. AHMED JUMA NGWALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ambavyo tunaelewa kuwa Wizara ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia, ni Wizara ya Muungano, hivyo ni mategemeo yangu kuwa Wizara hii itaratibu shughuli zake za utafiti, za maendeleo sehemu zote za Muungano, Tanzania Zanzibar na Tanzania Bara. Jambo la kusikitisha ni kwamba kama ilivyo katika Wizara zenyeze za Muungano na Taasisi zake kupuuza na kutokujali Zanzibar na hasa katika mpango wa kuinufaisha Zanzibar kimaendeleo, kwa mfano, katika ukurasa wa 21, kifungu cha 35, Waziri amesema Wizara yake inaendelea kushirikiana na Wizara ya Viwanda na Biashara katika kufanya tafiti mbalimbali zinazoweza kukuza viwanda vyetu hapa nchini na kuhawilisha teknolojia mbalimbali zinazoweza kutumika katika viwanda vyetu hapa nchini na hivyo kutoa ajira kwa wanasyansi na wanateknolojia na kuongeza pato la Taifa. Mpango wote huu wa Wizara ya Sayansi na Teknolojia haukuishisha pahali popote juu ya eneo lolote la Zanzibar kama vipi wanaweza kufaidika na maeleo yaliyotolewa na Mheshimiwa Waziri. Zanzibar kama sehemu ya mafanikio ya Wizara hii lakini Serikali ya Muungano haioni umuhimu wowote katika kuishirikisha Zanzibar katika ufanisi na utafiti wowote unaofanya na Wizara hii ya Muungano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, inashangaza sana kwa dharau inayofanywa na Wizara hii kwa Zanzibar kwa mfano, karibu miaka ishirini ya kuanzia kwake lakini mpaka leo 14/07/2011 inakodi nyumba katika Kisiwa cha Pemba, Chakechake kitendo ambacho sio dharau tu kwa Wazanzibar bali hata kwa Muungano wenye. Tayari Tanzania Bara wameshajenga maofisi mbalimbali kama vile Dar es Salaam, Arusha, Moshi, Mbeya na Mikoa mbalimbali. Hivyo basi ni sahihi kusema kuwa Wizara hii sio mahsus kwa Zanzibar ingawa ni Wizara ya Muungano. Katika hali isiyu ya kawaida na bila kujali umuhimu katika Muungano wetu huu wa miaka 47 sasa Wizara inajielekeza kujenga miundombinu katika sehemu mbalimbali katika Mikoa ya Tanzania Bara na sio Zanzibar hata sehemu moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukirejea hotuba ya Waziri katika ukurasa wa 26, kifungu cha 43, nanukuu:-

“Kupitia ushirikishwaji wa sekta binafsi katika kutoa huduma za TEHAMA, kampuni za simu za mkononi za Airtel, Tigo na Zantel zimeanzisha umoja (Consortium of Operators) kwa nia ya kujenga miundombinu ya TEHAMA yenye uwezo mkubwa wa kimawasiliano (Broadband) katika maeneo ya mji (Metro Network) ili kufikisha huduma za Mkongo wa Taifa wa mawasiliano kwa watumiaji wa mwisho (last mile connectivity). Kampuni hizo zitaanza kujenga miundombinu hiyo katika miji ya Dar es Salaam, Arusha, Mwanza na Dodoma”.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama kweli Wizara hii ina mapenzi ya kweli, ina muundo wa Kimuungano, ujenzi huu mkubwa kwa nini jengo angalau moja lisielekezwe Zanzibar kwa ushauri wangu.

MHE. BENEDICT N. OLE-NANGORO: Mheshimiwa Mwenyekiti, natoa pongezi kwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu na wataalamu kwa hotuba na bajeti nzuri kwa mwaka 2011/2012.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara itumie teknolojia iliyopo ya mawasiliano kupunguza shida ya uhaba wa Walimu. Hii ifanyike kwa kutumia TV mashulen na Mwalimu mmoja afundishe somo lake kwa wanafunzi katika shule nyingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, teknolojia ya nishati mbadala ifanyiwe utafiti na njia za nishati mbadala za kupikia ziendelezwe ili kupunguza matumizi ya miti (kuni) na mkaa ili kunusuru miti na mazingira. Teknolojia ya kuchoma matofali ibuniwe mapema ili kuzuia matumizi ya kuni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kodi na tozo mbalimbali kwa kampuni za simu za mkononi isimamiwe vizuri na kwa ukali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, simu za mkononi zitumike kwa kutuma sms za ku-popularise kilimo, mifugo na uvuvi kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, teknolojia ya mawasiliano itumike katika Utumishi wa Umma na masuala ya ajira ili kuondoa shida/tatizo la watumishi hawa. Teknolojia itumike kuunganisha Hazina, Utumishi na Halmashauri zote nchini ili *transactions* zote za Watumishi ziwe monitored on an hourly basis.

MHE. YUSSUF HAJI KHAMIS: Mheshimiwa Mwenyekiti, nachukua fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu ambaye yeye ndiye ametuwezesha kwa uhai na uzima na tukaweza kuhudhuria katika kikao muhimu kama hiki. Namwomba Mungu aniwezeshe kuchangia kwa ufanisi na kwa umakini pasipo ghadhabu wala kiburi, amina.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nachangia Wizara hii muhimu sana kwa kuanzia na tatizo kubwa linaloikumba nchi yetu, tatizo la umeme ambalo tunasema ni janga la Taifa pamoja na tatizo hili lakini ni asilimia 14 tu ya Watanzania ndio wanaotumia umeme. Kama utafanya utafiti utakuta asilimia 14 ya watumiaji wa nishati hii muhimu ni watu wa mijini na asilimia kubwa watu kutoka vijijini ambao karibu asilimia 80 ndio

wapatao tabu kwa nishati hii ya umeme. Vijiji kama utachunguza ni asilimia mbili tu ndio wanapata nishati hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ni lazima ibuni njia mbadala itakayowezesha kupata njia mbadala ambayo itarahisisha kupata nishati mbadala kuwawezesha watu wa vijijini kupata umeme. Mpaka sasa kupitia wataalamu wake Serikali hajifanya hivyo. Watanzania wanaendelea kutegemea nishati ya umeme ambao ni ghali hasa kwa watu wenye pato la chini yaani maskini wakati zipo njia mbadala ambazo ni rahisi na ni bora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mawasiliano kuhusu simu za mkononi. Simu za mkononi ni mawasiliano makubwa ambayo yamesaidia jamii kwa kiasi kikubwa sana. Mawasiliano haya yameunganisha miji na vijiji pasipo usumbufu wala gharama kubwa. Kwa hiyo, ni huduma muhimu sana ambayo inatumiwa na watu wengi sana. Teknolojia hii ya mawasiliano inatumiwa na watu mbalimbali pasipo ubaguzi. Inahudumia watu wenye malengo mbalimbali, kwa hiyo, watu wengi wanatumia kwa mazuri na wengine kwa mabaya. Msano, wengine wanatumia mawasiliano kwa kupanga uhalifu mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri Serikali kubuni mbinu ambazo zitabaini wahalifu na kufichua uhalifu wao na Serikali idhibiti uhalifu kabla ya matukio mfano, majambazi, wezi na wahalifu wengine. Vilevile kwa kuwa teknolojia hii inatumika kwa idadi kubwa ya Watanzania Mijini na Vijijini, wakubwa na wadogo, wanaume na wanawake, naishauri Serikali ifanye utafiti wa kina, je, teknolojia hii haina madhara kwa watumiaji hasa wale wanaotumia kwa muda mrefu wakiwemo Wabunge wa Bunge hili Tukufu? Je, hakuna athari kwa watumiaji mfano mama wajawazito kwa wao na mtoto aliye tumboni? Kama tayari utafiti umeshafanywa basi naomba Waziri anipe jawabu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sasa imekuwa ni jambo la kawaida kujengwa minara ya simu katika makazi ya watu. Minara ya kampuni mbalimbali utakuta imejengwa katikati ya nyumba za watu. Kwa kuwa mimi si mtaalamu, nataka kujua, je, hakuna madhara yoyote kwa wakazi ambao wamezunguka mnara huu? Vipi usalama wa mama mjamzito na mimba yake kuhusu mionzi inayotokana na mnara ambao upo karibu au ndani ya makazi ya watu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kupata ufanuzi, ahsante.

MHE. HERBET J. MNTANGI: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutoa pongezi kwa Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Watendaji wote wa Wizara na Taasisi zote kwa kazi nzuri na hotuba nzuri ya bajeti ya mwaka 2011/2012. Napenda kutoa maoni na ushauri katika maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tume ya nguvu za Atomiki, kwanza, utendaji na majukumu ya Tume yanagusa Wizara za Nishati na Madini na pia Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika, katika ukaguzi na usimamizi wa matumizi ya vifaa vyia mionzi na madini ya *uranium*. Ili kuondoa migongano inayoweza kujitokeza, muundo wa Tume uboreshwe ili kuunganisha Wizara hizo katika ukaguzi, usimamizi na utekelezaji wa ushauri wa Tume katika maeneo yanayogusa vifaa vinavyotumika katika sekta zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, Wizara na Tume zitoe elimu ya jumla juu ya majukumu ya Tume ili yawe wazi kwa Serikali Kuu, Taasisi na wananchi kwa jumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu, kuongeza uwezo na idadi ya wataalamu katika fani za Nguvu za *Atomic* na usimamizi wa matumizi ya madini hasa *uranium* na kuendeleza utafiti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (*TCRA*). Mabadiliko ya utendaji na uvumbuzi ni ya kasi sana na hivyo kulazimisha kuondoka katika mfumo mmoja kwenda mfumo mwingine, kwa mfano, sekta ya utangazaji kutoka Analogia kwenda Digital. Ili kwenda na kasi, *TCRA* lazima iwe tayari kusitisha utoaji wa leseni iwapo Taasisi zitachelewa kutekeleza umuhimu wa kuingia katika mfumo mpya wa sayansi na teknolojia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukarabati wa mabweni na madarasa *DIT*. Baada ya Taasisi ya *DIT* kupanda daraja kutoka Chuo cha Ufundı, hali ya mabweni na madarasa ya wanafunzi hairidhishi kuwiana na kiwango kipyä cha Taasisi. Tuongeze kasi ya ukarabati na kuboresha mfumo wa mabweni, madarasa na maabara, *DIT* ifanane na taswira ya mabweni katika Taasisi za Mbeya na Nelson Mandela.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuwatambua na kuwaendeleza wabunifu. Ukiondoa Watafiti na Wabunifu wasomi katika Taasisi na Vyuo Vikuu, wapo Wabunifu wengi wadogo katika maeneo mbalimbali. Ukienda katika Maonyesho ya Sabasaba, Dar es Salaam kila mwaka utaona jinsi Wabunifu hao wanavyoonyesha uwezo wao, mionganii mwao hujikita kupitia *SIDO*. Hata hivyo, ubunifu wao huishia katika maonyesho hayo na hakuna njia ya kuwaendeleza. Ni vema Wizara ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia ikajenga utaratibu na uwezo wa kuwatambua, kuwasaidia na kuwaendeleza wabunifu hao wadogowadogo na hatimaye kuwasaidia kumiliki ubunifu wao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kusaidia vifaa vya maabara katika shule za sekondari. Shule za sekondari ndio msingi wa awali wa kuwezesha kujenga uwezo wa Sayansi na Teknolojia. Hata hivyo, zaidi ya asilimia 90% ya shule hapa Tanzania hazina maabara wala vifaa vya maabara. Hata hivyo, zipo shule chache sasa zimeanza kujenga maabara lakini hazina vifaa vya maabara. Mfano, Shule ya Sekondari ya Misozwe, Kata ya Misozwe, Wilaya ya Muheza, imejenga maabara kubwa mbili za kissasa mwaka 2009/2010 lakini hakuna umeme wala vifaa vya maabara. Pamoja na jitihada za kuwezesha umeme kufika mwezi huu wa Julai 2011 lakini bado vifaa havijapatikana na Wizara husika kushindwa kutekeleza kikamilifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mazingira ya namna hii, Wizara ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia haiwezi kukwepa jukumu la Sayansi na Teknolojia. Lazima Wizara ijenge hoja na mfumo wa kuwezesha maabara katika Shule za Sekondari kuiwezesha kupata misaada ya vifaa vya maabara hasa katika masomo ya fizikia na kemia. Ni vema Wizara ikaanza kwa kuonesha mfano kwa shule niliyoitaja na shule

nyingine chache awamu kwa awamu na kujenga msingi wa baadaye kama sehemu ya majukumu yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuboresha mawasiliano ya simu za mkononi katika Tarafa ya Amani, Wilaya ya Muheza. Nazishukuru kampuni za simu nchini kwa kusambaza mawasiliano na kuchangia katika kuongeza ajira kwa wananchi kutokana na mfumo wa simu za mkononi na uwezeshaji wa malipo ya fedha kwa njia za M-Pesa n.k. Kwa kuwa Tarafa ya Amani yenyе Kata za Amani, Misalai, Mbomole, Zirai na Kisiwani iko milimani na pia kuwepo kwa mabonde ya milimani, bado mawasiliano hayajawa mazuri na yanahitaji kuboreshwa katika maeneo yafuatayo. Kwanza, Kata ya Misalai – eneo la Shule ya Sekondari Misalai na Kituo cha Afya Mgambo, Shule za Msingi Misalai na Kazita. Pili, Kata ya Zirai – Shule ya Sekondari Zirai, Shule za Msingi Zirai, Kambai, Antakar, Kwezitu na Kizerui na tatu, Kata ya Amani na Mbomole – Shule za Msingi Mbomole na Mikwinini. Tarafa ya Amani ina mashamba makubwa ya chai na wafanyakazi wengi wenye uwezo wa kutumia simu za mkononi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

MHE. MOHAMED H. MISSANGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. Nampongeza sana Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Naibu Waziri, Mheshimiwa Katibu Mkuu na Watendaji wote kwa maandalizi ya bajeti hii na utendaji kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Rais alitoa maelekezo kuwa Serikali itenye 1% ya bajeti kwa ajili ya utafiti. Agizo hili halijatekelezwa tokea limetolewa na Mheshimiwa Rais Kikwete. Hivi kama maagizo ya Mheshimiwa Rais hayatekelezwi ni maagizo ya nani yatakayotekelizwa? Hii ni *insubordination* kwa Mheshimiwa Rais wetu. Kiasi kilichotengwa mwaka huu kwa utafiti hakikidhi haja. Nasisitiza agizo hili litekelezwe. Hata hivyo, nashauri utafiti uliofanyika hadi sasa uenziwe na utumizwe kikamilifu. Tafiti hizi na matokea yake yatangazwe ili zieleweke kwa wananchi. Wagunduzi wa tafiti mbalimbali watambuliwe na kupongezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Shirika la Posta, ni jambo la kusikitisha kuwa hadi sasa suala la mtaji kwa Shirika hili halijapatiwa ufumbuzi pamoja na ahadi za mara kwa mara. Huu ni upungufu mkubwa, viyi Serikali inategemea Shirika hili lifanye kazi kwa ufanisi bila ya mtaji huku Shirika likiwa limekabiliwa na ushindani mkali kutokana na maendeleo katika teknolojia. Vilevile Serikali ilikubali na kuahidi kuimarisha Shirika la Posta kwa kufuta madeni ya zamani ya kampuni ya Afrika Mashariki ya Posta na simu na mengineyo na kulipa pensheni za wafanyakazi. Nasikitika kusema kuwa hadi sasa hakuna kilichofanyika kufanikisha masuala hayo. Inaelekea Serikali haina nia njema na Shirika hili la Posta, kulikoni? Shirika hili hivi sasa linashindwa kulipa hata mishahara katika wakati muafaka. Baya zaidi mishahara ya wafanyakazi wa Posta ni duni sana na wafanyakazi hawa wanafanya kazi katika mazingira magumu sana. Wamevumilia sana, je, watavumilia hadi lini? Naomba mishahara ya wafanyakazi wa Posta iboreshwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, malipo kwa uwekaji minara kijijini ina matatizo. Suala hili lishughulikiwe kitaifa na liwekewe maelezo kamili. Mfuko wa *UCAF* umechukua muda mrefu, kwa nini? Hebu harakisheni.

MHE. MOSHI S. KAKOSO: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimpongeze Waziri mwenye dhamana kwa kuwasilisha bajeti yake vizuri na kwa ufasaha zaidi. Nianze kutoa mchango kwa Wizara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bajeti ni finyu sana kwani Wizara hii inatakiwa iwe inajitosheleza kwa kutengewa tengo kubwa litakaloenda sambamba na hali halisi ya sayansi na teknolojia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha ndogo zilizotengwa kwa ajili ya utafiti. Kitengo hiki ni muhimu sana kwa maendeleo ya Taifa letu. Eneo hili ambalo ni muhimu lazima litengewe bajeti ya kutosha ili iweze kukidhi mahitaji yanayohitajika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, gharama kubwa zinazotozwa na makampuni ya simu zinawaumiza sana wananchi. Niombe Serikali kupitia Wizara husika iangalie kwa kina suala hili ili iweze kukaa kwa pamoja na hawa wawekezaji ili waweze kupunguza gharama za mawasiliano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, makampuni kutokutoa huduma za jamii mahali ambapo wamewekeza. Makampuni ya simu mengi yamekuwa yakipata faida kubwa sana lakini sehemu ya faida hawairudishi kwenye jamii ambayo kwa kiasi kikubwa wao ndio wanaochangia makampuni hayo yaweze kufanya kazi. Niwaombe Wizara iyashawishi makampuni hayo yaangalie juu ya kurejesha huduma kwa jamii kama kujenga mahospitali, mashule na kuhudumia wale mavu kuliko kuelekeza nguvu kwenye michezo tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niombe Wizara iweze kutuvekeea mitambo ya mawasiliano ya simu katika maeneo ya Kata ya Katuma na Kata ya Sibwesa ambako hakuna kabisa mawasiliano ya simu. Eneo hili ni muhimu sana kwani kuna shughuli za kibiashara na kilimo na kuna wakazi wengi ambao wanahitaji sana huduma za mawasiliano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, niombe Wizara iendelee kuboresha na kuhakikisha kunakuwepo na mipango mikakati ya kufanya uchunguzi juu ya uchimbaji wa Madini ya Uranium ambayo yatatusaidia wananchi wa Tanzania kuingia katika mfumo wa Nyukilia ambayo itasaidia mfumo mpya wa sayansi na teknolojia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

MHE. REGIA E. MTEMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, Kata za Uchindile, Tanganyika Masagati na Utengule, Wilayani Kilombero zina matatizo ya mawasiliano. Naomba kupitia mfuko wa *UCAF – Universal Communication Acess Fund*, Kata hizi zipatiwe mawasiliano kwenye bajeti hii ya mwaka 2011/2012.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Wizara yako ianzishe lugha ya alama kwa wenyewe ulemavu (viziwi) kwenye vyombo vya habari vya Taifa kwa kuanzia. Lugha ya alama ni mawasiliano muhimu na ya lazima kwa watu wenyewe ulemavu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bunge sasa liachane na mfumo wa kizamani wa kutumia makaratasi kwenye taarifa zake na badala yake itumie mfumo wa kisasa wa Teknohana kwa kupewa taarifa kwa njia ya *soft copy* kupitia *iPad* na *Internet*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wavumbuzi na Wagunduzi wa ndani waendelezwe na vitu vinavyovumbuliwa viendelezwe. Pia *COSTECH* ipatiwe Fungu lake la 1% ya GDP.

MHE. RUKIA KASSIM AHMED: Mheshimiwa Mwenyekiti, bajeti hii ni finyu katika masuala ya utafiti kutoka Shs. bilioni 30 mwaka jana na mwaka huu takribani shilingi bilioni 26 ambayo ni pungufu na haikukidhi maazimio ya *SADC* katika *paragraph* (k) ya Ibara ya 4 ya Itifaki ya mwaka 2008 ambayo imeridhiwa na Bunge hili Aprili, 2011.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utendaji wa *COSTECH* kutokuwa na sura ya Kimuungano, kwa mfano, Watendaji wengi ni wa kutoka Tanzania Bara. Napendekeza *COSTECH* ivunjwe na nafasi zitangazwe upya kwa watu wenyewe sifa na vigezo ili kuwe na uwiano wa pande zote mbili za Muungano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utendaji duni wa *COSTECH* katika kupita na kuruhusu *proposals* za watafiti. Kwa mfano inasadikiwa kwamba mtafiti anaambiwa atoe 10% ili *proposal* (miradi ya kitafiti) ipite. Kuwepo kwa urasimu, ukiritimba katika kusimamia shughuli za kitafiti, hii inasababishwa na kuwepo kwa usiri (*no transparency*), hakuna uwazi.

MHE. ANNE K. MALECELÀ: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianze kwa kusema kwamba naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika ulimwengu wa leo, ulimwengu wa utandawazi, mawasiliano ni muhimu sana kwani ulimwengu umekuwa mdogo kama kiganja cha mkono. Niipongeze Wizara hii kwa jinsi wanavyojitahidi kuboresha mawasiliano nchini. Mahali popote penye mawasiliano ya kisasa kama vile simu za kiganjani, *e-mail*, *internet* ambavyo vimeenea mpaka vijiji, nikiri kwamba vimeleta mabadiliko makubwa sana kiuchumi na kuonyesha kupunguza umaskini kwa Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza sana Ndugu Profesa Mascarenhas, kwa utafiti kamili, kwa *research* yake aliyoifanya ambayo imetupa picha kamili ya matokeo ya utumiaji wa mawasiliano ya simu za viganjani, *e-mail* na *internet* yanavyoweza kupunguza umaskini. Utafiti aliofanya Profesa Mascarenhas kati ya vijiji viwili vya Makambako na Njombe ulionyesha kwamba kijiji kilichopelekewa simu za mkononi, *e-mail* na *internet* kiliweza kupunguza umaskini na kuinua uchumi kwa zaidi ya asilimia 37. Niisihi Serikali iendelee kutumia utafiti wa Profesa Mascarenhas kama dira ya

kuhakikisha mawasiliano haya muhimu yanasantazwa Tanzania nzima kwani utafiti huu umetuhakikishia matunda mema kiuchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, umuhimu wa *address* za makazi, Serikali imeonyesha kutilia mkazo vitambulisho vya uraia. Naishukuru sana Serikali kwa kufikia kwenye maamuzi ambayo Watanzania waliyasubiri kwa muda mrefu sana. Ni vema Serikali ikaona umuhimu wa kutoa vitambulisho vya uraia uende sambamba na kuwa na anuani za makazi za Watanzania hao. Ni muhimu Serikali ikaona umuhimu wa kuipa fedha Wizara hii ili tuweze kupata anuani za makazi za Watanzania wote ili vitambulisho vya uraia viwe na maana. Niisihi Serikali ione umuhimu mkubwa wa kushughulikia anuani za makazi sambamba na utoaji wa vitambulisho vya uraia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

MHE. NYAMBARI C.M. NYANGWINE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kuchukua nafasi hii, kumpongeza Mheshimiwa Profesa Makame Mnyaa Mbarawa (Mb), Waziri wa Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia, pamoja na Naibu wake, Mheshimiwa Charles Muanga Kitwanga (Mb), kwa jitihada zao za kuendeleza Sekta ya Mawasiliano hapa nchini. Pia ninawapongeza kwa kuwasilisha Bajeti ya Wizara husika kwa makini.

Mheshimika Mwenyekiti, ni ukweli usiopingika kuwa, Sekta ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia, imepanuka sana hapa nchini kwetu. Ushahidi uliodhahiri ni utumiaji wa vifaa vya kieletronikia kama vile *fax*, simu za mezani, simu za mkononi, *telefax*, *e-mail*, *internet* na kadhalika. Kupanuka huko kwa masuala ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia hapa nchini kwetu, kumerahisisha sana suala la mawasiliano hususan masuala ya simu za mkononi. Simu za mkononi zimerahisisha sana upashanaji wa habari; kwa mfano, upashanaji wa habari hizo umesaidia sana kutatua matatizo baina ya jamii na jamii, familia na familia, mtu na mtu toka vijijini hadi mijini. Pongezi sana kwa Serikali na Wizara husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na pongezi hizo, ni dhahiri na wazi kuwa, dhana ya *transfer technology* katika nchi yetu, imetuathiri sana kiuchumi na hata kijamii. *Transfer technology* kwa maana ya teknolojia hamisha katika nchi maskini kama Tanzania, una lengo la kuinyonya nchi husika. Ukweli ulio wazi ni kuwa, mataifa yaliyoendelea yanajipenyeza kuzinyonya nchi zinazoendelea na zile maskini kwa mwavuli wa teknolojia hamisha. Nchi zilizoendelea kiteknolojia, zinadidimiza maendeleo ya sayansi na teknolojia katika nchi zinazoendelea kwa:-

- Kuwapelekea wataalam “feki” ambao mchango wao ni mdogo kiubunifu.
- Kuwapelekea wataalam ambao hawana uwezo wa kufundisha wataalam wa nchi maskini na hivyo kuzifanya nchi hizo ziwe tegemezi kiteknolojia.
- Kuzipelekea nchi hizo bidhaa feki ambazo zinaathiri kwa kiasi kikubwa watumiaji wa bidhaa hizo.

- Kuhakikisha kwamba nchi hizo hazikui kiviwanda hususan *Heavy Industries*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hali hiyo ni kweli kabisa kuwa, nchi yetu Tanzania haiwezi kukua kisayansi wala kiteknolojia ikiwa Serikali haitabuni mbinu mbadala. Hatua za makusudi zinatakiwa kuchukuliwa haraka iwezekanavyo ili kulinusuru Taifa letu lisiendelee kuditidimia kiteknolojia. Mbinu mbadala inayoweza kubuniwa kwa haraka ni kuwatafuta watu wenye ugunduzi wa kuzaliwa nao au wenye ubunifu unaotokana na mazingira ili kuwaendeleza kivipaji. Kwa mfano, Wakurya ni mabingwa wa kutengeneza silaha za asili na hata bunduki aina ya gobore. Pia kuna vijana wanaojaribu kubuni vitu kama gari, balskeli, pikipiki, ndege na kadhalika; waendelezwe vipaji vyao. Mwisho kabisa, ninashauri Serikali ianzishe Chuo kikubwa cha Sayansi na Teknolojia hapa nchini kwa lengo la kuibua na kukuza vipaji. Ninaamini itawezekana ikiwa kila mmoja atatimiza wajibu wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi yetu Tanzania ina utitiri wa mashirika ya simu za mkononi. Ninaamini kuwa, huenda nchi yetu ikawa ya kwanza katika Afrika hii kwa kuwa na makampuni mengi ya simu za mkononi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba ifahamike wazi kuwa, makampuni yote haya ya simu hasa ya watu binafsi kama vile *Airtel*, *Sasatel*, *Vodacom*, *Zantel* na *Tigo*, yanahujumu na kuwaibia Wananchi bila hata kukemewa na Serikali. Kwanza, mashirika haya yote yanakwepa kodi. Pili, yanaendesha michezo ya kubahatisha, yaani bahati nasibu kwa utapeli, lakini Serikali imekaa kimya kana kwamba haioni. Tatu, mashirika hayo yanauza na kubadili wamiliki pasipo kulipa ushuru. Huu ni wizi mkubwa. Nne, gharama zinazotozwa na mashirika haya ni mzigo kwa Watanzania na ndiyo maana yanakimbilia kuja kuwekeza hapa nchini. Hii ni dhahiri kuwa mashirika haya yanatengeneza faida kubwa sana. Tubadilike.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hakika ninaamini kuwa, simu za *TTCL* (mezani na mkononi), ndizo zitakuwa mkombozi kwa watumiaji wa simu walio na kipato cha kawaida. Ninaiuliza Serikali ni kwa nini *TTCL* imeshindwa kusimamia huduma bora za mawasiliano ya hapa nchini? Kwa nini *TTCL* imeshindwa kusambaza simu za mkononi nchi nzima? Chonde chonde, Serikali ihakikishe kuwa inafanya kila linalowezekana kuisaidia *TTCL* ili ihmili ushindani. Tukiamu tunaweza, tuamue sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Shirika la Posta Tanzania, ninaomba nichukue nafasi hii kuiuliza Serikali na Wizara husika kuwa Shirika hili linafanya kazi ya biashara; je, kwa nini limeshindwa kuhimili ushindani na hali inayopelekea hata kuzidiwa kusafirisha vifurushi na mabasi? Je, hakuna utaratibu maalum wa kuratibu shughuli za usafirishaji wa vifurushi? Je, Shirika linakabiliana vipi na changamoto kuhusu usafirishaji wa pesa kwa wateja? Serikali inakabiliana vipi na suala la M-PESA, ZAP, Z-PESA na TIGO-PESA? Ina maana sisi Watanzania, Serikali yetu imeshindwa kudhibiti huduma hizo za kutuma fedha ili pesa zote zitumwe kupitia Shirika letu la Posta? Je,

Serikali inanufaikaje na huduma hizo zinazotolewa na Mashirika hayo ya Simu? Kwa nini Serikali isiisaidie *TTCL* nayo ianzishe *TTCL-PESA*? Ninasisitiza tufikiri zaidi.

Mwisho kabisa, ninaomba sasa nichukue nafai hii kuisemea Sekta ya Mawasiliano katika Wilaya yangu ya Tarime. Wilaya ya Tarime inapakana na Nchi ya Kenya, ambayo ina mtandao maarufu uitwao *Safaricom*. Mtandao huu unakamata katika vijiji vyote vya mpakani na hivyo kuwaathiri watumiaji wa simu za mkononi kwa upande wa Tanzania. Watumiaji wa simu kwa upande wa Tanzania, huathirika kwa sababu hutozwa kwa gharama za simu ya kimataifa. Hivyo, watumiaji wa simu wa upande wa Tanzania, hulipishwa gharama karibu mara nne ya gharama ya kawaida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na hali hii, ninaomba Serikali ifanye kila linalowezekana ili kuhakikisha kuwa, mitandao ya simu za mkononi inawekwa katika Vilima vya Tagare, Mumwamu, Kagonga, Gibaso na Birira ili kurahisisha suala la mawasiliano Wilayani Tarime. Suala hili ni muhimu, lazima lizingatiwe, kwani karibu takriban watu 200,000 wanatumia simu za mikononi Wilayani Tarime. Hebu fikiria watu wangapi wanahujumiwa na mtandao wa *Safaricom* wa Kenya? Watu wangapi wanateseka kwa kukosa huduma ya mawasiliano Wilayani Tarime? Ninaomba kauli ya uhakika toka Serikalini leo hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kauli ya Serikali itawafariji Wananchi wa Tarime, ambao wakitaka kupiga simu hupanda juu ya mti huku wakihatarisha maisha yao, lakini kibaya zaidi wakibahatika kupata *network* ya *safaricom*, huibiwa zaidi kwa kulipa gharama ya juu sana. Ninaomba kauli ya Serikali ya uhakika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, ninaomba kuwasilisha na kuunga mkono hoja.

MHE. MKIWA A. KIMWANGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nami ninapenda kuchangia hoja ya Wizara iliyoko mbele yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara hii ni muhimu sana, kwani sasa hivi Dunia ni kama Kijiji na uvumbuzi na utafiti wa sayansi ni muhimu pia. Serikali yetu inasuasua kwa kutoa pesa za utafiti ili kwenda sambamba na utafiti pamoja na teknolojia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba Serikali itoe pesa kama Rais alivyotamka, kwa kuwa tamko la Rais ndilo tamko la mwisho. Tunaiomba Wizara ya Fedha itimize hilo na ninaomba Wizara ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia ni muhimu kwenu kukumbusha hilo kila wakati kwenda sambamba na utafiti.

Utafiti ni kazi ya muda mrefu; hivyo ni bora Wizara hii ikawa na pesa za kutosha muda wote. Pamoja na hayo, Wizara ina kazi ya kuyasimamia Makampuni ambayo yanakwepa kodi wakati wanapouzwa. Mfano, *DST* Kampuni ya *Celtel International* ilifungua Kampuni huko Netherlands, ambayo ndiyo inamiliki *Celtel Tanzania Ltd*. Kama tunavyofahamu, *Celtel* iliuzwa kwa Kampuni ya *Zain* na baadaye kwenda *Airtel*. Serikali haikupata chochote katika mabadiliko haya ya wamiliki. Ninaomba Serikali kuwa makini sana katika ukusanyaji wa mapato kama haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kusema pamoja na Wabunge kupitisha Bajeti ya Wizara hii, lakini haipati tunachopitisha na hasa katika fedha za maendeleo. Ninaiomba Serikali itembee kwenye maeneo ambayo wanayaomba hapa kwa Wabunge, kwani Wabunge inaonekana tunapitisha kisichoteklezeka, yaani fedha hasa za maendeleo. Mwaka 2010/2011, fedha ya maendeleo haikufika hata robo, ambayo walipewa na waliyoomba; hivyo ni bora Wizara hii fedha wanazoomba wapewe kwa wakati ili waende na wakati. Ahsante.

MHE. FAITH M. MITAMBO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kumpongeza Waziri wa Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia; na kwa kweli katika hotuba yake, kuna mambo mazuri sana, iwapo yatatekelezeka, basi yatakuwa ni yenye manufaa makubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninawashukuru pia Makampuni ya Simu ya *TIGO*, *VODACOM* na *AIRTEL*, kwa kazi nzuri wanayofanya na wametusaidia sana angalau kwa kiasi fulani sasa kuna mawasiliano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi binafsi ninaendelea kuwaomba sana, Makampuni ya Simu ya *TIGO*, *VODACOM* na *AIRTEL* ni kweli Wilaya ya Liwale immetuletea Minara, lakini minara hiyo bado haitoshi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kampuni ya *VODACOM*, Wilaya nzima ina minara miwili tu; mnara mmoja uko katika Kijiji cha Kiangara, ambao unasaidia kuunganisha mawasiliano kutoka Nachingwea kwenda Liwale na mnara wa pili uko Liwale Mjini na ndio unaosaidia kupata mawasiliano, Mjini Liwale tu na kuliacha robo tatu ya eneo la Wilaya hii kutokuwa na mawasiliano ya mtandao huu wa *Vodacom*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kampuni ya Simu ya *TIGO* nayo ina minara ipatayo mitatu na juzi juzi wameongoza mnara wa nne, lakini mnara huu wa nne uko pale na nimetaarifiwa kwamba, haufanyi kazi. Ninawashukuru kwa kutuongezea mnara huu wa nne, lakini ninaiomba Kampuni ya *TIGO*, warudi tena pale walipoweka mnara huu wa nne, wajiridhishe kwanza mnara ule unafanya kazi na kama haufanyi kazi makafanye marekebisho. Kwa ujumla, mawasiliano haya ya mtandao wa *Tigo* nayo yame-cover kama robo tu ya eneo zima la Wilaya ya Liwale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mtandao wa *Airtel*, nao una *sites* mbili tu; *site* moja iko Kijiji cha Kiangara, ambao pia una-pick mawasiliano kutoka Nachingwea kwenda Liwale, *otherwise*, Liwale mjini kuna mrana mmoja tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wilaya ya Liwale ina fursa nyingi za kiuchumi na kiutalii. Wilaya hii inazalisha sana Mazao ya Korosho, Ufuta, Mtama na mazao mengine. Wilaya hii ina fursa ya utalii katika Hifadhi ya Wanyama ya Selous (*Selous Game Reserve*) na vilevile sasa hivi ina fursa ya biashara ya madini. Kwa hiyo, ni wilaya ambayo ina mafao ya kutosha na nina imani kabisa kwamba, Makampuni ya Simu yakiwekeza ndani ya Wilaya hii, hayatapata hasara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Chama cha Msingi cha Umoja Wilayani humo, kimeweza kujenga godauni kubwa na kinaendelea kuweka mazingira mazuri kwa ajili ya mnada wa korosho msimu ujao. Korosho zenyewe zipo huko vijijini ambako hakuna mawasiliano. Katika kipindi hicho cha minada ya korosho, matajiri na wafanyabiashara wengi watakuja katika Wilaya hii kununua korosho, watahitaji mawasiliano mazuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo la kukosa mawasiliano katika Wilaya hii na hasa huko vijijini, limesababisha pia hata wagonjwa na akina mama wajawazito wanaohitaji kujifungua katika Hospitali ya Wilaya, kukosa msaada na huduma na hivyo wakati mwingine kupoteza maisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili linatokeaje, kuna viji ambavyo viko zaidi ya km 70 kutoka mjini, ambako Hospitali ya Wilaya ipo na hospitali ina *ambulance* na inapotokea kwamba, katika Kijiji hicho kuna mgonjwa wa dharura, basi mtu mmoja hulazimika kutembea kwa balskeli hadi nusu ili aweze kupata mahala ambapo mtandao unapatikana ili apige simu Hospitali ya Wilaya kuomba msaada wa *ambulance*. Kumbe kwa kupoteza muda wote huo, mgonjwa anapata madhara zaidi au anapoteza maisha. Kama kungelikuwepo na mawasiliano pale pale kijiji, wangeweza kuomba msaada huo wa gari mara moja na lingeweza kufika kwa wakati na kuokoa maisha ya mgonjwa huyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nichukue nafasi hii kuishukuru Kampuni ya Simu ya *Airtel*, kwa kunikubalia kutuongeza *sites* nyngine saba katika Vijiji vya Lilombe, Mihumu na Likombora, Makata, Mimi, Bankiwa, Nduruka na Nahoro. Ninawaomba ndugu zangu wa *airtel*, watu kule wana shida ya mawasiliano sana na kwa kuwa mmeshakubali kutuongeza *sites* hizo saba, basi *processes* nyngine zinazoendelea ni vyema mngeziharakisha ili watu katika vijiji hivyo waweze sasa kupata mawasiliano hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mara ya kwanza niliahidiwa kwamba, kufikia mwezi wa sita mwaka huu, *sites* hizo zingekuwa zimeshawashwa. Baadaye nikaahidiwa kwamba, hadi kufikia mwezi wa nane, *sites* hizo zitakuwa zimewashwa; ni mategemeo yangu kwamba, hautapita mwezi wa nane angalau nusu ya *sites* hizo zitakuwa zimewashwa. Tunaomba sana mtujengee kabla ya mwezi huo kuisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa niongelee kuhusu Mfuko wa Mawasiliano kwa wote (*UCAF*). Mpango huu wa *UCAF* ni mzuri sana na nina imani utatusaidia kwa kiasi kikubwa, kueneza huduma hii ya mawasiliano vijijini kote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niiombe tu Serikali kwamba, Mpango huu sasa ungeanza mara moja na nimesikia kwamba, kuna maeneo yatapangiwa ya kufanya *pilot study*, ninamwomba Mheshimiwa Waziri, hiyo *pilot study* ifanywe na kwenye Wilaya yangu ya Liwale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *logistics* za kuanzisha Mpango huu wa *UCAF* zimechukua muda mrefu mno, tangu 2006 hadi 2011, bado tuko kwenye *logistics* tu; ni lini sasa Mpango huu utanza kutekelezeka na watu wana shida ya kupata mawasiliano?

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika bajeti ya mwaka ujao, Mheshimiwa Waziri wa Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia, tunategemea atatueleza habari njema za kuanza kazi Mpango huu wa *UCAF* na siyo kuendelea na *logistics* tena.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kuwasilisha na ninaunga mkono hoja.

MHE. SELEMANI S. JAFU: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaipongeza Serikali kwa kuweka kipaumbele katika Miradi ya Maendeleo kwa kutenga pesa za kutosha kwa kutumia pesa za ndani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaiomba Serikali iangalie upya utaratibu wa makampuni ya simu ya kubadilisha majina ya makampuni kama vile Mobitel – *Buzz – Tigo*; na *Celtel – Zain – Airtel*. Hii inaonesha wazi huu ni utaratibu wa ukwepaji wa kodi ambazo ni muhimu sana kwa mustakabali wa maendeleo ya Taifa letu.

Kwa kuwa Mbuga ya Selous iliyo Kusini mwa Wilaya ya Kisarawe ni muhimu sana kwa uchumi wa nchi yetu. Kwa bahati mbaya, maeneo yanayopakana na Mbuga hii hayana mtandao wa mawasiliano, ambayo ni muhimu sana kwa kupashana habari kwa maeneo ya Mbuga hii ya Selous.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaiomba Serikali iwezeshe uwekwaji wa mitandao ya simu kwa Kata ya Vikumburu na ya eneo la Stesheni ya Tazara ya Gwata na Kidunga ili kuwezesha upatikanaji wa mawasiliano kwa maeneo hayo na Mbuga ya Selous inayopakana nayo; hivyo, kutoa fursa hata Watalii na Wawindaji kupata mawasiliano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kujua kama kuna madhara yoyote yanayopatikana kutokana na matumizi ya simu na kuwepo kwa minara ya mawasiliano. Je, kama kweli kuna madhara; Serikali inajipanga vipi kuwalinda Wananchi wake?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.

MHE. DKT. HARRISON G. MWAKYEMBE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapongeza sana Waziri wa Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia, Mheshimiwa Prof. Makame Mnyaa Mbarawa (Mb) na Naibu wake, Mheshimiwa Charles Muhangwa Kitwanga, kwa kuwasilisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha kwa Mwaka 2011/2012, kwa ufasaha mkubwa. Ninaunga mkono hoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuunga mkono hoja, ninapenda kuitaarifu Wizara kuhusu mchezo wa udanganyifu ulioanza kufanywa na Makampuni ya Simu za Mkononi ili Wizara iingilie kati bila kulazimisha wateja kwenda mahakamani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, udanganyifu huo ni wa kuwalazimisha wateja wao kulipia matangazo yao ya biashara bila ridhaa yao na kuwalazimisha kusikiliza matangazo hayo kabla ya kupata huduma yenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mteja anaponunua vocha ya Shs.1,000 lengo lake ni kuwasiliana na walengwa wake kwa muda unaotosheleza Shs.1,000 ya *air time*; lkini si hivyo, mteja anapiga simu anapokewa na tangazo la biashara kabla ya kumpata aliyemlenga: “Ndugu mteja hamia *AIRTEL*, furahia huduma zetu wewe, ndugu, jamaa na familia yako... au nunua muda wa maongezi kwa *TIGO* Pesa upate salio mara mbili...”! Hii si sahihi ni kuwaibia wateja muda wao wa maongezi na ni kuiibia Serikali kodi inayotoza kwenye matangazo rasmi! Vilevile ni kuwapotezea muda wateja, wasikilize kwanza matangazo yao kwa lazima ndipo waunganishwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara iingilie kati kuwashauri wenzetu hawa ambao kila kukicha wanatafuta mbinu za kupata *Super-profits!* Wasipojirekebisha, sitashangaa kuona kesi za madai zikifunguliwa *Commercial Court* kudai fidia kwa mchezo huu wa udanganyifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninarudia tena kusema ninaunga mkono hoja.

MHE. MASOUD ABDALLA SALIM: Mheshimiwa Mwenyekiti, gharama za mawasiliano ya simu za viganjani bado ni kubwa na Serikali hajjawabana wamiliki wa makampuni na makampuni husika kurekebishiwa hali hiyo, hivyo ninaomba Serikali itoe mchanganuo wa Makampuni ya *AIRTEL, VODACOM, ZANTEL* na *TIGO*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba Serikali itoe ufanuzi wa mkakati wa matumizi ya udhibiti wa rasilimali ardhi ambayo kila kampuni inapenda kujenga mnara wake peke yake. Jambo ambalo ni vyema Serikali itoe miongozo maalum kwa makampuni haya ya simu kujenga mnara mmoja ili kutumia ardhi vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tume ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia – *COSTECH*, ina mipango mbalimbali ikiwemo ya kiutendaji katika kuboresha utafiti, lakini fedha nyingi zinazotolewa kwa ajili ya utafiti haziwafikii walengwa; je, Serikali ina mkakati gani wa kulifuatilia na kulipatia ufumbuzi tatizo hili?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tume hii ina urasimu mkubwa katika utoaji wa huduma za miradi kwa watafiti, hali inayopelekea kuwepo kwa upendeleo; hivyo, naishauri Serikali kuliangalia tatizo hili kwa kulipatia ufumbuzi. Serikali inasema nini juu ya kuwepo kwa Ofisi ya *COSTECH* katika Visiwa vya Zanzibar (Unguja na Pemba)?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna Watanzania wapo katika Mataifa yaliyoendelea wapo kwenye nyanja za mawasiliano na wanategemewa na nchi hizo; je, Serikali imewafahamu hao ni wangapi na ina mpango gani wa kuwatafuta ili ujuzi walionao waje nao Tanzania ili kuweza kuboresha Sekta hii muhimu kwa manufaa ya Taifa? Serikali ina mkakati gani wa kulipatia ufumbuzi tatizo la kutokuwepo kwa mfumo wa utunzaji kumbukumbu za taratibu zote za teknolojia ya habari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Pemba hakuna kabisa Ofisi ya *TTCL*, je, Serikali ina mpango gani wa kulipatia ufumbuzi tatizo hilo? Naomba kuwasilisha.

MHE. HUSSEIN N. AMAR: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kuipongeza Hotuba ya Bajeti ya Mawasiliano; ni nzuri sana iwapo itakamilisha malengo yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Wananchi wa Jimbo la Nyang'hwale, ninaomba huduma hii iharakishwe sababu Wananchi wanapata tabu kubwa sana ya kuwasiliana kwa mambo mengi, ikiwa taarifa za ugonjwa, biashara, uporaji yaani ujambazi unapotokea na kadhalika. Kwa sasa huduma hii inapatikana katika Kata moja tu ya Khalumwa kati ya Kata 12 ambazo ni Bukwimba, Izunya, Kafita, Nyugwa, Kakora, Nyijundu, Nyang'hwale, Busolwa, Shabaka, Nyaburanda na Nyashiranga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba Waziri atuangalie kwa jicho la huruma Wana-Nyang'hwale ili twende kasi kuleta mapinduzi ya maendeleo ukizingatia kuwa, sasa Nyang'hwale ni Wilaya Mpya itakayoanza hivi karibuni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaunga mkono hoja mia kwa mia.

MHE. LETICIA M. NYERERE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaipongeza Serikali kwa mpango wake wa kufundisha matumizi ya kompyuta mashulen. Hili ni jambo la kutia moyo, kwani watoto wa nchi zingine huanza kutumia kompyuta tangu wakiwa chekechea, wenzetu matumizi ya kompyuta ni nyenzo wanazotumia katika masomo yao. Matumaini yangu ni kuwa na sisi tutaweza kufikia hatua hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni vyema Watanzania wote wawekewe mkazo katika matumizi ya *internet* ukizingatia utandawazi uliopo duniani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali iwaelimishe Wananchi kuhusu faida za matumizi ya teknolojia mpya kama ifuatavyo: Kurahisisha kazi; kuongeza uzalishaji; kuboresha mawasiliano; na kurahisisha utoaji wa elimu katika nyanja zote, yaani *on line training*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na faida zitokanazo na teknolojia ni lazima Watanzania waelimishwe kuhusu hasara au madhara yatokanayo na teknolojia kama ifuatayo: Kupunguza ajira; kuongeza uhalifu (*Cyber and Computer Crimes*); na kupunguza uwezo wa kufikiri

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ifuatilie zaidi makosa yanayofanywa kwa kupitia teknolojia mpya ikiwemo *child pornography*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kuwasilisha.

MHE. EUSTACE O. KATAGIRA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninampongeza Mheshimiwa Waziri na Watendaji, kwa kuanda bajeti nzuri na kuiwasilisha vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaipongeza Wizara na Mashirika husika kwa hatua wanazochukua kuleta maendeleo katika nchi yetu. Kweli Sekta hii inakwenda vizuri na shughuli zake zinasaidia na kuchochea maendeleo vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bei/gharama za mawasiliano kweli zimeshuka, lakini bado ziko juu na ninapendekeza bidii ifanywe ili ziendelee kushuka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna mwelekeo wa vijana wetu wengi kutopenda au kuogopa vipindi nya *Science* na Hisabati; ni muhimu tukaweka msisitizo katika vipindi nya *Science* na Hisabati.

MHE. KAIKA S. TELELE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kuunga mkono hoja hii. Vilevile ninaipongeza sana Makampuni ya Simu za Mkononi kwa jitihada zao za kupanua huduma za mawasiliano ya simu hadi vijiji kutoka kwa Babu wa Samunge hadi Masaini wamefika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninawaomba waendelee kujitanua hadi maeneo ya Hifadhi ya Ngorongoro ambapo wanyamapori na binadamu wanaishi pamoja. Wananchi hao kama Watanzania wengine, wanahitaji huduma hii hasa katika Vijiji nya Nainokanoka, Sendui, Naiyobi, Bulati, Engaresero, Pinyinyi na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninadhamini vilevile ajira ya moja kwa moja inatolewa na makampuni haya kwa Watanzania hususan walinzi wa minara vijiji. Ninashauri Wizara hii iangalie uwezekano wa kushawishi kampuni hizi za simu kulipa kiwango kimoja cha mshahara kwa walinzi walioko katika mazingira ya aina moja.

MHE. DESDERIUS J. MIPATA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaanza kwa kuunga mkono hoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mchango wangu ninaipongeza Wizara kwa hotuba nzuri, iliyozingatia kujikita katika kuiwezesha Nchi na Wananchi wa Tanzania kuingia katika zama za sasa za Sayansi na Teknolojia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sasa Wizara hii imepata umuhimu mkubwa, kwa sababu za utandawazi na hivyo kumekuwa na mahitaji ya matumizi ya Sayansi na Teknolojia kwa kila mtu. Kumbe ni lazima kueneza huduma hii muhimu bila kuangalia maslahi ya kibashara yanayoweza kupatikana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huduma hii sasa ni huduma muhimu ya kijamii, kiuchumi na kiutamaduni na kwa hiyo basi, lazima kuieneza kwa kasi inayotakiwa ili tuibebe nchi katika nyanja zote bila kupishana (*Desparity*) au kupunguza mpishano tofauti ya maendeleo Wilaya ya Nkasi iliyoko Mkoa wa Rukwa na hasa katika Jimbo la Nkasi Kusini, hawajanufaika vizuri na huduma za Wizara hii. Nkasi Kusini inazo Kata za Ninde, Kala na Wampembe, ambazo hazina kabisa huduma za simu za mkononi na Makao Makuu ya Jimbo yaliyoko Kata ya Kate.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huduma ya simu za *TTCL* pia hazijakuwa nzuri sana licha ya kujenga ofisi nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mawasiliano ya Redio ya *TBC* haisikiki kabisa katika eneo lote la Ziwa Tanganyika Wilayani Nkasi, ambapo vijiji vipatavyo 33 vinakosa kupata matangazo ya nchi yao; ninaomba mtusaidie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna michezo au niite kamali au wizi, kurubuni watu kwa kujiunga kwenye programu mbalimbali kwa *message* na anaendelea kukatwa kwenye salio lake na wakati fulani akiingia hajui namna ya kujitoa; mfano, kuletewa *message* za tahadhari mbalimbali, kupata milio ya simu na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, simu zimeingia hazina hata viwango takataka kabisa; hali hii inatakiwa idhibitiwe na siyo simu peke yake, *electronic appliance* zote ziwe na viwango.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamaliza kwa swal; je, wanafunzi walioko kule Kala, Ninde, Wampembe Shule za Sekondari Km 86 mbali na Barabara Kuu ulipopita Mkongo; wananaufaika vipi? Ahsante.

MHE. JUMA A. NJWAYO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kuwapongeza Waziri na Naibu Waziri wa Wizara ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia, kwa juhudhi zao kubwa za kuisaidia nchi yetu kwenye maeneo wanayoyasimamia. Pia ninawapongeza Watendaji wote nikianzia na Katibu Mkuu, Naibu wake na Viongozi wa Taasisi na Mashirika yaliyoko chini ya Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, ninapenda kushauri mambo yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kujua ni vigezo gani vilitumika kuchagua Mikoa itakayonufaika na ufadhili wa Mfuko wa Mawasiliano kwa wote na kuuacha Mkoa wa Mtwara?

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati simu za mkononi zikiwa siyo anasa kwani mawasiliano ni muhimu sana kwa maendeleo, baadhi ya Kata Jimboni kwangu wanapata matatizo ya mawasiliano. Kata hizo ni Chaume, Naputa, Mkoreha, Mihambwe na Maundo. Uhakika wa mawasiliano kuwa mdogo unatokana na ukosefu wa minara; ni vyema basi jitihada zifanywe kumaliza adha hii kwa watu wa maeneo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Nchi za Ulaya ziliridhia *EU Directive 46/95 on Data Protection* kwa njia ya kuzuia matumizi mabaya ya habari na taarifa. Pia baadhi ya nchi huko wameanzisha Sheria ya *Computer Cybercrime*, kwa ajili ya kuzuia vitendo vibaya kwenye mifumo, viwango na hivyo huduma salama za matumizi ya kompyuta.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi yetu ina vitendo vibaya kama vile *hacking and other related computer crimes*, vinavyopanda kasi na hivyo kudhalilisha Wananchi hasa Viongozi. Je, Serikali imejiandaaje kuiga *data protection directive* au kutunga sheria haraka zenye kuzuia vitendo vya aina hiyo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Chuo Kikuu Huria cha Tanzania, kimeanzisha Shahada ya Uzamili ya Sheria ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari. Shahada hii itasaidia kudhibiti matumizi mabaya ya mawasiliano na teknolojia ya habari. Je, ni vipi mchango wa Wizara au imejihusishaje kukisaidia Chuo hiki kwenye Shahada hii?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, ninaunga mkono hoja.

MHE. DKT. MARY M. MWANJELWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, ninaipongeza Serikali kuitia Wizara husika kuwa na Mradi wa Vitambulisho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia ninaipongeza Serikali kwa kuwa na *Pilot Project* katika Mji wa Arusha Kata saba na Mji wa Dodoma Kata saba. Hii bado haitoshi, Serikali inatakiwa kwanza ikamilishe Mradi wa *Physical Address* kabla ya kuendelea na Mradi wa Vitambulisho. Vinginevyo, itakuwa ni sawa na kujenga nyumba isiyo na msingi; itasimamaje ama gari isiyokuwa na *engine*? Mradi mzima hautakuwa na mantiki endapo utaanza na ule wa vitambulisho, kwani hautakuwa na *details* zote na hivyo vitambulisho havitakubaliwa na watoa huduma mbalimbali na ni rahisi *ku-temper* hata wale ambao siyo Watanzania kusema ni Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mradi wa *Zipp code-physical address* uta-simplify shughuli zote na kukubalika. Ikibidi pesa zingine za vitambulisho ziende kwenye Mradi wa Makazi.

Chuo cha Teknolojia cha Sayansi Mbeya, hakijaonesha bajeti iliyotengewa katika kukiinua chuo hiki na ujenzi wake unalegalega. Tunahitaji kipandishwe hadhi na ujenzi na upanuzi uishe haraka ili kiweze kuwa Chuo Kikuu.

Matokeo ya utafiti wa *COSTECH* yako wapi? Wanatakiwa wa-*coordinate* utafiti wa kisayansi na siyo kwenda kufanya kazi zingine kama za mawasiliano. Tunaomba tujulishwe tokea imeanzishwa imefanya nini?

Makampuni ya Simu yanafanya biashara hapa nchini; ni kweli tunavutia wawekezaji, lakini vilevile iwe ni *win-win situation*, kwani Makampuni ya Simu yote makubwa yanapewa *tax exemption*. Kwa nini wasilipe kodi? Uendeshaji wa nchi unategemea sana ukusanyaji kodi. Ikifika baada ya kila wakati fulani wanadai wameuza kampuni na kubadili jina, huku ni kuihujumu nchi kukwepa kulipa kodi. Mfano ni makampuni ya (*Airtel – Zain*), (*Vodacom – Vodafone*). Tupate maelezo ya kina.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kuunga mkono hoja.

MHE. SUBIRA KHAMIS MGALU: Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kunipa fursa hii ya kuchangia kimaandishi Hotuba ya Waziri wa Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwapongeze kwa namna ya pekee, Waziri, Naibu Waziri na Watendaji wote wa Wizara hii, kwa kazi kubwa ya kuandaa bajeti na hatimaye Hotuba ya Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaipongeza Wizara kwa mafanikio yote yaliyopatikana wakati wa utekelezaji wa Mpango wa Mwaka 2010/2011. Mchango wangu utajielekeza katika maeneo yafuatayo:-

Kwanza, utekelezaji wa Bajeti ya Mwaka 2010/2011. Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue fursa hii, kueleza masikitiko yangu kwa Wizara hii kupelekewa pesa pungufu ya zile zilizoidhinishwa na Bunge hasa pesa za maendeleo; kati ya pesa shilingi 44,426,910,000 zilizoainishwa ni kiasi cha shilingi 21,673,706,747 tu zilizopokelewa na Wizara hii; ambayo ni asilimia 49 tu. Kwa dhamana iliyopewa Wizara hii ya kuhakikisha kwamba, Teknolojia ya Habari na Mawasiliano, Sayansi, Teknolojia na Ubunifu, vinachangia kikamilifu katika maendeleo ya nchi yetu; ni ukweli usiopingika kuwa, kwa upungufu huu wa rasilimali fedha hasa za maendeleo, dhamana hiyo haiwezi kutekelezwa kwa ufanisi.

Pili, Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote (*UCAF*): Ninaipongeza Serikali kwa kuanzisha Mfuko huu katika jitihada za Serikali kupeleka huduma za mawasiliano hadi vijijini. Hata hivyo, ninaungana na Kamati kueleza masikitiko yangu ya ucheleweshwaji wa uanzishaji wa Mfuko huu mpaka sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Mkao wetu wa Pwani, kuna vijiji vingi havina mtandao wa mawasiliano ya simu za mkononi. Mfano; katika Wilaya ya Rufiji, vijiji vilivyopo Ukanda wa *Delta* (visiwani), vyote havina mawasiliano. Baadhi ya Vijiji vya Kisarawe (mfano Kata ya Mafizi, Vikumburu na Chole). Pia baadhi ya Wilaya ya Mkuranga. Ieleweke kwa sasa kuwa na simu za mkononi siyo jambo la anasa, kwani kupitia simu za mkononi, Wananchi wa Mkao wa Pwani wa maeneo yasiyopata huduma ya mawasiliano, wanakosa fursa za kupata taarifa mbalimbali; mfano, taarifa za masoko, taarifa za upatikanaji wa pembejeo na kadhalika.

Tatu, Mawasiliano: Juhudi za kuimarisha mtaji wa Kampuni ya Simu Tanzania zinazofanywa na Serikali kwa kweli haziridhishi. Katika Hotuba ya Mheshimiwa Waziri, ukurasa wa 35 anasema; Serikali inaendelea na juhudhi za kuiwezesha kampuni ya simu kupata mikopo kwa ajili ya kuijendesha kibiashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati Serikali inaitafutia mkopo Kampuni ya Simu, wakati huo huo inashindwa kuchukua hatua madhubuti ya kuhakikisha Wizara/Taasisi na Wakala, kulipa madeni yao. Kwa Serikali kulipa kiasi cha shilingi milioni 791 kati ya shilingi bilioni 7.2, Serikali imeweza kulipa asilimia 11 tu ya deni linalodaiwa na kampuni ya simu. Inatia uchungu kuona Serikali inahangaika kuitafutia mkopo kampuni ya simu, wakati yenyewe ndiyo yenze mtaji mkubwa wa kampuni hiyo kupitia deni inalodaiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninathubutu kusema, Serikali haina dhamira ya dhati ya kuona kampuni hii ya simu inaimarika kiutendaji.

Nne, Sayansi na Teknolojia: Nimesikitishwa na Serikali kushindwa kutekeleza Ilani yake ya Uchaguzi ya Mwaka 2010-2015, kwa mwaka wa kwanza wa utekelezaji wa Ilani hiyo, kwa kushindwa kutenga kiasi kisichopungua asilimia 1.0 ya Pato Ghafi la Taifa (*GDP*). Kwa mwaka 2010/2011, wizara imepokea shilingi milioni 19,494,651,700 kati ya shilingi milioni 30,746,000,000; ni wazi upungufu huu wa fedha umeendelea kuathiri shughuli za utafiti na maendeleo. Ninashauri Wizara ihakikishe kuwa, Ilani ya Uchaguzi ya Mwaka 2010-2015 inatekelezeka na kuhakikisha pesa zilizotengwa zinapatikana ili shughuli za utafiti zifanyike kwa ufasaha ili kuleta maendeleo yaliyokusudiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuunga mkono hoja.

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge sasa niwape nafasi Waheshimiwa Mawaziri waweze kuja hapa mbele na kutoa majibu ya hoja tulizochangia Waheshimiwa Wabunge. Kwa hiyo, nitamwita kwanza Mheshimiwa Naibu Waziri ambaye kwa mujibu wa Wizara, Naibu Waziri atatumia dakika 25 na zinazobaki atazitumia Mheshimiwa Waziri. Mheshimiwa Naibu Waziri!

NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa naomba nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kusimama mbele yenu na kutoa mchango wangu katika hoja hii iliyopo mbele yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue nafasi hii kumpongeza Dokta Jakaya Mrisho Kikwete kwa kuchaguliwa kuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Dokta Bilali Gharib kuwa Makamu wa Rais. Nimshukuru tena kwa mara nyingine, Mheshimiwa Rais kwa kunitfea kushika wadhifa huu wa Naibu Waziri wa Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda vile vile kuchukua nafasi hii kuwashukuru wapiga kura wangu wa Jimbo la Misungwi kwa kunichagua kwa kura za kishindo kuwa Mbunge wao, nawaomba tuendelee na tuendeleze ushirikiano wetu kwa kutumia kauli mbiu yetu ambayo ni mawe matatu, kwa maana ya msimamo, mshikamano, mnato katika kujenga na kuiletea maendeleo Misungwi yetu. (*Makofî*)

Namshukuru mke wangu mpenzi, Matlida Kitwanga, watoto wangu Vedastus, Misoji, Lubango na Milembe, kwa uvumilivu wao wakati wote nisipokuwepo nyumba na msaada wao katika utendaji wangu wa kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nikushukuru wewe binafsi, nimshukuru Mheshimiwa Spika, Naibu Spika na Wenyeviti wote wa Bunge hili kwa uwezo na umahiri mkubwa mnaoonesha katika kuendesha Bunge letu. Nichukue nafasi hii pia

kumpongeza kwa dhati Mheshimiwa Mizengo Peter Pinda, Waziri Mkuu kwa umakini wake wa kusimamia shughuli za Serikali hapa Bungeni kwetu. (*Makofii*)

Aidha, napenda kuwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge, wote kwa ushirikiano mliouunesha kwa muda huu mfupi niliokuwa hapa Bungeni katika kutekeleza majukumu yangu, nasema ahsanteni sana. Nimshukuru kwa namna ya pekee vilevile Mheshimiwa Waziri wa Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia kwa ushirikiano anaonipa katika utekelezaji wa majukumu yetu tuliyopewa na Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto nyingi zimejitokeza wakati wa kuchangia hoja hii na hii ni dalili ya dhati ya mwanzo ya mwamko mkubwa kwa upande wa kuendeleza maeneo ya mawasiliano, sayansi na teknolojia na ubunifu kwa umma wa Tanzania ili tuweze kupiga hatua zaidi katika maendeleo yetu. Aidha, katika michango hiyo imedhihirisha wazi juu ya mahitaji makubwa ya mawasiliano ya simu kama nyezo muhimu kwa maendeleo ya kijamii, kiuchumi na siasa hapa nchini kwetu. Vilevile umeonekana dhahiri kuwa masuala ya kuendeleza shughuli za utafiti yana umuhimu mkubwa katika kutekeleza programu mbalimbali za kiuchumi na kijamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, michango ya Waheshimiwa Wabunge ilikuwa ni mizuri sana iliyosheheni busara, hekima na changamoto, aidha, siyo rahisi kujibu kwa kina na kutosheleza hoja zote za Waheshimiwa Wabunge kwa muda huu mfupi. Tuwaahidi tu kwamba, hoja zote tutazijibu kwa maandishi na kuwapatia Waheshimiwa Wabunge wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja zote za Waheshimiwa Wabunge, zilikuwa zimelenga katika kuelekeza namna bora zaidi ya kushughulikia mahitaji ya wananchi wa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naomba nijikite katika hoja mbalimbali zilizochangiwa na Wabunge wakati wa kujadili hoja hii iliyo mbele yetu. Nianze na hoja ya kwanza ya Mheshimiwa Mussa Zungu Azan, hoja hii ililenga hasa hasa katika kuboresha ukusanyaji wa mapato. Lakini labda nianze tu kwamba katika ukusanyaji wa mapato, tuna chombo chetu *TRA*, lakini katika usimamizi kwa watoa huduma za simu tuna chombo chetu *TCRA*, na *TCRA* inaangalia maeneo mbalimbali katika utoaji wa huduma.

Kwanza ni zile huduma zinazotoka nchi za nje yaani *International*, kuna huduma za Kitaifa, huduma za Kimikoa na huduma za Kiwilaya. Lakini mpaka sasa hivi kama Wabunge wengi waliochangia inaonekana tunaliangalia suala la takwimu za mawasiliano kwamba kuna wananchi milioni 22 ambao wana simu, nadhani hili kidogo limepotoshwa. Tunachozungumzia hapa ni laini zaidi ya milioni ishirini zilizosajiliwa. Tukumbuke tu, hata sisi ni wangapi ambao tuna laini za *Zantel*, *Voda* na *Tigo*? Sasa ukiangalia kwa idadi ya watu yawezekana ni pungufu lakini haiondoi umuhimu wa kuhakikisha kwamba kila laini inayotumika iweze kuchangia katika pato la Taifa kama inavyotakiwa. Sasa ni nini Serikali yetu inafanya? Tuelewe kwamba sasa hivi tunapiga simu kwa uhakika na tusingependa kuleta usumbufu wowote na Serikali yetu kwa vile ni makini, inachofanya

na juzi nilijibu swali linalofanana na hili. Serikali inachofanya kwanza ni kufanya utafiti wa teknolojia ipi ambayo tutaiweka iweze kukidhi haja ya suala ambalo Mheshimiwa Zungu Mussa Azzan amelizungumzia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kufanya hivyo na-*declare interest* kidogo na mimi ni mtaalam wa *ICT*. Unapojenga *system* unaanza na kitu kinachoitwa *requirement specifications*. Unaanza kutambua kwanza mahitaji yako hurukii kwenye kuweka kitu au *solution* kabla hujajua ni nini unachohitaji. Kwa hiyo, kwa sasa hivi Wizara yetu na Serikali yetu inachofanya ni kutambua nini hasa tunachohitaji na siku moja nilisema kuna watumiaji wengi. Kwa hiyo, watumiaji wanaohitaji kujua mambo ya kiusalama nao walete mahitaji yao, watumiaji wanaohitaji kwa ajili ya ukusanyaji ushuru walete mahitaji yao na watumiaji wengine au wadau wengine walete mahitaji yao ili tukae na jopo la Wataalam tuamue ni kitu gani au chombo gani tukifunge ili kiweze kukidhi mahitaji haya bila kuathiri huduma inayotolewa kwa sasa hivi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi kwa mfano, leo hii tukifunga chombo halafu bei za utumiaji wa simu zikapanda juu nina hakika kidole tena kitaelekezwa kwetu. Kwa hiyo, mtupe nafasi tuweze kujipanga, tufanye utafiti, tuweke *system* na tunalifanya hili kwa uhakika kwa sababu Serikali yetu ni makini na italifanya hilo. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Zungu Mussa Azzan pamoja na Wabunge na Watanzania wote watuelewe kwamba, ni nia yetu na ni Watanzania wazalendo sana sisi tunaongoza katika Serikali iliyopo na tutahakikisha hili tunalifanya kwa uadilifu mkubwa na litakapofikia *solution* mtaona kitakachotokea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nijibu tena hoja iliyoletwa kwetu na Mheshimiwa Mbarouk Mohammed Rajab, nayo inahusu *TTCL* Pemba. Yeye alizungumzia kwanza kabisa ni kwa nini hakuna ofisi ya *TTCL* Pemba. Lakini twende tena kwenye misingi hiyo hiyo ya kufanya biashara, sasa hivi makampuni yetu tunataka yafanye biashara, yajitegemee, yatoe faida na yatoe gawio katika Serikali yetu. Zamani tulikuwa tunaangalia hata kujenga miundombinu, kujenga nyumba za wafanyakazi lakini sasa hivi kinachoangaliwa ni huduma. Je, *TTCL* yetu kwa kutokuwa na jengo haitoi huduma inayotakiwa?

Kwa hiyo, tuzingatie zaidi kwamba kinachotakiwa ni kutoa huduma na tumewashauri na Kamati mbalimbali zimekuwa zikiyashauri Mashirika ya Umma yaondokane na *non core business* yaani wa-*concentrate* kwenye *core business*. Kwa hiyo, *TTCL* kama itaona kuna haja ya kujenga jengo Pemba ni muafaka, lakini kama itaona kwa kutumika ofisi hiyo hiyo itatoa huduma zilizo bora katika wakati huu wa ushindani, basi tuishauri *TTCL* iendelea hivyo. Siku hizi kutokana na teknolojia watu wanakuwa na chumba kimoja tu, *computer* nzuri, wafanyakazi wengine wako nyumbani wanaingia kwenye *computer* wanafanya kazi yao na huduma zote zinatekelezwa. Kwa hiyo, Mheshimiwa Mbarouk Mohammed Rajab naomba unielewe na tunakuhakikisha kwamba ulalamike kwa huduma mbaya, usilalamike kwa kutokuwa na jengo. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu wafanyakazi Pemba kwamba, hawana vitendea kazi. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbarouk Mohammed Rajab kwamba *TTCL* kama shirika linaangalia sehemu zote sawasawa kabisa. Kama kuna vitendea kazi ambavyo havipatikani Pemba, tujaribu kufanya utafiti kuona kama vitendea kazi vimependelewa vikapelekwa mahali, pengine. Vitendea kazi vinavyopatikana vinagawiwa katika shirika lote sawasawa, labda sana sana wanachofanya ni kuweka kipaumbele, tunaanza hapa kesho tutakwenda hapa na keshokutwa tutakwenda pale, lakini hakuna mahali ambapo wanatengwa au hawapewi vitendea kazi. Kwa hiyo, nimhakikishie kwamba, vitendea kazi vitaendelea kuboreshwa kulingana na hali ya shirika itakavyokuwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika suala la maslahi, *TTCL* ni shirika linaloongozwa na Bodi na kila siku linasimamiwa na *Management* na lina utaratibu wa mishahara. Wewe kama ni Ofisa ngazi ya tatu, haijalishi kama wewe uko Songea, Pemba, Mwanza au uko Dodoma watu wote mlio na ngazi sawa mnapata mshahara ulio sawa. Kwa hiyo, hakuna kutengwa au kufanyiwa ubaguzi, hilo linafanyika kwa utaratibu wa Kanuni za mishahara na *scale* zote ambazo wamezipangia ndani ya *TTCL*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, labda niende kwenye suala la tatu ambalo Waheshimiwa Wabunge karibu wote wameligusia nalo ni suala la mitandao. Hili limegusiwa na Waheshimiwa Wabunge wengi kama Mheshimiwa Athuman Rashid Mfutakamba wa Igalula; Mheshimiwa Dokta Festus Limbu wa Magu; Mheshimiwa Hezekiah Ndahani Chibulunje wa Chilonwa; Mheshimiwa Diana M. Chilolo, Mheshimiwa George Gregory Teu wa Mpwapwa; Mheshimiwa Jerome Dismas na Mheshimiwa Stephen Hilary Ngonyani wa Korogwe, huyu ni mtani wangu na yeze sijui anatafuta nini na mnara umeshawaka lakini bado anauliza swali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wengine ni Mheshimiwa Joseph Livingstone Lusinde, Mheshimiwa Richard M. Ndassa, Mheshimiwa Hawa A. Ghasia, Mheshimiwa Margareth S. Sitta, Mheshimiwa Said Mohamed Mtanda, Mheshimiwa Faith Mohamed Mitambo, Mheshimiwa Salome Daudi Mwambu, Mheshimiwa Rosweeter Faustin Kasikila, Mheshimiwa Martha M. Mlata, Mheshimiwa Amos Gabriel Makalla, Mheshimiwa Faith Mohamed Mitambo tena, Mheshimiwa Seleman Said Jafo, Mheshimiwa John Paul Lwanji, Mheshimiwa Amos Gabriel Makalla, Mheshimiwa Nyambari Nyangwine wa Tarime, Mheshimiwa David Kafulila wa Kigoma Kusini; Mheshimiwa Ignas Aloyce Mallocha wa Kwera na Mheshimiwa Moza Abedi Saidy Mbunge wa Viti Maalum.....

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, nadhani ungekwenda tu kwenye mambo ya msingi ili kutumia muda vizuri.

NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA: Mheshimiwa Mwenyekiti, labda kwa ujumla tu niende moja kwa moja katika kujibu hii hoja ya mtandao.

Wakati tukiwa Bungeni hapa niliwataarifu kwamba, kwa mwezi wa Juni, Kampuni ya *Airtel* tayari imeshafunga *site 55* kwenye maeneo mbalimbali, na mwezi Julai itaweka mtandao *site 33* katika sehemu mbalimbali. Lakini kama ambavyo

nimekuwa nikitoa majibu katika maswali mbalimbali yanayoulizwa na Waheshimiwa Wabunge, ni dhamira ya Serikali hii kuhakikisha kwamba ifikapo mwaka 2013 Desemba, zaidi ya 90% ya nchi iwe imefikiwa na mawasiliano yaani kwa Watanzania wote. Sasa naomba kutokana na hali tuliyonayo kwa kutumia Mfuko wa mawasiliano, tumefanya utafiti, utafiti wa kwanza tuliofanya ni kuwasiliana na Makampuni ya Simu za Mkononi kuyaauliza wapi hamjafika na mpango wenu ni wapi mnaeleke? Baadaye tukapata takwimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia kwa kutumia *system* ya *GPS* na *GIS* tukai-map nchi yote na kuonyesha kwamba wapi kuna mtando na wapi hakuna. Lakini teknolojia hii kwa sababu unaangalia kutoka juu yawezekana mnara unamulika lakini haufiki baadhi ya sehemu kulingana na jiografia ya nchi yetu kwani kuna mabonde na milima. Sasa tunahitaji msaada kutoka kwa ndugu zetu Waheshimiwa Wabunge, mtupe takwimu sahihi, sisi katika awamu ya kwanza tumeorodhesha Vijiji karibu 239 lakini ili kuhakikisha hilo zoezi linafanyika na kuonyesha kwamba sisi tuko makini na tunataka likamilike tumemwomba Meneja wa Mfuko huu kesho awepo hapa Bungeni ili Wabunge wote wenye matatizo wakaorodheshe Vijiji vyao ili tuwe na takwimu sahihi. Tunachohitaji, mtuambie Wilaya, Kata na Kijiji ili tuweze kupata takwimu zote na ili dhamira yetu ya kuhakikisha kwamba ifikapo mwaka 2013 tunafikia zaidi ya 90%.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawaomba Waheshimiwa Wabunge, najua kwenye vifungu watataka kushika mshahara wa Waziri wangu, lakini pamoja na maelezo yote haya tena unataka jamani ukamate mshahara wa Waziri wangu? Kesho twende kwa Meneja wa Mfuko wa *UCAF* tukapeleke matatizo yetu yakatatuliwe na sisi tukisema tunafanya hivyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, juzi nilijibu swalii la Mheshimiwa Mbunge wa Rufiji, tukafanya uchunguzi tukaona kuna tatizo na tayari yule mtu aliyebomolewa nyumba yake kwa bahati mbaya ameshalipwa. Tunakwenda kwa kasi zaidi, ari zaidi na nguvu zaidi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naona muda unanitupa mkono, lakini kuna suala ambalo limezungumziwa na Waheshimiwa Wabunge, hili ni suala la *M-Pesa* na *Tigo-Pesa* kwamba halisimamiwi. Bahati mbaya au nzuri nina utaalam kidogo na hilo. Kilichofanyika sasa hivi, hayo Makampuni ya Simu yanasaajiliwa na kuwa *regulated* na *TCRA*. Lakini kabla hayajaanza kutoa huduma ya usafirishaji wa pesa ni lazima yajiorodheshe kwa Benki Kuu ya Tanzania na sharti mojawapo ni lazima yafungue *Trust Account* kwenye Benki ya Biashara na pesa zote zinazotumwa na kuchukuliwa ni lazima zitumwe pale ikiwa ni kuangalia vile vile na kwa utaalam wanaita *float*, zile hela ambazo ziko kwenye *account* hizo zimekaa pale na hazijachukuliwa na mwenyewe hizo wanaziita ni *float money* yaani zinalea hazijachukuliwa ziko kwenye ile *account*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge na wananchi kwamba hii huduma ya kutuma pesa kwa kutumia Makampuni ya Simu siyo kwamba inafanyika bila kuwa *regulated*. Inaangaliwa na Benki Kuu wakati wowote Benki Kuu inaweza kwenda kuangalia hiyo *account* kuona kama ina *transact* sawasawa.

Mbali na hayo bado kuna utaratibu wa kuangalia namna ambavyo Sheria ya Malipo ya *Electronic* itakavyoweza kujumisha suala hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwahakikishie tena Waheshimiwa Wabunge kwamba Wizara yetu tumejipanga vizuri na tuko tayari kwa ushauri ulio sahihi na ulio bora kwa ajili ya kuendeleza nchi yetu. Serikali yenu kama nilivyosema ni makini na ina watu makini, Wizara yetu ni makini pia ina watu makini na tutawatumikia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naomba kuunga mkono hoja. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Nakushuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri na sasa nitamwita Mtoa hoja Waziri wa Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia.

WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa naomba nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kusimama mbele yenu na kutoa mchango wangu katika hoja hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nikushukuru wewe binafsi, Mheshimiwa Spika, Naibu Spika, na Wenyeverti wa Bunge kwa uwezo na umahiri mkubwa mnaoonyesha katika kuliendesha Bunge letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue fursa hii pia kumpongeza kwa dhati Waziri Mkuu, Mheshimiwa Mizengo Peter Pinda kwa umakini wake wa kusimamia shughuli za Serikali Bungeni. Aidha, napenda kuwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge wote waliopata nafasi ya kuchangia hoja yangu niliyoiwasilisha hapa Bungeni leo asubuhi tarehe 14/7/2011, kwa michango yao mizuri na ya kina yenye lengo la kuboresha utekelezaji wa majukumu ya Wizara yangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto nyingi zimetolewa na hii ni dalili ya dhati ya mwamko mkubwa kwa upande wa kuendeleza maeneo ya mawasiliano, sayansi, teknolojia na ubunifu kwa umma wa Watanzania ili tuweze kupiga hatua zaidi katika maendeleo. Aidha, katika michango hiyo imedhihirisha wazi juu ya mahitaji makubwa ya mawasiliano ya simu kama ilivyo huduma ya usafiri wa reli, barabara na bandari kuwa ni nyenzo muhimu kwa maendeleo ya kijamii, kiuchumi na siasa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile imeonekana dhahiri kuwa masuala ya kuendeleza shughuli za utafiti yana umuhimu mkubwa katika kutekeleza program mbalimbali za kiuchumi na kijamii. Aidha, uendelezaji wa Vyuo vyta Sayansi na Teknolojia, utawezesha Taifa kuongeza wataalam wa fani hizo wenye ujuzi na weledi unaohitajika katika kuleta maendeleo katika nyanja za uzalishaji na huduma kwa jamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jumla ya Wabunge 110 walichangia katika sekta ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia kuititia hotuba ya bajeti ya Waziri Mkuu na Wizara yangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, sasa napenda kuwatambua Waheshimiwa Wabunge waliochangia hoja mbalimbali husika kuhusu sekta ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia. Kuna waliota maoni yao kwa kuzungumza hapa Bungeni na wengine kwa maandishi. Naomba sasa niwatambue kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, waliochangia wakati wa hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu ni wanne, waliochangia hotuba yangu kwa kuzungumza ni nane na kwa maandishi ni tisini na tatu (93). Majina ya Waheshimiwa Wabunge hao ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Charles M. Kitwanga, Mheshimiwa Rita L. Mlaki, Mheshimiwa Profesa Kalikoyela K. Kahigi, Mheshimiwa Rajab Mbarouk Mohammed, Mheshimiwa Pudenciana W. Kikwembe, Mheshimiwa Dokta Maua A. Daftari, Mheshimiwa Mussa Zungu Azzan, Mheshimiwa Dokta Binilith S. Mahenge, Mheshimiwa Eng. Ramo M. Makani, Mheshimiwa Augustino M. Masele, Mheshimiwa Kapteni John D. Komba, Mheshimiwa Eng. Athuman R. Mfutakamba, Mheshimiwa Dokta Festus B. Limbu, Mheshimiwa Hezekiah N. Chibulunje, Mheshimiwa Susan A.J. Lyimo, Mheshimiwa Diana M. Chilolo, Mheshimiwa Gregory G. Teu, Mheshimiwa Jerome D. Bwanausi, Mheshimiwa Stephen H. Ngonyani, Mheshimiwa Mariam N. Kisangi, Mheshimiwa Livingstone J. Lusinde, Mheshimiwa Said M. Mtanda, Mheshimiwa Angella J. Kairuki, Mheshimiwa Clara D. Mwatuka, Mheshimiwa Richard M. Ndasa na Mheshimiwa Gaudence C. Kayombo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wengine ni pamoja na Mheshimiwa Hawa A. Ghasia, Mheshimiwa Al-Shaymaa J. Kwegyir, Mheshimiwa Magreth S. Sitta, Mheshimiwa Dokta Seif S. Rashidi, Mheshimiwa Rachel M. Robert, Mheshimiwa Omar R. Nundu, Mheshimiwa Suleiman Nassib Omar, Mheshimiwa Amos G. Makalla, Mheshimiwa Anne K. Malecela, Mheshimiwa Nyambari C.M. Nyangwine, Mheshimiwa Mkiwa A. Kimwanga, Mheshimiwa Faith M. Mitambo, Mheshimiwa Goodluck J. Ole-Medeye, Mheshimiwa Eugine E. Mwaiposa, Mheshimiwa Said Suleiman, Mheshimiwa Namelok E.M. Sokoine, Mheshimiwa Godfrey W. Zambi, Mheshimiwa Augustino L. Mrema na Mheshimiwa David Z. Kafulila. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Amina Abdallah Amour, Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed, Mheshimiwa Josephine T. Chagulla, Mheshimiwa Ritta E. Kabati, Mheshimiwa Ignas A. Malocha, Mheshimiwa Salome D. Mwambu, Mheshimiwa Ali Khamis Seif, Mheshimiwa Rosweeter F. Kasikila, Mheshimiwa Susan L. Kiwanga, Mheshimiwa Rashid Ali Abdallah, Mheshimiwa Martha M. Mlata, Mheshimiwa Ahmed Juma Ngwali, Mheshimiwa Benedict Ole-Nangoro, Mheshimiwa Yussuf Haji Khamis, Mheshimiwa Mohamed H. Missanga, Mheshimiwa Moshi S. Kakoso, Mheshimiwa Regia E. Mtema, Mheshimiwa Rukia Hemed, Mheshimiwa Said Suleiman Said, Mheshimiwa Dokta Harrison G. Mwakyembe na Mheshimiwa Masoud Abdalla Salim. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile Mheshimiwa Hussein N. Amar, Mheshimiwa Leticia M. Nyerere, Mheshimiwa Eustace O. Katagira, Mheshimiwa Kaika S. Telele, Mheshimiwa Desderius J. Mipata, Mheshimiwa Dokta Mary M. Mwanjelwa, Mheshimiwa Subira K. Mgatu, Mheshimiwa Kombo Khamis Kombo, Mheshimiwa Haroub M. Shamis, Mheshimiwa Dokta William A. Mgimwa, Mheshimiwa Josephat S. Kandege, Mheshimiwa Pauline P. Gekul, Mheshimiwa David E. Silinde, Mheshimiwa Sabreena H. Sungura, Mheshimiwa Salum K. Barwany, Mheshimiwa Moza A. Saidy, Mheshimiwa John P. Lwanji, Mheshimiwa Sylvester Masele Mabumba, Mheshimiwa Kapteni John Z. Chiligati, Mheshimiwa Antony G. Mbassa, Mheshimiwa Riziki Omar Juma, Mheshimiwa Aggrey D.J. Mwanri, Mheshimiwa Amina Andrew Clement, Mheshimiwa Lolesia J. Bukwimba, Mheshimiwa Ummy Ally Mwalimu, Mheshimiwa Josephine J. Genzabuke, Mheshimiwa Mbarouk Salim Ali, Mheshimiwa Meshack J. Opulukwa, Mheshimiwa Amina Mohamed Mwidau, Mheshimiwa Maria I. Hewa, Mheshimiwa Eng. Gerson H. Lwenge, Mheshimiwa George B. Simbachawene, Mheshimiwa Stephen M. Masele, Mheshimiwa Albert O. Ntabaliba, Mheshimiwa Agripina Z. Buyogera, Mheshimiwa Luhaga J. Mpina, Mheshimiwa Hamad Ali Hamad na Mheshimiwa Anastazia J. Wambura.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naomba kujibu hoja za Kamati ya Bunge ya Miundombinu. Ninazo hoja nyingi lakini kwa vile muda wenyewe hautoshi, nitajaribu kuchagua zile hoja muhimu ambazo nitazipitia na kuzitolea ufanuzi. Hoja ya kwanza ambayo imetolewa hapa na Kamati ya Bunge ni kuhusu Makadirio ya Mapato ya shilingi milioni 1.9, kwamba ni kidogo kuliko kiasi kilichokusanywa cha shilingi 19,000,658,751/= katika mwaka wa fedha 2010/2011. Wizara iwe makini katika kukusanya makadirio ya mapato.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maelezo ya hoja hiyo ni kama ifuatavyo: Katika mwaka wa fedha 2010/2011, Wizara ilikadiria kukusanya jumla ya shilingi bilioni moja na laki tisa kutokana na mauzo ya nyaraka za zabuni mbalimbali. Hadi kufikia Mwezi Mei, 2011, Wizara ilifanikiwa kukusanya jumla ya shilingi 19,000,658,751.62/= ikiwa ni ongezeko la 1035% ya makisio. Makusanyo ya ziada ya fedha zilizokusanywa yalitokana na mambo yafuatayo:-

(i) Mishahara isiyolipwa shilingi 15,317,001.62/= kutoka Tume ya Sayansi na Teknolojia, baada ya watumishi kuacha kazi.

(ii) Uuzwaji wa nyaraka za zabuni, shilingi 736,750/=.

(iii) Marejesho ya masurufu ya safari ambayo ni shilingi 3,605,000/=.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kimsingi sababu zilizochangia makusanyo halisi kutowiana na makadirio ni kutokana na ukweli kwamba baadhi ya sababu zilizochangia huwezi kuweka katika matarajio ya Wizara kama chanzo cha mapato. Mathalan wafanyakazi kuacha kazi na hivyo mishahara yao kurejeshwa Hazina na kuhesabiwa kama sehemu ya mapato.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja ya pili ni kwamba, Wizara iwe makini katika mipango ya miradi ya maendeleo hasa pale ambapo fedha nyingi hutegemea wafadhili kwa kuwa fedha hizo hazitolewi kama itakiwavyo na kwa wakati. Ushauri huu umezingatiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja ya tatu ilihusu pongezi kwa Wizara kwa kutenga fedha nyingi zaidi katika miradi ya maendeleo kuliko matumizi. Wizara imepokea pongezi hizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja ya nne ni kuwa, Kamati imesikitishwa na kupungua kwa bajeti ya Wizara kutoka shilingi bilioni 71.017/= hadi kufikia shilingi bilioni 64.017/= katika mwaka wa 2011/2012. Majibu ya hoja hiyo ni kama ifuatavyo: Ni matarajio yetu kuwa bajeti ya Wizara itakuwa ikiongezeka kadri mapato ya Serikali yatakavyokuwa yakiongezeka na kwa kuzingatia maeneo ya kipaumbele yaliyoanishwa katika Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano uliozinduliwa hivi karibuni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimemsahau Mbunge mmoja ambaye amechangia hoja yangu, naomba nimirante, Mheshimiwa Eng. Gerson Lwenge ambaye amechangia kwa maandishi. Mheshimiwa Mbunge, naomba unisamehe sana kwa kufanya makosa hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja ya tano ilihusu Wizara kushindwa kutekeleza baadhi ya miradi ya maendeleo kutokana na kutopatikana kwa fedha. Jibu la hoja hiyo ni kama ifuatavyo: Wizara inakiri kushindwa kutekeleza baadhi ya miradi ya maendeleo kutokana na kutopatikana fedha. Hii ilitokana na baadhi ya matukio yaliyohitaji fedha nje ya bajeti ya Serikali na hivyo kupunguza fedha zilizokuwa zimeelekezwa katika miradi ya maendeleo. Miongoni mwa matukio hayo ni pamoja na njaa na uhaba wa umeme. Hata hivyo, ni matarajio ya Wizara kuwa katika mwaka wa fedha 2011/2012, Wizara kwa kushirikiana na Wizara ya Fedha, itahakikisha kuwa fedha za miradi ya maendeleo zinapatikana kama ilivyopangwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimewasahau tena Waheshimiwa Wabunge wengine wawili na naomba niwataje, Mheshimiwa Betty Machangu na Mheshimiwa Desderius J. Mipata. Hawa wamechangia kwa maandishi.

MWENYEKITI: Huyo ni Betty Machangu, siyo Mchangu.

WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA: Betty Machangu, ahsante sana. Naona maandishi sikuyafahamu vizuri, naomba mnisamehe. Mheshimiwa Mbunge, naomba samahani kwa hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja ya sita ilikuwa changamoto zinazoikabili Wizara kutoshughulikiwa ipasavyo. Wizara kwa kushirikiana na wadau wengine imeandaa mikakati ya kushughulikia changamoto mbalimbali inazokabiliana nazo. Mathalan kutafuta vyanzo vingine vya fedha, kushirikisha sekta binafsi katika miradi ya maendeleo, pamoja na kutumia rasilimali zilizopo kwa ufanisi zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja ya saba, Serikali ikamilishe mapema Mradi wa Anuani za Makazi na Posta. Jibu la hoja hii ni kama ifuatavyo: Mradi huu umewekwa katika mpango wa kazi wa Wizara katika mwaka 2011/2012. Aidha, Wizara kwa kushirikiana na wadau wengine ambao ni Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI) na Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, inaendelea kubaini vyanzo vingine vya fedha kwa ajili ya kuutekeleza mradi huu. Mazungumzo yameanza na Jamhuri ya Korea Kusini na Benki ya Dunia, vilevile juhudzi zinafanywa ili kuanza kutekeleza mradi huu Dar es Salaam.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja ya nane ilikuwa ni kwamba, Serikali iwezeshe Shirika la Posta kimtaji ili liweze kutoa huduma bora zaidi na kuhimili ushindani. Majibu ya hoja hiyo ni kama ifuatavyo: Serikali inaendelea kurekebisha mizania ya Shirika la Posta na kufanya tathmini ya mahitaji ya mitaji kwa ajili ya shirika hilo kwa nia ya kuboresha mtaji na kuweka mazingira mazuri ya kuliwezesha kupata mikopo kutoka taasisi mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja namba tisa iliyotolewa na Kamati ya Bunge ilisema, Serikali ifanye juhudzi za makusudi kuikwamua Kampuni ya Simu Tanzania (*TTCL*) kifedha na kiutendaji ikiwa ni pamoja na taasisi za Serikali kulipa madeni yote ya shilingi bilioni 6.3. Jibu la hoja hiyo ni kama ifutavyo: Katika jitihada za Serikali kuikwamua *TTCL* kifedha na kiutendaji, yafuatayo yamefanyika:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, tathmini imefanyika ili kuwezesha Serikali kutoa dhamana ili *TTCL* iweze kukopeshwa fedha inazohitaji kutoka kwenye mabenki yaliyoonesha utayari kuikopesha kuititia rasilimali zilizopo za *TTCL*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, utaratibu unaandaliwa ili *TTCL* iweze kupata mbia na mwekezaji mpya baada ya mbia aliyepo sasa hivi kuondoka kwenye shirika hilo. Kuhusu deni la shilingi bilioni 6.3 ambalo Serikali inadaiwa na *TTCL*, Serikali itaendelea kulipa deni hilo kuititia tengo la fedha za bajeti kwa kila Taasisi na Wizara zinazodaiwa na Kampuni ya Simu Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja ya kumi ilihu Serikali isifikirie kubinafsisha *TTCL*, badala yake ipewe mtaji wa kutosha ili isimamiwe na kuendeshwa na Watanzania. Serikali tumeipokea hoja hii na jibu lake ni kama ifuatavyo: Katika jitihada za Serikali kuwezesha *TTCL* kuijendesha yenyewe yafuatayo yamefanyika:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, tathmini ya kuwezesha Serikali kutoa dhamana ili *TTCL* iweze kukopeshwa fedha inazozihitaji kutoka kwenye mabenki yaliyoonesha utayari kuikopesha kuititia rasilimali zilizopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, utaratibu unaandaliwa ili *TTCL* iweze kupata mbia na mwekezaji mpya ili iendelee kuujengwa kibashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja ya kumi na moja ilikuwa inasema, Serikali ikamilishe ujenzi wa Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano. Awamu ya kwanza ya ujenzi wa Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano imekamilika na huduma za mawasiliano za mkongo

zimeanza kutolewa. Katika awamu hii jumla ya kilomita 4,300 za mkongo zimekamilika na mikoa 16 imeunganishwa. Mikoa hiyo ni Dar es Salaam, Pwani, Morogoro, Iringa, Mbeya, Dodoma, Singida, Arusha, Manyara, Kilimanjaro, Tanga, Shinyanga, Mwanza, Tabora, Mara na Kagera. Hii ni sawa na asilimia takribani sitini (60%) ya Makao Makuu ya Mikoa yote na asilimia takriban hamsini (50%) ya Wilaya zote nchini zimefikiwa na mkongo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, katika awamu ya kwanza, vituo sita vya kuunganisha mawasiliano vya nchi jirani zimeunganishwa. Ujenzi wa awamu ya pili ulianza rasmi Agosti, 2010. Awamu hii inahusisha njia kuu za Dar es Salaam, Lindi, Mtwara, Songea, Njombe, Makambako, Tunduma, Sumbawanga, Tabora, Kigoma, Biharamulo, Musoma, Sirari, Tanga, Horohoro, Ungunja na Pemba. Awamu hii inatarajia kukamilika katika kipindi cha miezi 18 tangu kuanza kwa utekelezaji, yaani mwaka 2012.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile Wizara imewasiliana na *TANESCO* ili kutumia mkongo uliopo kati ya Pemba na Tanga kwa ajili ya kuiunganisha Pemba na Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano. Pia Unguja, itaunganishwa na mkongo kwa kutumia njia hii hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja ya kumi na mbili ni kwamba, Serikali iimarishe ulinzi katika miundombinu ya mkongo wa Taifa. Kuna mikakati mbalimbali ambayo Serikali inafanya ili kukamilisha hatua hii ambayo ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara kwa kushirikiana na Manispaa, *TANROADS*, na Wadau wanaoshiriki katika ujenzi wa mkongo, wanaendelea kutoa elimu kwa wananchi wanaoishi karibu na maeneo ambayo mkongo unapita. Wananchi waelimishwe kuhusu madhara ya kuharibu mkongo, pamoja na manufaa yake kwa ujumla. Serikali inafanya kazi hiyo, hadi sasa wananchi wanatoa ushirikiano mzuri kwa ulinzi wa mkongo wa Taifa katika maeneo mbalimbali nchini ambamo mkongo huo umepita na kuna hatua nyingi ambazo tumechukua katika kuulinda mkongo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakwenda kwenye hoja nyingine na nitajaribu kuziruka nyingine kwa sababu muda hautoshi.

Hoja ya 15 kuhusu Mfuko wa Mawasiliano kwa wote uanze kazi zake sasa, kwani muda mrefu umepita tangu uanzishwe. Jibu la hoja hiyo ni kama ifuatavyo; tayari Mfuko wa Mawasiliano kwa wote umeshaanza kufanya kazi, hadi sasa kazi ambazo zimekwisha kukamilika ni pamoja na kuainisha vijiji 239 katika mikoa 17 yenye jumla ya kilomita za mraba 232,981. Katika maeneo yaliyoainishwa kuna idadi ya watu wasiopungua 700,000 wanaohitaji kufikishiwa huduma za mawasiliano. Aidha, vijiji 139 vimechaguliwa kwa ajili ya mradi wa majaribio yaani *pilot project* na uhakiki wa maeneo mengine unaendelea.

Naomba niruke baadhi ya hoja niende kwenye hoja ya 17 kuhusu usimamizi wa uchimbaji wa madini ya *Uranium*. Wizara chini ya utaratibu wa Tume ya Nguvu za Atomiki kwa kushirikiana na Wizara ya Nishati na Madini imetayarisha kanuni na

miongozo mbalimbali ambayo itasaidia kusimamia uchimbaji, usafirishaji na uhifadhi wa madini ya *Uranium*. Vilevile miongozo imeandaliwa namna ya kuelimisha jamii kuhusu usalama wa mionzi, suala hili la kuhakikisha uchimbaji na usafirishaji salama wa mionzi ya *uranium* limeanza kutekelezwa na kuna matumaini ya kupata mafanikio makubwa.

Hoja nyingine iliyopo hapa, Serikali ifanye juhudhi za makusudi za kuhamasisha wagunduzi mbalimbali kwa kutunga sera maalum na sheria. Jibu la hoja hii ni kama ifuatavyo; Wizara kupitia Tume ya Sayansi na Teknolojia hushirikisha watumiaji wa teknolojia kwa kuwasambazia teknolojia mbalimbali zilizojaribiwa na kuthibitishwa yaani *prototype* kama vile jiko bora na mashine za kuendeshwa na upemo au *windmills*. Watengenezaji wa zana za kilimo kwa kuwapa vitendea kazi aidha, aina mbalimbali za msaada kupitia mafunzo, warsha na semina zinatolewa ili kuwawezesha wagunduzi hao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja nyingine iliyotolewa ni Serikali kutenga shilingi bilioni 25.968 ikilinganishwa na Bajeti iliyopita ama ikilinganishwa na ahadi ya Mheshimiwa Rais ambayo ni shilingi bilioni 100. Ni kweli kwamba katika mwaka wa fedha 2011/2012 Serikali imetenga shilingi bilioni 25.968 ikilinganishwa na shilingi bilioni 100 kama ilivyoagizwa na Mheshimiwa Rais. Hii ni kutokana na kupungua kwa Bajeti ya Wizara kwa ujumla wake kwa takriban asilimia 10, katika hali hii isingeweza kuwa rahisi kuongeza fedha hizo. Hata hivyo ni matumaini ya Wizara kuwa Serikali itakuwa ikiongeza kiwango kila mwaka hadi kufikia asilimia moja ya Pato ghafi la Taifa kama Serikali ilivyodhamiria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja nyingine iliyoelezwa na Kamati ya Miundombinu ni kuhamasisha kutambua na kuendeleza vipaji vyta wagunduzi. Jibu la hoja hii ni kama ifuatavyo; Serikali inayo sheria na chombo kinachohusika na kutoa hataza kwa wagunduzi na wabunifu, chombo hiki ni *BRELA* (*Business Registration, Licensing Agency*). Aidha, Tume ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia inayo Kitengo Maalum cha kutoa ushauri kwa wabunifu, wagunduzi na Taasisi za Utasiti kuhusu umuhimu na faida za hakimiliki na hataza. Pia husaidia wagunduzi na wabunifu wote kusajili gunduzi zao huko *BRELA*. Vilevile sera mpya ya Sayansi, Teknolojia na Ubunifu inasisitiza kuwepo kwa mfumuko na mikakati ya kuendeleza wabunifu na wagunduzi yaani tunaita *Innovation Fund* itakayotekerezwa baada ya kukamilika kwa sera. Pia imekusudiwa kutunga sheria itakayosimamia masuala ya sayansi, teknolojia na ubunifu ambayo itaipa nguvu masuala yote ya ugunduzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulikuwa na hoja ya kuimarisha elimu ya sayansi katika shule ikiwa ni pamoa na walimu, ufundi sanifu wa maabara na kudhamini wanafunzi wanaofanya vizuri katika masomo ya sayansi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, majibu ya hoja hii ni kama ifuatavyo; Serikali kwa kuona umuhimu wa masomo ya sayansi iliweka utaratibu wa kutoa mkopo wa asilimia mia moja kwa wanafunzi wanaodahiliwa katika masomo ya vipaumbele ambavyo ni masomo ya sayansi ikiwemo udaktari. Wanafunzi wote wanaochukua masomo ya sayansi hupatiwa mikopo kwa ajili ya masomo yao katika Taasisi za Elimu ya Juu. Aidha, Serikali imeendelea kupanua na kuongeza Vyuo Vikuu na Vyuo vyta Sayansi na

Teknolojia nchini katika jitihada za kuhakikisha kuwa inapata wataalamu wa kutosha wakiwemo walimu wa sayansi na ufundi sanifu wa maabara. Vilevile Serikali imekuwa ikitoa tuzo kwa wanafunzi wanaongoza katika mitihani yao ya kumaliza masomo yao ya ngazi mbalimbali za elimu hapa nchini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna hoja namba 25 ambayo ni kuendelea kujenga uwezo wa tafiti nchini. Jibu la hoja hii ni kama ifuatavyo; Serikali inatambua umuhimu wa kada ya watafiti katika kuleta maendeleo ya sayansi na teknolojia nchini mambo yafuatayo yamefanywa:-

Kwanza, watafiti 198 wamedhaminiwa kwa masomo ya juu, kati ya hao 142 katika ngazi ya uzamili na 56 katika ngazi ya uzamivu katika mwaka wa masomo 2010/2011. Taarifa ya awali inayohusu hali ya miundombinu na vitendea kazi katika Taasisi ya Utafiti imekamilika na utaratibu wa kufadhili tafiti 106 zinazohusu kilimo kwanza kutoka kwenye maombi 380 yaliyopokelewa umekamilika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja ya 26 Serikali iendelee kugharamia utafiti bila ya kutegemea michango ya sekta binafsi. Jibu la hoja hii ni kama ifuatavyo; Serikali kwa kutambua umuhimu wa utafiti kwa maendeleo ya nchi umeanzisha mfuko maalum unaosimamiwa na Tume ya Sayansi Tanzania ambao katika mwaka wa fedha 2011/2012 kiasi cha shilingi bilioni 25.968 kimetengwa kwa ajili ya shughuli za utafiti kupitia fedha za maendeleo. Hata hivyo ushirikishwaji wa sekta binafsi katika kugharamia utafiti ni nyenzo muhimu sana katika maendeleo ya sekta ya sayansi na teknolojia, hivyo Serikali haiwezi kukwepa jambo hili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa niende kwenye hoja ambazo zimetolewa na Kambi ya Upinzani. Hoja ya kwanza Kambi ya Upinzani hairidhishwi na hali halisi ya utekelezaji wa majukumu ya Idara ya Sayansi, Teknolojia na Ubunifu katika kuratibu shughuli za utafiti na maendeleo nchini na kuratibu utekelezaji wa programu ya mageuzi ya sayansi, teknolojia na ubunifu mfano, matumizi ya nishati mbadala rahisi na nafuu za umeme kama *bio gas* na nyinginezo.

Jibu la hoja hii ni kama ifuatavyo; Wizara kupitia Tume ya Sayansi na Teknolojia imeendelea kuratibu shughuli za utafiti nchini, tafiti kadhaa zimefanywa hapa nchini na taasisi mbalimbali kuhusu nishati mbadala ambazo zimewezesha kutengeneza majiko sanifu yanayotumia mkaa na kuni kidogo zaidi. Matumizi ya teknolojia ya *bio gas* katika kupikia na kuwashaa taa na nishati ya jua yaani *solar power* pamoja na upopo kwa ajili ya kuzalisha umeme na kusukuma maji. Nishati hizi hupunguza gharama na uharibifu wa mazingira. Hivi sasa majiko sanifu yanasantazwa sehemu mbalimbali nchini na tume kwa kushirikiana na Shirika la Maendeleo la Ujerumanii pia hivi sasa kuna mradi mkubwa wa kujenga mitambo ya *bio gas* nchini unaofanywa na *CAMARTEC* ikishirikiana na Serikali ya Uhulanzi.

Pia tume imeanza ushirikiano na wadau mbalimbali ili wajasiriamali wawzeze kuandaa mpango maalum wa kusambaza teknolojia hizi nchini kibashara zikiwemo pia nishati jadilifu. Aidha, Wizara kwa kushirikiana na *UNESCO* imeendelea kuratibu

programu ya mageuzi ya sayansi na teknolojia. Naomba nimirata Mheshimiwa Ummi Ally Mwalimu kwa kuchangia kwa maandishi. Naomba unisamehe sana kwa makosa ya kukusahau. (*Makofit*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja ya pili iliyotolewa pamoja na kwamba tuna watalamu wenyе maarifa, ujuzi na mageuzi muhimu ya teknolojia yanayoweza kurahisisha kazi na kuongeza ubora na thamani ya mazao na bidhaa mbalimbali zinazozalishwa na wananchi, lakini uhaulishaji wa sayansi na teknolojia ni kiungo dhaifu katika shughuli za ukuzaji sayansi hapa nchini.

Jibu la hoja hii ni kama ifuatavyo; Wizara kwa kushirikiana na Tume ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia inaendelea kuratibu hatua mbalimbali za taarifa ya utafiti na maendeleo ya teknolojia kwa kupitia Taasisi ya Utafiti, Vyuo Vikuu na watafiti binafsi kwa kusambaza taarifa za matokeo ya utafiti na taarifa za teknolojia kwa kutumia vyombo vya habari, kushirikisha katika maeneo mbalimbali, mafunzo kwa wajasiriamali kwa kushirikiana na taasisi hiyo.

Pia Wizara ina tuhuma kuwa inapokea maombi maalum kutoka Serikali za Mitaa na watu binafsi kwa ajili ya kutoa mafunzo kwa wajasiriamali au kupata teknolojia. Kwa mfano mikoa ya Shinyanga na Dodoma ilitaka Tume iandae mafunzo kwa mafundi mbalimbali kutoka mikoa hiyo ili waweze kupata ujuzi wa ujenzi wa nyumba za gharama nafuu kwa kutumia udongo na sementi na teknolojia za nishati mbadala. Aidha, Tume inahimiza na kuwezesha uanzishwaji wa viatamizi (*incubators*) na kongano (*clusters*) ili kuwezesha kuahirisha teknolojia. Kongano ni ushirikishaji wajasiriamali, taasisi za utafiti na Serikali yaani *triplexes* katika kuzalisha mazao na bidhaa mbalimbali. Kwa hivi sasa kuna kongano kama vile kongano la Mwani Zanzibar, kongano la kilimo cha muhogo na uyoga Kibaha, kongano la ufuaji chuma na mitambo Morogoro, kongano la mafuta, mbegu za alizeti Mpwapwa, utalii Bagamoyo na Tanga na madini Tanga. (*Makofit*)

Hoja ya tatu ilikuwa udahili wa wanafunzi wanaosoma masomo ya sayansi katika vyuo uambatane na huduma zinazohitajika zikiwemo madarasa ya kutosha, maktaba yenye vitabu, maabara zenyе vifaa vinavyokidhi mahitaji ya mafunzo, Serikali itoe majibu kama inazingatia ushauri huo hatua za kimaendeleo zilizofikiwa hadi sasa. Serikali imezingatia ushauri uliotolewa wa kuhakikisha huduma muhimu kwa ajili ya wanafunzi wa masomo ya sayansi unazingatiwa. Mfano katika Taasisi ya Sayansi na Teknolojia Mbeya katika mwaka wa fedha 2010/2011 ilianza ujenzi wa mabweni mawili yenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 350 kila mmoja. Ujenzi wa mabweni haya umekamilika katika mwaka wa fedha 2010/2011 na awamu ya pili itaanza mwaka huu 2011/2012. Vilevile Taasisi ya Teknolojia ya Dar es Salaam katika mwaka wa fedha 2011/2012 kwa kuzingatia hilo inatarajiwa kukamilisha jengo la ghorofa kumi ambalo litakuwa na ongezeko la madarasa tisa yatakayokuwa na uwezo wa kuchukua wanafunzi zaidi ya 630. Aidha, Taasisi katika mwaka wa fedha 2010/2011 ilianza kwa upanuzi wa maktuba ya Taasisi ambayo itakuwa na uwezo wa kuchukua wanafunzi 350 kwa wakati mmoja kwa msaada kutoka IBM, Taasisi imepatiwa msaada wa vitabu zaidi ya laki moja

ambavyo vimeweza kupunguza kwa kiasi kikubwa ukosefu wa vitabu. Aidha, Taasisi imeanza kufanya ukarabati wa mabweni ya wanafunzi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitajaribu kuruka hoja nyingine kwa sababu muda hauturuhusu. Kuna hoja namba sita kuhusu Tume ya *TEHAMA* ianzishwe pamoja na kurekebisha sera ya *TEHAMA* ya mwaka 2003. Wizara imeshaandaa rasimu wa waraka kwa ajili ya kuanzisha Tume ya *TEHAMA* nchini, Tume hii imesimamia na kuratibu shughuli za *TEKNOHAMA* nchini kwa lengo la kusambaza na kumwezesha kila mwananchi kupata fursa ya kutumia *TEHAMA* ili kuongeza ufanisi na kuhakikisha maendeleo nchini, kijamii na kiuchumi yanapatikana. Aidha, chombo hiki kitasaidia kutatua changamoto zinazokwamisha kuenea kwa ujuzi wa matumizi ya *TEHAMA* katika shughuli za maendeleo nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja ya tisa Wizara iandae mkakati wa kukuza ubunifu katika sekta ya mawasiliano, Wizara itazingatia ushauri wa Mheshimiwa Mbunge. Hata hivyo Wizara kuititia Tume ya Sayansi na Teknolojia inasisitiza kuwepo kwa ubunifu kwa wananchi na inaendelea kufanya tathmini ya ubunifu mbalimbali unaobuniwa na watafiti hao. (*Makofi*)

Hoja ya 12 Serikali ifanye mabadiliko ya sheria mapema iwezekanavyo ili iwe inatoza kodi makampuni ya simu za mkononi yanapouzwa mfano *Celtel* na *Vodacom*. Hoja hii imejibowi kama ifuatavyo; Serikali itahakikisha kuwa makampuni ya simu yanapouzwa kodi zote za Serikali zinalipwa kwa mujibu wa sheria na kanuni za nchi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna hoja inayozungumzia ni suala gani linaloonekana kufanyika kwa *COSTECH* katika Bajeti ya Maendeleo iliyotengwa mwaka 2009/2010 ya shilingi milioni 200 kama fedha za ndani. Fedha hizi zilitengwa kwa mwaka 2009/2010 shilingi milioni 200 ziliikuwa kwa ajili ya kutengeneza na ukarabati wa jengo la Ofisi ya *COSTECH*, ila kutohana na uhaba wa fedha hizo hazikutolewa na Hazina. Wizara imetenga kiasi kama hicho kwenye Bajeti ya mwaka huu na natumaini yangu kuwa fedha hizo zitapatikana kwa ajili ya ukarabati huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja ya mwisho ambayo ningependa kuisemea kuna Wabunge wengi walichangia na kusema kwamba bei ya simu bado ipo juu. Lakini ndugu Wabunge naomba niwafahamishe kwamba bei ya simu imeshuka sana, kabla ya mkongo bei ya simu ilikuwa shilingi $2.50/=$ mpaka shilingi $3/=$ kwa sekunde moja. Leo hii bei ya simu ni baina ya shilingi moja mpaka nusu shilingi kwa sekunde moja ambayo bei hii ukilinganisha na nchi nyingine za *East Africa* kwa mfano Kenya na Zambia na nchi nyingine ni ndogo kabisa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kutoa maelezo hayo sasa naomba kutoa hoja. (*Makofi*)

(*Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa*)

MWENYEKITI: Nakushukuru sana Professa Mbarawa.

Waheshimiwa Wabunge, hoja imetolewa na imeungwa mkono kwa hiyo nitamwita Katibu kwa hatua inayofuata.

KAMATI YA MATUMIZI

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea sasa na Kamati ya Matumizi sasa nitamwita Katibu aweze kutuongoza.

FUNGU 68 – WIZARA YA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA.

MATUMIZI YA KAWAIDA

Kifungu 1001 - *Administration and General*.....Shs. 1,395,266,000

MWENYEKITI: Katibu, nisaidie kuwaorodhesha, tunaanza na Mheshimiwa Stephen Maselle.

MHE. STEPHEN J. MASELLE: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye mchango wangu wa maandishi nilimuuliza Mheshimiwa Waziri kwamba Serikali imejipangaje kudhibiti malipo ambayo wananchi wamekuwa wakitozwa na kampuni za simu kwenye milio ya simu maarufu kama *caller tune* na *ring tones* ambao wamekuwa wakitozwa kila mwezi. Pia nimemuuliza Serikali imejipangaje?

MWENYEKITI: Ni swali moja tu.

NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA: Mheshimiwa Mwenyekiti, *ringing tone* ni *service* ambayo inatolewa na makampuni ya simu na yanakuuliza kwamba kama umeupenda huu wimbo bonyeza alama fulani na malipo unaambiwa shilingi 300/= au 200/>. Kwa hiyo, ni hiyari yako kubonyeza hiyo alama, lakini kama hutaki acha. Ndiyo sababu wakati mwingine unataka kupiga simu mwingine anaku-*beep*, mwingine unampigia, lakini mwingine unaacha kumpigia. Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Stephen Maselle kwamba yanapoulizwa asibonyeze hiyo alama na wananchi kwa ujumla kama hawahitaji kuchajija.

MHE. REGIA E. MTEMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye mchango wangu wa maandishi nilikuwa nimeomba upendeleo wa pekee wa Kata za Tanganyika, Masagati, Uchindile pamoja na Utengule Wilayani Kilombero ambazo hazina kabisa mawasiliano ya simu, natambua kwamba Waziri ameshaeleza kwamba tuwaone huko nje lakini nimeamua kusema hapa kuomba msaada au upendeleo wa kipekee kwa kuwa Kata hivi ziko mbali sana na Wilaya ya Kilombero.

WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA: Mheshimiwa Mwenyekiti, maombi yake tumeyapokea na tutaendelea kuyafanyia kazi na tuna maombi mengi ambayo tutayashughulikia awamu kwa awamu.

MHE. PETER J. SERUKAMBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi sina shida ya mshahara wa Waziri lakini nilitaka kupata *clarification* kwenye jambo moja. Wote tunafahamu kwamba sayansi na teknolojia ndiyo jambo kubwa katika maendeleo ya nchi yetu. Moja ya maoni yetu ambayo ningependa labda Waziri atupe *commitment* tuliomba ikiwezekana Waziri ama Serikali ifikirie kuanzisha Mfuko wa *TEHAMA* ili tuweze kuwapeleka watoto wetu waliofanya vizuri sana kwenye shule za sekondari hasa *form six* waende kwenye vyuo vikuu bora duniani ili na sisi tuanze kupata jamii ya watu ambao wamesoma kwenye vyuo vingine ili tuchanganye hii jamii ya Watanzania na hiyo ambayo watakuwa ni *specific* kwa ajili ya sayansi na teknolojia pamoja na mawasiliano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaamini tukianzisha mfuko huo hasa watu wa *TCRA* wakiombwa waanzishe ninaamini watu wengi watachangia ili tuweze kupeleka watoto wetu hawa hasa wale ambao wamefanya vizuri zaidi kwenye mitihani yao, juzi tumewaona wamekuja hapa na Waziri Mkuu alisema tunaanza kufikiria, lakini sisi kama Kamati tumeenda mbele zaidi kwamba tunaomba sasa lianze kupewa msukumo wa kipekee ili lianze. Naomba Waziri atoe ufanuzi kwenye hili.

WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli sayansi na teknolojia ni kitu muhimu na bila ya sayansi na teknolojia nchi haiweze kuendelea na huu mfuko ni muhimu na tutaendelea kuufikiria na kuufanya kazi.

MHE. AMOS G. MAKALLA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Katika mchango wangu wa maandishi nilimuuliza Waziri juu ya ujenzi wa minara katika Kata za Kanga, Pemba, Kibati, Kinda na Maskati. Lakini katika majibu ya Waziri amesema kwamba Wabunge tuandike tena. Lakini mimi nakumbuka ndiyo maana katika kuchangia niliandika kabisa barua lakini Waziri alinipa orodha ya vijiji na mimi nikaongeza, sasa ananihakikishia vipi kwamba mawasiliano yatafika katika Kata ya Kanga yenye vijiji vitano visivyo na mawasiliano kabisa na Kata ya Kinda kuna vijiji vinne na Kata ya Kibati na Pemba kwenye Wilaya ya Mvomero?

WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kweli nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba alinipa hayo maombi na nimeyafanya kazi na vijiji vyake viko kwenye mpango wetu wa kwanza (*pilot project*) ya *UCAF*.

MHE. RAJAB MBAROUK MOHAMMED: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwanza nimtoe wasiwasni Mheshimiwa Waziri lile lengo langu la kushika shilingi nimeliondoa na kwa sababu lugha laini, nyepesi na nzuri aliyoitumia Mheshimiwa Mussa Zungu ilikuwa inatosheleza. (*Makofii*)

Katika mchango wangu wa maandishi nimezungumzia suala zima la ajali za barabarani. Sasa hivi kumeingia teknolojia mpya ya *u-track*, teknolojia ambayo inatumia mawasiliano kwa lengo la kupunguza ajali. Sasa hapa pamekuwa na malalamiko

kutokana na wamiliki wa mabasi. Nataka kujua kutoka kwa Waziri je, Wizara yake ilihuishwaji na mfumo huu wa *u-track* ili wananchi wasiendelee kuingizwa mkenge wa gharama zisizokuwa na ulazima? Ahsante.

WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA: Mheshimiwa Mwenyekiti, hilo suala lipo kweli lakini naomba nichukue suala lake na nilipeleke kwenye Wizara inayohusika ili tuweze kumpatia jibu sahihi.

NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI: Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri nilikuwa naomba kuongezea tu kwamba hili suala limechukuliwa na Wizara yangu na *SUMATRA* inalifanyia kazi, wamiliki wa makampuni ya mabasi wametuletea malalamiko na tunayafanya kazi, ufumbuzi utapatikana hivi punde.

MHE. MUSSA ZUNGU AZZAN: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye mchango wangu leo asubuhi nilizungumzia namna ya Serikali inavyopoteza mapato mengi sana kwenye makampuni haya ya simu kwa kutokuwa na *mechanism* ya *ku-monitor revenues* ambazo makampuni haya yanakusanya. Nilitoa mfano mdogo tu kwa Watanzania milioni 22 ambao wamekuwa *registered* kwenye simu hizi kila mmoja wao akipiga ile shilingi 200/= kwa siku basi ni *almost* trilioni moja na shilingi bilioni 500 kwa mwaka.

Niliishauri Serikali kuwa kuna mtambo unaitwa *calls accounting monitoring machine* na niliwahi kumsikia Naibu Waziri akizungumzia haraka haraka kwamba wapo katika utafiti na najua kazi nzuri inayofanywa na Wizara pamoja na Serikali, nilitaka kujua utafiti unaweza ukachukua muda gani na lini watatuhakikishia kwamba mtambo huu utakapofungwa basi tujue Serikali itakuwa ina *monitor* na kupata mapato sahihi yanayotakiwa kulipwa ili yaweze kuchangia kwenye Pato la Taifa kwenye masuala la *revenue* na kama nilivyosema kuna Kilimo Kwanza, lakini vilevile kuna Kodi Kwanza ambayo tunahitaji kwa kipindi hiki na naomba Waziri mwenyewe kwa sababu Naibu Waziri hana mshahara hapa.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mbunge unapozungumzia Wizara ni hiyo hiyo moja yoyote atakayejibu sawa.

WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA: Mheshimiwa Mwenyekiti, hili suala tunalifahamu Wizarani na tunalifanyia kazi na ni muhimu sana. Kuna nchi ambazo tunazifahamu mitambo kama hii imewekwa ambayo ni Ghana, Guinea - Conakry na nchi nyininge lakini tunalifanyia kazi na tutakapopata jibu sahihi tutaweza kujenga mtambo huu kuona itatusaidiaje, lakini hilo tunalijua na tunaendelea kulifanyia kazi.

MHE. FATMA A. MIKIDADI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba Serikali kwamba Mfuko wa Pamoja wa Mawasiliano (*UCAF*) uanzie katika Mikoa ya pembezoni ambako hakuna hata simu zile za *TTCL*. Kwa mfano Mkoa wa Lindi katika Wilaya zote na vijiji vingi ukiachia Makao Makuu ya Wilaya hakuna simu. Wilaya ya Kilwa, Liwale,

Nachingwea, Ruangwa, Lindi Vijijini, Lindi Mjini hakuna mawasiliano ya simu za mkononi, tafadhali tuoneeni kwa jicho la huruma. Naomba majibu.

WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kweli maeneo ambayo yapo pembedi tunajua yana matatizo na madhumuni makubwa ya *UCAF* ni kupeleka mawasiliano kule kwenye maeneo ambayo hayana mawasiliano na katika mpango wetu unaokuja yaani *pilot project* maeneo mengi ya Lindi yameidhinishwa mle na yatapelekewa huduma mara moja.

MHE. SAID M. MTANDA: Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mchango wangu wa maandishi nilizungumzia suala hili la Mfuko wa Mawasiliano na nikasema tunashukuru Mkoa wa Lindi kuingizwa vijiji 35 tatizo langu ni kwamba vijiji hivyo viko kwenye Wilaya chache na imeiacha Wilaya ya Lindi Vijijini. Kwa hiyo, nilitoa ushauri wangu na kumwomba Mheshimiwa Waziri kwamba sasa azingatie vijiji vya Jimbo la Mchinga katika Wilaya ya Lindi hasa katika vijiji vya Mpingo, Mivileni, Kiwawa na Rutamba. Nimezungumza na wataalam hawa wa *UCAF* wamesema wako tayari kufanya hivyo. Je, Mheshimiwa Waziri yuko tayari kuwashakikishia wapigakura wangu wa Jimbo la Mchinga kwamba maeneo hayo yatazingatiwa katika mpango na awamu hii?

WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kweli nimekubali yeye mwenyewe ameniambia kuhusu suala hili na sisi tunamhakikishia kwamba tutampelekea mawasiliano kwenye hayo maeneo aliyojasema. (*Makofi*)

MHE. LETICIA M. NYERERE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Mheshimiwa Waziri amezungumzia faida nyingi tu za *new technology* lakini hakugusia kabisa madhara ambayo yanaweza yakasababishwa na hiyo *new technology* ikiwepo *cyber crimes* na *computer crimes*. Je, anawaambia nini Watanzania kuhusu tatizo hili? (*Makofi*)

NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie tu kuhusu *cyber crimes*. *Cyber crimes* unaangalia katika pande mbili, ya kwanza ni katika mtandao wa simu na ya pili ni katika mtandao wa *internet*. Hili suala ni zito kidogo lakini Wizara yetu tayari imeunda timu ambayo italiangalia kwa undani zaidi kupitia *TCRA* namna ambavyo tutaweza kuhakikisha tunaweka taratibu zitakazoweza kudhibiti hili. (*Makofi*)

MHE. MARTHA M. MLATA: Mheshimiwa Mwenyekiti, na mimi wakati nachangia kwa maandishi nilikuwa nimeeleza kwamba *TCRA* inaweza ikawa ni mkombozi mkubwa sana hasa kwa kazi za wasanii ambazo zimekuwa zikiibiwa kupitia mitandao lakini bado na zile kazi za wasanii ambazo zimekuwa zikitumiwa kwenye vyombo kama televisheni na redio kwamba wao waweke utaratibu wa *ku-monitor* kazi hizi ili wasanii waweze kupata haki yao lakini pia zisiibiwe. Lakini Mheshimiwa Waziri hakunijibu, naomba ufanuzi.

NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumze tu kwamba ni kweli kama anavyosema makampuni haya yananunua hizi nyimbo pamoja na miito kutoka madukani. Sasa sina uhakika wa hakimiliki ambazo zinatolewa kutoka kwenye maduka hayo. Nimwombe tu Mheshimiwa Mbunge atupe muda tulifuatilie na ushirikiane na Wizara zingine tuone ni namna gani wasanii ambao wametoa hizi nyimbo wanaweza kufaidika na *service* hii ambayo inatolewa na makampuni ya simu. (*Makofi*)

MHE. ALBERT O. NTABALIBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Katika mchango wangu wa maandishi nimejaribu kuiomba Wizara kwa suala ambalo nilishawahi kuongea na Naibu Waziri kuhusu minara. Jimbo la Manyovu lipo mpakani na nchi ya Burundi. Kwa hiyo, tunavyo vijiji kama 13 vya Kata ya Kajana, Myegera, Myama, Mgela na Kibandeyake. Ni vijiji ambavyo vimepakana na nchi ya Burundi na vyote havina mawasiliano na pale wakimbizi huwa wanaingia na sasa hakuna namna ya kuwasiliana, nilikuwa nimeombwa Wizara kwamba ifanye kipaumbele sio mpaka mwaka 2013 kabla ya maeneo hayo kufanikiwa.

WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nimhakikishie tu rafiki yangu Mheshimiwa Obama kwamba haitafika mwaka 2013 kama anavyosema kwa sababu tayari maeneo anayoyataja, yapo kwenye awamu ya kwanza ya mpango wa *UCAF* pamoja na maeneo mengi ya Mkoa wa Rukwa.

MHE. SYLVESTER MASSELE MABUMBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye mchango wangu wa maandishi nilimuuliza Mheshimiwa Waziri kwamba siku hizi makampuni ya simu yana hizi *promotion* ya kutengeneza mamilionea. Lakini ukweli ni kwamba makampuni yenye yanatengeneza hela nyingi sana. Nilitaka kujua katika *promotion* hizi Serikali inapata kiasi gani kwa sababu kuna mchezo wa Kwanjuka, sijui *I ten, nini...* Watanzania wengi sana wanaibiwa kwa matumaini watakuwa mamilionea. Ahsante. (*Makofi*)

NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyojibu mwanzoni nilivyokuwa nikizungumza, *Gambling* inadhibitiwa au inafanyiwa *regulation* na *Gambling Board*. Lakini tuelewe tu kwamba teknolojia inayotumika kwa makampuni haya ya simu ni ya kawaida ya kutuma *message*. Kwa hiyo, *message* unayotuma kwenda kwenye namba fulani inapitia kwenye mtandao huo huo wa simu kama unavyoweza kumtumia mtu *message* kwenda kwenye namba aliyonayo. Kwa hiyo, mapato yote yanayopatikana kutokana na huo mchezo yanaonekana kwenye mapato ya kampuni husika. Sasa kama wanapata faida au wanapata hasara hilo ni suala ambalo linaonyeshwa katika vitabu vyao vya hesabu.

MHE. MASOUD ABDALLA SALIM: Nakushukuru Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mchango wangu wa maandishi nilizungumzia suala zima la *uranium*. Majibu ya Mheshimiwa Waziri amesema kwamba maeneo ambayo yanagundulika kuwa na *uranium* elimu itatolewa, usimamizi mkali wa uchimbaji na usafirishaji. Kwa kuwa Serikali katika miezi michache iliyopita ilikiri kwamba eneo la Bahi hapa Dodoma kuna dalili zote za

kuwepo kwa *uranium*, je, sasa Mheshimiwa Waziri, yupo tayari kutathimini, kutoa fidia kwa maeneo ambayo yaligundulika ambapo wananchi wameyamiliki kuepusha lile ambalo limetokea Shinyanga na Mwanza kuachiwa mashimo kama ambavyo madini mengine yametokea? (*Makofi*)

WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:
Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kumjibu Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo:-

Kwanza Wizara yangu chini ya *TCRA* kazi yake ni *regulator* siyo kutoa fidia. Sasa sisi tunajua kwamba Wilaya ya Bahi ipo hiyo *uranium* na kazi yetu sisi ni kwenda kusimamia, kuangalia lakini siyo kutoa fidia.

MHE. NYAMBARI C. M. NYANGWINE: Ahsante Mwenyekiti, katika mchango wangu wa maandishi nilisisitiza sana umuhimu wa Serikali kusaidia kuweka mitandao katika vilima vya Nyamwaga, Tazale, Mriba, Susuni na hata Kibaso na imeonekana kabisa kwamba wananchi wa Tarime wanatumia gharama kubwa sana wanapopiga simu kwani mitandao hiyo huingiliana na mtandao wa Kenya maarufu kama *Safaricom* kulipia gharama karibu mara tatu au mara nne. Naomba Mheshimiwa Waziri aniambie ni lini mpango huu utakamilika?

NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:
Mheshimiwa Mwenyekiti, rafiki yangu Nyambari nilishamwonyesha kabisa na *message* ambayo nimetumiwa na watu wa *Airtel* kwamba wiki ijayo pale kwenye milima yake ile aliyonieleza mnara utawaka. Kwa hiyo, nimwombe tu akashuhudie tendo hilo na tuko pamoja naye. (*Makofi*)

MHE. LUHAGA J. MPINA: Ahsante sana Mheshimiwa Mwenyekiti, nimshukuru Waziri kwa kukubali kupeleka mtandao katika Kata ya Sakasaka, Tindabuliki, Lindeka, Mwasengela na Mwabuma.

Swali, kwa kuwa hapa nchini na katika Wizara hii tuna Tume ya Sayansi na Teknolojia, tuna Mamlaka ya Mawasiliiano na leo tena tumeletewa pendekezo la kuundwa kwa Tume ya *TEHAMA*, kazi ambazo tayari zinafanya na hizi Tume mbili na kwa kuwa tuna tatizo la Kibajeti ambapo tunashindwa hata kuzihudumia hizi Tume tulizonazo. Ushahidi tunao wa Kibajeti hata kwenye Wizara yake Mheshimiwa Waziri, katika Bajeti ya Maendeleo mwaka uliopita ameleteewa asilimia 49 tu katika matumizi ya kawaida ametumia asilimia 82 tu. Sasa leo tena tunapendekeza kuletwa kwa Tume nyingine, tume juu ya tume ambayo itatupelekea ku-*divert* zile fedha za maendeleo ziende kuhudumia matumizi ya kawaida kui-service hiyo Tume inayoundwa ya *TEHAMA*. Naomba ufanuzi wa kutosha katika hili.

MWENYEKITI: Ahsante Mheshimiwa Waziri ufanuzi wa kutosha.

WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:
Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kumjibu Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo:-

Kwanza naomba afahamu kazi ya Tume ya Sayansi na Teknolojia (*COSTECH*). Kazi yake ni kusimamia sera na uendeshaji wa mambo ya sayansi na teknolojia. Halafu naomba Mheshimiwa Mbunge afahamu kazi ya *TCRA*, *TCRA* ni *regulator* wa mambo ya simu na mambo ya matangazo mengine kwa mfano ya habari, radio na televisheni. Sasa Tume ya *TEHAMA* kazi yake itakuwa kusimamia mambo ya miundo kwa mfano ya Mkongo wa Taifa, mambo ya *fibre security* na vitu vingine. Kwa hivyo, tume hizi zitakuwa na kazi tofauti.

MHE. SELEMANI S. JAFO: Ahsante Mheshimiwa Mwenyekiti. Mimi nampongeza sana Mheshimiwa Waziri na timu yake kwa kutuhakikishia kwamba hata kwangu kule Kisarawe sehemu za Vikumburu, Dororo, Gwata ambazo nimeziomba zitapata suala zima la mtandao. Lakini naomba nijielelekeze moja kwa moja katika kitabu chetu hiki katika *code number 2103100* ambayo ni suala la *education material supplies and services*. Kitabu chote katika *units* zote 12 ni *unit* moja ya *legal service* peke yake ndiyo ina shilingi 800,000. Kwa hiyo, ina maana kwamba katika *unit* zote hakuna pesa kwa ajili ya kununua hizo *education materials and supply service*. Hali kadhalika katika *code number 231...*

MWENYEKITI: Swali moja!

NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba tu nimfahamishe Mheshimiwa Mbunge kwamba fedha hazikutengwa kwa sababu shughuli hizi zimehamishwa na zinafanyika katika *Government Community Unit*.

MHE. SUSAN L. A. KIWANGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Ningependa kumuuliza Mheshimiwa Waziri kwamba sasa hivi katika shule zetu za msingi kuna mtaala umeingizwa kuhusu masuala ya sayansi, kompyuta. Tunashuhudia wenyewe, baadhi ya shule za msingi zimeshaanza, walimu wanafundisha wanasema “sipiyu” sijui nini, wanachora ubaoni. Lakini kibaya zaidi walimu hao hawajapata mafunzo. Je, Wizara yake imeshirikishwa vipi katika suala zima la kutoa elimu hiyo ya sayansi huko chini na kuwapotenza muda wanafunzi badala ya kujifunza mambo mengine, wanafunzwa vitu ambavyo hawataenda kwenye *practical?*

WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kumjibu Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo:-

Wizara yangu tunao mpango wa kuendeleza wafanyakazi wa Serikali na kwa kuanzia tu kama nilivyosema kwenye hotuba yangu leo, tulishawaendeleza wafanyakazi wa *TTCL* jinsi ya kutumia Mkongo na baadaye tutakwenda kuwaendeleza baadhi ya walimu wa shule zetu jinsi ya kutumia hayo mambo ya *TEHAMA*.

MHE. MARIA I. HEWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri ukurasa wa 59 na ndiyo huo nilirejea katika mchango wangu wa maandishi, amezungumzia changamoto za mwaka 2010/2011 akitaja moja ya eneo ni kuhusu kiwanda ambacho kilikuwa kimejengwa kwa minajili ya kuwa kiwanda cha

ngozi ikawa sasa kimebadilishwa kuwa cha taaluma. Lakini akiwa anaongelea kwamba ndiyo kinaanzishwa na fedha zinatafutwa. Ilikuwa mwaka 2010/2011, sasa je, 2011/2012 kwa kuangalia katika vitabu, labda sikuona vizuri je, pesa sasa zipo walau kuanzisha taaluma ya ngozi katika kiwanda hicho Mwanza ambacho kiko Wilaya ya Illemela?

NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba na mimi niweze ku-*declare* kwamba na mimi ni mdau katika kiwanda hicho. Lakini nimweleze tu Mheshimiwa Mbunge kwamba kwa mwaka jana hatukuwa na pesa za kutosha kuweza kufanya ukarabati. Lakini mwaka huu tumetenga pesa kwa ajili ya kufanya ukarabati. Lakini kozi zenyewe za teknolojia ya ngozi hazitaanza moja kwa moja kwa sababu inabidi mitaala yake itengenezwe na ipitishwe kulingana na taratibu zinazohusika. Ila tutakuwa na kozi fupi fupi ambazo zitafanyika pale zinazohusiana na teknolojia ya ngozi pamoja na teknolojia ya *ICT* kwa mwaka ujao wakati tukijiandaa kukamilisha taratibu zingine.

MHE. DKT. MAUA ABEID DAFTARI: Ahsante Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi sihitaji mshahara wa Mheshimiwa Waziri, lakini nataka ufafanuzi mdogo tu. Je, Mheshimiwa Waziri anajua kwamba Kampuni ya Simu ya *Tigo* imeuza minara yake yote ya mawasilano kwa Kampuni ya *Heliac* ya Denmark, anajua hilo? Na kama anajua, je,...

MWENYEKITI: Swali ni moja Mheshimiwa Dkt. Maua Daftari. Mheshimiwa Waziri unajua hiyo taarifa kama kuna biashara imeshaendelea?

WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kumjibu Mheshimiwa Dkt. Maua Daftari kuwa Kampuni ya *Tigo* haijauza minara yake badala yake *ime-lease*, imekodisha siyo kuuza. Hiyo tunafahamu. (*Makofii*)

MHE. STEPHEN H. NGONYANI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kwanza nataka niishukuru Wizara ya Mawasiliano kwa kazi nzuri wanayoifanya, kwa sababu mimi niliomba kwa simu, tulituma *message* kwa Waziri na leo hii ameanza kunifungia *boom*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ila nina sehemu nyingine katika vijiji vyangu nimeweka kwa maandishi. Kijiji cha Kizara, Bombo Mtoni, Dindila, Mgwasho, Mhale, Magamba kwa Lukonge na Toronto, hivi vijiji havina mawasiliano kabisa na mifugo ndiyo inatoka huko. Nataka na huko anihakikishie Mheshimiwa Waziri kwamba vile alivyofanya kwenye simu anifanyie na huko. Ahsante sana. Mimi nitamwongeza mshahara, sipunguzi mshahara. (*Makofii/Kicheko*)

WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kumjibu Mheshimiwa Mbunge kuwa ni kweli namhakikishie Mheshimiwa Mbunge tutampelekea lakini awamu kwa awamu, kwa sababu mahitaji ni mengi na *resources* ni kidogo.

MHE. SALIM HEMED KHAMIS: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kama tujuavyo hivi sasa shughuli zote za utafiti zinaratibiwa na Tume ya Sayansi na Teknolojia (*COSTECH*). Lakini kuna tetesi kwamba kuna urasimu mkubwa katika kutoa pesa za utafiti kwa watafiti. Mara nyingine watafiti hulazimika kutoa rushwa ili kupata fedha zilizoidhinishwa. Je, ili kuepuka na hayo yanayozungumzwa, kwa nini fedha hiyo isipelekwe moja kwa moja katika vyuo vilivyohusika ili usimamizi uwe wazi zaidi na Zanzibar kwa nini hakuna ofisi ya *COSTECH*?

MWENYEKITI: Swali moja!

WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:
Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kumjibu Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo:-

Kwanza na-*declare* kwamba hakuna *corruption* kwenye *COSTECH*. Hakuna kitu kama hicho, na sisi kwenye *COSTECH* tunajaribu kufanya au kufuata *international standard practice* ya *research evaluation*, kwa vile vitu vyote viko katika *standard* nzuri na hata ukienda Zanzibar ukiuliza Chuo cha Kilimo pale wamepata pesa toka kwa *COSTECH* na tunategemea karibuni tutafungua ofisi Zanzibar ili kuhamasisha shughuli hizo. (*Makofi*)

MHE. LOLESTIA J. M. BUKWIMBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa nafasi hii. Na mimi katika mchango wangu wa maandishi nilionyesha kuna baadhi ya Kata katika jimbo la Busanda - Geita, Kata za Nyamarimbe, Kamena na Kata ya Nyamigota pamoja na Nyanyachilulumu, kwa kweli hazina mawasiliano kabisa. Nilitarajia pia katika mfuko wa *UCAF* zitakuwepo Kata hizi au Wilaya ya Geita au Mkoa wa Mwanza lakini haupo kabisa katika mpango. Sasa basi ningependa kujua kwamba Serikali ina mpango gani katika kuhakikisha kwamba mawasiliano katika kata hizo nilizozitaja?

NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:
Mheshimiwa Mwenyekiti, nimhakikishie tu dada yangu Mheshimiwa Bukwimba kwamba orodha aliyoona ni ya awamu ya kwanza. Kwa hiyo, tusingeweza ku-*cover* kila kitu kwa wakati mmoja. Lakini bado tunaendelea na kama nilivyotoa maelezo mwanzoni ni kwamba makampuni nayo yana programu yake peke yake ambayo yanaangalia mahali ambapo panavutia kibashara tayari yameshaweka mikakati hiyo. Kwa hiyo, inawezekana akapata kutoka kwa makampuni moja kwa moja au atapata katika awamu ya pili ya *UCAF*.

MHE. SULEIMAN NASSIB OMAR: Ahsante Mwenyekiti. Mashirika ya Simu ya *Vodacom*, *Tigo*, *Zantel* na *Airtel* yana-*operate* Zanzibar. Katika haya manne *Zantel* peke yake ndiyo inalipa ushuru kwa Serikali ya Zanzibar yaani kodi. Je, Mheshimiwa Waziri atachukua hatua gani ya kuhakikisha mashirika matatu yaliyobakia yanalipa kodi kwa Serikali ya Zanzibar?

WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:
Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kumjibu Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo:-

Mashirika yote ya simu yanalipa kodi kwa *TRA*, kama yanalipa Zanzibar najua Shirika la *Zantel* ni Shirika la Zanzibar yaani Serikali ya Zanzibar ina *percentage*. Nafikri wanalipa ile hisa yao kuliko kodi. Lakini mashirika yote ya simu yanalipa ushuru *TRA*.

MHE. DKT. TITUS M. KAMANI: Ahsante Mwenyekiti, sasa hivi katika makampuni ya simu unapopiga simu yanaanza na tangazo la kukuambia jiunge na nini... kabla hata hujajua kama unayempigia ameshapata mwito au hapatikani. Sasa hii ni kupoteza wakati wa mteja na wakati wewe ni mwanachama wa hiyo kampuni halafu inakuambia jiunge na simu hii. Naomba tupate ufanuzi kwa nini wanatupotezea muda Watanzania wa kuzalisha? (*Makofi*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, hilo swali la muhimu sana! (*Kicheko*)

NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninavyofahamu ukipiga simu moja kwa moja ikaita na uliyempigia akapokea hakuna hayo maelezo. Isipokuwa kama ukapiga, ukamkosa au ukakuta ile simu inazungumza, basi wanaanza na hiyo *advertisement*. Sasa sielewi ni kwa namna gani, lakini nadhani mtuachie kama wengine linawakera, tutajaribu kuona namna ambavyo tutazungumza na haya makampuni kuweza kulitatu hili tatizo. (*Makofi*)

MHE. LIVINGSTONE J. LUSINDE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Katika mchango wangu wa maandishi niliiomba Wizara iangalie Tarafa nzima ya Mpwayungu yenyе Kata tano, vijiji 22, hakuna mawasiliano kabisa. Sasa hata gari la *ambulance* mlilotupatia pale hakuna simu ya kulipata. Sijui Waziri ananiahidi nini katika hilo?

WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kumjibu Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mbunge alishaniandikia barua na hii ni moja kati ya ahadi za Mheshimiwa Rais na tunazifanyia kazi. Tunamhakikishia hivi karibuni mawasiliano yatapatikana. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge fungu hilo nadhani tumemaliza huyo ndiyo msemaji wa mwisho.

(*Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote*)

Kifungu 1002 – <i>Finance and Accounts</i>	Shs. 325,306,000
Kifungu 1003 – <i>Policy and Planning</i>	Shs. 575,519,000
Kifungu 1004 – <i>Internal Audit Unit</i>	Shs. 95,400,000
Kifungu 1005 – <i>Legal Unit</i>	Shs. 54,315,000
Kifungu 1006 – <i>Information, Edu. and Comm. Unit</i> ... Shs. 160,711,000	

Kifungu 1007 – *Procurement Management Unit*.....Shs. 176,275,000
Kifungu 1008 – *Management Information System*...Shs. 112,352,000
Kifungu 2001 – *Communication Division*.....Shs. 425,105,000

(*Vifungu viliviyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote*)

Kifungu 2002 – *Information, Comm. and Tech*.....Shs. 568,634,000

MHE. RAJAB MBAROUK MOHAMMED: Mheshimiwa Mwenyekiti, *sub-vote 2002, item 410700 - feasibility studies, project preparation and design*. Hili fungu halikuwekewa hata senti tano. Naomba maelezo kutoka kwa Mheshimiwa Waziri.

WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kumjibu Mheshimiwa Rajab Mbarouk Mohammed. Hili haliwekewi pesa kila mara, linawekewa pesa pale ambapo uko huo mradi wa kufanyiwa hiyo *feasibility study*.

(*Kifungu kilichotajwa hapo kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote*)

Kifungu 3003 – *Science and Technology*.....Shs. 19,910,294,000

MHE. ZAINAB R. KAWAWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Nimejaribu kupitia maeneo yote kwa ujumla wake lakini nitaizungumzia hii *sub-vote 3003 - basic salaries pensionable terms*. Nilikuwa naona mshahara wa wafanyakazi...

MWENYEKITI: Kifungu gani?

MHE. ZAINAB R. KAWAWA: Kifungu 210100 ambacho kinahusu *basic salaries and pensionable posts*.

MWENYEKITI: Ehe, sawa!

MHE. ZAINAB R. KAWAWA: Nilikuwa nataka kujua, naona kwa ujumla katika vifungu vyote kumekuwa kama ongezeko ni la mshahara mdogo sana kati ya mwaka wa fedha uliopita na mwaka wa fedha huu. Lakini hapa mshahara unaonekana umeshuka zaidi ukilinganisha na mwaka wa fedha uliopita. Sasa nataka kujua kama je, watumishi hawatopata nyongeza ya mshahara au hii nyongeza kidogo ina maanisha kwamba labda mtaajiri watumishi wachache sana katika hayo maeneo? Nashukuru.

WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kumjibu Mheshimiwa Mbunge kuwa hii kuwa imepungua ni kwa sababu sisi tunakadiria kifungu kutokana na *payroll* ya mwisho wa mwaka.

(*Kifungu kilichotajwa hapo kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote*)

FUNGU 68 – WIZARA YA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA
MPANGO WA MAENDELEO

Kifungu 1003 – *Policy and Planning*.....Shs. 100,000,000
Kifungu 1008 – *Mgt. Information System*.....Shs. 1,191,700,000
Kifungu 2001 – *Communication Division*.....Shs. 3,109,586,000
Kifungu 3003 – *Science and Technology*.....Shs. 35,816,971,000

(*Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote*)

(*Bunge lilirudia*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa mtoa hoja, taarifa!

TAARIFA

WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:
Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa taarifa kuwa Bunge limekaa kama Kamati ya Matumizi na kuyapitia Makadirio ya Matumizi ya fedha ya Wizara Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia ya mwaka 2011/2012 kifungu kwa kifungu na kuyapitisha bila mabadiliko yoyote. Hivyo basi, naliomba Bunge lako Tukufu liyakubali Makadirio haya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja. (*Makofi*)

WAZIRI WA UJENZI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki! (*Makofi*)

(*Hoja ilitolewa iamuliwe*)
(*Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa*)

(*Makadirio ya Wizara ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia kwa mwaka 2011/2012 yalipitishwa na Kamati ya Bunge*)

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, hoja imetolewa na imeungwa mkono na basi Bunge hili limeyapitisha Makadirio ya Bajeti ya Wizara hiyo ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia na nichukue nafasi hii sasa kuwatakia kila la heri Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na watendaji wote wa Wizara katika kusimamia utendaji wa Wizara hiyo kwa mwaka huu wa fedha ambao tumeshaupitisha mafungu yake na tunawatakia kila la heri ili Watanzania wote waweze kusikika katika nchi nzima kama mlivyoona. (*Makofi*)

Baada ya kuwapongeza na kuwakia kila la heri Waheshimiwa Mawaziri katika utekelezaji, basi naomba nimalizie kabisa na tangazo lao.

Waziri ametuomba kesho tukutane na huyo Mkurugenzi Mtendaji wa *UCAF*. Sasa tumekubaliana Waheshimiwa Wabunge ili kuweza kuwasilisha zile taarifa zetu za maombi ya vijiji vyote kama tulivyoambiwa maeneo ya Kata, Wilaya na Mikoa yetu, basi tuonane na huyo Mkurugenzi, Ukumbi wa Pius Msekwa saa saba mchana.

Kwa hiyo, saa saba mchana nawaomba sana Waheshimiwa Wabunge, maeneo yetu yale yanayohitaji simu kama yale ya kwangu ya kule Muhukuru, kule Kilagano na kule Mwepai, basi na mimi nitakwenda kushiriki katika kikao hicho ili nikayaseme maeneo hayo yaweze kupatiwa hizo simu. Kwa hiyo, nawaomba sana Waheshimiwa Wabunge tuhudhurie kwenye huo mkutano utakuwa ni mkutano muafaka kabisa kwetu. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, niwakumbushe Wabunge wa Chama cha Mapinduzi tutakuwa na kikao cha *party caucas* baada ya kuahirisha shughuli hizi sasa hivi katika Ukumbi wa Pius Msekwa. Mwenyekiti wa Kikao anaomba sana muwahi ili tuweze kumaliza kikao hicho mapema. (*Makofi*)

Baada ya matangazo haya naona ratiba yetu na shughuli zilizopangwa katika siku hii leo zimekamilika zote. Basi niwatakie jioni njema na ninaahirisha kikao hiki mpaka kesho saa tatu asubuhi ndani ya Ukumbi huu wa Bunge.

(*Saa 1.07 usiku Bunge liliahirishwa mpaka siku ya Ijumaa,
Tarehe 15 Julai, 2011 saa tatu asubuhi*)

